

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 8 Julai, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 195

Marekebisho ya Maslahi ya Madiwani

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE - (K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELÀ)
aliuliza:-

Katika Mkutano wa ALAT uliofanyika Dodoma Mheshimiwa Waziri Mkuu alikubali na kuahidi kurekebisha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani ili yaendane na ugumu wa kazi zao.

(a) Je, mchakato huo umeanza?

(b) Kama jibu ni hapana, je utaanza lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Same Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alikubali na kuahidi kulifanya kazi kwa kuangalia upya maslahi upya ya Waheshimiwa Madiwani na kuyaboresha. Utekelezaji wa ahadi, hiyo umeanza kufanyiwa kazi kwa kupitia upya maslahi ya madiwani yanayotolewa na Serikali.

Maslahi ya Waheshimiwa Madiwani pamoja na posho za wenyeviti wa mitaa yatazingatiwa wakati wa kufanya mapitio ya Bajeti ya nusu mwaka na utekelezaji wake utaanza mwaka wa fedha 2012/2013 kama ilivyoelezwa wakati kuhitimisha majadiliano ya hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali nia ya Serikali ni kuendelea kuboresha maslahi ya Madiwani kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu na kwa kuzingatia majukumu walijonayo katika kusimamia mipango ya Maendeleo ngazi ya kata na vijiji yaliyoongezeka kutokana na utekelezaji wa sera ya upelekaji madaraka kwa wananchi yaani *D by D* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amesema kwamba mpango huo wa kuboresha maslahi ya Madiwani utaanza mwaka wa fedha 2012 mpaka 2013.

Je, kwa sasa Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuongeza posho ya Madiwani walau waweze kujikimu wakati huu mgumu kabla hivyo viwango vyao havijaboreshw rasmi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lusinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu Lusinde yeye anafahamu kabisa kwamba kabisa hapa mimi ninachoeleza ni msimamo wa Serikali na ninaomba anisaidie asije akanitia majoribuni. Kwa sababu hapa baba aniokoe na yule mwovu. Hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama hapa akatueleza sisi wote hapa kwamba kimsingi Serikali imekubali kuhusu suala la kutoa posho zaidi kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani pamoja na wenyeviti wetu wa vijiji na mitaa. Na akasema kwamba kwa vile jambo hili liliuja hapa wakati *position* ya Serikali ilishakuwa *established*, Serikali isingeweza kulipa malipo hayo kwa wakati huu. Na ndipo kwenye hotuba yake na nawaomba wote Waheshimiwa Wabunge tuende tukaiangalie kama tumesahau kidogo, akasema sasa tunalipitia na sisi tumepata maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia sasa na kuangalia na kutoa mapendekezo ili tuweze kuona kwamba ni kiasi gani kitatolewa. (*Makofi*)

Sikusikia katika maelezo yale aliyotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba alisema kwamba tutaangalia hata kwa kipindi hiki tulichonacho sasa hivi kwamba posho ile itapanda. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Lusinde avute subira ili tuweze kushirikiana wote kwa pamoja, hasa tukijua kwamba kuna huo mpango unakuja, nimesema kwamba kuna *Budget-Review* itafanyika hapa ndiyo tutaangalia kwa undani zaidi na kutekeleza yale anayosema.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Madiwani wanafanya kazi ngumu sana na kila mmoja wetu ni shahidi kwamba wenzetu hawa kipato chao kwa kweli hakiendani na wajibu ambao wanao, wajibu wa kuunganisha majukumu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anakiri na anajua kwamba Serikali mara kwa mara inakuwa na mipango ya dharura kutatta tatizo la dharura inapokuwa ni lazima. Na ahadi ya Serikali Kuu kuboresha maslahi ya Madiwani haijatolewa mara moja imetolewa mara nyingi na siyo mwaka huu wa fedha na tuko katika Bajeti ya Serikali. Na nina hakika vilevile Serikali inatambua kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kufanya utaratibu katika misingi ya dharura, au kupitia *Mini-Budget*, kuona kwamba hatusubiri mpaka mwaka 2013 wakati Madiwani wetu wenye wajibu mkubwa wanateseka. (*Makofi*)

Je, Serikali haioni kwamba ina wajibu kutoa kauli na kama Naibu Waziri anafikiri ye ye hana mamlaka kwa sababu ni msimamo wa Serikali, kwa nini asiahidi kulifuutilia suala hili badala ya kulifunga kabisa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Freeman Mbobe jirani yangu, rafiki yangu, *home boy*, na wakati huo huo kiongozi wa Upinzani. Hapana hatuna misimamo tofauti hapa, msimamo ni mmoja tu wa Serikali. Mimi nimeshiriki katika vikao hivi ambavyo vimejadiliana jambo hili, nimekuwemo mle ndani. Nikitoka hapa nikawaambie Wabunge kwamba kwa hiyo sasa nakubaliana na ninyi nitarudi tena nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu tuangalie tena upya hapa suala la kuwalipa sasa hivi hapa nitasema nalipata wapi, lililosemwa na tukiangalia kwenye *Hansard*, siyo kwamba napinga, mimi ninao madiwani pale katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha, ninawapenda kwa sababu ndiyo wasaidizi wangu wakuu, ndiyo wanaonisaidia kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama anavyosema Mheshimiwa Mbobe, Madiwani baada ya *D by D, Decentralisation by Devolution* majukumu yao yameongezekana sana tunapozungumza shule za sekondari zinazojengwa katika nchi hii *basically*, wanaofanya kazi ile, ni madiwani ndiyo wanafanya kazi ile. Tunapozungumza habari ya kujenga zahanati moja katika kila kijiji katika Tanzania kimsingi wanaosimamia miradi ile ni

wao, tunapozungumzia mambo haya kupeleka madaraka kule wilayani, hao ndiyo wanaofanya kazi hiyo na tunatambua kwamba wanafanya kazi nzuri katika nchi hii.

Ninachokisema tu hapa wala sikisemi kwa ugomvi, ni kwamba sisi tunafahamu wote Mheshimiwa Waziri Mkuu alipohitimisha jambo hili hapa, alisema sasa tunakwenda kuangalia hivyo viwango na ili tuangalie jinsi ya kutekeleza. Sikumsikia anasema kwamba sasa hivi tutalipa, yako mawazo hayo, mawazo hayo watu wanayasi kia lakini kwamba mimi naahidi kwamba nitayapeleka, mimi sioni jinsi nitafanya limekuja, mmesema na kama mnafikiri vinginevyo, tulikuwa na nafasi hapa lakini mimi nachokijua kinachoendelea sasa hivi ni kwamba kazi hii inafanyika kwa nguvu kubwa. Sasa hivi tumekaa wataalam wetu pale TAMISEMI wameketi, kuangalia, hawaangalii hili eneo tu wanaangalia na maeneo mengine yote ambayo yamezungumzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nichukue nafasi hii kwa niaba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba wote tuvute subira katika jambo hili. Mimi ninahakika kwamba mambo mazuri yanakuja tu, suala ni wakati gani tutaanza kutekeleza jambo hili.

Sasa imezungumzwa hapa habari ya *contingency* na vitu vingine kwamba tunaweza kuja kwa mujibu wa dharura, hayo yote tutayaangalia sasa kwa msingi huo wa kuona kama kuna uwezekano wa kufanya hivyo, ili tuweze kufanya nisije nikaona kama nakuwa mgumu sana tutaliangalia kwa sura hiyo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, jibu ni kwamba maslahi ya Waheshimiwa Madiwani, Wenye viti wa Vijiji na Wenye viti wa Mitaa yatazingati na kuboreshwa katika bajeti ijayo 2012/2013. Tuendelee na Wizara hii hii, Mheshimiwa Salum Khalifani Barkway, Lindi Mjini, namwona Mheshimiwa Khalifa, nani anamwulizia swali lake?

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mimi.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mama kule Lindi.

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Napaswa kumwulizia mimi.

NAIBU SPIKA: Swali Namba 198, sasa ndilo ninaloshughulika nalo.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni swali namba 196, la Mheshimiwa Salum Khalifani Barwany.

NAIBU SPIKA: Swali 196, samahani, endelea Mheshimiwa Khalifa.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Salum Khalifani Barwany, naomba swali lake Na. 196 lipatiwe majibu, ahsante.

Kata Zilizoingizwa Manispaa ya Lindi

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.ny. MHE. SALUM K. BARKWAY) aliuliza:-

Tarehe 1 Julai, 2011 Serikali ilitangaza rasmi Halmashauri ya Mji wa Lindi kuwa Manispaa na kuongeza kata tano za Ng'apa, Mnazi Mingoyo, Mbaja, Chikonji na Tandangongoro zilizokuwa kwenye Manispaa ya Lindi Vijijini, kwenye Bajeti ya 2010 kabla ya kuhamishwa kwenye Manispaa ya Lindi Mjini.

- (a) Je, Serikali iko tayari kuhamisha miradi ya kata hizo iliyokwishapitishwa kwenye Bajeti ya 2010/2011 kuhamishwa kwenye Manispaa mpya zilimohamishiwa kata hizo?
- (b) Je, ni miradi mingapi katika kata hizo ambayo Bajeti ilipitishwa na Halmashauri ya Lindi Vijijini katika kipindi cha 2010/2011?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miradi iliyoidhinishwa katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 ya Kata zilizohamishiwa Halmashauri ya Mji wa Lindi ambao umetangazwa kuwa Halmashauri ya Manispaa itaendelea kutekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi kwa kuwa fedha zinaendelea kutolewa na Serikali Kuu. Halmashauri hizi mbili zinaendelea kushirikiana katika usimamizi wa miradi hiyo. Bajeti ya mwaka 2011/2012 ya Manispaa ya Lindi inayoanzishwa ambayo inaendelea kutayarishwa imejumuisha miradi ya kata zilizohamishiwa katika Manispaa hii.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Bajeti ya 2010/2011 Kata tano za Ng'apa, Mbanja, Mingoyo, Tandangongoro, na Chikonji, zilihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya Lindi ili kuongeza eneo la Halmashauri ya Mji wa Lindi ambao Serikali imiteitangaza kuwa ni Halmashauri ya Manispaa. Aidha, fedha hiyo kiliyoidhinishwa ni kiasi cha shilingi 76,707,600. Jumla ya miradi mitano iliidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi katika mwaka wa fedha, mwaka 2010/2011.

Miradi hiyo ya sekta kilimo afya, elimu na maji ambayo imepokea ni kiasi cha shilingi milioni 62,707.600. Mradi mmoja bado haujapokea fedha kiasi cha shilingi milioni 14, kwa ajili ya kujenga nyumba ya mganga wa Zahanati ya Mnari.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kujua ni sababu gani iliyopelekea mpaka pesa za mradi wa kitu muhimu sana nyumba hiyo ikawa mpaka hazijapatikana ?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalifan kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hela zinazozungumzwa hapa ni hela za *Local Government Capital Development Grand*, ndizo tunazozingumza hapa. Hela hizi sehemu kubwa sana ni zile hela ambazo zinatoka kwa wahisani na kama nilivyoeleza hapa hela zote hizo ambazo nimezitaja hapa zimebak tu milioni 14 ambazo ndizo hazijapokewa na Serikali kwa maana ya kupeleka katika ile Halmashauri kwa ajili ya kujenga nyumba hiyo ya daktari katika hiyo zahanati ya Mnari.

Nimezungumza mimi na Mkurugenzi mtendaji wa Manispaa na nimezungumza pia na Mkurugenzi wa ile *District Council* wote wawili kwa pamoja wameniambia kwamba wameniambia kwamba wanashughulikia kuhakikisha kwamba hela hizi zinapatikana kwa ajili ya kwenda kujenga nyumba hii tunayozungumza hapa.

Nina hakika kwamba hata tukienda katika majimbo mengine, wilaya nyingine, Halmashauri nyingine, hata kwako Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kongwa, hela zote zile za *Local Government Capital Development Grand*, hamtakuwa mmeshazipata zote sasa hivi tunawasiliana na Hazina kuhakikisha kwamba hizi hela zinapatikana ili tuweze kumalizia ile miradi ambayo ilikuwa imekuwa *marked* kwa ajili ya kufanya kazi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Khalfan uwe na hakika kwamba, mimi namshukuru tu kwamba Mheshimiwa Mbunge huyu ni makini kwamba anaweza, akafuatilia kwa sababu sasa Halmashauri mamlaka imehamika kule Manispaa, kama hata *trace* akafuatilie kama anavyofuatilia zinaweza zikabaki kwenye Halmashauri ya zamani halafu zikawa hazikutumika kwa ajili ya mradi ule.

Kwa hiyo, awe na hakika tutafuatilia tutasaidiana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinapatikana. (*Makofi*)

MHE. SAID MOHAMED MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, kwa kuwa eneo la Chiponji, lilikuwa mionganii katika jimbo la Mchinga na kwa kuwa kwa muda mrefu utekelezaji wa mradi wa maji katika eneo hilo umekuwa ukisua sua na kila mwananchi pale Chikonji, anamiliki shimo lake kwa ajili kwa ajili ya kutafuta maji.

Je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za dharura hasa Waziri Mkuu kutembelea kijiji cha Chikonji na Namkongo, kwa sababu miradi ya maji katika eneo hilo imekuwa ikisuasua sana ?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Said Mtanda, Ndugu yangu na rafiki yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema ni kweli, hiki anachosema kuhusu haya maeneo anayoyazungumzia Mchinga, ni kweli kwamba wale wana matatizo makubwa mimi nilikuwa sijui kitu kinaitwa Bavua, Bavua nilikuja kujifunza nilipokwenda kule ndiyo nikajua maji yanakutana, kama nilitamka vibaya basi atanisamehe. (*Makofi*)

Kuna tatizo, wana tatizo la maji pale na kama anavyosema kuna shida sasa si tu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda kule, suala ni sisi wasaidizi wake kwenda kule. Sasa mimi nataka nimwahidi Mheshimiwa Said Mtanda kwamba tutashirikiana wote kwa pamoja. Kama ni mimi, ni Mheshimiwa Mkuchika au Ndugu yangu Mheshimiwa Majaliwa, yoyote yule kati yetu ili tuweze kwenda vizuri ili tuweze kusaidiana na wenzetu hawa waweze kupata maji. (*Makofi*)

Na. 197

Hali ya Usafiri katika Ziwa Tanganyika

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Wakazi wa Vijiji vya Karema, Kapalambsenga, Ikola, Isengule, Kasanga na Tongwe vilivyo mwambao mwa Ziwa Tanganyika wanategemea usafiri wa Meli ya *MV. Liemba* ambayo inafanya safari mbili tu kwa mwezi na kuwalazimu wakazi wa vijiji vilivyotajwa kutumia maboti ambayo si salama kwa maisha yao.

Je, kwa nini Serikali isirejeshe utaratibu wa zamani wa kutumia Meli ya *MV. Mwongozo* na *MV. Liemba* ili kwa pamoja kuondoa tatizo la usafiri liliopo kwenye maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, wananchi wa vijiji vya mwambao wa ziwa Tanganyika hutegemea meli za kampuni ya huduma za meli kwa ajili ya usafiri wao kutoka kituo kimoja kwenda kingine. Aidha, ni kweli kuwa hivi sasa wananchi hao wanategemea meli ya *MV. Liemba* peke yake kutokana na meli ya *MV. Mwongozo* kusitisha safari zake tangu mwaka 2008 baada ya kufanyiwa ukaguzi na mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa nchi kavu na majini *SUMTRA* na kugundulika kuwa na matatizo ya utengamano yaani *stability problems*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada za kurejesha huduma katika hali yake ya kawaida kwa kurekebisha tatizo ya meli ya *MV. Mwongozo* kuifanyia matengenezo makubwa meli ya *MV. Liemba*. Hivi sasa tayari mapendekezo ya matengenezo ya meli ya *MV. Liemba*, yameshawasilishwa Serikalini Ujerumani, nao kwa ufadhili nao wameonyesha nia ya kutupa msaada yaani *grant* ya *Euro* milioni 8 sawa sawa na fedha za kitanzania bilioni 16. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezitembelea meli zote mbili mwezi Aprili, 2011.

MHE. MOSHI SELEMAN KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imebaini na kuona matatizo ya meli hizo za *MV. Liemba na Mv. Mwongozo*.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za dharura wakati meli hizo zikifanyiwa matengenezo wananchi wanaoishi katika ukanda wa ziwa waweze kupata chombo mbadala ambacho kitawasaidia katika kuboresha shughuli za usafiri katika eneo hilo?

(b) Kwa kuwa meli ya *MV. Liemba* ni meli ya zamani sana imetengenezwa toka enzi ya Mjerumani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia chombo kipyta kitakachofanya shughuli za usafiri katika mwambao wa ziwa Tanganyika?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso Mbunge wa Mpanga Vijijini kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi Serikali kwa kutambua matatizo ya usafiri yanayowabili wananchi wanaotumia Ziwa Tanganyika, inafanya juhudzi za haraka kuhakikisha huduma za usafiri zinarejea katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matatizo ya usafiri, abiria na uchukuzi katika maziwa makuu, Serikali ina mpango wa kujenga meli mpya katika kila ziwa yakiwemo Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Aidha, upembuzi yakinifu yaani feasibility study imeshafanyika ili kujua ni aina gani ya meli inafaa katika kila ziwa na gharama zake ambazo sasa hivi upembuzi huo unafanywa na kampuni ya *OSC shiftech AS* ya Denmark kwa msaada wa Serikali ya Denmark kuititia Shirika la Maendeleo la DANIDA na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Nimefika Karema na Kagunga

kwa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, matatizo nimeyaona na nimesafiri kwa boti. Kweli tunahitaji hizi meli mpya.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo la usafiri katika Ziwa Tanganyika Serikali imekiri kupitia kauli na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri. Meli ya *MV. Mwongozo* imesimama toka mwaka 2008. Je, huku ndiko kujali matatizo ya wananchi kuchukua miaka mitatu meli haijatengenezwa?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Amour Arfi Mbunge wa Mpanda Mjini kama majibu yangu ya nyongeza niliyoyatoa kwa maswali ya Mheshimiwa Kakosi.

Serikali inafanya upembuzi yakinifu na tumekwishapata mtaalamu wa kufanya *feasibility study* naomba tu awe na subira kwani hayo tutayakamilisha katika kipindi ambacho Serikali imeahidi kutatua matatizo hayo ya usafiri.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea naomba nitambue kuwakumbusha kwa wasiofahamu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko safari lakini nitambue uwepo wa Mheshimiwa Samuel J. Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambaye ndiye anaongoza shughuli za Serikali humu Bungeni. (*Makofii*)

Naomba sasa swali namba 198 liulizwe.

Na. 198

Fidia kwa Wananchi wa Ilungu na Songwe International Airport

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Suala la fidia kwa wananchi wa Ilungu na *Songwe International Airport* halijapata ufumbuzi mpaka sasa. Je, ni lini Serikali itamaliza suala hilo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijiji kama ifuatavyo;

Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe kinajengwa katika eneo la Songwe kama jina linavyoonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001 tathmini ya mali za wananchi waliokuwa katika eneo la Songwe ilifanyika na wananchi wote waliohusika walilipwa fidia walizostahili kwa mujibu wa Sheria na waliondoka kupisha ujenzi wa kiwanja kuanza.

Serikali pia ilifanya tathmini ya mali za wananchi wa Kitongoji cha Iweleje ambacho kipo katika uelekeo wa barabara ya kutua na kurukia ndege lakini kutokana na umbali ambao kijiji hiki kipo kutokea kiwandaji, ilionekana kuwa wananchi hao hawatalazimika kuhama na waliendelea kubaki katika kijiji chao. Hivyo, suala la fidia kwa Wanancni hao halipo kwani hawakuathirika na ujenzi wa kiwanja. Hali kadhalika, kitongoji cha Ilungu hakipo kwenye eneo la mradi wa kiwanja hiki bali kwenye eneo lililopo chini ya Mamlaka ya Hifadhi ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali imetenga eneo katika kitongoji cha Ikumbi kwa ajili ya hoteli, maduka na makazi ya wafanyakazi wa kiwanda cha Songwe cha kimataifa. Tathmini ya fidia kwa wananchi katika eneo hilo inakadirwa kuwa shilingi milioni 60.6. Malipo haya yanatarajiwa kufanya katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa mwaka jana Bunge lililopita Waziri wa Miundombinu ambaye alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa alipita pale na kuongea na wananchi na akawaahidi wananchi kwamba atatumta Tume ya kushughulikia suala la fidia kwa wananchi wa Songwe. Je, Waziri au Serikali inasemaje kuhusu suala hili? Je, itatuma watu wa kwenda kushughulikia suala hilo?

La pili ilikuwa ni kuhusu fidia ya wananchi wa Kata ya Ilungu, Serikali itatuma Tume pia kwenda kuzungumza na wananchi kuhusu suala la fidia kwa wananchi Ilungu ambao wameathirika na *TANAPA*?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo.

Sehemu ya (a) Wizara yangu haina tatizo tunaweza kwenda kule na tukaongea na wananchi ili kama tathmini bado ya madai bado inahitajika itafanyika lakini pia nina taarifa kwamba Mkurugenzi wa Mbeya Vijijini naye anafanya tathmini sasa hivi kuona kama wananchi wote ambao malipo hayakufanya utaratibu huo unafanyika.

Kuhusu suala la kwenda kuzungumza na wananchi, Wizara yangu naamini itakuwa tayari kufanya ziada hiyo, Mheshimiwa Waziri wangu alikwishafika hapo wiki moja iliyopita lakini tuko radhi pia kwenda ili kuongea na wananchi ili haki zao kama zipo ziweze kutimizwa.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuendelea kujenga uwanja wa ndege wa Songwe, Mbeya na kwamba sasa uwanja huo utakamilika mwezi Desemba mwaka huu, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia hiyo nzuri wananchi wa Kijiji cha Ikumbi Mtoni au Iwejele sasa hivi hawana barabara ya kutoka Ikumbi Mtoni kwenda barabara kuu ya lami, na kwa maana hiyo wanashindwa kusafirisha mazao yao hasa Mahindi na mazao mchanganyiko kwa njia ya usafiri wa gari. Serikali inatamka lini sasa kwamba wananchi hao watajengewa barabara baada ya barabara yao kukatwa na uwanja wa ndege ambao ni muhimu pia kwa wananchi wa Mbeya?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wananchi hawa walikuwa wanatoka kijijini kwao kwenda kutafuta mahitaji yao wakipitia sehemu ambayo sasa hivi ni uwanja wa kurukia ndege katika uwanja wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imelitathmini hilo na tumeamua kuwa tutawajengea barabara ya kuwafikisha kijijini kwao na mikakati ya kufanya hivyo imeshaanza kufanyika na TAA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 199

WAMILIKI WA MASHAMBA PORI – KIBAHA MJINI

MHE. SILVESTRY FRANCIS KOKA aliuliza:-

Zaidi ya 50% ya maeneo yaliyoko Kibaha MJINI ni mashamba pori yaliyohodhiwa na matajiri kwa miaka mingi bila kuendeleza:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu wamiliki wa mashamba hayo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuepusha migogoro kati ya wenye mashamba hayo na wananchi wasio na mahali pa kuweka makazi yao?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaelekeza Halmashauri za Miji na Wilaya kuitia kwa uongozi wa Mikoa yote nchini kuorodhesha mashamba yaliyotelekezwa na wamiliki wake ama wamiliki wasiotimiza masharti ya uendelezaji tangu mwaka 2005 ili ardhi hiyo itwaliwe na Serikali na kumilikishwa wananchi wengine wenye mahitaji ya ardhi.

Baadhi ya Halmashauri zilikwishawasilisha mapendekezo na hatua za ufutaji wa hatimili zilizokuwa hai ulifanyika na nyingine ziko katika hatua mbalimbali za kufutwa.

Baada ya kukamilika kwa utwaaji ardhi hiyo hupangiwa matumizi na kugawiwa waendelezaji. Kabla ya kuwasilisha mapendekezo uongozi wa Mkoa hauna budi kujiridhisha kuwa ardhi inayopendekezwa kufutiwa umiliki ama haijaendelezwa kwa mujibu wa matumizi yaliyoidhinishwa au imetekelozwa.

Wizara yangu inapoyapokea mapendekezo hayo huyashughulikia kwa kuzingatia Sheria ya ardhi. Hatua muhimu za kuzingatia ni pamoja na kuhakiki matumizi ya ardhi hiyo na kutoa taarifa (*notice*) kwa mmiliki ya kusudio la kufuta hatimiliki.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuepusha migogoro baina ya wananchi wasio na ardhi ya kujenga makazi na wamiliki wa mashamba katika Wilaya ya Kibaha Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Pwani itahakiki matumizi ya mashamba hayo na ikithibitika kuwa wamiliki wamekiuka masharti ya hatimiliki yatatwaliwa na kugawiwa kwa wananchi ili wendeleze.

Namshauri Mheshimiwa Mbunge kuwa ashirikiane na uongozi wa Wilaya yake ili kutambua mashamba yaliyotelekezwa na kuwasilisha mapendekezo Wizarani ili hatua zifaazo zichukuliwe ikiwemo kupanga upya matumizi ya ardhi husika na kuwamilikisha wawekezaji wengine wakiwemo wananchi wa eneo hilo.

Vilevile natoa wito kwa uongozi wa Mkoa na Wilaya washirikiane kutoa Elimu kwa umma ili wananchi waheshimu Sheria na haki za watu waliomilikishwa mashamba hayo kihalali ili waepuke kuyavamia kwani kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuhimiza uongozi wa Halmashauri za Miji na Wilaya zote nchini kuorodhesha mashamba yaliyotelekezwa au yasiyotumiwa kwa kuzingatia masharti ya hatimiliki na kuwasilisha mapendekezo Wizarani kwangu mapema iwezekanavyo. (Makofi)

MHE. SILVESTRY FRANCIS KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mashamba pori haya yamekuwa yanahifadhi wanyama pori hatari ikiwa ni pamoja na Chatu, ambao kwa mwaka huu wamekwishaua wananchi wawili kutoka Jimbo la Kibaha Mjini, ikiwa ni pamoja na Nguruwemwitu pamoja na jamii ya Nyani ambao wamekuwa wakiharibu takribani nusu ya mazao yanayolimwa na wananchi hawa maskini katika mashamba yao. (*Makofî*)

Kwa kuwa sasa wenyewe mashamba haya wamekwishaandikiwa barua na notisi na Mkuu wa Wilaya pamojana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji bila wao kujibu wala kujali. Serikali ina mpango gani wa dharura kuokoa maisha ya wananchi hawa ambao ni maskini na mali zao?

Waziri sasa yuko tayari kutembelea mashamba pori haya kwa ajili ya hatua zaidi za kiserikali?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Koka Mbunge wa Kibaha Mjini kwa namna ambavyo amekuwa akishughulikia kero zinazowakabili wananchi wake.

Kuhusu suala la hatua ya dharura ya kuchukuliwa ili kuwasaidia wananchi ambao wanakabiliwa na matatizo yanayotokana na mashamba hayo kutelekezwa, ni hatua ambayo Serikali inaweza ikachukua ya haraka ni kuhimiza uongozi kwamba uharakishe kuleta taarifa hiyo ya mashamba hayo kwetu, orodha ya mashamba na hali ya mashamba hayo ili hatua zichukuliwa.

Naomba nieleze kwamba kwa mujibu wa Sheria mwenye Mamlaka ya kufuta hati miliki ya shamba au ardhi yoyote ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, *notice* ambayo imetolewa na uongozi wa Wilaya ni hatua ya awali na watakapokuwa wamewasilisha taarifa hiyo kwetu tunalazimika kwa mujibu wa Sheria yaani Kamishna wa Ardhi kwa mujibu wa Sheria anapaswa kutoa taarifa ya siku 90 kwa wamiliki hao kwenye gazeti la Serikali. Baada ya hapo ndipo hatua ya kufuta hati hizo itachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu kutembelea maeneo hayo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya utaratibu ili ikiwezekana kabla ya katikati ya mwezi Septemba, 2011 tuwe tumefika katika Jimbo la Kibaha na kukagua mashamba hayo na kuhakiki hali yake na baada ya hapo tutashauriana na Uongozi wa Mkoa na Wilaya juu ya hatua za kuchukua za dharura ili kuwaepusha wananchi na kero zinazowakabili hivi sasa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia kuhusu mashamba pori yenye hati. Lakini sehemu kubwa ya mashamba pori huwa hayana hati na eneo ambalo analizungumza la Kibaha Mjini linapakana na Jimbo la Ubungo ambapo vilevile kuna matatizo ya mashambapori maeneo ya Kiluvya, Hondogo, Kibwegere, kwenye Kata ya Kibamba na Mpigimagoe Kata ya Mbezi. Je, Naibu Waziri anatoa kauli

gani kuhusu mashambapori yasiyokuwa na hati lakini hayajaendelezwa na wananchi wako tayari kupata maeneo kwa ajili ya kuendeleza maisha yao?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo kama ifuatavyo:-

Kwanza katika jibu langu la msingi sikutamka neno mashambapori kwa sababu huo msamiati katika sekta ya ardhi hatuna. Tunayo mashamba kwa sababu akishamilikishwa mtu linakuwa ni shamba lake, matumizi aliyopangiwa anapaswa kuyazingatia isipokuwa asipozingatia ndipo tunachukua hatua ya kubatilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashamba ambayo hayalimwi ama hayatumiki ipasavyo katika Jimbo la Ubungo, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu imeshafanya uhakiki wa mashamba hayo ambayo awali maeneo haya yalikuwa ni ya vijiji na yalikuwa yakigawiwa kwa mujibu wa Sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 mpaka hapo yalipotangazwa kwamba maeneo yote yale sasa ni mji na kwa maana hiyo maeneo yale ni mitaa na Serikali imeshaanza mkakati wa kuyapangia mpango yaani *planning area* na kwa maana hiyo viwanja vitapimwa na wawekezaji pamoja na wananchi wa maeneo hayo watapimiwa.

Kwa utaratibu wa sasa hivi ni kwamba mashamba yale hata kama hayana hati lakini wako wenyewe ambao walikuwa wamemilikishwa vijiji na Serikali inaheshimu ugawaji huu ambao ulifanywa na Serikali za Vijihi zilizokuwepo na kwa sababu hiyo hatuwezi kuyatwaa bila kuzingatia Sheria lazima taratibu zilizolezwa chini ya Sheria ya utoaji ardhi ya mwaka 1967 lazima yazingatiwe tunapotaka kutoa ardhi yoyote.

NAIBU SPIKA: Bado tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali linalofuata Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 200

Maeneo ya Wazi kwenye Master Plan za Miji Nchini

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA aliuliza:-

Kabla na baada ya uhuru miji yetu ilikuwa na *Master Plan* ambayo imekuwa ikihuishwa kulingana na maendeleo yanayojitokeza katika miji hiyo na kabla ya miaka ya 80 miji karibu yote ilikuwa na maeneo ya wazi (*Open Spaces*) kwa matumizi ya umma.

Lakini mwishoni mwa miaka ya 80 maeneo hayo yalianza kugawiwa watu bila kuzingatia Mipango miji husika na kufanya kukosekana kwa mahali pa wananchi kupumzika na watoto kukosa maeneo ya michezo yao na kuwafanya wadumae kiafya na kimaendeleo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani kurejesha maeneo hayo?
- (b) Je, ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya Watendaji waliogawa na wanaoendelea kugawa maeneo hayo kinyume cha Sheria, wakiwemo Majaji na Mahakimu na waliohalalishiwa uuzaaji wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikwishaanza kutekeleza mkakati wa kurejesha maeneo ya wazi yaliyovamiwa kwa ajili ya matumizi mengine kwenye Halmashauri za Miji na Wilaya. Kazi inayofanyika kwa sasa ni kukusanya taarifa za maeneo yaliyotengwa kuwa ya wazi kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 nchi nzima ili kujuu hali halisi ya maeneo hayo. Mara kazi hiyo itakapokamilika, hatua za kuyarejesha maeneo hayo kwenye matumizi ya awali zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipojibu swali la Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo, tarehe 1 Julai, 2011 nilieleza kuwa Serikali kwa kuzingatia Sheria za Ardhi na nyingine husika inaendelea kusitisha na kuondoa maendeleo yaliyofanyika kwenye baadhi ya viwanja vya wazi. Mfano, Serikali ilivunja ukuta katika kiwanja Na. 1006 Upanga kilichokuwa karibu na Hoteli ya *Palm Beach* na kiwanja Na. 59 *Ocean Road* kilichokuwa karibu na Hospitali ya Agha Khan na kwenye ufukwe ulio kat i ya viwanja Na. 934 na *615-616 Mbezi Beach*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huwachukulia hatua watumishi ambao hubainika kuwa walishiriki katika kugawa maeneo ya wazi kwa matumizi mengine. Hatua hizo ni pamoa na kuwaachisha kazi, kuwashitaki Mahakamani na kuwafungia leseni za kufanya kazi za kitaaluma. Mfano tarehe 28 Juni, 2011 watumishi wapatao sita (6) wa sekta ya ardhi walifishwa Mahakamani wakituhumiwa kuhusika na kugushi nyaraka na kugawa maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kuwa washirikiane nasi katika harakati hizi za kulinda maslahi ya wananchi walio wengi yasipokonywe na watu wachache wenye tamaa. (Makofi)

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoa na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa kwenye swali langu la msingi kipengele (b) kilikuwa kimezungumzia pia uwajibikaji wa Majaji na Mahakimu, Mheshimiwa Naibu Waziri sijaona akilijibu hilo, ningeomba atoe maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nashindwa kuelewa ina maana kwamba hao watendaji wanachukuliwa hatua baada tu ya kupata msukumo wa Waheshimiwa Wabunge, ningeomba Serikali itueleze ina mkakati gani kuhakikisha kwamba hili halitokei tena? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali langu la msingi liko *very much relevant* na suala hili la ardhi ambalo ni la nchi nzima na siyo Dar es Salaam peke yake. Kwa mfano kwenye Manispaa ya Mbeya, maeneo kama Mwakibete, Mwanjelwa, Isanga, Nzovwe, Ilomba na Ilemi ni maeneo ambayo ni makazi holela ‘squatter’ hususani kwenye eneo la Nzovwe ambalo lilikuwa limeishapimwa, wananchi hawakushirikishwa hata fidia hawakulipwa ikabidi warudi tena kuvamia yale maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa katika kurekebisha hili?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu suala la Mahakimu na Majaji. Ni kweli kwamba yako maeneo ambayo maamuzi ya Mahakama hayakwenda vyema na sheria, tunakiri hilo na napenda niseme kwamba nilikwishawasiliana na Mheshimiwa Jaji Mkuu na tumekubaliana tutakutana ili kwa pamoja tushauriane na kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili kwa lengo la kuhakikisha kwamba halitokei kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mohammed Chande Othuman, kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania. Ukweli kwa muda mfupi ambaa mimi nimekaa na kushauriana naye juu ya masuala mbalimbali nimetambua kwamba Mahakama sasa inae kiongozi ambaye wananchi watapata matumaini makubwa juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linanipeleka katika sehemu ya pili ya swali lake kwamba kuna mkakati gani wa kuepuka makazi holela. Mkakati ni kwamba, kwanza nimeona Mheshimiwa Jaji Mkuu ana dhamira kabisa ya kubadilisha taswira ile ya Mahakama. Tunayo matumaini *image* itabadilika. Lakini peke yake pamoja na Majaji peke yao hawataweza kufanya hivyo, ni lazima tushirikiane nao wote kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetokea Mahakamani mara kadhaa kwenye ama kutoa ushahidi au kumwakilisha Mwajiri katika kesi mbalimbali. Uzoefu unaonesha kwamba *Our Learned Brothers and Sisters* walio mahakamani hawaombi rushwa bali wanakuwa *induced*, tuepuke basi kusijihukumu kwa sababu unaposema kwamba unataka kumu-*induce* Hakimu au Jaji, umejihukumu wewe kwamba una kosa na kwa maana hiyo unahitaji kuhurumiwa ama unataka kununua haki. Tuache kununua haki, tusimame

tukijua kwamba unaposhitakiwa wewe hujahukumiwa bali ni mtuhumiwa tu na una haki na uwezo wa kushinda mbele ya sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili kuhusu makazi holela katika maeneo ya Mwakibete, Mwanjelwa na Nzovwe na maeneo mengine ya mji wa Mbeya, niseme kwamba hali ya makazi holela katika miji yetu yapo katika maeneo mengi sana, miji mingi inalo tatizo hilo kwa sababu ya mazingira ambayo tunayajua kwamba wananchi wengi wamekuwa wakikimbilia mijini kutoka vijijini na wanapofika mijini wanapokosa nyumba za kuishi huamua kujenga popote pale palipo wazi. Sasa kurekebisha hali iliyoko kule Mbeya naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashauriana na wenzetu wa MKURABITA ili tuone ni jinsi gani tuta – *reguralize* makazi ya wananchi walio katika maeneo aliyoyataja hususani yale ya Nzovwe, Mwanjelwa, Mwakibete na maeneo mengine ili kufanya maeneo hayo kuwa ya kissasa zaidi. (Makofi)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Suala la mipangomiji kama halikuwekewa mkakati wa dharura ni janga la kitaifa. Wote ni mashahidi kwamba maeneo mbalimbali ya miji yote mikuu ya mikoa na hata baadhi ya Wilaya katika nchi, ilikuwa na maeneo yaliyopimwa na makazi ya watu yalijengwa kwa madaraja mbalimbali kwa ufanisi na barabara na miundombinu yote ya *ku-support*. Lakini kama Naibu Waziri alivyokiri *rural – urban migration* imesababisha makazi kupanuka kiholela bila kuthibitiwa.

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Serikali itupe kauli hapa kuna mkakati gani wa makusudi wa kudhibiti hali hii kwa sababu inazidi kuwa mbaya na inasababisha watu wengi wanaoishi katika maeneo ya miji kukosa huduma muhimu kama barabara, maji, umeme na hata huduma za uokozi kama za zima moto pale majanga ya moto yanapotokea.

(ii) Je, Serikali itakiri kwamba lawama hii iende kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kushindwa kudhibiti hali hii hadi ikafika kiwango ilichofikia?

SPIKA: Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani ni swal moja tu la nyongeza, lingine umechomekea. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Freeman A. Mbowa, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba ni kweli kama nilivyosema awali kwamba wananchi wengi wamekuwa wakitoka vijijini kwenda mijini (*the rural – urban migration*) imekuwa ni kubwa sana. *The urbanisation Process* imekuwa ni kubwa na niseme kwamba huwezi ukaisimamisha, *process* hiyo itaendelea, siyo Tanzania tu bali

ni Dunia nzima, *the urbanisation process can not be stopped, you can only limit it*, unaweza ukapunguza kasi ya rural – urban migration kwa kuhakikisha kwamba kuna *the basic social amenities in the rural areas*, kuhakikisha kwamba kuna ajira kwani wengi wanaokuja mijini ni vijana, wanapomaliza shule wanakuja mjini kutafuta kazi.

Sasa ili kuhakikisha kwamba tunapunguza kasi hiyo ni lazima tushirikiane, Waheshimiwa Wabunge sote tuna majimbo, katika mipango yetu kwenye Halmashauri zetu tuhakikishe kwamba tunaweka mipango ya kuanzisha ajira kwa ajili ya vijana. Tukifanya hivyo tutapunguza kasi ya vijana kutoka shamba kuja mijini, hiyo ni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nije kwenye sehemu ile ya kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ibebe lawama kwa sababu ya makazi holela kuwepo mijini. Nasema hapana, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haitalaumiwa kwa hili, bali sisi wenyewe tulioko kule kwenye majimbo yetu, tujilaumu kwa sababu tumeshindwa kutengeneza mazingira ya kuwa- *retain* vijana wasije mijini, siyo Serikali, sisi Wabunge tunahusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kupunguza ukuaji wa makazi holela mijini naomba nitoe ushauri hivi, Waheshimiwa Wabunge wote sisi tunazo Halmashauri ambazo hapa tunaziwakilisha kama majimbo, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, kuanzia kifungu cha 58 hadi 62 vinaruhusu eneo lililo karibu na mji ambalo tunaona kwamba lina hatari ya kugeuka kuwa makazi holela kama lisipodhibitiwa. Halmashauri inayohusika kupendekeza kwa Kamishina wa Ardhi kwamba eneo hilo lipangiwe matumizi pamoja na kwamba labda ni kijiji hata kama haliko ndani ya mji. Sasa kama tutashirikiana kufanya hivyo kwamba sote tufanye uhakiki wa Halmashauri zetu maeneo yale ambayo tunayaona kwamba tusipoyashughulikia sasa hivi yatageuka kuwa makazi holela, basi tulete mapendekezo kwa Waziri ili kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 tuweze kufanya uchunguzi na hatima yake kuona uwezekano wa kuyapangia kazi maeneo yale ili kupunguza yasigeuke kuwa makazi holela, hilo lifanyike katika Halmashauri zote. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta, karibu sana.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, karibu nyumbani. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, lakini nawajibika kuongeza kidogo kwa sababu imetajwa Serikali nzima. Simshangai Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kuikandia Serikali ya CCM, ni wajibu wake lakini ningeomba jambo hili litazamwe kwa upana. Serikali ya CCM inafanya mambo mengi kuhakikisha wananchi wanabaki vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumeunda *REA* ili tupeleke umeme vijijini kwa haraka sana, na kazi inaendelea kuwawezesha watu kuona kwamba vijijini nako wanawenza kupata huduma na wakafanya biashara. Kuna mradi mkubwa sana wa maji vijijini lengo ni kuboresha mazingira ya vijijini. Isitoshe tuna MKURABITA, lengo ni

kurasi misha ardhi ambayo ndiyo raslimali aliyonayo mwanakijiji maskini. Sasa ni lazima mipango hii itazamwe kwa upana wake ndiyo uelewe Serikali inafanya kitu gani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sikubaliani na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani kwamba Serikali ya CCM ilaumiwe wakati inafanya mambo makubwa kama haya kuwezesha wananchi wabaki vijijini. Ahsante! (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa tunahamia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, swali namba 201.

Na. 201

Mauzo ya Hisa za TTCL kwa Makampuni ya MSI/DETECOM

MHE. SAID AMOUR ARFI aliuliza:-

Kutokana na mauzo ya hisa za *TTCL* kwa makampuni ya *MSI/DETECON* ambayo yalikuwa na thamani ya *USD 110* millioni na kulipwa kiasi cha *USD 65* millioni na kubaki Salio la *US\$ 45* millioni:-

- (a) Je, salio hilo limeishalipwa au halijalipwa?
- (b) Je, Kampuni ya Ubia ya *CELTEL* iliyouzwa kwa *ZAIN* na kisha *AIRTEL* imeleta faida au hasara kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kuwa makubaliano ya awali kuhusu bei ya mauzo ya hisa asilimia 35 za *TTCL* kwa Ushirika wa Makampuni ya *MSI* na *DETECON* yalikuwa ni bei ya dola za Kimarekani 120 milioni na siyo 110 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya awali ya dola za Kimarekani 65 milioni yalifikiwa baada ya kufanyika uhakiki wa mapato ya *TTCL* kwa mwaka 2000 kama ilivyokubaliwa na pande zote mbili katika mkataba wa uuzaaji na wanahisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikubalika kwamba bei halisi ya hisa asilimia 35 katika *TTCL* kwa *MSI/DETECON* itafikiwa baada ya kupata uhakiki wa hesabu za *TTCL* za mwaka 2000 na endapo mapato ambayo kwa kiingereza wanayaita “*Earning Before*

Interest, Depreciation, Taxes and Amortisation – EBIDTA” yatakuwa pungufu ukilinganisha na yale ya mwaka 1999, bei ya mauzo ya hisa husika ingepungua kwa kiasi kisichozidi US\$ 60 millioni.

Baada ya kufanyika uhakiki wa kina wa hesabu za *TTCL* za mwaka 2000, ilibainika kuwa *TTCL* ilipata hasara ya Tsh. 7,296 millioni tofauti na mwaka 1999 ilipopata faida ya Tshs. 5,521 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hili, baada ya majadiliano ya muda mrefu kati ya Serikali na ushirika wa *MSI* na *DETECON* na suala hili kufikishwa kwa Wanasheria na usuluhishi wa Kimataifa, muafaka ulifikiwa kwamba bei ya mauzo ya hisa asilimia 35 katika *TTCL* iwe US\$ 65 milioni na hivyo ushirika wa *MSI* na *DETECON* ulilipa jumla ya US\$ 65 milioni tu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijapata hasara wala faida ya moja kwa moja kutokana na Kampuni ya ubia ya *CELTEL* kuuzwa kwa *ZAIN* na kisha *AIRTEL*, bali kama mbia mwenza katika Kampuni hizo, Serikali imekuwa na itaendelea kupata gawio lake kila mwaka kutokana na faida zinazotokana na uendeshaji wa kampuni hizo.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni dhahiri Watanzania wamewasikia, Watanzania watawahukumu mali ya dola milioni 120 kama ulivyosema, kuuzwa kwa dola milioni 65 hatuna tatizo na hilo, nilikuwa na swali moja la nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yaliyotolewa na Waziri wakati akifunga majumuisho ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010, kwa mujibu wa *Hansard* ya tarehe 20 Julai, alisema maneno yafuatayo; kwa ruhusa yako naomba kunukuu kwamba: -

“Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *shares* ni kwamba, Kampuni ya *CELTEL* ilichukua asilimia 35 ya *share* kwenye *TTCL* na Serikali kubakia na asilimia 65; lakini hivi karibuni *CELTEL* imeonesha nia ya kujiondoa; hivyo kunahitaji kuwa na mashauriano na wale *shareholders* ambao kwa sasa ni *TTCL* yenyewe. Mkutano wamefanya tarehe 17 Julai, 2009 na kimsingi wamekubaliana kuachana ili kusudi *CELTEL* iondoke na zile *shares* asilimia 35 zirudi Serikalini kwa asilimia mia moja.” Mwisho wa kunukuu.

NAIBU SPIKA: Sasa swali!

MHE. SAIDI A. ARFI: Tarehe 17 Julai, 2009 ulifanywa mkutano huo; nini matokeo ya mkutano na hisa hizo mpaka hivi sasa mmefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na mazungumzo kati ya mwekezaji na

Serikali, kuweza kununua hisa asilimia 35 zilizokuwa zikimilikiwa na *ZAIN* wakati ule katika *TTCL*, lakini mwezi Aprili, 2010, *ZAIN* iliuza *share* zake kwa *AIRTEL*.

Mkutano mwingine uliitishwa mwezi Agosti kati ya *ZAIN*, *AIRTEL* na Serikali, kuzungumzia suala hili hili la namna gani makubaliano ambayo yamekaribia kufikiwa ya kuuza zile *share* asilimia 35 kwa Serikali yafanyike.

AIRTEL waliomba wapewe muda waweze kufanya tathmini kujua *share* hizi asilimia 35 zina *value* kiasi gani na kama wanaweza wakaziachia au wa-*invest* kwenye *TTCL* kwa kuzingatia kwamba, wana hizo *share* 35. *AIRTEL* inaendelea kufanya tathmini na hivi karibuni imetuhakikishia kwamba, itakamilisha ili tuweze kuendelea na majadiliano.

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho kwa leo, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa.

Na. 202

Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya TCRA

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Matumizi ya Simu za Mkononi yanaongezeka kwa kasi sana hapa nchini, lakini kuongezeka huko hakuendani na kukua kwa mapato ya Serikali kupitia kodi ya Sekta hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) ili kuruhusu Mamlaka ya Mapato (*TRA*) kuweka chombo kwenye mitambo ya *TCRA* cha kusajili matumizi ya simu hizo ili kukuza Pato la Taifa?

(b) Je, *TCRA* iko tayari kuyashauri Mampuni ya Simu za Mkononi kuchangia minara sehemu mbalimbali ili kupunguza gharama na hivyo kuongeza Pato la Serikali?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika kipindi cha miaka michache iliyopita, Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi kubwa sana na kuongeza matumizi ya simu za mikononi na kufikia kiasi cha laini za simu zilizosajiliwa zaidi ya milioni ishirini na moja kwa sasa. Makampuni ya simu hukusanya mapato kutoka kwa wateja wake na hulipa kodi mbalimbali kwa mujibu wa sheria za nchi na kuziwasilisha katika Mamlaka ya Mapato (*TRA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakikishwaji wa matumizi ya simu kwa mwezi ili kulipiwa kodi sahihi, hili ni jukumu la Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato (*TRA*). Kwa sasa hakuna mitambo iliyofungwa na *TCRA* ambayo *TRA* inaweza kuunganisha mitambo hiyo ili kujua matumizi halisi ya simu hizo na hivyo kutoza kodi. Hata hivyo, Serikali imeanza kufanya utafiti ili kupata chombo kitakachowezesha kufahamu matumizi halisi ya simu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*), imekua iyazishauri Mampuni Ya Simu pamoja na Mampuni mengine yanazotoa huduma za mawasiliano nchini, kuchangia miundombinu ya mawasiliano, ikiwemo minara katika sehemu mbalimbali nchini ili kupunguza gharama zao za uendeshaji. Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mampuni haya yanachangia miundombinu hususan minara, Sheria mpya ya Mawasiliano, yaani *Electronics and Postal Communications Act (EPOCA)* ya Mwaka 2010, imeainisha kifungu kinachoelekeza Mampuni ya Mawasiliano, namna yanavyoweza kuchangia miundombinu ikiwemo minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kutengeneza kanuni zitakazotumika katika kutekeleza Sheria hii mpya na moja ya kanuni hizo ni kanuni ya kuchangia miundombinu ya mawasiliano nchini, yaani (*Infrastructure Sharing Regulation*).

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake. Pamoja na hayo, nina mshangao kidogo:-

Kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka huu, bajeti nzima ni shilingi trilioni 13.5. Mapato ya ndani ni shilingi trilioni 6.7, ambayo imechangiwa na kodi shilingi trilioni 6.2 na maduhuli shilingi bilioni 540, lakini matumizi ya kawaada ni shilingi trilioni 8.6. Kwa hiyo, ingekuwa Serikali imefunga chombo hiki na kukusanya kodi halisi, ingekuwa imepunguza ukubwa huu wa tofauti. Vilevile kodi ya mshahara kwa mfanyakazi ni kubwa mno. Mishahara mingine inafikia hata asilimia 30. Serikali ingekusanya kodi hii, ingepunguza kodi hiyo. Sasa maswali yangu ni mawili:-

(i) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri analihakikishia Bunge hili kwamba ifikapo mwaka ujao wa bajeti mtambo huu wa kusajili matumizi ya simu utakuwa umefungwa?

(ii) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari nimpeleke kwa nchi jirani ambazo zimefunga mtambo huo na zinakusanya kodi kubwa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, anataka kujua kama itakapofika mwaka kesho tutakuwa tumefunga hiki chombo. Ieleweke kwamba, unapofanya mpango wa kufunga chombo ni lazima uzingatie vigezo mbalimbali katika sekta hiyo. Kwa sisi tunachokizingatia katika kuhakikisha kwamba, tunafunga chombo hiki; kwanza tunajiuliza chombo kitakapofungwa kita-*maintain* ubora wa huduma kama ilivyo au

kuongeza. Pili, kwa kufunga chombo hiki gharama zitapanda, zitapungua au zitabaki pale pale. Tuelewe kwamba, unapofunga chombo hiki kuna *interconnection charges* ambazo zipo; je, unafunga kwenye kila mtambo wa kila mtoa huduma ili upate hizo habari au unafunga chombo katikati ili *interconnection charges* ziondoke. Hivyo, hilo nalo lazima tulizingatie.

Vilevile tutakopofunga chombo hiki tunazingatia kama tutapata taarifa sahihi zinazohitajika kwa wadau wote, tuelewe kwamba si *TRA* peke yake wanaohitaji taarifa hizo; kuna Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilevile vingependa vipate taarifa hizo. Kwa hiyo, chombo kitakachofungwa lazima kitahakikisha kwamba wadau wote wataridhika na wateja wataendelea kupata huduma ikiwezekana kwa bei ile ile.

Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ninakubali endapo anapenda kunipeleka ila kama atalipia hiyo gharama ya kunipeleka kule, tutakwenda pamoja. Nimhakikishie kwamba, tayari tumeshaunda timu ya wataalamu ambayo watatembelea nchi mbalimbali, kuangalia ni muundo upi au ni *system* ipi tuweze kuitumia kuweza kutekeleza hili.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi ninaomba nikukaribishe vilevile nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swalilifuatalo la nyongeza:-

Makampuni ya Simu yameweka minara ya mawasiliiano karibu kila mahali nchini katika maeneo yaliyo chini ya mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa. Chini ya Sheria ya Fedha za Halmashauri za Mitaa, Halmashauri zina haki ya kutoza kodi ya mpaka asilimia 1.4 ninafikiri ya biashara zote zinazofanyika katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na biashara za haya Makampuni ya Simu.

Sasa swalilangu dogo la nyongeza; ni kwa nini Makampuni haya ya Simu za Mkononi hawalipi kodi hiyo kwa hizi Halmashauri za Mitaa kama inavyotakiwa na Sheria ya Fedha za Halmashauri za Mitaa? Ninashukuru.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tuelewe kwamba, haya Makampuni yamesajiliwa sehemu moja na minara imeenea nchi nzima. Sasa *host* ya *transaction* moja kama kila mnara utatozwa kwenye kila eneo lililopo sijui itakuwaje. Nimpe mfano mwingine; hivi kwa mfano mkandarasi aliyepata usajili wa Kampuni yake Kibaha, lakini anajenga barabara inayotoka Dar es Salaam kuja Dodoma; je, kila anapojenga mle anapofika kwenye kila Manispaa nako atozwe? Sasa tuliangalie kwa namna hii, ndiyo sababu ile sheria inasema kwamba, mahali ambapo Kampuni imesajiliwa ndipo itakapolipia. Sasa sina uhakika kama haya Makampuni ya Simu yamejisajili kila mahali ambapo yameweka mnara.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa majibu hayo. Imebakia Wizara moja ya Maji, maswali mawili hayakupata nafasi, tutayapangia wakati mwingine. Waheshimiwa Wabunge, tukifanya tathmini ya haraka kwa kipindi cha maswali cha leo kama majaribio, sikutaka kuwaingilia kumwambia kila mmoja kwamba, jibu kwa kifupi, uliza kwa kifupi na kadhalika; mtaona kwamba, tumemaliza *almost* na robo saa imezidi na bado maswali mawili hayakupata nafasi katika maswali kumi tu.

Sasa cha kujiuliza ni nini hapa? Cha kujiuliza ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sana tushirikiane na Ofisi ya Bunge na upande wa Serikali ili kipindi chetu hiki cha saa moja kiwe na maana kubwa zaidi kwetu sote na kwa Wananchi tukitumie vizuri kama inavyopasa, kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, maswali yetu ambayo tunatunga kuyapeleka Serikalini kwa ajili ya kupata majibu; baadhi yetu imekuwa maswali yale ni marefu sana na tukitakiwa na baadhi ya Wataalamu wetu Bungeni tuyafupishe tunakataa. Ningombwa tutoe ushirikiano mkubwa na kwa jinsi hiyo, nilifanya utundu kidogo hapa nikasema tuyapitie kidogo nikifanya swali moja, mawili, itakuwa kama nime-*single out* moja, mawili, tuyapitie tu kwa dakika chache sana.

Kwa mfano, ukichukua *Order Paper* ya leo, swali namba 195 lingelizwa hivi: Je, mchakato wa kurekebisha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani umefikia wapi? Swali hilo lingekuwa limepungua sentensi moja tu. Lile la pili, kama jibu ni hapana, likawa ni swali la nyongeza baada ya kusubiri Waziri amejibu nini. Siyo lazima liandikwe hapa. Swali 196 refu sana. Je, Serikali iko tayari kuhamisha Miradi ya Maendeleo ya Mwaka 2010/2011 ya Kata tano zilizokuwa Lindi Vijijini na kuhamishiwa Halmashauri ya Mji wa Lindi? Tayari. Lile la (b) likawa ni swali la nyongeza wakati wa kuzungumza. Kwa sababu kanuni yetu hapa unatakiwa uulize swali moja. Hivi kama umeambiwa uliza swali moja wewe unaweka (b), ile (b) itatokana na nini na uliambiwa uulize swali moja. Katika mazingira machache sana, unaweza ukawa na swali moja lenye (b). Katika mazingira ya kawaida, swali litakuwa ni swali tu haliwezi kuwa na (a) na (b). Swali Na. 197 ni refu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo la usafiri kwa Wakazi wa Vijiji vya Mwambao wa Ziwa Tanganyika? Ukisema hivyo katika swali lile utakuwa umebakiza kitu gani ambacho hakijawa-*covered*.

Swali Na. 198 ndiyo swali la mfano ambalo ninampongeza sana Mheshimiwa Luckson Mwanjale. Yeye ameuliza Kibunge kabisa, amesema; Suala la fidia kwa wananchi wa Ilungu na *Songwe International Airport* halijapata ufumbuzi mpaka sasa; je, ni lini Serikali itamaliza suala hilo? Hili ni swali moja kwa moja Serikalini, linampa nafasi ya Waziri *ku-focus* na kuweza kujibu moja kwa moja ni kitu gani kinatakiwa. Swali Na. 199 nikilifupisha; Je, Serikali ina mpango gani kwa matajiri wanaohodhi kwa miaka mingi mashambaporii Kibaha Mjini? Litakuwa limepungua nini swali lile. Swali Na. 200 refu kweli. Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha maeneo ya wazi (*Open Spaces*) yaliyoporwa mijini kwa matumizi ya umma? Itakuwa imepunguza nini?

Swali Na. 201; Je, salio la USD milioni 45 limeshalipwa kutokana na mauzo ya hisa za *TTCL* kwa Kampuni ya *MSI/DETECON*? Yale mengine yote yakawa ni

nyongeza hapa Waziri atakapojibu. Swali Na. 202; Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria ili kuruhusu *TRA* kuweka Chombo katika Mitambo ya *TCRA* cha kufuatilia matumizi ya simu? Swali Na. 203, bahati mbaya hatukuliuliza, kwa hiyo, sitalifupisha lakini nalo ni fupi sana. Swali Na. 204 ndiyo kabisa ni refu sana; maneno yote yale ni swali tu la kusema kwamba; Je, Serikali ina mpango gani kwa kuhakikisha maji yanafika kwenye Kata zote zinazounda Mji wa Kahama ambayo imo ndani ya lile lile swali ambalo ni refu sana.

Kwa hiyo, hilo ni moja ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge, kila mnapotunga swali jaribuni kujua unataka kuuliza nini na kulenga pale zaidi. Katika maswali yetu utakuta swali ni moja lakini lina maswali mawili, matatu, manne, ndani ya swali hilo hilo moja. Jambo hili ni kinyume na kanuni. Inatakiwa liwe swali siyo tunachomekea chomekea maswali, yaani humu humu katika swali ambalo tumeuliza sina muda tu, lakini ningechambua tungejikuta tuna maswali matatu, manne. Likija kwenye nyongeza vilevile nako kunakuwa na maswali mengine ambayo yanatoka nje ya pale na majibu upande wa Serikali vilevile nayo yanatakiwa kama swali lilivyosema, Mheshimiwa Waziri anapokuja moja kwa moja bila ya kupoteza muda naye akalenga pale pale kwenye majibu. Kwa hiyo, matokeo yake katika muda wa saa moja, Wabunge wengi tutaweza kuuliza maswali ya nyongeza na muda wetu utakuwa umetumika vizuri zaidi.

Mimi ninaamini kwa sababu Bunge letu bado ni jipy, kipindi hiki cha Bajeti hii, tutaendelea na utaratibu huu, lakini kuanzia Bunge la mwezi Oktoba, lazima tufupishe maswali. Ofisi yetu ya Bunge itashirikiana nanyi katika kuyafanya yawe mafupi, yanayoleweka, yasiyopoteza nia na lengo la swali la Mbunge ili kuyafanya majibu ya Serikali yawe *focused* ili muda wetu wa saa moja kusiwe na swali lolote ambalo halijaguswa na Waheshimiwa Wabunge, ambao wana nia ya kuuliza maswali ya nyongeza, wawzezwe kupata nafasi wengi kadiri iwezekanavyo, lakini wote tuwe *focused*. La kwanza.

La mwisho, katika eneo hili la maswali, tutaliangalia huko mbele, wenzetu wengine katika Mabunge haya ya *Commonwealth* wanakuwa na siku, kwa mfano, leo labda ni Wizara ya Elimu; kwa hiyo, maswali ya elimu tuliyoyapata tunaya-*cluster*, tunayaauliza siku moja. Kesho ni Wizara nyingine. Tutaangalia tuone jinsi gani bora zaidi, je mwenendo tulionao ni sawa sawa, imefika mahali tuangalie maana hii ya moja moja hapa, moja pale, mwisho wa siku unaweza usipate picha ya nini hasa *way forward*, lakini hilo tutaliampanga Wabunge wenye.

Waheshimiwa Wabunge, bila kupoteza muda, matangazo: Mheshimiwa Amos Makalla, Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, kesho tarehe 9 Julai, 2011 kutakuwa na mechili ya mpira wa miguu pamoja na mpira wa pete, kati ya Timu ya Waheshimiwa Wabunge na Timu ya *Global Publishers*, wachapishaji wa magazeti. Mechili hizo zitachezwa katika Uwanja wa Jamhuri, Mjini Dodoma, kuanzia saa tisa na nusu alasiri. Aidha, Kamati ya Ufundsi imekwishafanya vitu vyake; hivyo, Waheshimiwa Wabunge, wategemee ushindi mnono na Wabunge wote wanapaswa kufika uwanjani na kuishangilia timu yao. Tangazo

hilo linatoka kwa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* na nimehakikishiwa na Mwenyekiti wa Ufundu wa Timu hii, Profesa Maji Marefu kwamba, mambo ni mazuri. (*Kicheko*)

Tangazo kutoka kwa Afisa Habari wa Bunge, hili nitalifanya liwe la mwisho. Mkurugenzi wa TOT, Mheshimiwa Capt. John Komba, lisikilizeni vizuri tangazo hii na hasa wale wa upande wangu wa kushoto; anaomba niwatangazie Wabunge wote, kuanzia saa tatu usiku, katika Ukumbi wa Kilimani, kutakuwa na burudani ya taarab itakayotolewa na kikundi cha TOT kikiongozwa na Gwiji wake Malkia Hadija Kopa. Wote mnakaribishwa hasa wale wa kushoto wakiongozwa na Kiongozi Mkuu wa Upinzani Bungeni. (*Kicheko*)

Tangazo la Semina; ninaomba niwatangazie Wabunge kwamba, Siku ya Jumapili, tarehe 10 Julai, 2011 kutakuwa na Semina juu ya shughuli na majukumu ya Bohari Kuu ya Taifa ya Madawa (*MSD*), itakayoanza saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa na itahusisha Kamati zifuatazo: Kamati ya Huduma za Jamii, Hesabu za Mashirika ya Umma na Masuala ya UKIMWI. Wajumbe wote wa Kamati hizi, wanaombwa kuhudhuria. Sijui kwa nini wameamua kubagua, *MSD* walipaswa wakutane na Wabunge wote, kwa sababu Wabunge wana malalamiko mengi sana na *MSD* na hata mimi nimempelekeea nyingine Mheshimiwa Waziri wa Afya na tunapopata fursa ya kukutana nao, ingekuwa bora sana ili watujibu moja kwa moja kwa nini yanatokea ambayo yanapaswa kutokea.

Umoja wa Wabunge Wanawake wa Bunge letu (*TWPG*), unapenda kuwaarifu Wabunge Wanawake wote kuwa, kesho Siku ya Jumamosi, tarehe 9 Julai, 2011, kutakuwa na Semina ya *Gender Budgeting*, itakayofanyika katika Ukumbi wa Msekwa. Nao tuwashauri tu hawa, mkitaka kufanikiwa katika *gender budgeting* ni vizuri mkahusisha Wabunge wote.

Kaimu *DAP*, Ofisi ya Bunge, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, leo tarehe 8 Julai, 2011 jioni, kutakuwa na tafrija ya Wabunge kwenye Viwanja vya Bunge, baada ya kuahirishwa Bunge. Tafrija hii imedhaminiwa na Kampuni ya *Zantel*, itakuwa na vionjo mbalimbali vya burudani ikiwemo Bendi ya Muziki ya Extra Bongo na Mwimbaji wake Maarufu Ali Choki; nyote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa kwamba, Wabunge wote mnakaribishwa kwenye shughuli itakayokuwa pale Kilimani ya *AKUDO Impact*, leo tarehe 8 Julai, 2011, pamoja na mambo mengine kuipongeza Timu ya Simba kuingia fainali. Aliyetangulia katangulia na wengine wanakuja. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Simba Oyee!!!

NAIBU SPIKA: Tangazo la mwisho, wageni walioko Bungeni: Kwanza ni wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (*Mazingira*), Mheshimiwa Dkt. Terezya Huvisa, ambao ni Anna-Maria Pius Luoga, mama yake mzazi; Anasigali

Mapunda, Mjomba; na Ndugu Godfrey Mosha, Mwenyekiti Mtendaji *Mufindi Environmental Trust*. Karibuni sana.

Pili, wanafunzi 20 wa *Tambaza High School*, Ilala, Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwalimu Sostenes Ngowi; karibuni sana watoto wetu wa Tambaza. Ninatumaini jina la shule yenu linazidi kuwa zuri, ninawapongezeni sana maana zamani lilikuwa na shida kidogo.

Tatu, wanafunzi 73 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi Lugalo, Dar es Salaam; ahsanteni sana na karibuni sana wanafunzi wote pamoja na Walimu mlifuatana nao.

Mwisho si kwa umuhimu, Waremo 20 wa *Tanzania Vodacom Higher Learning Zone*, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Ahsanteni; karibuni sana. Baada ya matangazo hayo yote Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Majadiliano yanaendelea na ninaomba mahudhurio yawe mazuri mpaka jioni ili tuweze kulifanya haki suala hili linaloendelea hivi sasa. Mchangiaji wetu wa kwanza asubuhi hii ni Mheshimiwa Halima Mdee; karibu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Muungano pamoja na Mazingira. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambapo Wizara inayoshughulika na masuala ya Muungano ipo chini yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri pia ni mara yangu ya kwanza tokea nimekuwa Mbunge, hii ikiwa ni *term* yangu ya pili kuchangia Wizara yetu ya Muungano. Nimeona nichangie nikiwa Mwanakamati ili nipate majibu kwa kiasi gani Serikali yetu iko *serious* katika kutatua masuala ya Muungano. Ninaliuliza hili kwa sababu kiutamaduni imekuwa ikizoelekeea na Bunge hili ninaona litakuwa limeweka *precedent* mpya kwa Wabara wengi kuchangia hii Wizara yetu. Kwa hiyo, inaonekana kwamba, Wabara wameanza kuujua Muungano na wameanza kuona kwamba wana jukumu la kuisimamia Serikali kuweza kutekeleza wajibu wake katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mjumbe wa Kamati, tunaona ni kwa kiasi gani hii Wizara iliyokuwa chini ya Makamu wa Rais inavyopuuuzwa. Kwanza, kwa idadi ya wafanyakazi. Waziri anatuambia wanahitaji wafanyakazi 22, lakini wana wafanyakazi tisa tu. Kupuuuzwa huku kwa Wizara hii ambayo kimsingi inasaidia kuboresha mahusiano katika ya Zanzibar na Tanzania Bara, inathibitishwa hata katika ule mchakato

wetu wa Katiba. Wenzetu tunaona wanalamika lakini wana hoja. Moja kati ya sababu za Muswada kurudi ni kwa kuwa Serikali ya Zanzibar haikuhusishwa. Walipuuzwa kama hawapo, haikuhusishwa ndiyo maana umerudi. Sasa hivi tunasikia sijui utakuja na mabadiliko gani. Kuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia kero zote kumi na tatu, katika kero hizi ambazo zimetatuliwa na kuingia maridhiano ni mbili. Hizi nne zimefikiwa mwafaka lakini bado Mawaziri hawajakaa kupeana hati ya makubaliano. Utakuta kwenye hizi kero 13 za msingi, ambazo zinagusa maslahi ya Wazanzibari, hazijatafutiwa ufumbuzi. Mimi ninazo kero saba hapa. Ukiangalia zilizotafutiwa maridhiano ni haki za binadamu na uwezo wa Zanzibar kujunga na Taasisi za Kimataifa za Masuala ya Uvuvi, ukija masuala ya Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hakuna kitu, ukija masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia hakuna kitu. Hata *status* yake sasa hivi hatujui. Sisi tumekaa na madini yetu huku hawatuulizi, tukisikia mafuta yao mbio mbio. Lazima tutafute suluhu kuепusha kero zisizo na msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uvuvi kwenye Ukanda wa Bahari Kuu, halijatafutiwa ufumbuzi. Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za nje, Mgawanyo wa mapato na faida ya Benki Kuu, masuala yanayohusiana na uchumi kwa wenzetu Wazanzibari, yenye umuhimu wa kubadilisha mustakabili wao kwa nini hatuyatatu? Tatizo liko wapi? Mimi ninakuomba Mheshimiwa Waziri, ninajua wewe ni mmoja wa wadau na wakereketwa wa masuala ya Muungano, umepewa jukumu hilo ili hizi kero ziishe! Mambo ya kuwekeana vikwazo kwenye Katiba, eti masuala sijui ya Muungano yasijadiliwe; hakuna kuweka vikwazo, acheni watu wajadili; waseme kama wanataka Muungano ama la au wanataka Muungano wa mfumo gani? Hii ndiyo inajazisha nyama hoja ya kwamba, huu Muungano ulifanywa kiujanja ujanja kwa ajili ya watu kulinda maslahi yao. Ndiyo hoja zinakuja hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao vya wenzetu wanaoshughulika na masuala ya Muungano; tunaambiwa kwamba, Kamati hazikai mpaka wakiona Wabunge wanataka kukutana kwenye Kamati za Bunge. Kumekuwa na malalamiko dhahiri kwamba, inakuwa ni ngumu kwa Wizara kuratibu hawa Viongozi wa juu watatu. Lazima tuyaseme haya, tusiposema kama Wanakamati, hatumsaidii Waziri na hatuusaidii Muungano wetu. Huku Waziri Mkuu ana ratiba yake, huku Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, ana ratiba yake na Makamu wa Pili wa Rais na yeze ana ratiba yake; mambo hayaeleweki. Sasa ikibidi huu mfumo ama huu utaratibu wao wa kukutana, tuuveke kisheria ili kuwalazimisha wakutane. Hili suala tukisema funika kombe mwanaharamu apite, tunaweza tukajikuta kero ndogo ndogo ambazo zingweza zikatatuliwa, zinashindwa kutatuliwa na vuguvugu za ugomvi zinatokea bila sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, achukue Urais kwa Awamu ya Kwanza mwaka 2005 na sasa hivi Awamu ya Pili, vimefanyika vikao sita tu kwa miaka saba. Hivi kweli tuko *serious*? Tuna dhamira kweli ya kutatua masuala ya Muungano? Tumeambiwa Tume ya Pamoja ya Fedha iliundwa kwa madhumuni ya kuangalia ni kwa namna gani tutagawana mapato baina ya Bara na Visiwani. Imetoa Ripoti sijui tokea 2008 sasa hivi 2011, hakuna kinachoeleweka. Mimi

nitaomba Mheshimiwa Waziri mtupe taarifa sahihi. Mtuambie kwamba, haya masuala ya Muungano na kero hizi zake ambazo hazina mashiko tuna dhamira ya kuzimaliza, *tumove* pamoja kama nchi. Kila siku ikiwa kwenye Wizara ya Muungano ni malalamiko yale yale. Kuna malalamiko kwamba wenzetu Wazanzibar wanapuuzwa linapokuja suala la safari za nje. Zanzibar ni nchi; sawa tunalijua hilo halina ubishi; si ziliungana nchi mbili! Sasa kama Tanganyika tulimezwa imekula kwetu, lakini Zanzibar ni nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema vikao vya nje hakuna taarifa za mapema ili na wao waweze kijiandaa, mtu anaibuka kama mzigo hizi ni kero lazima mtuambie. Vitu vidogo vya kupeana taarifa, mkienda nje mnasimama kama nchi. Taarifa hazitolewi. Kwa hiyo, tunaomba hivi vitu tupewe maelezo ya kina. Tulishamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, Bajeti ijayo mkija na *stories* hizi za kero za Muungano, Bajeti yenu hatutaitisha kwenye Kamati tumechoka. Tunataka haya mambo tuyamalize, kuonekane kuna dhamira ya kweli ya kufanya kazi. Waziri anatuambia *TRA* wameshakubaliana kuhusiana na kodi mbili kwamba, wafanyabiashara wa Zanzibar wasitozwe kodi mara mbili. Ukija kwenye uhalisia hilo suala halipo. Sasa inakuwaje mnakubaliana na kuwekeana maandiko, lakini linapokuja kwenye utekelezaji haionekani; tatizo liko wapi? Tatizo ni *TRA* ama ni ninyi wenyewe mnafanya mambo ambayo yako kinyume na Sheria na Taratibu za nchi.

Ninakuja kwenye suala la mazingira na hapa nitazungumzia zaidi Jimboni kwangu. Kwanza, sijui Wizara inafanya shughuli gani; kwa sababu huko tunakotoka matatizo ya mazingira ni makubwa mno? Mimi nimetoka Jimbo la Kawe, ambako ndiyo mnakaa lakini tatizo la mazingira lipo na ninyi wakubwa hamlion! Sasa nina-*imagine* huko vijijini hali ikoje. Jimboni kwangu asubuhi liliulizwa swali la *open spaces*; maeneo ya wazi yameuzwa, maeneo yaliyokuwa yanatakiwa yapitishe mikondo ya maji kwenda baharini yameuzwa, yamejengwa maghorofa, matokeo yake mvua ikinyesha, ninajua mnapita sana pale Mikocheni kwa Warioba; mvua ikinyesha pale hapatoshi. Hii ni kwa sababu kuna mjanja mmoja ana hela kajenga Shopaz pale, kuna mtu mwengine amejenga ile Makam wanazuia mkondo wa maji. (*Makofi*)

Wananchi wangu wa Bonde la Mpunga, mvua ikinyesha maji yanajaa kwenye maeneo yao na kusababisha mafuriko. Kwa hiyo, kule kwangu Wananchi maskini ikifika mvua maana yake ni kwamba; ni mafuriko mpaka mwisho. Wizara ya Mazingira inatuambia nini kuhusiana na hili? Ukienda kwenye mito karibia yote ya Jimbo la Kawe, watu wanachimba mchanga. Pia kuna eneo pale taarifa ya Mheshimiwa Lukuvi alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Kiwanja Namba 856, Msasani Beach, kulitolewa taarifa kwamba, lilikuwa ni eneo kwa ajili ya mkondo wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuja mtu na pesa zake, ameomba matumizi ya ardhi yabadilishwe; kuna mtu yupo Wizara ya Ardhi sijui kwa hongo, sijui kwa matamano yake, akabadilisha matumizi ya ardhi, leo hii pale mvua ikinyesha panatisha. Mimi ningeomba nipate taarifa kutoka kwa Waziri wa Mazingira, kwa sababu

ninaambiwa majamaa wa *NEMC* wanakwenda kule ndani wakirudi nje ni wapole; sasa sijui wanapewa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nipaye taarifa isije ikawa watu wanaingia kule wanashikishwa kidogo halafu wanapotea wanakauka, mtuambie mustakabali wa ile barabara yetu ambayo kila mvua ikinyesha kunakuwa na mafuriko. Tuambieni mustakabali wa wakazi wa bonde la mpunga, Wananchi maskini ambao kutohuna na kuzibwa mikondo ya maji, mvua ikinyesha wanapata mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kibaya zaidi, hivi karibuni Kawe Darajani kaibuka Bwana anaitwa Robert Mugisha, amejenga ndani ya mto. *NEMC* wamekwenda, imeundwa Tume ambayo inajumuisha watu wa ofisi yenu, wamekwenda wametoa mapendekezo yenu, Wizara ya Ardhi wamekwenda wametoa mapendekezo yao, kwamba huyu mtu anatakiwa azuiliwe, imetolewa *stop order*, lakini jamaa anaendelea kujenga; na tunaambiwa kuna mtu anayemlinda, Kigogo Wizara ya Ardhi, sitaki kutaja majina hapa. Mimi ninaomba Waziri wa Mazingira, ufuatilie hili suala ambalo mmetumia fedha nydingi kuunda Tume ili kuokoa mito na vyanzo vya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kigogo anahusika, imethibitika *documents* ni feki, imedhahirika kabisa hana hati zilizo na uhalali, lakini kwa kiburi anaendelea kujenga. Ninaomba Waziri wa Mazingira, tekelezeni wajibu wenu, tusiwe Mawaziri kwa Vyeo, tusiwe Mawaziri kwa ujiko, tutekeleze wajibu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda vikubwa vinajengwa kwenye makazi ya watu na wanamwaga maji machafu sana kule Mikocheni, ninaomba mliangalie suala hili. Wananchi wangu wanaumwa na kupata maradhi ambayo hayaeleweki, viwanda ukivicheki kwa nyuma ndiyo wale wakubwa ama marafiki zao, tunaomba hivi viwanda ama visimamishe au vitengeneze mfumo ambao maji machafu yanayotoka viwandani yataweza kwenda kumwagika baharini pasipo kuwadhuru wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NEMC* walikwenda wakatoa maagizo hakuna kilichofanyika, sasa kama *NEMC* kuna rushwa tujue. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, muda wako umekwisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ahsante sana.

TAARIFA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kutoa taarifa kwa Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza hivi sasa kwamba, kwa mujibu wa Sheria yetu ya Mazingira, siyo ruhusa kwa viwanda na makampuni yoyote kumwaga uchafu baharini. Kwa hiyo, kinachotakiwa haya makampuni na

viwanda, yaweke utaratibu wa kuhakikisha huo uchafu unadhibitiwa bila kuchafua mazingira. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana; na mimi ni mwanamazingira, ninakubaliana kabisa na wewe katika hilo.

Mheshimiwa Faustine Ndugulile ni mchangiaji anayefuata.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchagia katika Hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Mengi yamesemwa kuhusiana na suala hili la Muungano, lakini ninadhani ni jambo jema kadiri muda unavyokwenda na sisi tuweze kufanya tafakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wetu wa zama za enzi za mawe, walikuwa wanatumia zana za mawe lakini na wao waliweza kufanya tafakari ya jinsi gani wanawenza wakaboresha maisha yao ili maisha yao yaweze kwenda vizuri. Vilevile wazee wetu ambao walipigania uhuru wa nchi hii wangeweza kuridhika kula, kulala na kuvala katika mazingira ya ukoloni, lakini nao waliweza kutafakari na kuona kwamba, maisha yao yanaweza yakawa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kusema kwamba, kuhoji siyo dhambi na kufanya tafakari siyo dhambi, kwa sababu tangu Muungano wetu mwaka 1964, tunafikia karibu miaka hamsini sasa. Ili kuboresha zaidi Muungano wetu, tunahitaji tukae na tuuangalie upya jinsi gani tunaweza tukaondoa hizi kero. Kero ni nyingi kama zilivyoainishwa na baadhi ya wasemaji waliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Katiba ya Zanzibar, ambayo imeandikwa mwaka 2010, imeainisha baadhi ya maeneo ambayo yanahitajiwa sasa yaoanishwe na Katiba mpya ambayo tutaiandika. Tulipoungana mwaka 1964, tulisema kwamba, tunaungana kutengeneza nchi moja, lakini Katiba Mpya ya Zanzibar, imemtaja Rais wa Zanzibar kama Mkuu wa nchi, imetaja mamlaka ambayo Rais wa Zanzibar atakuwa nayo pamoja na kugawa mikoa. Vilevile imetaja kwamba, Mahakama ya Rufaa haitakuwa na maamuzi katika suala la Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna changamoto nyingine ambazo zipo; mfano ni hizi ambazo tumezungelea; mgawanyo wa mapato na rasilimali, mfumo wa kodi, umiliki wa mali na uwakilishi katika vyombo mbalimbali vyatolye. Sasa tunakaribia miaka hamsini, lengo letu ni kuboresha na kuuimarisha huu Muungano wetu. Kwa hiyo, ninatoa ushauri kwamba, wakati tunaendelea na huu mchakato wa kujadili Katiba Mpya, ninadhani ni wakati mwafaka tukatumia fursa hii kujaribu kukaa na kuangalia huu muundo wa Muungano uwe wa namna gani na aina ya Muungano ambao tunataka tuwe nao. Hii itatusaidia sana sisi ili tutakapokuwa tumefanya maamuzi kwa kuwashirikisha na Wananchi wetu, basi muundo na aina ya Muungano utakaokuwepo, uweze kuwa na tija kwa pande zote mbili, tuuangalie kwamba kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiusalama muundo wetu wa Muungano uwe namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kugusia kidogo katika masuala ya Mazingira. Waziri husika ameleezea vizuri sana katika hotuba yake ya nini Wizara yake imekuwa inafanya, lakini kuna programu nyingi sana ambazo amezigusia katika kitabu chake cha hotuba. Tatizo langu ambalo ninaliona siyo wingi wa programu ambazo zipo zimeainishwa au ubora wa zile nyaraka, tatizo letu lipo zaidi katika utekelezaji.

Bado tuna tafsiri mbovu au potofu ya nini maana ya utunzaji wa mazingira, watu wengi tunafikiria kwamba, utunzaji wa mazingira ni pale tu inapohusisha upandaji wa miti na hii inajionesha wazi hata katika zile Sherehe za Kitaifa, ambazo tumekuwa tunazifanya mara nyingi tunaishia kupanda miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo yanaendelea hivi sasa katika nchi yetu ambayo kwa kweli yanatishia mustakabali wa nchi yetu. Miti bado inaendelea kukatwa ovyo, biashara ya mkaa ambayo miaka ya nyuma tulisema kwamba, tutaidhibiti bado inaendelea kwa kasi, tumekuwa tunaongelea masuala ya mabadiliko ya tabianchi na haya yameshaanza kujidhihirisha taratibu. Sasa hivi tunaongelea kwamba kina cha Ziwa Tanganyika kinazidi kupungua, theluji juu ya Mlima Kilimanjaro inapungua, misimu ya mvua sasa hivi nayo imeanza kubadilika na inawezekana kabisa hili baa la njaa ambalo linatunyemelea, pamoja na mgawo wa umeme nao unaweza ukawa unachangiwa na haya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumekuwa na uingizaji mkubwa sana wa vifaa chakavu kutoka nje ya nchi. Sasa hivi ukipita hata hapa Dodoma, Dar es Salaam na mikoa mingine mikubwa, kuna majokofu mengi sana ambayo mengi hayapo *CFC free*, pamoja na kompyuta na zana zingine za *electronics*. Inafaa sasa tukaanza kuviangalia vifaa hivi na ikiwezekana, sheria kali ziweze kutungwa za kudhibiti uingizaji wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka kuliongelea ni kwamba, katika Pwani zetu sasa hivi uvuvi haramu unashika kasi kubwa sana. Kule Kigamboni, kuanzia Kigamboni, Mjimwema, Somangila, Kimbiji mpaka Pemba Mnazi, kila siku tunasikia milio ya mabomu, tukiacha hili likaendelea, uvuvi haramu utapunguza sana mazalia ya samaki na kutafanya sasa wavuvi wetu amba walikuwa wanawenza kupata samaki katika maeneo ya karibu, waende mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Wizara husika nao waweze kuliangalia suala la uvuvi haramu na ikiwezekana waweze kuboresha vitengo ambavyo vinasimamia suala hili ili viweze kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, baadhi ya viwanda na migodi inachafua mazingira na vyanzo vya maji. Mengi yamesemwa lakini ninaomba nami nigosie jambo langu moja katika eneo langu la Kigamboni.

Katika eneo la Vijibweni, kuna eneo linaitwa Kidongoni, kuna kiwanda cha gesi kinaitwa Mihan; kiwanda hiki kimejengwa katika maeneo ya makazi ya watu, kinatoa

harufu kali na mara kwa mara hata mimi juzi nimepita pale mitungi ya gesi ilikuwa inalipuka na Wananchi hawa wametoa taarifa katika sehemu zote zinazohusika, wamekuja Wizara ya Mazingira, wamekwenda Manispaa, wamekwenda *NEMC*, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Wananchi hawa wanaishi kwa wasiwasi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri wa Mazingira, apate fursa aende akajionee hali halisi ambayo Wananchi wa Kidongoni Vijibweni wanakabiliana nayo na hali ya mashaka iliyopo katika kile kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbagala pia kuna kiwanda cha *KTM* na kiwanda cha simenti. Kwa taafira ambazo zipo, inasemekana kwamba, hata hati ya *Environmental Impact Assessment* hususan katika hiki kiwanda cha simenti ni ya mashaka. Vilevile mfumo wa maji taka kutoka katika viwanda hivi viwili imemelekezwa katika makazi ya watu. Ninaomba Waziri tutakapokuwa tunafanya ziara, basi tuweze kupita na kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ninataka kuligusia ni hili la mifuko ya plastiki. Serikali imesema kwamba, mifuko ya plastiki ambayo inapaswa kutumika nchini ni ile ambayo ina unene usiozidi *micron* 30. Sasa hii lugha ni ya kitaalamu sana kwa sababu hata mimi Mbunge ukiniuliza mifuko wenyewe unene wa *micron* 30 siujui na wala siufahamu, nina uhakika kabisa hata Wananchi wa kawaida kule mtaani nao pia hawalielewi vizuri suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti hali hii kwa nini Serikali isitoe tamko kwamba tunafuta matumizi ya mifuko ya plastiki na badala yake tukaweza mifuko ya karatasi ili tuondokane kabisa na dhana hii kwani mifuko hii kwa kiasi kikubwa sana inachafua sana mazingira katika maeneo yetu. Katika Hotuba ya Waziri amegusia kwamba, katika usimamizi wao wameweza kutembelea Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, na Mbeya; hii haitoshi, bado elimu inahitajika kwa Wananchi na bado usimamizi unahitajika kuboreshwa na ikiwezekana tuifute kabisa mifuko hii ili tuweze kutumia mifuko ya karatasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaomba nitoe rai kwa Serikali, majukumu ya Wizara ya Mazingira ni makubwa na ya msingi kwa mustakabali wa nchi yetu, lakini nyenzo zilizopo hazitoshi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuboresha na kuongezea bajeti ya Wizara hii na kuwajengea uwezo Halmashauri ili ziweze kusimamia vyema Sheria ya Mazingira na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, ninashukuru sana. (*Makofii*)

MHE. MOHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa na kunijalia kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa mchango wangu kuhusu Hotuba ya Waziri wa Nchi (Muungano na Mazingira). Pia ninakushukuru wewe, kwa kunipa nafasi hii nami nitoe mchango wangu kidogo kuhusu masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaipongeza Hotuba ya Waziri, lakini pia ninawapongeza wataalam walioshirikiana naye katika kutayarisha Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kuchangia katika suala la Muungano. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mimi ni mmoja kati ya Watanzania wachache, ambao wapo sasa hivi wanaoukumbuka Muungano ulivyoanza mwaka 1964. Mimi nilizaliwa Zanzibar wakati wa Ufalme wa Raiyat u Sultani, kwa hiyo, mwaka 1964 wakati wa Muungano, nilikuwa tayari ni kijana, niliyaona Mapinduzi ya mwaka 1964. Sikusikia, nina bahati hiyo kwamba, niliyaona kwa macho yangu. Yalikuwa pale Zanzibar Mjini na mimi nilikuwa Mjini, nilitoka kwetu Makunduchi siku ya tarehe 12 Januari, nilikuwa Zanzibar. Kwa hiyo, ninayafahamu Mapinduzi nimeyaona. Mapinduzi yale ndiyo yaliyoleta Muungano. Sitathubutu na wala sitamshawishi mtu hata siku moja, kuudharau Muungano huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa ushauri tu, kwa vijana waliozaliwa Tanzania, ambao wapo sasa hivi wasiubeze Muungano. Ninaamini humu ndani ya Bunge tupo wachache sana waliozaliwa Tanganyika, wengi wamezaliwa wakati wa Tanzania na wachache sana waliozaliwa Zanzibar wakati wa Raiyat u Sultan, lakini wengi wamezaliwa Tanzania Zanzibar. Muungano ni kitu muhimu kuliko jambo lingine lolote katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati mwafaka wa kuujadili kwa sababu miaka karibu 47 ya Muungano ni muda mrefu, wengi wa Watanzania waliopo hivi sasa hawajui kilichokuwepo hapo kabla. Kwa hiyo, kuna haja ya sisi tulikuwepo kuwaelimisha kwamba, kulikuwa na nini na ndiyo maana ikawa hivi. Ile sababu ya kusema kwamba, kuna watu au kuna viongozi walifanya kwa maslahi yao tu, hiyo siyo sababu; kulikuwa na mambo muhimu sana yaliyofanya nchi hii kuungana, mengi na ya muhimu sana. Pia ni muhimu kabisa kuweza kuimarissha Muungano wetu kwa hali yoyote.

Matatizo yaliyopo, mnapokaa watu wawili pamoja mmeungana au mnashirikana kitu, ikiwa kuna *hewallah hewallah* tu, basi ujue kuna mmoja anamdhulumu mwenzake; lakini akitokea mwingine akiuliza mbona hivi basi mtakwenda sawa.

Kwa hiyo, wanapotoa hoja Watanzania Zanzibar au Watanzania Bara kuuliza mbona hivi, ni wajibu wao na nia yetu naamini ni kuimarissha Muungano. Kwa hiyo, tukae, na sasa hivi ni wakati muafaka wa kuweza kujadiliana hilo kwa sababu kuna mpango wa Katiba Mpya ili tuweze kuimarissha Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kuliko yote, isitokee hata siku moja kudharau ukubwa na udogo. Zanzibar ilikuwa ni nchi yenye miliki kamili katika Kiti cha Umoja wa Mataifa na ika-sacrifices kuungana na ndugu zao wa Tanganyika tukafanya nchi moja. Kwa hiyo, lile suala la kubezana au kudharauliana kwamba nchi ni ndogo, watu wake ni kidogo, hilo litoke katika matamshi yetu, mwelekeo wa mtu ye yole yule ambaye ni Mtanzania anayoitakia mema nchi hii ndiyo tutakuwa tumemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero zipo, ni wajibu wetu sisi kuzikabili na kuweza kuzitataua na kuendeleza kwamba kila siku tumeshakaa, tumeshajadili, vikao vimekaa, hakuna lililokuwa halijasawazika. Hiyo siyo suluhu, tufike mahali tuseme hili limekwisha ndio tutaweza kuimarisha Muungano. Kuna matatizo ya msingi kabisa, kama mnavyofahamu kwamba Zanzibar ni kama visiwa ambavyo uchumi wake mkubwa sana unategemea mambo ya biashara na soko la Zanzibar, lote liko Tanzania Bara. Sasa unapowekea vikwazo Zanzibar isifanye biashara zake kwa kutumia soko la huku maana yake ni kwamba unaikatisha kabisa ustawi na uchumi wa visiwa vile. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunawaomba ndugu zetu wale wenye majukumu waliopewa mamlaka hasa *TRA* watimize wajibu wao kwa mujibu wa taratibu na sheria hakuna kukomoana. Mnapofikia mahali pa kukomoana, ninyi ndiyo mtasababisha Muungano huu kuvunjika. Kwanza mlilue hilo. Kama kuna sehemu ambayo itasababisha Muungano huu kuharibika au kuvunjika, basi ni Idara ya *TRA*. Hiyo itakuwa chanzo kikubwa sana, kwa sababu ndiyo njia kuu peke yake ya Wazanzibar kupita kuja kufanya biashara huku. Wakiwekewa vikwazo pale na wakija wakisema sasa potolea mbali, basi ni potelea mbali na hawachelewi hawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbuka siku waliyosema potelea mbali tumechoka sisi kutawaliwa na Sultan, basi tutumie rungu, shoka, panga na nchi ikakamilika. Wanayo desturi hiyo. Twendeni vizuri ili tuweze kustawisha Muungano wetu. Mimi najua *policy* ya nchi ni kuimarisha Muungano, lakini maafisa wahusika wale waliopewa dhamana ya kuweza kufuatilia mambo yale wanakuwa na maslahi yao binafsi, kwa sababu ni maslahi yao binafsi tu hawatazami nchi kwanza, wakatazama na ule mustakabali wa maendeleo ya watu unakwenda vipi kwanza. Hawafahamu hicho!

Kwa hiyo, tunaomba sana msisababishe suala letu zuri likawa baya kwa jinsi ya ubinafsi tu, kwa sababu wengi sana ni ubinafsi tu. Nalizungumza hilo kwa sababu mkisikia hizo kero nyangi sana zinakuja kwenye maslahi ya biashara au maslahi ya wafanyabiashara wanatoka Zanzibar kuja kufanya biashara zao hasa wanapopita aidha bandarini, *airport* na kwingineko, tusaidiane na siyo kusaidiana tu bali tutekeleze kwa sababu ni suala la msaada, ni suala la sheria na utaratibu. Tufanye vile ambavyo tunakubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikupenda leo kusema sana kwa sababu nilishazungumza sana huko nyuma. Cha msingi zaidi ni kwamba tuimarishe Muungano kwa sababu Muungano ni kitu muhimu sana na vijana wetu waliopo hapa sasa hivi Tanzania wana umuhimu wa kuelimishwa. Lakini ni wakati mzuri sana wa kuweza kujadili suala hili la Muungano wakati huu wa Katiba Mpya tunapoitegemea. Tuondoe tofauti zetu na tushirikiane kwa kila hatua. Mliona yaliyotokea Zanzibar ulipopelekwa Muswada tu, Tume ya Kuratibu Taratibu za Muungano, watu walivyokuja kwa sababu tu ya kutoshirikishwa mapema. Suala hili ni muhimu sana, tusidharauliane, tuheshimiane. Viongozi wetu waliheshimiana huko nyuma wakaimarisha Muungano. Kwa sisi tuliokuwepo hapa tuliorithi, basi tuendelee na heshima ile ile. Kila mmoja ana haki sawa sawa katika Muungano huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Napenda kuchangia kwa upande wa Wizara ya Mazingira na nitajielekeza zaidi kwenye Mgodi wa *North Mara*. Kuna shule ambayo ipo karibu na shughuli zinazofanyika za Mgodi wa *North Mara* inaitwa Nyabigena. Ile shule inaathirika kwa namna tatu. Kwa namna ya *noise pollution*, kwa maana ya uchafuzi kwa njia ya kelele kwa sababu wakati wakiendelea na shughuli zao za migodi wanapofanya *blusting* ya miamba inakuwa inawa-*disturb* wanafunzi kwenye madarasa yao. (*Makofi*)

Ningependa Waziri wa Mazingira atueleze labda amefika kwenye hiyo shule na akaona. Kwa sababu nina taarifa kwamba alitembelea kwenye Mgodi wa Nyamongo kati ya tarehe 13, 14 Mei, 2011. Je, alifika na akaona uchafuzi wa ile Shule ya Msingi ya Nyabigena? Pili, pia wakati wanafanya *blustering* inasababisha nyufa ya Shule ya Msingi, ukienda sasa hivi kuna nyufa nyingi sana kwenye hiyo Shule ya Msingi ya Nyabigena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, *dust pollution* ambayo pia ni kitu kibaya sana kwa afya. Kuna kipindi wanapofanya zile shughuli inawabidi *at a time* hata walimu wanafunga shule, maana inawabidi wawaruhusu wanafunzi waende nyumbani. Sasa tunajiuliza, hawa wanafunzi wanaosoma kwenye Shule ya Msingi ya Nyabigena, watapata elimu stahiki? Je, hawatapata madhara ya *brain*? Kwa hiyo, ningependa pia Waziri wa Mazingira alizingatie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, katika mgodi wa *North Mara* ni dhahiri kabisa wote tuko *aware* na uchafuzi wa Mto Tighite. Tunajua kabisa kwamba wananchi walidhurika, kuna vifo vilitokea, kuna vifo pia vya mifugo, kuna mimea ilidhurika, kuna viumbe hai kwenye Mto Tighite pia kama samaki na vingine vilidhurika pia. Waziri wa Mazingira katika hotuba yake, *page* namba 64 mpaka 65 ameelleza kwamba mwekezaji kwa maana ya *Barrick Gold Mine* ametimiza masharti aliyopewa na Serikali ya kurudisha mazingira katika hali yake na anaendelea kufanya hivyo. Lakini kulingana na *Environment Management Act* ya mwaka 2004, yaani Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, inatamka rasmi kwamba ikitokea mtu yeoyote au *institution* yoyote ikafanya uchafuzi wa mazingira, basi inakuwa *responsible* kulipa fidia ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. (*The polluter pays for social economic and environment costs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameelleza tu kwamba *Barrick* imetimiza masharti ya *ku-re-store the environment into its original shape*, lakini hajaeleza zile fidia nyingine ambazo ni za kiuchumi kwa maana mifugo iliyoharibika, mimea na samaki katika ule mto. Hajaeleza pia fidia ya kijamii kwa maana ya wale watu walioathirika. Tuliona watu walipata *skin discolouration*, ngozi zao zilibabuka. Kuna akina mama walipata *miscarriage* kwa maana mimba zao zilitoka, kuna watu walipofuka na madhara mengine mengi. Kwa hiyo, ningependa kujua Waziri anapofanya majumuisho ya hotuba yake leo atueleze bayana kabisa ni masharti yapi Serikali imetoa kwa mwekezaji huyu *Barrick* kwa maana ya hiyo *compensation* ya kijamii na kiuchumi. (*Makofi*)

Vile vile ningependa na ningeitaka Serikali kuitia Wizara ya Mazingira, iweke bayana ripoti ya Hifadhi ya Mazingira, yaani ripoti ya *NEMC*, ituweke wazi tuweze kujua ni nini hasa kilijiri kutokana na ule uchafuzi wa mazingira wa Mto Tigite. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusia kidogo sana kwa upande wa Muungano. Kwa upande wa Muungano, Waziri wa Muungano ametueleza kwamba wameondoa ile kero ambayo inatugusa wengi, wafanya biashara na watu ambao wanunua vitu kutoka Zanzibar, *double taxation*. Waziri amesema kwamba wameiondoa, kwangu mimi naona kwamba imekaa sana kinadharia kuliko kivitendo. Kwa sababu hiyo sheria ni sheria ambayo ipo katika *Financial Act*. Tulivyokuwa tunapitia *Financial Bills* hapa, hicho kipengele hakikuletwa hapa.

Sasa: Je, ni kwamba wamedhamiria kuondoa lakini itatoka kwa mwaka wa fedha ujao au wataiondoa *just to chop it out?* Inabidi Mheshimiwa Waziri atueleze, maana yake tunaelezwa hapa tunafurahia tunapiga makofi, tukienda *in the reality* unakuja na TV ya *LCD* ukifika Bandarini unaambiwa *you have to pay 400,000/= shillings*, kwamba walifanya *under estimation Zanzibar* wakati *Zanzibar* kuna *TRA* na *TRA* ndio wanaotoza ushuru siyo *ZRA*. Kwa hiyo, ningependa sana Waziri wa Muungano atuweke bayana kwa hili kwamba sheria ile ndogo imeondolewa kabisa au imetolewa waraka kwamba sasa hivi watu hawatafanyiwa *double taxation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha na kuishia hapo. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. JADDY SIMAI JADDY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya kwanza nami niweze kuchangia katika mada iliyopo mbele yetu katika Ukumbi wako Mtukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, napenda kumpongeza Spika - Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuteuliwa kwake kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia nitakuwa mpungufu wa fadhila iwapo sitawashukuru kwanza wapigakura wangu wa Jimbo la Mkwajuni kwa kuniwezesha kufika hapa katika Bunge lako Tukufu kwa maana ya kwamba niwawakilishe. Nami nawaahidi kwamba nitaonyesha utumishi uliotukuka na kwamba sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano. Kwanza nampongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri wa hoja yake. Lakini pia napenda nimpe pole kwa kile Wazanzibar tunachokuwa tukikisema kule kwetu. Samani lazima nimirage Mheshimiwa Waziri wangu, Mama Samia, kule kwetu tuna usemi unaosema, mchawi mpe mwana alee. Mama Samia wewe ni mchawi umepewa mwana ulee Wizara ya Muungano. Imeonekana kwamba kwa Wazanzibar ndio wengi sana tunapiga kelele kuhusiana na Muungano. Kwa sababu hiyo sasa mama Samia kaambiwa kapata motto,

lea wewe. Akifa hata kama amekufa kwa *pressure* bado itaonekana kwamba Mama Samia umemnyonga wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa la matatizo ya Muungano ni kutokuwepo na uwazi katika ile Tume ambayo imeteuliwa kutatua matatizo au kero za Muungano kutokana na kutokuwepo uwazi katika utatuzi wa hizo kero ndio inapelekea haya yote kutokeea. Ningeshauri Wizara pengine ijaribu kuweka utaratibu wa kuweka *awareness* kwa *public* kuweza kutambua nini kinachoendelea katika hiyo Tume kwa kila hatua ambayo inafikia katika suala la utatuzi wa matatizo. Kutokana na kutokuwepo uwazi wa utatuzi wa haya matatizo, ndio maana leo inatokea kwamba kila kukicha tunajadili masuala ya Muungano, imekuwa ni agenda ambayo inachukua mazungumzo yote ya jamii ya Watanzania sasa hivi. Yametajwa hapa baadhi ya mambo mengi sana na mojawapo kati ya hayo ni kutokuwepo dhana ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uelewa wangu mdogo ambaa nimesoma katika makala fulani nilivyolielewa mimi, suala hili sababu mojawapo ambayo imepelekea kwamba Rais wa Zanzibar asiwe Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nia pale ulipokuja mfumo wa Vyama vingi Tanzania mwaka 1992. Baada ya kuonekana kwamba siasa za Zanzibar zina upinzani mkubwa sana kiasi kwamba kulikuwa na hatari kwamba Zanzibar yawezekana kuna wakati ikafika mahali kwamba Chama cha Upinzani kama kitapata madaraka na kwa sababu Katiba inasema kwamba: “Iwapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hataweza kufanya kazi zake, basi Rais wa Zanzibar ambaye ndiye atakayekuwa Makamu wa Rais, akamate nafasi hiyo,” ikaonekana pale itakapotokea kwamba Zanzibar itakapokuja kuona Kiongozi kutoka upande wa Upinzani, haitawezekana kabisa kuja kuchukua nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika dhana ya kwamba atakuwa ni Rais ambaye hakuchaguliwa na wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yapo, yanazungumzwa na viongozi au yamejadiliwa na viongozi. Cha kushangaza, kwa nini wasiuambie umma kwamba hili ndilo wazo lililopo? Mpaka leo wamekaa kimya, watu wanaskotana. Kwa nini wewe? Serikali ya Zanzibar inatengwa! Makamu wa Rais wa Zanzibar siyo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania! Haya mambo viongozi yapo na mnayatambua na nyie ndio mmeyaanzisha. Rais wa Zanzibar hawezi kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu, kuna hiyo *idea* kwamba labda pengine Zanzibar inaweza kupata Kiongozi kutoka Upinzani, kwa hiyo, haitawezekana siku moja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakaposhindwa kufanya kazi zake na Makamu wa Rais kuchukua nafasi ya Rais wa Tanzania kwa kuwa tu hatakuwa amechaguliwa na wengi. Kwa hiyo, waeleze wananchi waweze kuelewa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani hizi chokochoko za Muungano nimebahatiwa kwamba nimekaa Urosi miaka mingi sana. Urosi wakati fulani ilipoanza kuamua kutaka kutengana, nchi ambayo ilikuwa ni kubwa sana duniani, iliyokuwa imejengwa na mataifa 15 walipoanza chokochoko za namna hii hii, tulianza sisi hapa Tanzania. Nakumbuka wakati ule kiongozi alikuwa ni *Gorbachev*, aliwaambia kwamba tusijaribu kuuchokonoa

Muungano kwa sababu Muungano wetu ndiyo utafanya sisi tuwe na nguvu duniani. Hasa hasa tukijaribu kuuchokonoa Muungano wakati ule alisema, iwapo *Ukraine* ambayo ni mojawapo kati ya *Republic* zilizokuwa zinaunda Urosi wakati ule, ikitokea kwa kweli Muungano wetu utayumba kwa maana ya kwamba Warusi, *Gorbachev* aliwaambia vile kwa kutumaini kwamba wakati ule *Ukraine* ilikuwa na nguvu kubwa na ilikuwa ndiyo *centre* ambayo zana nyngi za kivita zilikuwa zikitengenezwa pale. Vifaru, ndege kubwa za kivita, nyukilia nyngi zilikuwa zikitoka pale *Ukraine*. Wakaenda mpaka wakafika mahali wakatengana. Nasi tutakuja katika mfumo ule ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako, wengi tulimo humu sisi ni mazao ya Muungano huu. Kwa sababu tumezaliwa, tumekua, tumesomeshwa na tumejiweza ndani ya Muungano huu. Sababu hiyo, sasa hatuwezi kukataa ukweli kwamba Muungano ndiyo moyo wetu. Lakini sasa leo hii tunaanza kuwashukumu walioanzisha Muungano huu. Tumeweka kati sasa tunashitaki kwamba kila mtu, huyu alikuja na lake huyu ananyonywa, huyu kaja kwa mawazo yake peke yake, hakushauriana na wengine! Siyo kweli kabisa. Walisha *foresee* nini hatima ya Tanzania na ndiyo maana wakaamua kuunganisha Tanganyika na Zanzibar. Nasema kweli kwamba Muungano ambao tunauhitaji Watanzania na ili uweze kuendelea kudumu, basi ni Muungano wa Serikali mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna namna nyngine, ni Muungano wa Serikali mbili na kama tunataka Muungano wa Tanzania ufe, tuje na ajenda ya Muungano wa Serikali tatu. Kama tunataka Muungano huu ufe, tuanze Muungano wa Serikali tatu. Namkumbuka Mwalimu wangu aliyenisomesha *philosophy*, Mr. Balozi alinifundisha namna ya matumizi ya *comer* katika sentensi na alinipa sentensi moja akaniambia kwamba, “*kill him not, let him go*”. Akachukua *comer* akaiweka katika *kill him, not let him go*. Akachukua tena *comer* ile akaiweka katika *kill him not, let him go*. Sentensi ni ile moja, lakini sote tunakubaliana kwamba maana ni tofauti. (*Makofi*)

Humu ndani tumo tunapiga kelele kwa jazba, sote tunazungumza kauli moja kuboresha Muungano, lakini yawezekana katika mawazo yetu kuna *comer* inatembea kati yake. Sasa kwa sababu haijulikani nani, *comer* ameiweka wapi, ndiyo tatizo hilo. Hilo linatutatiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mtu alikuwa anakata tawi la mti, amekaa upande ambao tawi litaanguka. Akatokea msamaria, akamwambia, bwana utaanguka. Akamwambia haiwezekani kuanguka. Hakuchukua muda, akaanguka na kwa sababu yule mtu alishakwenda na kwa sababu aliyeambiwa na yule msamaria mwema na yakatokea kweli, aliamua kumfuata, akamwambia bwana uliyoniambia kwamba nitaanguka, nimeanguka kweli.

Sasa nakuomba uniambie kitu kimoja, siku gani nitakuwa? Akamwambia siku utakayokufa ni siku utakayokwenda kulala katika njia itakayokuwa inapita msafara wa ngamia kwa muda wa siku saba, hapo utakuwa. Kweli akaenda kulala katika ile njia, haikufika siku saba msafara wa ngamia ukapita katika njia ile, matokeo yake wenye ngamia kwa sababu ngamia walitishika na kuona kitu ambacho siyo cha kawaida,

wakampiga mikwaju na kwa sababu nyumbani alishaaga kwamba anakwenda zake ahera, aliporudi mtaani aliulizwa, hebu tuambie habari za ahera, akasema ahera juu kali, baridi na mikwaju mingi. Hakuendeki ahera. (*Makofi/Kicheko*)

Hapa jamani tunaujadili Muungano, tunachukua kitanzi tunakitia ndani ya shingo zetu, roho zetu, Mungu Bariki tusije kukutwa na mawazo ya kufyatua *stool* tukaja tukaacha kitanzi kikatukaba kooni mwetu. (*Makofi*)

Jamani Wazanzibari tunalalamika sana habari ya Muungano, ni sawa na mgonjwa mwenye sukari. Sukari ikianza kula kidole, kikate. Lakini ikifika nyongani, huwezi kumkata nyonga mtu, utammaliza. Siyo rahisi. Ninachokisema, jamani tuwe makini katika kujadili hatua za Muungano wetu, sisi hasa Wazanzibari ndiyo tegemeo letu, ndiyo roho yetu, mkituacha, tumeumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoyasema haya, nilianza kusema hakuna uwazi katika utatuza wa kero za Muungano, laiti kungewa na uwazi katika utatuza wa Muungano, kila hatua ambayo inafikiwa katika kutatua kero za Muungano, basi yasingetokea haya yote. Wazanzibari wanapouliza asilimia 4.5 ya mgao wa benki na misaada inatokea wapi? Tupeni maelezo tu, basi. Tumeamua kutoa asilimia 4.5 kwa sababu ninyi idadi yenu ni ndogo, lakini hakuna maelezo. Kwa hiyo, kila siku haya yatakuwa yanaendelea kukua. Huwa yanakuja yanalundikana, baadaye itakuja kushindikana kuja kutatuliwa. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri Mama Samia kama nilivyotangulia kusema mwanzo, umepewa mwana ulee, kwa sababu wewe ndiye unaonekana kwamba ndiyo mchawi na ole wako yule mtoto afe, hata kama amekufa kwa *pressure* tutasema umemnyonga wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotuma Wazanzibari, ni tofauti yetu kiuchumi iliyopo kati ya Bara na Zanzibar. Siyo rahisi kumwona baba anakula nyama ya kuku, mtoto unamtazama macho, akaendelea kukutazama tu. Atakuwa anaumia rohoni, ataondoka, baba anafaidi nyama. Wewe unapomtupia shingo haina nyama na wenzetu tunawaoneni mnanyanyuka, Zanzibar tunaendelea kudidimia! Eeh, Zanzibar inaendelea kudidimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani aliye kuwa Rais wa Marekani John Kennedy alipota...

(*Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jaddy Simai, umeongea vizuri sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya nzuri,

kuniondolea yale maradhi makubwa sana mpaka sasa, na ninamshukuru mke wangu ajue hilo, na pia nashukuru Jimbo langu kwa kunipa kura nyangi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzanzibari yeoyote kama hakushukuru watu wawili, basi huyo mtu hana fadhila nzuri. Namshukuru sana Rais wa Zanzibar aliystaa fu Mheshimiwa Karume na Mheshimiwa Seif Shariff Hamad. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar baada ya utawala wa muda mrefu wa Chama cha Mapinduzi, tuliadhibika sana pale, tulinyanyasika sana mpaka wengine wakafa. Sisi wengine tukitembea mle njiani kuna watu tukiwaona, basi tunainama chini, kule jela tulivyokuwa tukifanyiwa. Lakini watu wawili hawa walipokaa na wakayaangalia madhara haya yaliyotokea na wakakubali kuunda Serikali hii iliyopo leo, sisi sote tunafurahi, tunatembea kifua mbele. Lazima tuwashukuru kwa nguvu zote, Mungu awape afya njema na awafungulie baraka kubwa katika maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea juu ya Muungano, kwanza suala la Naibu au Makamu wa Rais wa Muungano au wa Tanzania kuchukuliwa kisiasa ni makosa makubwa sana, kwamba CCM itashindwa Zanzibar, kwa hiyo, Makamu wa Kwanza wa Rais atakuwa *CUF* au chama kingine, ni kosa kubwa sana. (*Makofi*)

Nchi mbili hizi zina heshima zake katika Muungano. Makamu wa Kwanza wa Rais, Rais wa Zanzibar ni nembo ya Zanzibar katika Muungano, siyo kwamba CCM imeshinda Rais wa Muungano, basi Makamu wa Rais atoke kwenye Chama cha CCM. Siyo nembo ya Zanzibar, ni nembo ya CCM. Naomba sana lifahamike hilo. Mfumo mzuri Rais wa CCM, Makamu wa Rais wa Zanzibar anaweza kuwa CCM, anaweza kuwa *CUF*, lakini anayeongoza nchi hii, Serikali ni Waziri Mkuu. Sasa Waziri Mkuu atatoka kwenye kile Chama ambacho kimeshinda. Lakini kumwondoa Rais wa Zanzibar kumfanya kuwa siyo Makamu wa Kwanza wa Rais na ni Cabinet Minister, ni kuidhalilisha Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nilitaka kuzungumzia, fadhila nzuri za Muungano lakini kwanza tuitazame katika historia yake. Muungano baada ya kuunganishwa Zanzibar na Tanganyika haina haja kutafuta sababu yake ni nini. Watu wote wanajua. Lakini ilipoundwa Katiba ya Muungano walitoka 20 Tanganyika na 20 Zanzibar. Tume ile ilikuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Thabit Kombo ya kuunda Katiba ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazanzibari wanaijua elimu ya Mheshimiwa Thabit Kombo iliviyokuwa na wenzake wote waliokuwemo kutoka Zanzibar. Tume hii ya Bara Katibu wake ni Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa CCM - Mheshimiwa Pius Msekwa aliyekuwa na *Degree* ya Sheria. Nafikiri tunafahamu Waheshimiwa, ikapita Katiba ya mwaka 1977, muundo wenyewe ndiyo huo. Nawaombeni sana wananchi wa Zanzibar, wananchi wa Tanganyika nafasi hii ambayo inakuja ya Katiba mpya lazima tuangalie nini maamuzi yetu ya nchi yetu tunayoamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, tulikubaliana katika Muungano, hati za Muungano ni 11, lakini baada ya kuletwa katika Bunge hili na kwa sababu ni mabadiliko ya Katiba, ikakataliwa, zikaongezwa mpaka 23 kiholelaholela namna hiyo kwa manufaa ya wengine. Hatari kubwa imetokea, watu wanunung'unika, manung'uniko yalikuwa hayana kiasi.

Kwa mfano, hapa hapa Bungeni, leo watu wanalichukua Jimbo langu mimi la Chakechake lina watu elfu tatu, lakini Jimbo la Mkuu wa Upinzani lina watu elfu sitini au laki tatu, halina msingi na ndiyo sababu ukakuta chama changu cha *CUF* kina Majimbo 26, lakini Chama cha CHADEMA kina Majimbo 23. Lakini Majimbo 23 yamechukuliwa mengi sana kwa sababu ya kura zinazotoka Bara.

Kule Zanzibar kura za nchi nzima ni laki moja au laki nne ambalo ni Jimbo moja la hapa, na nimekosa heshima ya utawala wangu au Utaifa wangu kwa sababu natoka kwenye kisiwa kidogo. Hakina watu ndani ya Bunge hili na kila mtu anajua. Hata katika mgao wa Vyama hivi vinavyotolewa na Serikali, wenyewe Wabunge ndani ya Bunge wanahesabiwa watu wenyewe kura nyingi, hawahesabu watu wenyewe *sits*. Huo ni udhalilishaji wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipounganisha Benki Kuu au ilipoundwa Benki Kuu, Zanzibar ilikuwa na *share* yake kwa sababu ilikuwa ni pesa inayotoka katika *East African Community* baada ya kufa. Utengenezaji wa noti moja haizidi 20% ya pesa ile na 80% ni *profit*. Iko wapi *profit* ile? Zanzibar imepata kiasi gani? Tumepata nini? Tunaungana na *East Africa Community*, sisi Zanzibar hatuna Kiti wakati Muungano wana Wizara sita ambazo ni za Muungano, sisi zile za kilimo, zile zilizokuwa siyo za Muungano, atazitetea nani? Haki yetu iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilitaka ufanuzi wa petroli. Unakuta kuna *road toll*, kuna *EWURA, TPC, TPA, TPDC* kodi zote hizi ziko huku Bara, kwa nini Zanzibar kodi hii iingie kule *road toll*? Sisi hatuna mchango wa barabara, sisi mafuta yetu tunayoagizia nje yanakuja moja kwa moja kwenye matenki yetu, yanachukuliwa yanakwenda zake. Hatuna sababu ya kulipa. *EWURA*, sijui nini sasa, naomba Waziri akija atusaidie, atupe ufanuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano ni chombo kizuri, kinaweza kikasaidia maendeleo ya nchi zote mbili. Lakini kiburi, batra, udhalilishaji wa watu kidogo na watu wengi ndiyo *problem* tunayoipata. Wale ambao walikuwa na nia njema ya kuunga Muungano walikuwa wanahitaji tuwasifu na tuwaheshimu sana.

Ni kweli Marehemu Karume hakusoma, hakuwa na elimu kubwa, lakini alikubali kushirikiana na mtu ambaye ana *Degree*, Mwalimu Nyerere. Hata kama kulikuwa na njia ambazo zilimsababisha afanye hivyo, lakini sisi tuliopewa sasa, tuliokabidhiwa huo Muungano, leo elimu ya juu ni ya Muungano. Waziri anakwambia ah, mimi natoa tu watakaopata watapata. Ah, unanichanganyishaje mimi ndani ya watu milioni 40 kwa watu milioni moja? Lazima Zanzibar iwekewe *share*. *Share* yenu ni 25% au 10% au 5%,

wanatoka milioni mbili, sisi tunatoka watu elfu moja kwa sababu dharau na kibri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda katika utumishi wa Muungano, Ofisi hii tunayoizungumza leo ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mzanzibar mmoja, nenda kwenye Ofisi ya Rais mwenyewe, hamna. *Why? Nini tatizo? Umoja huu uko wapi?* Umoja ni maslahi, kumwondo huyu katika shida. Ukimchagua Mzanzibari akawa anafanya kazi pale, ye ye haitamsaidia na mwenzake na familia yake, nyote mko pale. Jamaa mmoja ananiambia kumbe hata Ofisi ya Bunge, kwani ina haja gani?

Juzi nazungumza habari ya kujengwa kile Chuo cha Uongozi Zanzibar, mwingine anasema, ah, Kile Chuo siyo cha Muungano. Sasa Waheshimiwa, tena ni Wabunge hebu tusome tuwekewe heshimiwa yetu, tuwekewe haki yetu, tusifikiri kwamba Jeshi tu ndiyo linaweza kufanya kazi, hapana. Angalieni nchi za kiarabu, wameuziwa ndege na wale wale wanaowapiga sasa. Tujengeni Muungano mzuri ambao unaweza kupendeza na kwa nchi yetu ukaendelea vizuri. Ndiyo sababu nchi nyingi za kiafrika zikakataa Muungano. Haidhuru nyie mnasema ndiyo sababu ya Muungano huu kuwa mzuri. Wengine watakubali kuungana, hawakubali, siyo kweli. Kama watu ambao wangeungana, basi wangeungana wakati wa Kwame Nkuruma na Pafu Meka. (*Makofi*)

Walijua hivi hivi tu, mmoja atanung'unika. Bahati mbaya unasikia watu wanachimba gesi, petrol, kule tulipata mradi tangu mwaka 1986. Canada walitoa dola milioni mbili msaada, hakuna taarifa yoyote, hakuna chochote, tunadanganyana tu, 26 tuna 10, keshokutwa tutachimba, kumbe hatuna chochote. Hebu fungueni jamani msije mkatafuta mchawi kumbe wachawi tunao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu ndiye Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, nitamsikiliza maamuzi yake, ndiyo nitaamua nimuunge mkono. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Haji Kombo kwa mchango wako. Sasa naomba namwita Mheshimiwa Fakharia Shomar na mchangiaji wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, inabidi nimshukuru Mwenyezi Mungu, vile vile nawashukuru na wazazi wangu, vile vile nawashukuru wanawake wa Mkoa Mjini Magharibi kwa kuniwezesha kufika hapa leo na vile vile kuwapongeza Mawaziri wawili ambao ni Waziri wa Muungano na Waziri wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kuzungumzia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Mimi nilikuwa nataka kuzungumzia kwamba mfumo wetu wa Muungano uliokuwepo hivi sasa ni mzuri, hauna tatizo. Lakini hapa katikati kumetokea waandishi wengi wa vitabu na waandishi hao kila mmoja ana utashi wake. Sasa hao ndio wanaopotosha umma. (*Makofi*)

Mhesimiwa Naibu Spika, kama inavyojulikana kwamba Muungano wetu ulikuwa wa nchi mbili Tanganyika na Zanzibar na viongozi walikaa, hata kiongozi akikaa wakati alikuwa na nchi hatakaa peke yake, lazima atashauriana na Wasaidizi wake. Lakini kwa sababu viongozi hawa wawili wameshakufa, lakini watakuwa wanaao wandaamizi wao wanaolielewa hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Bunge lako Tukufu lifanyiwe Semina, tuelenze kwa kirefu kuliko kila mmoja kuinuka na utashi wake, akasema vyake. Kwa sababu bila shaka viongozi wamefariki, lakini wako watu wanaelewa, wako watu wanaoelewa kwa upande wa Visiwani, wako watu wanaelewa kwa upande wa Bara na hao wataalam ambao wanaandika hivyo vitabu, tukachanganyishwa nao ikafanywa Semina, kutakuwa kuna upande wa kuuliza, wa kufahamishana na kuelewana. Semina hii ingefanya kabla ya mwaka 2014 wakati Katiba mpya inafanya kazi. (*Makofi*)

Kwa sababu kumeshakuwa na misemo mingi na watu wanasema mingi na hao wanaosema, wengi wao ni watoto wa Tanzania siyo kama ilikuwa Tanganyika au Wazanzibar, wanajua toka mwanzo tumetokea wapi. Sasa mimi ilikuwa tahadhari yangu hiyo, tupate Semina ili umma tuueleweshe hali halisi ikoje katika Muungano wetu. (*Makofi*)

Nikija kwenye suala langu la pili, Idara ya Muungano. Idara ya muungano ambayo kwanza ilikuwa Sekretarieti ya Muungano sasa imekuwa Idara ya Muungano. Idara hii inashughulikiwa na Waziri wa Muungano. Inapendeza hasa Waziri awe na Wizara yake ya Muungano ambayo awe na Katibu wake wa Muungano, au apewe Naibu wake wa Muungano na Idara zake za Muungano. Nasema hivi kwa sababu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Muungano, iko katika Ofisi ya Makamu wa Rais, yuko Katibu Mkuu na yuko Naibu Katibu Mkuu. Hawa wanashughulikia maslahi tu, siyo mambo ya Muungano. Ingawa wanafanya kazi chini yake, lakini wakati anapokuja kufanya masuala hasa ya Muungano, inabidi *direct* iende kwenye Kitengo cha Muungano.

Kitengo cha Muungano kina wafanyakazi kidogo. Kuna Wakurugenzi watatu, na wafanyakazi wake, hata kama atajipanga kwa sababu wanatakiwa waratibu wa Muungano na yaliyokuweko Visiwani, ndiyo hao hao wanakwenda mbio tu. Leo yuko Bara, na kesho yuko Visiwani. Sasa ni wakati wa kupanua wigo akawa na Ofisi zake Unguja za kutosha, ana ofisi zake Bara za kutosha, atakuwa hana shida kiutendaji. Kwa sababu Wizara zikikaa zinapokaa kufanya vikao vya ushirikiano, zinataka kufuatiliwa. Sasa kelele hizi tunazopiga na vikao vinakaa, vinaamua lakini, wafuatiliaji hawako, kwa sababu wafanyakazi hawatoshi.

Hata akisema atajipanga, inabidi wakija Zanzibar waikamate Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, waikamate *Private Office* ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. uende nayo mbio. Sasa hayo pia kwa upande wa pili ni tatizo. Tunajua kwa sababu hii Wizara inashughulikia nchi mbili ya Tanganyika na Zanzibar kwa kufanya Tanzania, ilikuwa inatakiwa iwe na wigo mkubwa kwa kufanya kazi ili hizi kero zimalizike. Lakini kwa hao waliokuweko idadi yake, kero hazimaliziki.

Ukitazama kwa Zanzibar utakuta kuna Maafisa watatu na hao hawana nguvu, hawana *mandate* ya kuamua au kufanya kitu. Lakini hawa Wakurugenzi watatu waliokuwa nao mmoja wangemleta Zanzibar wakati Ofisi tayari iko Zanzibar wakaihuisha Ofisi ile wakawa na Vitengo pale vyta Muungano vinafanya kazi vizuri wanafuatalia kinachoamuliwa wanakimbia mbio, wanakitolea *feedback* tunajua nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili unakuja kwenye jengo. Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyokuwepo Zanzibar ambayo iko Tunguu, jengo hili limezinduliwa au limefunguliwa toka Oktoba mwaka 2010. Tatizo mpaka leo halijatumika. Ukiuliza juu ya tatizo hili unaambiwa kwamba halina samani za kufanya kazi ili jengo liweze likatumika. Jengo zuri, jengo linapendeza, lakini ukipita unaliangalia tu halina kazi inayofanyika.

Tuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wafanyakazi wa Muungano ambao wametupa jengo tunafanya kazi humo na tuwapongeze kwa sababu hawatubughudhi, tunafanya kazi mpaka samani tunazotumia ni zao. Hilo ndiyo limefanya tumeshindwa kuhama, kwa sababu tunapotaka kwenda kule inabidi twende na samani zetu na hizi siyo zetu. Tutaondoka nazo, na kama hatuwezi, inabidi tubakie pale pale.

Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri afanye kila mbinu kwa sababu jengo ni zuri ambalo limetengenezwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Vitengo vyake vyote mpaka jengo la Mheshimiwa Makamu wa Rais vimo humo humo kwa sababu ni sehemu kubwa.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri afanye kila mbinu kwa uwezo aliokuwanao na Mungu atajalia bajeti hii ikipita atapata fedha, kitu cha kwanza kuweka samani na vijana waende wakahamie katika jengo letu, tutazame mengine sasa utekelezaji wake. Maana utekelezaji ndiyo mgumu na utekelezaji unakuwa mgumu na hasa ukiwa pa kukaa huna. Ni mtu anayepanga panga siyo mwenye nyumba yake. Sasa ningewomba Mheshimiwa Waziri kwa haya niliyoyaeleza na pia ninajua ni mahiri na mtendaji mzuri na hii Idara. Kwa hali halisi ilivyo, unaiweza, maana tumeona kuwepo kwako wewe hatua nzuri zinazifikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja, nikisema ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami nitoe yangu machache kuhusiana na hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na kuchangia mada ya Muungano wetu, yaani muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar. Nadhani ni Muungano pekee uliodumu hapa Afrika. Ipo miungano mingine ambayo ilitokea katika historia, tunaifahamu, mathalan Senegal na Gambia ilivunjika na mingine iliyotokea kule Afrika ya Kaskazini

ilivunjika na hivi karibuni kuna nchi ambayo ilikuwa ni moja imeshagawanyika badala ya kuendelea kuwa moja imegawanyika. Hii inatueleza nini kuhusu Muungano wetu?

Huu Muungano ni wa kipekee na umedumu kwa sababu ya uongozi ambao tumekuwa nao. Kama viongozi wangekuwa ni wabinagsi, wangeamua kuondokana na huu Muungano. Lakini pia nadhani umedumu kwa sababu wananchi wa nchi hizi mbili (mimi naziita nchi), wananchi wa nchi hizi mbili wamekuwa karibu, wamekuwa na ukaribu wa kihistoria. Muungano wetu umedumu siyo kwa sababu hakuna matatizo, yapo mengi na yameshasemwa, sina haja ya kurudia, labda nitasema tu machache kwa kuyatilia mkazo tu.

Tatizo la kwanza ambalo nalionna ni la muundo wenyewe. Zanzibar ikiwa na kero haiongei na Tanganyika, inaongea na Serikali ya Muungano. Toka zamani sana mimi niliona hili ni tatizo, maana sisi wengine Muungano huu umetukuta tupo. Tulikuwa wadogo, lakini tulikuwepo na tuliusherehekeea mwaka 1964. Toka nikiwa Sekondari niliona kwamba hapa kuna tatizo: hapa kuna Serikali ya Muungano, hapa kuna Serikali ya Zanzibar. Serikali itaongea na nani hapa? Kwa sababu Muungano uko juu, Serikali ya Zanzibar iko chini, mwenzake ambaye Serikali ya Zanzibar ingeongea naye, hayupo, yaani Serikali ya Tanganyika hayupo. (*Makofi*)

Hilo ni tatizo ambalo sisi tukiwa vijana, tulianza kuliona mapema sana wakati huo. Hilo tatizo tumeendelea kuwa nalo, tumelivumilia. Watanganyika walanza chokochoko wakasema na sisi tunataka Serikali yetu, wakapigwa konzi. Wakavumilia tu. Lakini nadhani ni wakati muafaka wa kujadili kinaganaga muundo wa Muungano. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo ni changamoto ambayo labda hajatajwa, lakini naona kwamba tatizo ni kugawana gharama za uendeshaji wa Muungano. Kwa sababu hii miungano kuna gharama zake. Sasa ili kuwe na mgawanyo sawa, lazima kuwe na washiriki wa huo Muungano wanaochangia kuendesha huo Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Umoja wa Mataifa ni Muungano wa namna fulani, ni umoja wa namna fulani. Serikali zote ambazo ni wanachama wanachangia gharama za uendeshaji wa huo umoja. Ingawa mchango huo sidhani kama una uwiano wowote. Sidhani kama Tanzania inachangia kama Marekani inavyochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama Tanzania inalalamika kwamba inadhalilishwa kwa sababu haipati haki ambazo Marekani inapata katika Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spikam jambo lingine ambalo kwa hakika ni la haki na lazima liwe wazi ni kugawana nafasi za kazi katika Idara mbalimbali za Muungano. Hili limezungumziwa na mifano mbalimbali imetolewa. Hili ni jambo ambalo Waziri anayehusika inabidi alitolee kauli namna linavyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililozungumzwa ni kugawana faida ya uchumi wa Muungano. Hili ni tatizo kubwa na siyo rahisi kulitatua, lakini ni lazima lizungumzwe. Vigezo vya mgawanyo huo lazima viwe wazi, vijadiliwe. Itafaa tutumie mifano mingine ya Muungano kama mfano wa Marekani.

Marekani ina nchi ambazo zinaitwa *States* (Majimbo); sisi tunaziita Majimbo, lakini hasa ni nchi. Zilikuwa ni nchi, zikaungana. Nyingine ziliunganishwa kwa nguvu, kwa hiyo, ile vita inaitwa vita ya wenye we kwa wenye we ambayo ilipambanisha Marekani Kaskazini na Marekani Kusini; walilazimishwa wale watu wa Kusini baada ya kushindwa na watu wa Kaskazini. Muungano huo pamoja na kwamba walilazimishwa bado upo. Ni marufuku kwa nchi yoyote au *State* yoyote kule Marekani kujitenga. Imeandikwa kwenye Katiba ya Marekani.

Jambo lingine ambalo limezungumzwa, linahusu habari ya mafuta na mambo kama hayo, yaani shughuli zifi za kimuungano na zifi ambazo zibaki ni shughuli za nchi husika. Hilo pia linazungumzika.

Tunaweza kutoa mfano wa Muungano wa Uingereza ambao unaitwa *United Kingdom (UK)* ambao unajumuisha *England, Scotland, Wales* na *Ireland* Kaskazini. Huo Muungano pamoja na kwamba hauna Katiba ya kweli kama ambayo sisi tunayo, hapa wao wana mapokeo ambayo ambayo wamekuwa wanatumia katika kuamulia mambo yao, lakini shughuli zote ni za kimuungano isipokuwa michezo tu.

Katika Muungano huo wa Uingereza shughuli zote ni za kimuungano isipokuwa michezo, na katika Umoja wa Ulaya wanakwenda kama *United Kingdom* katika shughuli zote za kimataifa. Isipokuwa nchi moja moja inaweza kuwa na mahusiano na nchi nyingine.

Katika Umoja wa Mataifa wanaenda kama *United Kingdom* na katika shughuli zote za Kimataifa wanaenda hivyo isipokuwa nchi moja moja inaweza kuwa na mahusiano na nchi nyingine, mahusiano ambayo sio makubwa sana ya kimataifa, lakini ruksa ipo hata miji inaweza kuwa na mahusiano na miji mingine katika nchi nyingine, yapo matatizo hayo. Napenda tu kusema kwamba haya yote yanazungumzika. Katika Katiba Mpya ambayo tutaandika, tuyazungumze, tufikie mahali tukubaliane. Zile Kamati ambazo zimekuwa zikiendelea kufanya kazi, zifanye kazi, zisiwe zinafanya kazi ya kimazingombwe-mazingombwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumza pia kuhusu mazingira. Nitazungumzia mazingira kwa kutoa mfano wa Shinyanga. Sehemu kubwa ya Shinyanga ni nusu jangwa, sio yote lakini sisi ambao tumezaliwa na kukulia huko kwa hakika tulipokuwa wadogo Shinyanga haikuwa hivyo. Ilikuwa na misitu mingi, miti mingi, yaani kila sehemu ulipokuwa unapita kulikuwa na mazao lakini uharibifu wa mnyama anayeitwa binadamu ndiyo amesababisha hilo nusu-jangwa. Binadamu ni mnyama ambaye amesababisha matatizo haya yote yaliyopo Shinyanga kwa ufugaji na kilimo kisichozingatia taratibu nzuri za uhifadhi mazingira, uchomaji wa misitu, ukataji miti bila

kupanda miti kwa ajili ya kuni na mkaa, hayo yote yamesababisha Shinyanga ya leo ikawa kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri husika atueleze kuna mkakati gani wa kuokoa haya maeneo, sio Shinyanga tu bali maeneo yote hapa Tanzania, ambayo ni nusujangwa ili yarejeshwe katika hali yake ya zamani. Kuna mkakati gani? Kwa sababu, nimekuwa nikiangalia bajeti, naona ni ndogo sana! Ni kweli Serikali ina Sera tayari, kuna Sera ya Misitu, kuna Sera ya Ardhi, kuna Sera ya Mazingira na pia kuna hata Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 lakini utekelezaji wa Sera hizi na Sheria hiyo, haupo! Kuna vimiradi vidogovidogo vya hapa na pale, hata upandaji miti ambao unatekelezwa, hakuna usimamizi wala ufuutiliaji wa hiyo miti, mingapi imeendelea kuwepo na mingapi imekufa, hakuna kitu kama hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atueleze kuna mkakati gani? Sio hizi Sera tu, Sera zipo ndio na Sheria ipo lakini tunachohitaji ni utekelezaji, usimamizi na ufuutiliaji, kwenye ngazi za Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Tungependa kuona hasa sisi ambaao tuko huko Shinyanga na maeneo yote ambayo yanazunguka eneo hilo, tungependa kuona mipango thabiti na utekelezaji makini wa hizo Sera na Sheria. Hadi sasa hakuna chochote kwa kweli na kile kilichopo ni kidogo, wala hakiletii mabadiliko ambayo yanatakiwa. Mimi nilitegemea kwamba Wizara ingetangaza kwamba uharibifu wa mazingira hapa nchini ni janga la Kitaifa, kwa sababu huko tunakokwenda ni kubaya. Naomba Wizara au tuseme Serikali itusaidie kutueleza mipango thabiti, kwamba kuanzia sasa hivi huko mbele tutafanya nini katika hii miaka mitano? Tutafanya nini kubadilisha hii hali kabla mambo hayajawa mabaya zaidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kushika kalamu na kuandika machache kuhusu Muungano wetu na pia mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahenga walineni, “Umoja ni Nguvu na utengano ni udhaifu”. Kabla sijaenda mbali, napenda nimpongeze Rais wetu mpewda Dkt. Jakaya Khalfan Mrisho Kikwete, kwa uzalendo wake wa kuupenda Muungano na kufanikisha uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kule Zanzibar, historia itamuenzi. Ili umoja uwe ni nguvu ya kweli, ni lazima umoja huo uwe na nia, azma na dhamira ya dhati. Kinyume cha kutokuwa na mtazamo (*vision*) ya pamoja, umoja huo hautoweza kuleta nguvu bali utaleta upungufu (kusinyaa).

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaupenda Muungano, lakini tunaona kama hakuna dhamira ya dhati na mtazamo (*vision*) ya pamoja wenye lengo la kuleta manufaa kwa pande zote mbili za Muungano. Dhamira inayoonekana ni ya kuuneemesha upande mmoja (Bara) na kudhoofisha upande mwengine (Visiwani).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kulipishwa kodi mara mbili wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoleta bidhaa zao Tanzania Bara bado lipo na limezidi kuongeza adha na usumbufu. Pamoja na Waziri wa Nchi, Muungano, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan (Mb), kulieleza Bunge hili kuwa kero hii imeshatatuliwa sio kweli, kero hii bado ipo na usumbufu umezidi! Tatizo hili la kero ya kulipishwa kodi mara mbili limewakumba hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Wametozwa kodi mara ya pili walipoleta magari yao Dar es Salaam kutoka Zanzibar kwa ajili ya matumizi yao binafsi. Ikiwa kwa Waheshimiwa Wabunge hali ni hiyo, je hali itakuwaje kwa wafanyabiashara wadogo wa kawaida, wanaojituma ili kupata angalau mkate wa familia zao? Tatizo hili bado lipo na ni kero kubwa sana kwa wananchi maskini wa visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine ni uanzishwaji wa Akaunti ya Pamoja. Ripoti iliyasilishwa Serikalini Agosti 2006, mpaka sasa ni July 2011, bado mwezi mmoja tu kutimia miaka mitano akaunti hii haijafunguliwa. Hii inadhahirisha Serikali isivyokuwa (*serious*) makini katika kutatua kero za Muungano. Wataalamu wamepewa kazi waifanye, wamemaliza na kukabidhi ripoti, miaka mitano (5) imepita haijafanyiwa kazi! Hivi kweli Serikali hii ni sikivu na ina nia na dhamira ya dhati ya kutatua kero za Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichangie kuhusu mazingira yetu. *No Environment, no life* (Bila mazingira hakuna maisha). Bila ya kuhifadhi mazingira, uhai wetu sisi binadamu na viumbe wengine uko mashakani. Vitu vyote vilivyomo ulimwenguni vikiwemo anga, hewa, ardhi, bahari, mito, maziwa, misitu, wanyama na hata wadudu, vyote vimeumbwa na Mwenyezi Mungu kwa faida ya uhai wetu sisi binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchafuzi wa mazingira umekithiri sana, Serikali haina budi kuwa makini sana na uchafuzi huo. Umakini huo ni pamoja na kudhibiti uchafuzi wa hewa na vyanzo nya maji kunakosababishwa na viwanda vinavyokiuka taratibu za uhifadhi wa mazingira. Pia migodi mikubwa inachafua mazingira kwa kiasi kikubwa na bila hata ya nchi kufaidika na chochote kutokana na migodi hiyo, zaidi ya athari za uharibifu wa mazingira. Ni lazima hatua za kudhibiti uchafuzi huo zianze kuchukuliwa leo na siyo kesho. Keshokesho inaumiza matumbo. Serikali iwe kali katika kudhibiti uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili iwe rahisi kuhifadhi mazingira, ni lazima pia Serikali iwe na dhamira ya dhati ya kusambaza umeme pamoja na upatikanaji wake mijini na vijijini ili kuwezesha nishati mbadala na bei iwe *affordable* kwa wananchi wa vijijini ili kuепusha ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuchoma makaa. Sambamba na hilo, Serikali iwe na mkakati endelevu wa kupanda miti na kuihuisha miti inayopandwa ili ikue. Kwa kushirikiana, kuelimishana na kusaidiana hakuna lisilowezekana. La muhimu ni kila mmoja wetu kujua na kutimiza wajibu wake. Ahsante sana.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi (Mazingira), Watendaji wake Wakuu wa Wizara na Watendaji wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kwa

mipango mizuri yenye lengo la kusimamia vema suala la mazingira hapa nchini. Pamoja na pongezi hizo, ninao ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi hivi sasa ni kubwa na lina athari kubwa kwa maisha ya jumla ya Watanzania, kuna haja ya Serikali kulichukua suala hili kwa uzito mkubwa, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilichukulie suala la Hifadhi ya Mazingira na kuzitaka Halmashauri zote nchini ziwajibike katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya 2004 (Cap.191) na sheria nyingine kama za Misitu pamoja na sheria ndogo zote za mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) iratibu na kufanya kazi kwa karibu na ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Kwa kufanya hivyo, Halmashauri zote zitahusika na usafi wa Miji, Majiji, masuala ya udhibiti wa mifuko ya plastiki, utunzaji wa vyanzo vya maji, udhibiti wa uchomaji moto misitu na maeneo ya wazi, vichaka na milima. Halmashauri pia zitakiwe kuzitumia *NGOs* zinazosimamia Hifadhi ya Mazingira ikiwa ni pamoja na kuzipatia fedha. Napenda kupongeza utaratibu mzuri wa kuzishirikisha Miji, Majiji na Manispaa nchini katika mashindano ya usafi wa Miji. Ili mashindano haya yawe na maana, ni muhimu yajengwe katika fikra za Watanzania wote za kuchukia uchafu. Hivyo ni muhimu kufikiria pia kuliingiza somo la Mazingira katika mitaala kuanzia madarasa ya Chekechea hadi shule za msingi na kuendelea. Kwa njia hiyo, tutakuwa tumejenga misingi mizuri ya kujali mazingira yetu, kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uchimbaji wa madini ya Dhahabu, Almasi n.k. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kujiajiri kwa njia ya uchimbaji mdogomdogo, ni muhimu kuwekwa kwa taratibu za sheria za kuwataka wachimbaji hao wanafukia mashimo yanayotokana na uchimbaji huo. Inasikitisha kuona mashimo mengi huko Chunya, Shinyanga, Mbarali yameachwa wazi bila kufukiwa, ni uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). Pamoja na umuhimu na majukumu makubwa yanayotokea kwa Baraza hili, Baraza limekuwa likifanya kazi katika mazingira magumu. Miradi ya maendeleo inayoibuka sasa hivi ni mingi sana, yote inatakiwa kufanyiwa *EIA* kabla ya utekelezaji wake. Kuna miradi pia ya zamani kabla ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, sasa hivi imeanza kuleta uchafuzi wa mazingira na inahitaji *Environment Audit*). Nashauri Baraza liongezewe wataalamu na vitendea kazi vya kutosha. Pamoja na upungufu huo, napenda kupongeza kazi kubwa ambayo Baraza limekuwa likifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 14/15, Waziri ameeleza na kutoa takwimu za fedha ambazo zimepelekwa SMZ ambazo ni gawio la 4.5% kwa mwaka 2010/2011 tu. Kwa kuwa utaratibu huu ulikubalika kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa kuanzia mwaka 1994 na kwa kuwa Naibu Waziri wa Fedha SMT, alipokuwa akijibu swali Na.162 liloulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kiembe-

Samaki, Naibu Waziri alitoa takwimu ya fedha zilizolipwa kwa SMZ kwa kipindi cha 2001-2010 ambapo alieleza SMT imeipatia SMZ gawio lake la 4.5% ambapo kati ya Tshs.5.5 trillioni zilizopatikana (SMT), Tshs.196.127 bilioni zilipelekwa SMZ. Kutokana na mahesabu ya uhakika ni kwamba asilimia 4.5 ya 5.5 Triliioni ni 247.5 bilioni na sio kama alivyo sema Naibu Waziri. Kwa kuwa SMT imeipaitia SMZ gawio pungufu katika kipindi hicho, ambapo kunabaki gawio la Tsh.51,373 bilioni ambazo ni haki ya SMZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba Mheshimiwa Waziri (Muungano) nipate maelezo, je, fedha hizi ziko wapi? Zimehifadhiwa na nani na ni kwa idhini ya nani? Je, ni lini bakaa hii italipwa kwa SMZ? Je, SMT itakubali kuilipa *interest* SMZ kwa kucheleva kuwalipa fedha hizo ndani ya kipindi hicho cha miaka 10 ambapo SMT imekaa na fedha hizo?

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora umeathirika sana na uharibifu wa mazingira hasa kwa ukataji ovyo wa miti katika mapori ambayo tunayategemea sana kwa upatikanaji wa asali. Je, Serikali itatusaidiaje katika kutoa elimu kwa wananchi ili tulinde misitu yetu? Je, Serikali iko tayari kusaidiana nami Mbunge wa Mkoa wa Tabora katika kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi wa Mkoa wa Tabora? Lazima tuokoe misitu ya Miyombo ambayo ni urithi wa vizazi vijavyo.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukataji miti ovyo na uchomaji wa misitu holela likiendelezwa katika maeneo mengi nchini hali ambayo inapelekea ukame na upungufu wa mvua hivyo nashauri Serikali iandae mazingira ya kutoa elimu vijijini ili kunusuru hali hii isiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la gugumaji katika Ziwa Victoria linapaswa lipewe umuhimu wa kutosha katika kukabiliana nalo na isiwe ni mpango wa muda mfupi, ni vyema Serikali ijipange upya juu ya ongezeko la gugumaji katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujengaji holela katika fukwe za Bahari ya Hindi na kwenye baadhi ya Maziwa unaleta uharibifu wa mazingira ambapo maeneo mengine mmomonyoko wa ardhi (*Soil erosion*) unaendelea kukua siku hadi siku. Nashauri Serikali kulifuutilia tatizo hili na elimu kwa umma itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasema nini juu ya kupungua kwa theluji katika Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya bandari ya Itungi (*Itungi Port*) katika Ziwa Nyasa sio nzuri juu ya mchanga unaongezeka na miti inayoendelea kufanya msitu katika bandari hii. Serikali inasema nini juu ya gugumaji katika Ziwa Nyasa – Itungi Port.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kero za Muungano zimekuwa zikipigwa kelele siku zote na ufumbuzi wake ni kero chache sana hivyo naishauri Serikali ufumbuzi wa hili pamoja na kuelekeza kutafuta maoni ya mchakato wa Katiba Mpya, Serikali

iangalie mapendekezo ya Jaji Kisanga na wengine wa Tanzania kuelekea katika muundo wa Serikali tatu, ile ya Zanzibar, Tanganyika na ile ya Shirikisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii muhimu ya kuchangia hoja hii.

Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa hotuba yake nzuri iliyojaa malengo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika baadhi ya maeneo ya hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze Mawaziri wote wa Wizara hii, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao pia uandaaji wa hotuba hadi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji huo, naomba nichangie machache kwa mantiki ya kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la Muungano ni makubaliano yaliyofanywa na Waasisi wetu wa Muungano hapo awali kwa niaba ya wananchi wa pande zote mbili, lakini pia wananchi nao walikubali suala hilo kwa maslahi yao wenyewe na vizazi vya sasa na vijavyo, ni jukumu letu kuuenzi na kuendelea kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza na zinazoendelea kujitokeza siku hadi siku ili kuboresha Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuundwa Kamati Maalum ya kushughulikia masuala ya Muungano na kuendelea kujadiliwa siku hadi siku, ni vema sasa Kamati hiyo kuondoa dhana ya “majadiliano bado yanaendelea” imalize sasa masuala hayo yashughulikiwe kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Sheria ya Kodi kulipia kodi Zanzibar na Bara kwa mara ya pili, hili kwa mujibu wa hotuba hii imesema “Mamlaka ya Mapato Tanzania imetengeneza mfumo mpya ambao unathamanisha sawa viwango vya kodi kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na ikasema kwamba mfumo huo umeanza kutumika tarehe 25/2/2011. Pia mamlaka ya Mapato Tanzania imeahidi kufanya ufuatiliaji wa tathmini ya utekelezaji wa mfumo huu. Napenda kulijulisha Bunge hili Tukufu kwamba hadi sasa suala la kodi mara mbili bado linaendelea. Hivi hiyo Mamlaka ya Mapato imeahidi kufanya ufuatiliaji kwa namna ipi na utekelezaji unaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi kilichopita tulikuwa tunaiomba Serikali kuangalia utaratibu mzuri wa kuruhusu magari yanayotoka Zanzibar kuruhusiwa kutembea Tanzania Bara bila kulipiwa tena na kupatiwa *plate* namba nyingine, tukaambiwa majadiliano bado yanaendelea na hadi leo hii gari inapofika Tanzania Bara

lazima utafute namba nyingine na hiyo katika harakati za kutafuta namba nyingine ndio unapokumbana na suala la kulipia ushuru mwingine ili uruhusiwe kutembea Tanzania Bara. Sasa naomba niiulize Serikali, hivi gari zinazoingia nchini Tanzania kutokea nchini Kenya ni ruhusa kutembea bila ushuru kuliko kutokea Zanzibar, hivi huu ni Muungano wa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu kwamba wananchi wa Zanzibar bado ni maskini sana na hawana soko la biashara na hadi sasa jambo hili linaendelea kuwapa vikwazo ambavyo vinaendelea kuleta mizozo ya kuona kwamba wanadharauliwa, wananyanyaswa, wanatengwa. Serikali inatoa tamko gani kupitia kero hii ambayo bado inaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo ya Jamhuri ya Muungano ambayo yapo Zanzibar, mfano Ofisi ya Makamu wa Rais na Ikulu iliyopo Wete kule Pemba. Ili kutambua kwamba viongozi wanapofanya ziara Visiwani Zanzibar wamefikia katika majengo haya lazima yawekwe katika hali iliyotukuka. Tunaomba kupitia bajeti hii, Ofisi ya Makamu wa Rais iwekewe mdhamini wa Ofisi Zanzibar, watumishi kamili ili tuepukana na kuazima Ofisi nyingine wakati majengo yapo na yamegharamiwa kwa fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ikulu Wete iwekewe Afisa Mdhamsini, watumishi katika vitengo mbalimbali, usafi, bustani na wapishi. Tunakumbuka kwamba Serikali ilitenga fedha nyingi kipindi kilichopita na kufanyiwa ukarabati mkubwa jengo hili pia ununuzi wa thamani lakini bado watumishi hawajaajiriwa kwa maana ya kuwa Ikulu kamili inayostahili kufikiwa na viongozi wa kitaifa. Naiomba Serikali iajiri watumishi niliyowataja ili majengo hayo kuweza kuwa na hadhi inayotakiwa na sio kuazima majengo wanapofika viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano imejitahidi kutoa na kutenga fedha nyingi kuhakikisha kwamba majengo haya yamekuwa yenyeye thamani na kuwa na hadhi ya kufikiwa na viongozi wetu akiwemo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wengineo. Basi isijiweke nyuma Serikali yetu kuhakikisha kwamba majengo haya yamepatiwa watumishi wanaostahili kuwepo katika majengo haya na kugharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo machache, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia kwa bahati mbaya sana nimesahau kuzungumzia mambo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri wa Mazingira anaeleza, *page number 64* na *65* kwamba Serikali ya Wilaya ya Tarime, Mwekezaji Barrick na *NEMC* wanashiriki katika kuleta mahusiano mazuri kwa wananchi. Mahusiano mazuri bila ya waathirika kulipwa fidia kweli hapa tunamaanisha tunachokisema au tunasema tu *by the way?*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia Mheshimiwa Waziri wa Mazingira atueleze ni kwa nini ametoa taarifa ya uongo kwa kusema visima saba vimeshachimbwa ili hali ni visima viwili tu ndio inasemekana vimechimbwa? Je, Mheshimiwa Waziri alienda tu na kupokea taarifa ya mezani au alifanya *physical visit* na kuona hivyo visima au la? Ningetaraji kufikia leo tangu *incidence* ya kuchafuliwa maji basi mwekezaji angekuwa ameshachimba mabwawa ya kutosha katika kila Kata, visima labda viwili au vitatu katika kila kijiji ili watu wapate maji kwani maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Waziri katika hotuba yake kasema kwamba Wizara ya Afya na Mifugo zinaendelea na utafiti ili kujua hali halisi ya binadamu na mifugo iliyoathirika, hii ni fedheha sana kwa Serikali na wananchi wake kwa ujumla. Hivyo basi, naomba Waziri katika majumuisho yake atoe majibu katika masuala haya, la sivyo nitashuka shilingi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na uhusiano mzuri kati ya mwekezaji na wananchi lazima na wananchi washirikishwe. Hii tu ndio njia pekee ya kuweka suluhisho la kudumu na mwekezaji awe tayari kujiweka na kuwa mmoja wa wanajamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite na hoja moja tu ya mifuko ya *plastic* ambayo kwa kiasi kikubwa ni uchafuzi wa mazingira namba moja. Kumekuwepo na mikakati mingi na maelekezo mengi na amri kadhaa wa kadhaa lakini bado mifuko ya *plastic* ni tatizo na imeendelea kuwepo, tatizo ni nini, ni kusimamia sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, ufumbuzi wa kweli na wa kudumu ni kufuta matumizi ya *plastic* na kuwepo kwa mifuko ya karatasi. Nchi nyingi zimechukua hatua, tatizo ni nini tunashindwa kupiga marufuku mifuko hii kwa maslahi ya mazingira ya nchi yetu na ustawi wake? Kama wenzetu wameweza kufanya maamuzi magumu na sisi tunaweza kama hatuna maslahi na biashara ya mifuko hii ya *plastic*. Najua uamuzi utawagusa matajiri na utamaduni wetu tunaogopa kugusa maslahi yao, kuogopa ni kuendelea kuliua Taifa letu. Nashukuru.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchangia kwa maneno, naomba kuchangia kwa maandishi suala la mazingira hususani suala linalomhusu Bwana Robert Mugisha, ambaye kinyume na utaratibu anajenga ndani ya Mto Mbezi (Kawe Dajarani). Mtu huyu alishapewa amri na *NEMC* ya kurudisha udongo ili kuacha mkondo wa mto. Tume ilishaundwa iliyojumuisha watu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Ardhi na *NEMC*, ilithibitisha kwamba, ndugu huyo alikuwa na *documents fake*, ameghushi hati na ramani, akaagizwa asimamishe ujenzi, amekaidi na inasemekana nguvu anaipata Wizara ya Ardhi. Naomba nipate majibu katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la uwepo wa viwanda katika maeneo ya makazi imekuwa ni kero kubwa. Katika Jimbo langu, viwanda vimekuwa vikimwaga sumu

inayopita kwenye makazi ya watu. Watu wa *NEMC* walishakwenda na kuweka zio la kuendelea na kumwaga maji machafu na hakuna kilichofanyika mpaka sasa. Viwanda vinavyotuhumiwa/vinavyolalamikiwa sana ni *Quality Foams, Quality Plastics, Super Meals, Chemi Cotex Industries Ltd, Bidco Oil and Soap Limited* na *MM 1* (Kiwanda cha Nondo). Naomba nipate majibu ya hatua ambazo Serikali itazichukua kuhusiana na viwanda husika. Hali kadhalika kiwanda cha *Tegeta Gas Plant (Songas)* kuna makelele na mitetemo mikubwa sana inayopelekea wananchi kupata matatizo makubwa ya masikio na kuvunjwa/kupata nyufa kwa nyumba za wakazi wa maeneo yanayozunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero kubwa sana ya uchimbaji wa michanga ovyo katika maeneo mbalimbali (katika Jimbo langu la Kawe) hususani katika maeneo mbalimbali ya mito. Kuna tatizo kubwa katika Mto Tegeta, Mto Nakasangwe, Mto Mbezi na kwa kiasi kikubwa sana maeneo ya Changanyikeni na Makongo. Cha kusikitisha katika maeneo yote hayo kuna ushiriki mkubwa sana wa viongozi wa Serikali ya Mtaa pamoja na Vituo vya Polisi vilivyopo katika maeneo husika. Naomba Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) wakati anajumuisha anipatie maelezo ya kina kuhusiana na mkakati wa mahsusni wa kutatua kero hizi Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu nataka kupata taarifa juu ya mikakati ya Wizara hii (Mazingira), kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi katika ufunguaji wa maeneo yote yalivyokuwa ya mkondo wa maji ambayo yamevamiwa na kujengwa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono maelezo yaliyotolewa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 20 kuhusu uchafuzi wa mazingira unaotokana na Kiwanda cha *Mkuani Traders/Azania Wheat Flour Ltd* na utiririshwaji wa majitaka toka Mabibo Hosteli za UDSM kwenye Mto Ubungo Kisiwani eneo la Mabibo. Naomba kujua hatua mahsusni ambazo zimechukuliwa na Wizara ya Mazingira pamoja na *NEMC*. Zimekuwepo taarifa potofu kwamba wanaotiririsha majitaka eneo hilo ni wananchi pekee. Mimi nimetembelea eneo husika nimejionea na nina ushahidi wa picha ukionyesha bomba la hosteli ya UDSM likitiririsha majitaka Mtoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yaliyotolewa kwenye hotuba ya Waziri wa Nchi, Mazingira, aya ya 97, ukurasa wa 64 kuhusu udhibiti wa uchafuzi uliotoka katika mgodi wa North Mara hayaonyeshi hatua thabiti ambazo zimechukuliwa na Serikali. Maelezo ya Waziri kwamba Barick imetekeleza masharti yote, ni vizuri Serikali ieleze bayana ni masharti gani ambayo walipewa na kama masharti hayo yalihusisha fidia ya kijamii na kimazingira kutokana na uchafuzi uliotokea kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA) ya mwaka 2004. Ripoti kamili ya *NEMC* pamoja na ripoti ya Kamati zote zilizoundwa ikiwemo na Bunge kufuatilia uchafuzi husika zitolewe Bungeni. Aidha, maelezo kwamba Wizara ya Afya, ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuwa utafiti unaendelea hayatii matumaini kwa kuwa mwaka mzima umepita toka utafiti uanze. Kwa kuwa EMA inatoa mamlaka kwa Wizara ya Mazingira kuratibu, iweke bayana ni lini utafiti utakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 52 na 53, Waziri ameeleza utekelezaji wa Programu ya Mtandao wa Taarifa za Mazingira Afrika, imeelezwa kuwa kabla ya mwaka wa 2011/2012 taarifa ya Hali ya mazingira ya Jiji la Dar es Salaam itaandaliwa. Naomba kutoa rai kwamba, katika kuandaa taarifa hiyo Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa ikiwemo na Jimbo la Ubungo washirikishwe ili kuchangia maoni na taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ni kwa nini Wabunge hatukupewa nakala ya randamu hii baada ya Hati Kuwasilishwa Mezani. Hii ingeepusha kuuliza maswali ya kutaka ufanuzi ambayo yasingekuwa ya lazima. Mathalani nataka kufahamu mchanganuo wa matumizi yaliyopangwa kwenye Fungu 31, kifungu cha 5001, programu 50, kasma 270800 sababu ya kuongeza toka bilioni 2.7 mwaka 2010/2011 mpaka bilioni nne mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitabu cha Nne cha Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo, naomba kutaka maelezo ni kwa nini fedha za ndani zinapangwa zaidi kwenye ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais pekee badala ya shughuli zinazowagusa wananchi moja kwa moja. Jumla ya fedha zote za maendeleo za miradi ya mazingira Kifungu cha 5001 ni shilingi bilioni moja na laki moja (1,167,014,000) wakati jumla ya fedha za maendeleo za Sekretarieti ya Muungano ni shilingi laki moja na elfu thelathini (133,861,000) kwenye Kifungu 2001. Hivyo jumla ya fedha za miradi ya maendeleo hazifiki hata robo ya fedha za maendeleo za utawala ambapo ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais pekee Jijini Dar es salaam ni shilingi bilioni 3.4 na upande wa Zanzibar ni shilingi bilioni 1.5. Kama tungewekeza fedha nyingi za ndani kwenye kasma 6571 ya EMA tungesimamia Sheria ya Mazingira na kuwezesha mipango ya Wizara, Serikali za Mitaa na jitihada za dhati za kulinda mazingira, badala ya kutegemea fedha za nje zisizo na uhakika kupatikana (bilioni 12.4).

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili, anayeshughulika na masuala ya Muungano na wa Mazingira, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba nzuri lakini vilevile kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Wizara/Ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara sasa umetimiza miaka 47. Wote tumeona na tunatambua umuhimu wa Muungano. Muungano umesaidia kudumisha amani Tanzania na kuchochea maendeleo pande zote mbili. Tusikubaliane na wanaobeza Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Muungano umedumu kwa miaka takribani miaka 47, kuna haja sasa ya kuziangalia changamoto zilizopo na kuendelea kuzitafutia suluhu kama ilivyokwishafanywa kwa kero zilizokwishamalizwa. Pili napendekeza, inaelekea wapo ambao hawatambui tulikotoka, kuna haja ya kutoa elimu ya kina hadi vijijini ili watu wote watambue umuhimu wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu na Watanzania wote, hivyo kila Mtanzania inabidi ajihusishe na utunzaji wa

mazingira. Viwanda vingi kama Viwanda vya Samaki vinavyozunguka Ziwa Victoria, wanachukua maji kwenye Mito na Ziwa Victoria wanayatumia, yanachafuka lakini yanarudishwa kwenye Ziwa/Mito pasipo na ubora unaotakiwa. Hakuna Wakaguzi wa Serikali ambao *constantly* wanapima ubora wa maji haya yatokayo viwandani. Matokeo yake maji yanachafuka, samaki na viumbe hai vingine kwenye maji wanaathirika. Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuyapima maji yatokayo viwandani kila siku ili wasiozingatia viwango wachukuliwe hatua za kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji mingi hawana mifumo ya majitaka, uchafu wa chooni, mahotelini, sokoni unaelekezwa kwenye mifereji ya maji ya mvua na kuelekezwa kwenye Ziwa, Mito au Bahari. Ni lini sasa Serikali itajenga mifumo ya majitaka kila Mji ikiwemo mifereji na *oxidation ponds* ili mazingira yasiendelee kuchafuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi ni kweli yameathiri uoto wa asili, kilimo, hali ya hewa, joto limeongezeka, jangwa linaongezeka, ukame, njaa inaongezeka. Majira yanabadilika, wakulima wamechanganyikiwa, hawajui tena lini walime na lini wapande. Hivyo suala hili inabidi lichukuliwe kwa umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iandae *programme* kabambe, Watanzania wote waelimishwe kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na namna ya kujikinga na athari hizi. Kwa sababu masuala ya mazingira ni mapana sana na bila mazingira bora hakuna maisha, napendekeza Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii, ili kuimarisha uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALI KHEIR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wa Tanzania ni kitu ambacho kinatakiwa kujadiliwa kwa makini zaidi. Muungano wa Tanzania ni silaha ya Watanzania dhidi ya maadui wa ndani na wa nje ya nchi hii. Muungano wa Tanzania umetokana na ridhaa ya Watanzania wenyewe na siyo viongozi wawili yaani Mwalimu Nyerere na Mzee Karume. Mzee Karume waliwaita Wazanzibari katika Uwanja wa *Karume House* mwaka 1964 na kuwaauliza wananchi kama wanautaka Muungano au hawautaki na wote wakakiri kuwa Muungano wanautaka. Mzee Karume alifanya hivyo kwa vile Baraza la Mapinduzi la wakati huo lilikuwa linachaguliwa na Rais badala ya kuchaguliwa kwa kura za wananchi na kwa hivyo uwakilishi wa wananchi usingepatikana. Mwalimu Nyerere aliwasilisha Bungeni pendekazo la Muungano ili kupata ridhaa yao kwa vile wao walichaguliwa na wananchi na kwa hiyo wanawakilisha mawazo ya wananchi wao. Kwa maana hiyo wananchi wa Tanganyika waliridhia Muungano huo kupitia kwa Wabunge wao. Kwa hiyo Muungano wa Tanzania uliridhiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wa Tanzania wa Serikali mbili ni Muungano wa kisiasa na Muungano wa Serikali tatu ni mwelekeo wa Shirikisho ambao ni Muungano dhaifu. Ni kuzigawa nchi na mwelekeo wake ni kama ule wa Urusi alioufanya Goberchev kuigwa USSR. Mwalimu Nyerere alisema ukianza kuigawa nchi

mwisho wake utaigawa hata familia yako, kwa hiyo, Watanzania kuna haja ya kuwa makini na watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuimarisha Muungano kwa kushughulikia kero zilizojitokeza ndani ya Muungano ili uwe imara zaidi chini ya muundo wa sasa wa Serikali mbili, naunga mkono hoja.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara hii, Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *TRA* kulipisha kodi mara mbili limekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Zanzibar. Naiomba Serikali kulitatu tatizo hili kwa vitendo ili wananchi waepukane na usumbufu huo. Tunatambua kwamba Tanzania Bara na Visiwani ni moja kwa mujibu wa taratibu za Muungano, hivi ni kwa nini Ushuru wa Forodha uwe tofauti na Zanzibar? Wazanzibar tunaomba suala hili litatuliwa kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa umma kuhusu Muungano wetu, kabla ya mchakato wa Katiba Mpya ni vyema Serikali iandae mafunzo maalum kwa wananchi kuhusu tafsiri ya Muungano wetu tokea mwanzo hadi kufikia kuungana kwa nchi mbili hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya mikopo ya Elimu, naiomba Serikali kuweka utaratibu mzuri kwa fedha inayopelekwa Zanzibar kwa madhumuni ya kupatiwa mikopo wanafunzi walioko Zanzibar kwani utaratibu wake haufahamiki, wanaopata mikopo idadi ni ndogo na utaratibu wake hauendani kama mikopo inavyotakiwa kutolewa. Naiomba Serikali iweke ufanuzi kupitia Bunge hili, ni fedha kiasi gani inapelekwa Zanzibar kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kupata fursa ya kuchangia japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchangano wangu niuelekeze zaidi katika suala la mazingira. Ni ukweli usiopingika kuwa nchi yetu sasa inageuka kuwa jangwa muda si mrefu, suala hili linajadiliwa zaidi kinadharia na si kivitendo. Suala hili liangaliwe kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Biharamulo Magharibi kuna Hifadhi ya Burigi. Hifadhi hii sasa imegeuzwa kuwa eneo la ufugaji kwa watu wenye fedha na raia wa nje na kufanya suala la mazingira au hifadhi kuwa kinyume chake. Hali hii imepelekea wanyama toka sehemu zao kuanza kuvamia makazi ya binadamu hususani Kata ya Nyakahura na kusababisha uharibifu wa mazao na mazingira kwa ujumla wake.

Kana kwamba haitoshi ukataji wa mkaa kwa ajili ya nishati limekuwa ni jambo la kawaida lakini kasi ya uhamasishaji upandaji miti imekuwa ndogo mno na bado hakuna jitihada mahsusizi za kuleta nishati mbadala kwa ajili ya matumizi haya makubwa ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika maadhimisho mbalimbali wanahimiza upandaji miti, lakini suala hili halina mkakati madhubuti na Halmashauri nyingi unakuta wameandika taarifa nzuri kuhusu misitu lakini Serikali haifanyi jitihada za makusudi kufanya ukaguzi wa misitu hiyo. Fedha nyingi zimekuwa zikitumika kutunza misitu hewa na hivyo suala la utunzaji wa mazingira kutokuwa endelevu. Naishauri Wizara hii hususani wanaoshughulikia mazingira kuhakikisha kuwa wanashirikiana kwa dhati na Wizara nyingine mfano Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Nishati na Madini, Maliasili na Utalii n.k. kwani hawa watu ni wadau wakubwa wa mazingira. Leo hii kuna idadi kubwa ya wananchi wanaochimba madini (wachimbaji wadogowadogo) hawa wanavamia maeneo mbalimbali na matokeo yake ni kuharibu mazingira na kuacha mashimo wazi. Nashauri kuwepo na mchakato wa dhati wa kufanya suala hili la utunzaji wa mazingira kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vyote hususani ngazi za Vitongoji, Vijiji na Kata, kwani Watendaji Wakuu wapo katika ngazi hizo.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) pamoja na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri pamoja na kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nia ya dhati, napenda kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namuombea afya njema pamoja na ulinzi wa Mwenyezi Mungu katika kipindi chote cha utumishi wake kwa umma wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni mdogo sana nauelekeza katika Wilaya yangu ya Morogoro Vijijini. Naomba ikubalike pamoja na kujulikana kwamba upatikanaji wa maji kwa Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, inategemea sana hali ya mazingira katika Mkoa wa Morogoro hususani Wilaya ya Morogoro Vijijini, mazingira katika Milima ya Uluguru yanaendelea kuharibiwa kwa sababu za kiuchumi, ukosefu wa elimu ya mazingira pamoja na kutokuwepo kwa ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua matatizo haya ya mazingira katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, napendekeza yafuatayo:-

(i) Wananchi wa maeneo ya milimani washirikishwe kikamilifu katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo ya mazingira katika ngazi ya vijiji hata ikiwezekana katika vitongoji.

(ii) Ziundwe Kamati za Mazingira ambazo zitapata mafunzo sahihi kuhusu utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.

(iii) Wizara ya mazingira iunge mkono juhudzi za wadau hususani Wabunge wa Morogoro za kuanzisha vikundi vya kiuchumi ambavyo shughuli zake zinachangia sana katika uboreshaji na utunzaji wa mazingira, kwa mfano mradi wa upandaji miti katika Tarafa ya Mkuyuni na mradi wa ufugaji wa wanyama wadogo kama Sungura ili wananchi wasichome misitu kwa nia ya kuwinda Ndezi. Mradi wa ufugaji wa wanyama wadogo kama Sungura umeanza katika Kata ya Kiloka na mradi huu umepokelewa vizuri sana na jamii ila wanaomba wawezeshwe.

(iv) Wananchi wa kijiji cha Kalundwa ambao wanaongoza kwa juhudzi za kutunza vyanzo vya Mto Ruvu wanaomba wasaidiwe kupata mradi wa maji ili waondokane na adha ya kuchimba chemchem katika msitu wa hifadhi ya chanzo cha Mto Ruvu. Kupata mradi huu wa maji kutakuwa motisha kwa hawa wananchi kupanda miti mingi pamoja na kuendelea kutunza hifadhi ya chanzo cha Mto Ruvu.

(v) Naomba sana Wizara ya Mazingira iangalie suala la wananchi kuchimba Dhahabu na Rubi katika Mto Ruvu pamoja na maeneo yanayozunguka vyanzo vya Mto huu. Napendekeza Wizara iangalie uwezekano wa makusudi kabisa wa kuwawezesha vijana wachimba madini waweze kupata miradi mbadala ya kiuchumi ili waache kuchimba madini kila mahali bila mpangilio. Shughuli ya uchimbaji wa madini ndio sababu kubwa ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira Morogoro Vijijini.

Naamini kwamba kama Wizara husika itakubali kushirikiana na wananchi katika eneo hili ni kwamba vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira itashinda kwa mafanikio makubwa. Sisi Wabunge pamoja na viongozi wengine wote wa kuchaguliwa na wananchi tuko tayari kuongeza bidii katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira katika Wilaya yetu, tunaomba ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata wasaa huu ili kuweza kutoa mchango wangu juu ya hotuba zilizotolewa kuhusu Muungano na Mazingira. Aidha, nawapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Samia wa Muungano na Mheshimiwa Huvisa anayesimamia mambo ya mazingira kwa hotuba zao nzuri zilizotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kuzungumzia suala la Muungano. Sipangi nia njema ya Waasisi wetu wa Muungano Wazee wetu Marais Nyerere na Karume kwa wazo lao jema la kuziunganisha nchi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano huu umekuwa na kero nyingi ambazo ni za muda mrefu, sidhani kuwalaumu Waasisi kama kutawezza kuleta tija. Viongozi waliofuata baada yao, ndio walipaswa kurekebisha ama kuzimaliza kero hizi. Mfano mgawanyo wa vyeo katika Serikali ya Muungano hauwatendei haki Wazanzibari, pia Zanzibar wangeweza kuachiwa TRA yao ikajitegemea kuliko hii ya Bara kuimeza ya Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni nini nafasi ya Rais wa Zanzibar anapokuja Bara kwa sababu zamani ilikuwa kama Rais wa Jamhuri akitoka Bara basi Rais wa Zanzibar anakuwa Makamu wa Rais hivi sasa kitu hicho hakipo, nayo hiyo ni kero. Si hivyo tu mtu anaponunua bidhaa Zanzibar huilipia ushuru lakini mara afikapo Bara pia hutakiwa kuilipia ushuru ni kwa nini iwe hivyo, zote hizo ni kero. Ni muhimu wananchi wakawekwa wazi juu ya ni kitu gani hasa kilikuwa ni Muungano na kipi siyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nizungumzie suala la mazingira hususani katika viwanda, uchafu mwingi unaotokana na shughuli za viwanda ni kero kubwa. Mbali na harufu mbaya pia ni hatarishi kwa afya za watu. Kwa mfano, Kiwanda cha Bia cha Serengeti, kimekuwa kikitiririsha maji yenye harufu chafu kiasi kwamba wanafunzi wa shule za Kibasila Sekondari na Kibasila Primary wanaathirika sana na harufu hizi na hivyo wakati mwingine kuathiri mtiririko wao wa kujisomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazalia ya mbu yamekuwa ni kero kila kukicha kutokana na mitaro ya maji machafu maeneo ya Jangwani na hata Muimbili. Tunaitaka Serikali kutokomeza mazalia ya mbu hayo kwa kunyunuzia dawa kwenye mitaro ya maji machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo malori makubwa makubwa yanasisimamia (*Parking*) imekuwa ni kero kubwa kwani barabara zetu za mitaani zinaharibika lakini pia pale yanaposimama (*parking*) ardhi inamomonyoka na mazingira kuharibika kabisa hususani maeneo ya Kigogo (Dar es Salaam) na Tabata Dampo (Dar es Salaam). Maeneo hayo yanatisha, watu wanafanya biashara katika mazingira hatarishi. Tunaitaka Serikali ishughulikie maeneo hayo na Dar es Salaam kwa ujumla.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo yote mawili Muungano na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Muungano, napenda kutangulia kusema kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni Muungano pekee uliodumu hapa Afrika. Miungano yote (Senegal na Gambia na kadhalika) ilivunjika. Muungano wetu umedumu si kwa sababu ni bora, bali kutokana na uongozi mahiri wa Marais wa awamu zote nne. Hii haimaanishi kuwa hakuna matatizo, matatizo yapo na baadhi ni haya yafuatayo:-

- Ulalamishi wa watu wengi kuhusu Muundo wa Muungano. Watu wengi wanataka Muungano wa Serikali tatu.
- Tatizo la kugawana gharama za uendeshaji wa shughuli za muungano.
- Tatizo la kugawana nafasi za kazi katika idara mbalimbali za Muungano.
- Tatizo la kugawana faida ya uchumi wa Muungano.

- Tatizo la shughuli au rasilimali zipi zibaki za Muungano na zipi ziwe za nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na wachangiaji wanaosema sasa ni wakati muafaka wa wananchi kujadili Muungano na changamoto zinazoukabili. Watu waulizwe kama wanataka Muungano au la. Katika kujadili na kutafakari Muungano upi unafaa (baada ya kukubali kuwa na Muungano) ingefaa tuitupie jicho miungano mbalimbali ya nchi, mathalani, Muungano wa Uingereza (*UK*) – unaoundwa na England, Scotland, Wales na Northern Ireland na Muungano au Shirikisho la Marekani na kadhalika. Kule *UK*, Serikali ya Muungano inahusika na shughuli zote isipokuwa michezo. Katika Muungano wa Marekani, Serikali ya Muungano inahusika na mambo jumuifu na ya Kimataifa na Serikali za Majimbo (*States*) zinahusika na mambo yote yanayohusu maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la namna ya kugawana vyeo na faida za shughuli za Muungano linahitaji kutafakari vigezo vya kutumia. Je, tutumie idadi ya watu (Tanganyika Milioni 43; Zanzibar milioni 1.2) au tutumie kigezo cha kiuchumi, mathalan mchango wa nchi katika kugharamia shughuli za Muungano. Hata suala la shughuli zipi ziwe za kimuungano na zipi zibaki za nchi binafsi litatatuliwa baada ya kutafakari na kuchunguza miungano mingine imefanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ni kushirikisha wananchi kwenye ngazi zote ili wakiukubali Muungano pamoja na vigezo vya kugawana nafasi za kazi na faida, kero zote kubwa ziwe zimekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nitakalochangia ni mazingira. Suala la mazingira nitaliangalia kwa kutoa mfano wa mazingira ya Shinyanga. Hivi leo Shinyanga ni mfano mzuri wa eneo ambalo ni nusu jangwa. Lakini shinyanga haikuwa hivi, sisi tukiwa wadogo Shinyanga haikuwa nusu jangwa. Wakati tukikua tulishuhudia mazingira ya Mkoa wa Shinyanga yakiharibika taratibu. Mambo yaliyosababisha uharibifu huu, ni haya yafuatayo:-

- (1) Ufugaji na kilimo visivyofuata taratibu za kuhifadhi mazingira;
- (2) Ukataji miti bila kupanda miti kwa ajili ya kuni au mkaa; na
- (3) Uchomaji wa misitu kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni hatari kwa mazingira ni uchafuzi wa mazingira migodini. Uchafuzi huu unasababishwa na Zebaki inayotumiwa na wachimbaji wadogo wadogo, kadhalika husababishwa na Sainaidi inayotumiwa na makampuni makubwa. Hatua za haraka zinahitajika kuchukuliwa kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, Serikali imeshachukua hatua muhimu za kisera na kisheria.

- Sera ya Ardhi ya 1995
- Sera ya Mazingira ya 1997
- Sera ya Misitu ya 1998
- Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, utekelezaji wa sera na sheria unasuasua. Kwa maoni yangu, udhaifu uko kwenye ngazi zote Wizarani, Mikoani, Wilayani na kadhalika. Udhafu upo katika usimamizi, ufuatiliaji na tathmini katika miradi mingi iliyopo hasa ile ya upandaji miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, napendekeza kuwa, uharibifu wa mazingira utangazwe kuwa ni janga la Kitaifa. Mpango mkakati wa upandaji miti kwenye maeneo yaliyo nusu jangwa kama Shinyanga uandaliwe. Bajeti iongezwe ili vyombo vy ya utekelezaji viimarishwe kwenye ngazi zote. Ngazi muhimu ya utekelezaji iwe kijiji, wananchi washirikishwe. Serikali ingeanza kwa kutoa semina elekezi kwa Madiwani ili wao watoe semina elekezi kwa Viongozi wa Vijiji na Vitongoji kuhusu utekelezaji wa Sera ya Mazingira.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa mazingira unazidi kuongezeka kutokana na hatua mbalimbali za maendeleo ya binadamu. Nchi zilizoendelea zimekuwa na uharibifu wa mazingira kutokana na maendeleo ya viwanda. Lakini kwa nchi zinazoendelea hasa za ulmwengu wa tatu, mambo ni tofauti. Uharibifu mkubwa unatokana na uharibifu wa misitu ya asili ambayo ilitunza vyanzo vy maji. Hii inatokana na Serikali kutoweka mikakati ambayo ingeweza kutoa njia mbadala ya kuzuia ukataji ovyo misitu yetu. Yapo baadhi ya mambo ya msingi ya kuyaangalia mfano, ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa, uchimbaji wa madini, kilimo cha kuhamahama kwa kukata miti ovyo. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kutafuta nishati mbadala kwa matumizi ya nyumbani, badala ya mkaa lakini kama hilo halitawezekana misitu yetu itaendelea kufyekwa. Wachimbaji wa madini wanaacha mashimo makubwa ambayo yanaendelea kuathiri mazingira yetu. Napendekeza Serikali iweke sheria ya kudhibiti wachimbaji wa madini wasiache mashimo wazi, iwe ni moja ya sharti la kuruhusiwa kuchimba madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi unaofanywa na NEMC juu ya kuruhusu shughuli fulani ifanyike au isifanyike wasiwe na upendeleo, hasa pale inapoonekana na shughuli fulani ifanyike yenye maslahi kwa uchumi wa Taifa, huwa mara nyingi mambo yanarahisishwa, hii haitasaidia katika kutunza mazingira badala yake ushauri wa namna ya kufanya mradi wowote uzingatie ushauri uliotolewa na *NEMC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la kutoa matokeo ya uchunguzi wa uharibifu wa mazingira, kwa kuchelewa kupita kiasi. Ni vema Serikali ikahimiza utoaji wa uchunguzi mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NEMC* ni chombo kilichoundwa kwa ajili ya kusaidia ustawi wa nchi na kuleta maendeleo, lakini mahali pengine inakuwa kinyume kwani wataalam wa uchunguzi wa mazingira huhitaji gharama kubwa mno. Hii imetokea

Mbarali wakati wa uchunguzi wa eneo la kuboresha banio la maji ya kutegwa Igomelo. Wananchi wa Kata za Rujewa, Ubaruku, Songwe Imalilo na Vijiji vya Isunura, Igawa, Igunda, Vikaye, Invalanje na Ikanutwa wameendelea kukosa maji ya uhakika kutokana na urasimu uliofanywa na wataalam wa mazingira. Nashauri Serikali iwe karibu na chombo hiki kisiwe kikwazo kwa shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuangalia uharibifu wa mazingira tusioneane aibu pale ambapo taasisi za Serikali zinapojiingiza kwenye vitendo vya uharibifu wa mazingira. Mfano, Wizara ya Maliasili na Utalii wamekuwa wakichoma moto maeneo ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, miti mingi huungua, wadudu, wanyama wasioweza kukimbia moto, mazalia ya ndege huharibiwa. Mfano mwagine, ni eneo la Ihefu mwanzoni mifugo ilikuwa inaharibu nyasi ambazo ndizo zilikuwa zinahifadhi chemichemi kwa kutengeneza sponji iliyotokana na mrundikano wa nyasi kwa miaka mingi kiasi kwamba wanyama kama tembo, viboko walikuwa na uwezo wa kupita juu bila kutumbukia na maji yakiwa chini. Lakini uharibifu huo unaendelea baada ya eneo hilo kuwa chini ya *TANAPA* kwa kuchoma moto wakati wa kiangazi na husababisha nyasi zote kuungua na hivyo kuharibu mazalia ya ndege wengi wanaoishi kwenye eneo hilo oevu. Nashauri Serikali kuzuia kabisa kuchoma eneo hilo ili chemichemi ziendelee kuhifadhika.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Makamu wa Rais kwa kazi njema anayotufanyia, nawapongeza Mawaziri wote wa Mazingira na Muungano kwa juhudu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nizungumzie kero za mazingira. Naomba mradi maalum kwa kupanda miti kuzunguka Ziwa Nyasa ili lisikauke.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, zile kero zote za Muungano zishughulikiwe mapema na haraka ili maneno maneno ya wasioutakia mema Muungano wetu yaishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, Tabata Bima kuna maji taka mengi yatiririkayo kutoka maghorofani na kusambaa katika majumba yote yaliyo chini ya maghorofa hayo. Tunaomba Waziri, tafadhalii, uende ukaone ili kuwanusuru wakazi wa Tabata Bima.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la mazingira (*Carbonate Credit*- Biashara ya Hewa Ukaa). Tangu Februari 2008 nikiwa *DC Kilolo Iringa* tilitayarisha Andiko la Hewa Ukaa kwa misitu ya kupanda na asili ili tufaidike na biashara ya hewa ukaa (*Carbon Credit*) Mkurugenzi alikuwa Erick Muguruse na Mkurugenzi Msaidizi Richard Muyungi (alifika na kukagua misitu Kilolo). Mpaka sasa Kilolo haijafaidika. Wilaya ya jirani Mufindi Kampuni ya *Green Resources* wamefaidika. Wizara itoe msukumo ili pia wananchi wa Igalula Tabora wafaidike kwani wamehifadhi misitu mingi ya asilia na ni vifyonzo (*carbon sinks*) vya hewa Ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kupimia Hewa Chafu Mlima Kilimanjaro (*Air Pollution Monitoring Facility*). Tulipokuwa EAC Mei 2011, Baraza la Mawaziri wa Sekta za Uchumi tulijadili pia uwepo wa Kituo hicho Mlima Kenya. Ni vema pia Kituo hicho kikawepo katika Mlima Kilimanjaro. Wizara yako na yangu tushirikiane ili kituo hicho pia kianzishe Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ni suala mtambuka na lina uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya viumbe hai akiwemo binadamu. Kwa msingi huo suala la mazingira ni suala tete kabisa, mazingira yamekuwa yaharibowi na mharibifu mkuu ni binadamu. Kwa maana hiyo uharibifu wa mazingira unatokana na shughuli za binadamu katika kutafuta mahitaji ya msingi au katika harakati zake za maendeleo. Bahati mbaya hatua za kukabiliana na uharibifu wa mazingira hazilingani kabisa na umuhimu au hatari kubwa itakayotukabili baada ya mazingira kuharibowi katika hatua ya mwisho kwani itakuwa ndiyo mwisho wa maisha yetu na viumbe wengine. Hii ni changamoto kubwa kwa binadamu wa leo. Binadamu aliyeelimika, anayeandaa bomu huku akijua na hachukui hatua madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara makubwa katika uharibifu unatokana na mambo yafuatayo, ufulgaji mifugo mingi kuliko uwezo wa ardhi yetu na tunaogopa kulishughulikia hilo, hili ni hatari kuliko vyanzo vya uharibifu vingine kwani *Decision makers* wamefuga mifugo mingi, *Politician* wamefuga mifugo mingi na Viongozi wa Serikali wamefuga mifugo mingi na sasa wanashindwa kudhibiti mifugo huku wakijua athari zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wafugaji mifugo yao imesababisha vyanzo vingi vya maji kupotea kwa sababu wanakata miti ovyo na wanachoma miti ovyo. Wingi wa mifugo wala haujakuwa msaada kwa mfugaji zaidi ya kumfanya mtumwa wa mifugo yake. Wafugaji wametawanyika huku na kule na Serikali imeshindwa kuwadhibiti, wanaendelea kuharibu miti, mito, ardhi na kuzalisha migogoro ambayo wangeelimishwa na pakawepo na sera ya kuwaelimisha wangeleta manufaa kwa Taifa na kwa kuwekeza katika mambo ya msingi ikiwa ni pamoja na elimu.

MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano umekuja kwa nchi mbili ya Tanganyika na Zanzibar kuungana na wakati huo kila nchi ilikuwa na Serikali yake na waliendelea kivyake vyake. Lakini kilichoshangaza Serikali ya Tanganyika ilijikita katika Serikali ya Muungano ambayo haistahili, kwani mambo ya Muungano yalipaswa kuwa na Serikali yake na yasiyo ya Muungano yajikite katika Serikali mbili za nchi Tanganyika na Zanzibar. Ili Muungano uwe mzuri na bila ya upande mmoja kulalamika, sasa ni wakati muafaka wa kubadilisha mfumo wa Muungano

na kuifanya Serikali ya Tanganyika kutohudumiwa na Serikali ya Muungano. Kwa Lugha nyingine kuwe na Serikali tatu, ya Tanganyika, Zanzibar na Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu Akaunti ya Pamoja. Kero zote za Muungano zinabebwa na Kamati inayoshughulikia kero za Muungano. Kuna tatizo gani leo Akaunti haikufunguliwa? Kuna kigugumizi kipi! Hapa pana jambo na halitakiwi kuzungumzwa. Kuna haki na mafao ya Wazanzibar yanabanwa na Serikali ya Muungano. Kama hayabanwi kwa nini akaunti haifunguliwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, atapokuja kufanya majumuisho tafadhali alieleze Bunge sababu hasa ya kutofungua akaunti mpaka sasa, kwani vikao vingi vimefanywa lakini matunda bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mikataba ya Kimataifa. Serikali ya Muungano kuizua Zanzibar kujiunga na mikataba ya Kimataifa mfano *OIC* wakati ambao Rais wa nchi alikuwa Mheshimiwa Salmin Amour Juma, aliezwa ajitoe au nchi ijitee na akafanya hivyo. Zanzibar ni nchi na inayo haki ya kujiunga na kuamua itakavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu Rais wa Zanzibar kufanywa mjumbe wa Baraza la Mawaziri. hapa Rais wa Zanzibar ameteremshwa hadhi yake akiwa Zanzibar ni Rais, akija Bara ni Waziri, hamuoni kwamba mnambhalilisha? Ni vizuri arejeshewe hadhi yake kama zamani. Huyu ni Rais na ana nchi anaiongoza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Makamu wa Rais kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni katika Miji yetu uchafuzi wa hali ya hewa umekuwa mkubwa sana. Kwa kiasi kikubwa uchafuzi huu unatokana na Moshi utokanao na viwanda pamoja na magari mabovu. Sijui ni kwa nini, kwa mfano, magari mabovu yasiondolewe barabarani ili kupunguza hali hii? Sambamba na hilo wenye viwanda wakaagizwa kuweka vifaa maalum vya kupunguza moshi unaotoka katika viwanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuchangia suala la uchafu Mijini. Kwa maoni yangu suala hili linatokana na uzembe. Tunao viongozi ngazi ya Mitaa, kwa nini wasitunge Sheria Ndogo kuwalazimisha wakazi kuwa na vyombo vya kudumu vya kuhifadhiwa taka wakati zikisubiriwa kuchukuliwa? Hivi sasa utakuta mifuko michafu iliyokwishatumiwa ambayo nayo ni uchafu mbele ya nyumba. Tena tabia ya kuanzisha madampo ya taka mitaani nayo inaweza kuondoshwa. Nadhani uchafu wa Mijini hasa unatokana na utashi wa wananchi kukataa uchafu na pia Viongozi wa Mitaa kushindwa kusimamia sheria zilizopo kikamilifu. Naishauri, Wizara kutoa maagizo ya kuundwa kwa Kamati Ndogo za Usafi katika kila Mtaa na Kata ambazo zitasimamia suala la usafi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa hapa pia niongelee kuhusu magari ya kuzoa taka. Magari yenyewe nayo ni taka, mengi ni mabovu na humwaga taka kila

mahali yanapokuwa yakielekea dampo. Kila mtu hata viongozi wanaona. Je, kwa nini hakuna viwango maalum na aina ya magari ambayo yanapaswa kutumika katika kuchukua taka? Nadhani tumekuwa dhaifu sana katika usimamiaji. Kutokana na hayo taka zinatupwa ovyo hata zile za hatari kama madawa na mfano ni zile ambazo zilitupwa mwanzoni mwa mwaka katika eneo la Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni uchafu katika kilele cha Mlima Kilimanjaro. Pale kileleni hakuna vyoo, kwa sababu hiyo watalii na wapanda Mlima hujisaidia ovyo na kutupa taka ovyo kileleni. Mlima unatuingizia fedha nyingi, kwa nini Mamlaka husika zisijenge vyoo pale kileleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika Theluji ya Mlima Kilimanjaro inayeyuka. Maji yatokanayo na kuyeyuka kwa Theluji hiyo yametengeneza mito ya chini ambayo inamwaga maji yake katika nchi jirani ya Kenya. Naishauri Serikali kufanya utafiti ili kupata mbinu za kudhibiti uyeyukaji wa Theluji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukataji miti ovyo. Hili ni janga, tani nyingi za kuni na mkaa zinavunwa kila siku. Tunazungumza habari ya umeme vijiji, *Biogas*, makaa ya mawe, mkaa utokanao na bura (vumbi la mbao) na kadhalika tafiti zimeshafanywa kwa nini zisisambazwe? Miti yetu ya asili inamalizika kwa kuvunwa ovyo kwa ajili ya mkaa na mbao. Miti maarufu kama Mininga, Mipochi, Mirule na kadhalika inamalizika. Naishauri Serikali, pamoja na jitihada za kupanda miti, msisitizo tuweke katika kuandaa vitabu kwa ajili ya kuineza miti yetu ya asili ambayo inaelekeea kupotea au imeshapotea kabisa. Nashauri pia Wizara hii ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Maliasili ili kudhibiti vibali vya uvunaji wa magogo na kuweka masharti ya kupanda miti ya aina wanayotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya Mazingira naipongeza kwa kuwasilisha Bajeti nzuri. Tumekuwa tunaongea kuhusu hifadhi ya misitu yetu ya asili, kupanda miti tumehamasisha kila mwaka na zawadi kutolewa kwa Wilaya zinazofanya vizuri. Tatizo kubwa ni kushindwa kusimamia Sheria tulizoziveka kuhusu kuzuia uharibifu wa misitu yetu. Tunasema panda miti mitatu na kata miti mmoja lakini hii haitekelezeki kwa kuwa hakuna nishati mbadala vijiji, wananchi wataendelea kukata miti na kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilete jibu la namna wananchi watakavyokuwa na nishati mbadala. Napendekeza wakati tunasubiri nishati mbadala tuseme basi panda miti 50 kata mmoja na Serikali ya vijiji itunge Sheria Ndogo ambapo kila mwananchi suala la kupanda miti liwe la lazima na siyo la hiari kama ilivyo sasa kwa Taifa lenye umri wa miaka 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchoma mkaa. Leseni zitolewe kwa mtu anayechoma mkaa kwa miti aliyopanda yeye au avune kwenye msitu wake lakini si wa miti ya asili. Serikali itoe adhabu kubwa sana eneo hili kwani ndilo linavuna miti ya asili na kwa kasi

kubwa. Ukipita barabara kuu kwa kweli ni aibu, kama kuna Idara iliyokasimiwa kusimamia hili utaona mamia ya magunia yamepangwa kama vile ni ruksa ya biashara hiyo na hakuna hatua zinachukuliwa mfano, Mkoa wa Morogoro, Dodoma, Singida na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchoma mashamba. Eneo hili nalo pamoja na Sheria za kuomba kibali kwa Mwenyekiti wa Kijiji lakini bado kuna kasoro kubwa kuhusu kudhibiti uchomaji mashamba ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Hoteli karibu na Maziwa Makuu. Kama Ziwa Victoria au Bahari kuu ya Hindi zipo Hoteli nyingi kama Hoteli Tilapia pale Mwanza na zinginezo zimejengwa ndani ya mita 60 kutoka kingo ya Ziwa Victoria kinyume na Sheria. Lakini Wizara yako imeshindwa kuchukua hatua inayotakiwa ndani ya Sheria. Wakati unajumuisha Hotuba hii nitafurahi kama ortalizungumzia hili ili watu wengine waogope kujenga ndani ya mita 60 zilizopo kwenye Sheria ya Kutunza Rasilimali za Maji na Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzaji wa vyanzo vya maji. Tatizo kubwa katika eneo hili ni kilimo cha kiangazi. Wananchi wanalima ndani ya mita 60 isiyoruhusiwa na wale tuliwapa madaraka kukataza kilimo hicho wameshindwa na hasa wanasiwa hawawezi kuwazuia wapiga kura kwa hofu ya kutochaguliwa. Hapa tunahitaji maamuzi magumu, vinginevyo mito yote itakauka na athari yake ni kubwa, nchi yetu itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumzi ya plastiki. Nashauri Serikali ichukue maamuzi magumu kwa kuja na kauli ya kuzuia kabisa matumizi ya plastiki kama vifungashio vya bidhaa mtu akienda dukani au sokoni. Nchi ya Rwanda imezuia kabisa matumizi ya plastiki. Ukipita *Airport* umebeba bidhaa ndani ya plastiki umezuiwa kupita na nchi ile mazingira yake ni safi sana. Kama nchi ndogo kama Rwanda imefanikiwa kwa nini tusiige mambo mazuri kama hayo? Wakati unahitimisha Hotuba yako iridhie “Kauli ya kuzuia kabisa vifungashio vya Plastiki” na kama somo halieleweki nendeni Rwanda mkajifunze mbinu wanazozitumia.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, suala la mafuta na Madini kutokuwa ya Muungano. Ni kwa nini suala la mafuta, kwa upande wa Zanzibar na madini kwa upande wa Tanzania Bara sio ya Muungano, wakati kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi sote ni nchi moja na ni kwa nini makubaliano waliyofanya waasisi wa Taifa letu kwenye Muungano, waliyatenganisha masuala hayo. Hatuwezi kuzungumzia Muungano bila haya kuzingatiwa. Naomba ufanuzi ili Watanzania wafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, suala la taarifa za maeneo yote ambayo yameathirika na ukame. Serikali inapaswa kutueleza maeneo yote tata ambayo Serikali kwa jitihada zake imeshindwa kupata ufumbuzi wa kudumu na nini sababu za kushindwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, suala la Mazingira hususan katika mmomonyoko wa udongo uliokithiri katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Mbozi Magharibi. Maeneo hayo ni kama Bonde la kutoka Yala, Kata ya Chitete kwenda Kanyala, Kata ya Chilubumo kupitia Mto Momba, barabara kuu itokayo Ntungwa, kupitia Chilulumo, Vijiji vya Mweniemba na Itelefya, kwenda Mkulwe na kuishia Kamsamba. Barabara hii inasumbuliwa na mmomonyoko wa udongo ambao haujapatiwa suluhisho. Sasa Serikali ieleze kiasi gani cha fedha kinahitajika katika utatuzi wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Napenda kuipongea Serikali kwa kuandaa mwongozo rahisi wa namna ya kuandaa mipango ya usimamizi wa mazingira ya kisekta na Serikali za Mitaa. Ni imani yangu kwamba, elimu zaidi itatolewa kwa wananchi ili waweze kuandaa mipango ya usimamizi wa mazingira. Aidha, naipongeza pia Wizara kwa kubuni mradi wa vijiji mfano, vya hifadhi ya mazingira. Ni imani yangu mgawanyo wake utafanyika kwa usawa na uwiano, ili Mikoa mingi iweze kunufaika.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kwa uwasilishaji wake mzuri. Pia napenda kutoa shukrani kwa Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Dokta Terezya Luoga Huvisa na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Hotuba nzuri inayosomeka na kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie kwenye hifadhi ya mazingira. Masuala ya mazingira si masuala ya Muungano lakini tunapokuwa Kitaifa masuala yote yanajadiliwa Tanzania. Kwa hiyo, kuna *documents* nydingi za Kitaifa zinazohusiana na hifadhi ya mazingira zinakuwa zinatayarishwa hapa Tanzania. Ukiziangalia *documents* hizo kwa undani utaona kuwa Zanzibar haionekani sana kwenye *documents* hizo kwa mfano, *document* ya *NAPA (National Adaption Programs of Action)* ambayo ukiangalia utagundua haijawakilisha Zanzibar hata kidogo. Pia hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Rais, Tanzania inaandaa mkakati wa Kitaifa wa mabadiliko ya Tabia nchi (*Climate Change Strategies*). Hadi hivi sasa hakuna ushirikishwaji wowote kutoka Zanzibar juu ya mkakati huo. Ukizingatia kuwa Mkataba wa Kitaifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio imeridhia kwa niaba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kumejitokeza aina mpya ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na bidhaa chakavu za umeme na elektroniki (ambapo kwa jina la kitaalam zinaitwa *e-waste*). Bidhaa hizi zinatokana na TV, radio, kompyuta, majokofu na vifaa vingine vya umeme ambapo kemikali zilizomo ndani ya bidhaa hizi ni sumu kali na

ni hatari kwa afya za watu na mazingira. Hivi sasa takriban nchi nyingi duniani zimeshajiwekea mikakati imara kukabiliana na changamoto hiyo. Mheshimiwa Waziri, Wizara yako imejiwekea mikakati gani kukabiliana na changamoto hizi za kimazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kwa uwasilishaji wake mzuri na wa kutia moyo. Lakini napenda kumshukuru Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Dokta Terezya Huvisa na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Muungano limekuwa kero kwa sababu moja tu. Maamuzi yanapotolewa na viongozi yanakuwa hayawafikii wananchi. Hivyo, utekelezaji wa Muungano unakuwa kama hauonekani. Pia unatokana na wananchi wengi hawafahamu Katiba ya Jamhuri hivyo inazungumza nini kuhusu Muungano. Lakini kweli kama Serikali ina dhamira ya kweli hivyo ni lazima ihakikishe utekelezaji wa masuala ya Muungano unatimizwa kikamilifu na kuwekwa wazi kwa kila raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi naunga mkono Muungano wetu, uwepo na udumu kama sera ya Chama changu cha Mapinduzi inavyoeleza. Tumekuwa tukifaidi matunda ya Muungano kwa kila hali, hivyo, udumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero zilizopo kama, *TRA*, gawio la fedha za Muungano, ajira za Muungano, nafasi za viongozi wanapokwenda misafara na pia Elimu ya Juu na mengineyo vitekelezwe kwa mujibu wa makubaliano ya Muungano. Suala la Zanzibar kupewa nafasi za Ubalozi pia lifanyiwe kazi kwani Ofisi za Ubalozi zote Wazanzibar ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Mazingira na Muungano pamoja na wataalam wao kwa kuandaa Hotuba hii na kuleta Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu suala la mabadiliko ya tabia nchi. Nchi zote duniani kwa sasa suala la mabadiliko ya tabia nchi ni *agenda* muhimu sana. Pamoja na kuwa hapa Tanzania tumeanza kuchukua hatua za kushughulika na tatizo hili lakini bado hatujaweka mikakati mizuri ya kupambana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana Serikali kuendelea kubariki nishati ya mkaa kama nishati kuu kwa Watanzania walio wengi. Kila mmoja anaewela uchomaji wa mkaa umekithiri na hata Serikali haina takwimu sahihi ya idadi ya miti inayokatwa kwa siku kwa ajili ya mkaa. Serikali imechukua juhudhi gani kupatia wananchi nishati mbadala kwa nishati ya kupikia? Ipo sera ya kila Mkoa kupanda miti katika maeneo yao. Kuna utaratibu gani wa uhakika wa kufuatilia kuona kweli miti inapandwa. Takwimu, zilizopo kwenye jedwali (kiambatanisho Na. 1) katika kitabu cha Hotuba ya Waziri inaonyesha

kabisa miti mingi inayopangwa kupandwa haipandwi na hata ile inayopandwa mingi inakufa. *Data* hizi ni za Ofisini ukienda kwenye *ground* uhalsia ni tofauti. Kuna kila sababu sasa Serikali kuajiri Maafisa Mazingira kuanzia ngazi ya Kata ili waweze kufanya *follow-up*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana (Bajeti ya mwaka 2010/2011) Serikali iliongeza ushuru kwenye mifuko milaini (*plastic bag*) ili kupunguza matumizi ya mifuko hiyo ambayo *disposal* ni ngumu sana. Bajeti ya mwaka huu 2011/2012, ushuru unaondolewa. Kwa maana hiyo hali ya miaka ya 2002 – 2008 ambapo mijini *plastic bags* zilizagaa leo tunairejesha tena ili kuharibu mazingira yetu. Ni kwa nini Serikali haina mipango endelevu ya kupambana na uharibifu wa mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *programme* gani ya kutoa elimu ya mazingira kwa wakazi wa mijini wanaoziba mifereji ya maji machafu kwa kutupa takataka Dar es Salaam inaongoza. Kuna utaratibu gani kuwabana Makampuni yanayochimba kokoto na mawe katika maeneo mbalimbali na kuacha mashimo makubwa bila kuyafukia? Mikataba yao inasemaje pale wanapomaliza kazi ya kuchimba mawe au kokoto? Huu ni uharibifu mkubwa sana wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye viwanda vyetu hapa nchini bado hakuna mikataba mizuri ya kuhakikisha majitaka yanayotokana na shughuli za viwanda hivyo hayaharibu mazingira. Maji machafu yanayotiririka mitaani na tumeshuhudia wananchi wanaoishi jirani na viwanda wanavyolalamika na tumeona kwenye vyombo vya habari kama vile TV. Huu ni udhaifu mkubwa kwa Serikali na ni muda muafaka sasa Serikali, Baraza la Mawaziri kuandaa *programme* ya kuvitembelea viwanda vyote na kukagua mifumo yao ya majitaka ili kuondoa usumbufu uliopo na uharibifu wa mazingira unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Environment Impact Assessment* ni muhimu sana kwa kila mradi unaotaka kuanzishwa popote. Kitendo cha *EIA* kulipiwa na mwekezaji yaani gharama kutolewa na mwekezaji ni tatizo kubwa. Hili linasababisha miradi kuanzishwa kwa kufuata matakwa ya *Investor*. “Mlipa zeze ndiye mchagua wimbo”. Lazima Serikali iangalie utaratibu wa kuwezesha hizi tathmini kufanyika *then* mwekezaji atalipa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mikopo katika Muungano wetu. Mfumo wa ukopaji na ulipaji madeni hadi hivi sasa unasimamiwa na Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada, Na. 30 ya mwaka 1974 ambayo ilirekeblishwa mwaka 2004. Kwa bahati mbaya au kwa makusudi hata baada ya marekebisho hayo bado Mamlaka ya kutekeleza Sheria hiyo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika (au Tanzania Bara) iliyovaa koti la Muungano na Mheshimiwa Waziri hii sio haki kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa haina na haiwezi moja kwa moja kupata dhamana, kufutiwa madeni au kupata misaada moja kwa moja bila ya kupitia Jamhuri ya Muungano, mtindo wa SMZ kutumia mikataba ya ndani (*on lending agreement*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu Mikopo, Dhamana na Madeni. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri (ukurasa wa 7) ameeleza mambo saba ambayo yanalamikiwa sana na zaidi upande wa Zanzibar na katika Hotuba yake ameeleza kufanyiwa marekebisho na kuendeleza miradi ya pamoja ya kiuchumi na kadhalika. Hoja hapa haya mambo yote yamezungumzwa miaka mingi na bado hayajatekelezwa. Hivyo basi, Mheshimiwa Waziri atuhakikishie muda maalum (*timeframe*) na atufafanulie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyeo vikuu upande mmoja wa Muungano. Katika Bunge hili niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maswali ya papo kwa papo kuhusiana na mfumo huu wa Muungano ambapo nafasi nyeti za Jeshini, Polisi mara zote zinateuliwa kutoka Tanzania Bara. Hivyo, Zanzibar haistahiki kuwa na vile vyeo vitatu vya juu vya Jeshi la wananchi (JWTZ) au *IGP*? Je, ni kwa nini katika Hotuba yako mambo haya hayajaainishwa? Ofisi ya Makamu wa Rais italitatu vipi jambo hili? Namwomba Mheshimiwa Waziri aliahidi Bunge hili haya marekebisho ya vyeo yatarekebishwa lini? Hali kadhalika Makao Makuu ya Jeshi, Usalama, Uhamiaji na Polisi kwa nini yote yawe upande mmoja tu wa Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inayotumika Zanzibar ni ya Tanzania nzima. Uchumi wa Zanzibar ni mdogo na Watanzania Bara ni mkubwa kiasi. Je, endapo Bajeti ya Zanzibar iliyopitishwa hivi karibuni ikaharibiwa kutokana na kuanguka kwa shilingi ambayo *BOT* ndiyo inayo-regulate. Je, Serikali ya Jamhuri italipia tofauti kwa SMZ?

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na wafanyabiashara wa Zanzibar (bidhaa za kawaida na magari) kutozwa kodi mara mbili limeshatatuliwa na yanayotokea ni utendaji wa baadhi ya maofisa wa *TRA*. Namuomba Mheshimiwa Waziri akifafanulie watendaji wa *TRA* wanafanya kazi kwa maelezo au Sheria? Kama ni Sheria, je, Sheria inayoruhusu “*double taxation*” imerekebishwa”

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini naomba kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mazingira. Iko haja ya kila Halmashauri ya Wilaya hapa nchini ikapewa “viriba” vya kuoteshea miche ya miti ili kuotesha katika bustani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Muungano. Wageni kutoka nje ya nchi yetu wanapoingia Tanzania kupitia uwanja wa ndege wa Dar es Salaam wanapita na pasi zao kugongwa mihuri na Uhamiaji Tanzania. Mgeni huyo huyo akitoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar kwa Boti au Ndege anakutana na Uhamiaji Zanzibar wanagonga muhuri wa kuingia na kutoka Zanzibar. Mgeni anapoondoka nchini kupitia *KIA* anagongewa tena muhuri na Uhamiaji. Sasa jamani *is this called for?* Mbona Idara ya Uhamiaji ni moja!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Hotuba hii. Ninayo machache tu ya kutaka kujuua masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujuua habari za Muungano, hivi kuna tatizo gani kwa Wanzazibari? Kulalamika kila mara kwamba wanapunjwa au kuonewa kwa mambo mengi? Je, kuna gawio lolote ambalo hawapati na kama hawapati, ni kwa nini? Pamoja na maswali hayo naomba kujuua yafuatayo:-

- (a) Ni asilimia kiasi gani Zanzibar inapata gawio toka Serikali Kuu?
- (b) Ni kiasi gani Zanzibar inapata kama msaada toka Serikali Kuu na ni kwa nini wapewe?
- (c) Je, kuna asilimia ngapi Zanzibar inachangia kwenye mfuko au pato la Taifa?
- (d) Mheshimiwa Naibu Spika, je, kama vyote hivyo wanapata, tatizo ni nini? Kama inaonekana wanapunjwa si wapewe waache kulalamika, kwani inachosha sana na inatutia unyonje wengine tunaonekana kama wakandamizaji, mimi sipati raha wala amani moyoni. Kama hakuna madai yoyote, waulizwe wanataka nini ama la sivyo, bora ndoa ivunjike kuliko kuendelea na ndoa isiyo na amani ndani ya nyumba. Naomba Serikali ifanye haraka kutatua hilo. Tumechoka kusimangwa mara Makamu, mara Serikali tatu, vyote vinatudhalilisha sana. Kwani hawakuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kwa nini Baraza la Wawakilishi linateuwa Wabunge kuja huku na hali kuna Wabunge wa Majimbo? Mbona sisi Wabunge wa Bara hatuendi kwenye Baraza la wawakilishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mazingira, naomba Sera ya Mazingira ifanye kazi isibakie kwenye maandishi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ishirikiane na Wizara ya Madini na Nishati kupeleka Umeme wa gharama nafuu vijijini na hata mijini, ili watumia kuni na mkaa wapunguze kukata miti. Pia majiko ya umeme yawe bei karibu na jiko la mkaa ili wengi wanunue hata wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Mazingira anisaidie kufuatilia uliokuwa msitu wa Ushora Ndago hadi Urughu (Mirungu) eneo la Magereza ya Ushora, Tarafa ya Ndago, Wilaya ya Iramba, Singida. Msitu huo naufahamu, nikiwa mdogo kulikuwa hakupitiki, wanyama wakali wakiwemo simba, chui, tembo na kadhalika waliishi kule, lakini tangu Magereza ilipojengwa kule kwa kilimo, lakini mara baada ya kusitisha shughuli za kilimo, waliingia katika shughuli za kukata mkaa, kwa sasa inaniuma sana kwani hata ile miti ya asili inayochukua muda mrefu kukua wamekata na

nitaomba tupatiwe fidia kwa ile miti iliyokatwa, ni ya matunda ya asili inaitwa mipana, twende tukafanye tathmini ili vijiji husika vilipwe fidia kwani wao wamefanya biashara. Waziri toa tamko wasitishe, okoa eneo hilo, inaniuma, Magereza waache kukata ile miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kuhusu wakata mkaa. Kwa uzoefu nilionao wananchi wengi wanaojishughulisha na kukata mkaa, imekuwa ndio shughuli pekee inayowaingizia kipato kinachowasaidia kuwasomesha watoto na kujikimu. Hivyo, naomba Waziri, awaangalie wachoma mkaa na kuitisha Semina mahususi ya jamii hiyo ili kuwaelimisha na kisha kuwapatia mtaji na biashara mbadala ili waachane na ukataji wa miti kwa kuchoma mkaa. Hii inaweza kusaidia sana kupunguza ukataji wa miti. Pia iwape mradi wa kupanda miti kwenye maeneo yale yale waliiyokata miti. Pamoja na hayo yote, ni lazima kuzingatia nishati mbadala ya wananchi kutumia kwa kupikia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Waziri naomba anifahamishe, hivi nasikia tu Kankuni Kankuni, jamani kuna nini huko? Kankuni ni nini? Tanzania tunafaidika?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawatakia Baraka za Mungu katika kulitumikia Taifa letu huku tukidumisha amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu, Waziri wa Nchi, Muungano kwa Hotuba nzuri. Naomba nielekeze mchango wangu kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu kero za muungano. Nianze kwa kusema kuwa Muungano ni muhimu sana na hakuna anayechukia lakini una kero nyingi na ni muhimu sana kutatuliwa hivi sasa. Baada ya Muungano tarehe 26 Aprili, 1964 Bunge la Tanganyika lilipitisha Sheria za Muungano na zilithibitishwa na Baraza la Mawaziri kati ya yaliyopitishwa Rais akitoka Bara, Makamu wa kwanza wa Rais ni Rais wa Zanzibar na Waziri Mkuu kuwa ni Makamu wa pili wa Rais, ni Waziri ambaye atamsaidia Rais kwa masuala yahusuyo upande wa Tanganyika na kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza leo hii Rais wa Zanzibar siye anaye kaimu Rais akiondoka, sijui kipengele hiki kimemezwamezwa vipi. Mheshimiwa Waziri tunajua kuwa Muungano huu umeshapitia misukosuko na dhoruba za kila aina lakini bado unaendelea kuwepo hata kama kuna hali ya mashaka, huku nchi nyingi za Kiafrika, Kiarabu na hata Asia zilizokuwa zimeungana kama sisi miaka ya nyuma zikishindwa kuendelea. Hali ya mashaka ninayoizungumzia hapa inatokana na kile kinachodaiwa kuwa, kuundwa kwa Muungano wetu kulikuwa siri na tangazo la kutiwa saini, mkatuba wa Muungano kati ya waasisi hao wawili liliwashangaza watu kutoka pande zote za Muungano, Bara na Visiwani. Suala hili watu wa pande zote mbili za Muungano hawakushauriwa, utadhani hawakuwa na haki yoyote ya mustakabali wa nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuujadili Muungano sasa ni wakati muafaka kwani kuendelea kuyafumbia macho masuala ya Muungano tutakuwa tunajidanganya, kwani kuficha au kudharau maradhi ni ugonjwa hatari na ipo siku mauti yataatuumba. Imekuwa ikisemwa kwamba Serikali ya Tanganyika imefutwa kwa makusudi na Bunge la Tanganyika kinyume na makubaliano ya Muungano ili kujipa nafasi kuitumia Serikali ya Muungano, kama kwamba ndio Serikali ya Tanganyika. Kimtazamo hapa, malalamiko ya Wazanzibari ni kule kuendelea kutambua kuwepo kwa Sheria zisizo za Muungano, ni kutambua kuwepo kwa Mamlaka ya Tanganyika ambako Sheria hizo kwa mambo yote yasiyo ya Muungano ziliendelea na zinaendelea kutumika hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, manung'uniko ya Wanzazibari yameenda mbali zaidi wanapodai kuwa mionganoni mwa mambo yaliyodhahirisha kuwa hakukuwa na nia njema katika Muungano huu tokea awali ni pale wafanyakazi wa Serikali ya Tanganyika wote walipandishwa vyeo kwa pamoja na kuwa wafanyakazi wa Muungano kama kifungu cha 3(i) cha *Provisional Transitional Decree*. Vivyo hivyo, kifungu cha 6(i) cha *Decree* kinasema mara tu baada ya kuanza Muungano, Mahakama ya Tanganyika na Majaji wake wote nao watakuwa ndio Mahakama na Majaji wa Jamhuri ya Muungano kinyume na makubaliano ya Muungano. Mpaka leo Katiba zote mbili hazitambui Mahakama kama ni suala la Muungano. Nembo ya Tanganyika na Idara ya Mwanasheria Mkuu wa Tanganyika inachukuliwa kama Idara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Muungano wetu kijuujuu utaona kuwa ni mfano mzuri sana wa maelewano kwa watu wa Bara la Afrika, lakini chini kwa chini kunafuka moshi ambao ukiachwa hivi hivi bila kutafutiwa ufumbuzi utakuja kujitokeza moto mkubwa ambao tunaweza kushindwa kuuzima. Kwa kuwa tupo katika kipindi cha kuelekea kwenye mchakato wa kupata Katiba mpya, nadhani ni wakati muafaka kila Mtanzania aweke maslahi ya Taifa mbele bila ushabiki, Viongozi nao wawe mstari wa mbele kuonesha njia na sio kuwa na sauti ya mwisho juu ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Watanzania wengi kutoka pande zote zinazohusika na Muungano, inaonekana wazi hawapingi kuungana, kwani Muungano huu ni baraka. Ila hiki kinachoitwa kero za Muungano lazima kiangaliwe kwa macho yote. Mojawapo ya mambo yaliyo na mashaka na hayaeleweki yalipotelea wapi ni kuhusu Rais wa Zanzibar aliyetakiwa moja kwa moja awe Makamu wa Rais wa Serikali ya Muungano kama Rais atatoka Bara na pale Rais atakapotoka upande wa pili yaani Zanzibar mwenzake wa Bara awe Makamu wa Rais. Mheshimiwa Waziri naomba tafadhali katika majumuisho yako ultolee ufanuzi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa nchi, Mazingira, ufuatao ni mchangano wangu katika mazingira. Umuhimu wa mazingira kwa uchumi wa Tanzania uko katika sura nne zifuatazo:-

- Mazingira ndiyo makazi ya viumbe vyote mimea na wanyama ambao ndiyo urithi usiokuwa na badala yake.

- Mazingira yanaipatia nchi, mahitaji yote ya msingi kwa ajili ya kufanikisha masuala ya jamii na uchumi.
- Mazingira ni chombo cha kuweka yale yasiyofaa.
- Mazingira ni msingi ambao ndiyo itakuwa jawabu la kupunguza unyonge wa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba msukumo mkubwa wa uongozi wa mazingira ni kulinda sehemu asili ya kuishi binaadamu na kuanisha upungufu uliopo kwenye mazingira katika kusaidia kufikia maamuzi yanayohusu masuala na shughuli za uchumi. Licha ya kusikika kwa kauli za *NEMC* bado Baraza hilo linaonekana tu kuwa na uwezo wa kutoa ushauri panapotokea tatizo la uharibifu wa mazingira badala ya kuchukua hatua thabiti za nguvu kukomesha balaa hili. *NEMC* imetoa maelezo na ushauri kwa watu binafsi na wenyewe viwanda ambao hadi sasa haujazaa matunda hata kidogo kutokana na waliopewa ushauri huo kukaidi na wengine kusingizia kutoelewa huku wenyewe viwanda vinavyodaiwa kuharibu mazingira wakitia pamba masikioni na kuendelea kuzalisha uchafu mwingu katika sura ya dunia na angani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 – 2006, Tanzania ilipata fursa adimu kwa mara ya kwanza kuongoza dunia katika harakati za mazingira pale ambapo Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, aliyekuwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira alipopewa dhamana na ulimwengu kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Licha ya kuwa na kiongozi wa juu kabisa duniani nchi imekuwa ya kwanza katika kipindi cha mwaka 2005 – 2006 kupata balaa la pekee ambalo hadi sasa ni msumari wa moto moyoni mwa wanaharakati wa Mazingira nchini, ukame mkubwa, baa la njaa, kupungua kwa maji ya bwawa la Mtera vimekuwa gumzo masikioni mwa Watanzania na hakuna juhudhi endelevu zinazofanywa kulinusuru Taifa na uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi milima imekuwa kana kwamba hakukuwahi kuwa na miti, misitu mingi imemalizwa kwa kukata magogo na kusafirisha nje, moto unamaliza mapori huku wananchi wakidhani ya kale ndio sana kwamba moto ni sehemu ya ulinzi katika kaya zao. Hili ndilo jinamizi haya ambalo liko mikoani mwetu na katika fikra zetu viongozi na wanachi kwa pamoja tuna jukumu la kuona na kuamua kuliondoa kutofanya hivyo ili mradi tuone kuwa mazingira na uhai wetu ni ndugu kama mama mjamzito na mimba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika tatizo la mgao wa umeme ambalo limekuwa gumzo kwa wananchi wengi na kuwalaza viongozi tongo macho kwani nchi iko gizani, sasa ni matokeo au sehemu tu ya matokeo ya uharibifu wa mazingira unaofanywa na binadamu wakitafuta riziki. Kusema kweli Mheshimiwa Waziri, imefikia wakati kwa Watanzania kufanya kila tuwezalo kuhakikisha tunakuwa na mazingira mazuri, hali ni mbaya sana katika maeneo mengi ya nchi yetu, kutokana na ukweli kuwa athari za uharibifu ni kubwa mno kwa ustawi wa jamii yetu. Changamoto zinazoikabili Tanzania ni nyingi ikiwemo hali ya jangwa inayoikabili, kwani inaelezwa zaidi ya asilimia 60 ya Tanzania inakabiliwa na hali ya jangwa na ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotia hofu huenda baadhi ya sehemu za Tanzania zikawa jangwa ni kutokana na kukithiri kukatwa kwa miti, kwani taarifa zinazoonyesha kuwa takriban hekta 220,000 za misitu kufyekwa kila mwaka kwa mahitaji ya nishati hususan mkaa, kilimo kisicho endelevu na biashara ya magogo. Takwimu hizo zinatisha sana hasa ikizingatiwa kwamba takwimu za miaka ya nyuma zilionyesha kuwa, Tanzania inapoteza uoto wa asili na misitu kwa hekta 92,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, iko haja kwa kila Mkoa kufanya mikakati maalum kuhakikisha hatufikii kwenye athari hii ambayo tayari wataalam wameshatuonya kwamba inaweza kutoke. Ni wazi Wakurugenzi wa Mazingira na misitu wanapaswa kukutana ili kujadili nini kinatakiwa kufanyika kukabiliana na changamoto hiyo. Inavyoonesha ni kwamba uwezo wa malisho katika Mikoa mingi umezidiwa na wingi wa mifugo na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na uvamizi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna tatizo jingine la kukithiri kwa uchafu, huku viongozi wengi wakionekana wazi kutoshukua hatua za maana, takwimu zinaonyesha kuwa takribani tani 10,000 za taka ngumu huzalishwa kila siku nchini na asilimia 80 hadi 90 ya taka hizo hazizolewi, mifereji inayopitisha maji ya mvua ni michafu sana hasa Dar es Salaam, mvua ikinyesha kidogo uchafu wote uko juu hali ni mbaya. Je, tunachukua hatua gani katika hali kama hii? Katika hali hii Tanzania inahitaji kuweka mikakati mbalimbali ya kumaliza tatizo hilo ikiwemo kutunga Sheria kali ili kuhakikisha udhibiti wa taka ngumu mijini unafanikiwa. Mfano, jiji la Dar es Salaam ni moja ya mikoa inayokabiliwa na uchafuzi wa mazingira, kwa mujibu wa mkakati wa usafi wa jiji hilo, inakadiriwa kuwa Dar es Salaam huzalisha tani 3,900 za taka ngumu kwa siku, ikiwa ni asilimia takribani 40 za taka zinazozalishwa nchini, ni wazi kwamba kila mkoa unatakiwa kuwa na mkakati wa kuhakikisha inakuwa na mazingira bora. Imani yangu ni kwamba tukidhamiria na kuazimia hakuna litakaloshindikana hata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hakuna nishati mbadala ya kupunguza matumizi ya mbao, mkaa na shughuli mbalimbali zinazotokana na miti, Serikali inatakiwa kufanya jitihada za makusudi za kutafuta nishati mbadala kama gesi na mkaa ya mawe ikiwemo kupunguza ushuru wa gesi na mafuta ya taa kwa asilimia tano mpaka kumi. Hata hivyo, uelewa mdogo wa wananchi katika masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira unatajwa kuwa mionganoni mwa vikwazo vikuu vya juhudhi mbalimbali zinazofanywa kudhibiti uharibifu wa mazingira. Kwa sasa wananchi wengi wanadhani suala la kudhibiti uharibifu wa mazingira ni jukumu la Serikali, Mashirika, Taasisi na vikundi vilivyoanzishwa kwa ajili hiyo. Ndio maana hawaoni shida kushiriki vitendo vya uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya pori, misitu, maeneo ya biashara na maziwa yao. Hivyo, ni lazima washirikishwe kwa hali na mali ili kuweza kuwa na uchungu na kuyatunza mazingira hayo.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Hifadhi ya Mazingira. Pamoja na elimu ya kuhimiza na kuhamasisha utunzaji wa mazingira kuna

mkanganyo wa kuingiliana katika kazi. Idara ya Kilimo inahamasisha kilimo na kilimo lazima kung'oa miti, kufyeka vichaka, ndipo upate shamba zuri na kuhusu viwanda, tunahamasisha uwekezaji na ufunguzi wa viwanda vingi. Viwanda hivyo vinatumia kemikali nyingi na zinaelekezwa kwenye vyanzo vya maji na moshi unaotoka ni sumu.

Kuhusu matumizi ya binaadamu, wengi wa wananchi kwa kuwa na hali duni ya maisha hutumia kuni, mkaa kwa kuweza kupata huduma ya chakula. Uchafuzi wa mazingira katika miji kwa kutupa taka ngumu na laini kwa kukosa maeneo ya kuchoma taka na kutupa katika mashimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ushirikiano toka ngazi ya chini hadi Wizara hakuna mafanikio. Hivyo kunahitajika fedha za kutosha kwa Wizara hii ili miti mingi ipandwe na miti haioti bila maji, Wizara ya Mazingira ipewe kipaumbele na Wizara ya maji ili tupate mafanikio. Bajeti iliyoombwa ni ndogo iongezwe shilingi 12,410,379,00 katika fedha za Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutaka mafanikio yawepo kwa Serikali, Halmashauri za Wilaya, Serikali za vijiji kutunga Sheria na Sheria ndogo ndogo za hifadhi za mazingira. Bila Serikali yenyewe kuandaa mazingira hayo kwa kuwapatia wananchi nishati mbadala; hiyo ni kazi ya muhanga na ni zoezi lisiloteklezeka, kwa kuwa watumiaji wa mkaa kwa kupikia ni wengi (mijini) watumiaji wa kuni vijijini ni wengi, wajenzi wanaotumia tofauti za kuchoma ni wengi kwa kuwa Serikali inahitaji Mtanzania awe na nyumba nzuri. Serikali itafute kwa haraka nishati mbadala ili zoezi hili lifanikiwe na iwe manufaa kwetu kupunguza gharama za ujenzi ili itumike *cement* kwa ajili ya matofali ya *block*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, kupunguza mashamba makubwa na kilimo bora. Lazima Serikali ilione hili kupunguza na kuondoa mmomonyoko wa ardhi na nchi kuwa jangwa kwa kuwa miti mingi kukatwa, pia mashamba yote yalimwe kwa kutumia kontua na kupandwa miti ya asili ya sehemu husika, badala ya kulima kiholela na kuacha jangwa na mbuga zisizo na maana.

Pia kuhamasisha wananchi kupanda matunda maeneo ya kuishi au kwenye bustani ili wale wanaona hakuna manufaa ya kupanda miti, basi watashawishika kupata matunda endapo watashawishiwa kupanda matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda, Serikali iangalie na kukagua vizuri viwanda hivyo wapeleke wapi maji machafu yenyе kemikali na pia viwanda visijengwe karibu na makazi ya wananchi. Idadi isiwe kubwa ya viwanda kwa sehemu moja. Kuwe na ufuatiliaji wa karibu na kupunguza upokeaji wa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchafuzi wa utupaji taka ovyo kila Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji kutenga maeneo ya kutupa taka ngumu na taka laini. Kuwe na maeneo ya maji machafu.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kupongeza hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wa kuwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye upande wa mazingira. Suala la mazingira ni suala mtambuka hivyo basi ni vyema Serikali ipange Bajeti ya kutosha juu ya mazingira. Bajeti hii itokane na vyanzo vya mapato vya ndani. Nashauri suala la mazingira kukumbwa na tatizo la tabia nchi linatokana na uchafuzi wa mazingira. Inasikitisha kuona kwa mwaka wa fedha 2010/2011 baadhi ya miradi ya maendeleo katika eneo la mazingira haikuweza kutekelezwa. Mfano, ni kiasi cha asilimia 3.5 ya ahadi ya pesa za nje zilizotolewa kwa ajili ya miradi hiyo tu. Moja ya miradi ambayo haikutekelezwa ni kufuatiwa utekezaji wa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Pwani tatizo hili ni kubwa sana. Kuna uharibifu mkubwa wa mazingira ya bahari, maziwa, mito na mabwawa. Kuna uvunaji wa Mikoko isiyofuata taratibu. Maeneo ya Ukanda wa Delta, wananchi wanalima kwenye maeneo wanayovuna Mikoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wa misitu katika Mkoa wa Pwani ni tatizo la msingi. Kwa bahati mbaya sana, uvunaji wa misitu kwa ajili ya kuzalisha mkaa unaohudumia Mikoa ya jirani hasa Jiji la Dar es Salaam. Hali ya upandaji miti haiendani kabisa na kasi ya uvunaji wa misitu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kusikitisha Mkoa wetu wa Pwani katika mradi wa *Participatory Forest Management* (*vote 71 ukurasa wa 155* wa Kitabu cha Maendeleo Volume IV) ni kiasi cha shilingi milioni 42 tu, tena ni fedha za nje. Ugawaji huu wa rasilimali fedha katika eneo la mazingira haukuzingatia ukubwa wa tatizo la mazingira katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali wakati wa ugawaji wa rasilimali fedha za kushugulikia mazingira, basi ifanye tathmini ya ukubwa wa tatizo katika Mikoa yote na ugawaji huo uegemee ukubwa wa tatizo na athari zake katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwapongeza Mawaziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa shughuli zote nzuri wanazozifanyia Taifa. Aidha, napenda pia kuwapongeza watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa shughuli zao za kila siku. Napenda kushauri ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi nchi yetu na pengine dunia nzima ina changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabia nchi na mazingira yanachafuliwa sana. Kutokana na hali hiyo basi napenda kuishauri Serikali kuanzisha Idara za Tabia ya Nchi na Mazingira

kwenye maeneo ya vijiji (Rural Areas), hapa nina maana ngazi ya wilaya. Kule yapo matukio na vitendo vingi sana ambavyo huchangia sana uchafuzi wa mazingira na tabia ya nchi kuitia matumizi ya kemikali, kilimo na kadhalika. Aidha, kwenyewe ndiko kuna watu wengi. Wataalamu wakiwa wengi karibu na wananchi watasadid a sana kuelimisha na hivyo kuhifadhi mazingira ya nchi yetu. Baadhi ya maeneo ukame umeanza kwa sababu mazingira yanaharibiwa bila wananchi wenye na kawaida kujua na hivyo kukosa pia elimu na ushauri kuhusu mazingira yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuwa matumizi ya mkaa kwa kukata miti na kuharibu misitu hakujachukuliwa hatua madhubuti kuzuia au kutoa njia mbadala ya mapishi hivyo kusababisha athari ya mabadiliko ya nchi kuwa makubwa. Ni vyema kama Taifa tutafute njia mbadala ya kuendesha mapishi badala ya kuni kama njia kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tunao mpango wa kupanda miti kila mwaka kwa nia ya kuhifadhi mazingira yetu, lakini ikumbukwe miti mingi hufa kwa kukosa maji kwani sehemu kubwa ya nchi ina tatizo la maji kwa muda mrefu wa mwaka. Ni vyema basi kuwepo na mkakati mkuu wa Kitaifa wa kuhakikisha kila penye maji, maji hayo yanatengenezewa mazingira mazuri ya kufikisha maeneo yasio na maji ya kutosha ili miti istawi na hivyo kupunguza majangwa na hivyo kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuanzisha mitaala ya mazingira kuanzia shule zetu za msingi ili vijana wetu wafahamu tangu wakiwa wadogo haja na umuhimu wa kuhifadhi mazingira yetu na hivyo kujenga uchumi imara wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita kuzungumzia Muungano. Awali ya yote nitaanza kuzungumzia huu Muungano huu na wananchi. Pili, nchi ya Zanzibar na nchi ya Tanganyika na tulipoungana tulikuwa kwenye mfumo wa chama kimoja na Mheshimiwa Abeid Amani Karume alikuwa Rais wa Zanzibar, ana Baraza lake la Mawaziri na ana Chama chake cha *Afro-Shiraz* na Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere alikuwa Rais wa Tanganyika, ana Baraza lake la Mawaziri na ana Chama chake cha *TANU* na pia wakati wakuungana hatukujali wingi wa watu na wala wingi wa rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza haya nataka nijikite katika uchangiaji na mgawano wa mapato ya miaka iliopita. Mapato yote ambayo yalikuwa yanakusanywa na *TRA* huko Zanzibar yalikuwa yanaletwa Bara na mpaka sasa hatuelewi ni kiasi gani zimekusanywa na hatujui yako wapi kwa hivyo, namuomba Waziri atueleze haya mapato yamewekwa wapi na chetu yaani ni kiasi gani ili tuweze kukijua kabla huu mfumo ulioanza hivi sasa ambao ninauelewa, pesa zetu zinawekwa *Peoples Bank of Zanzibar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu leseni za magari ya Zanzibar huwa haziwezi kutumika Bara, wenye leseni za Zanzibar huwa wanapata usumbufu sana,

wanaadhibiwa na kutozwa faini na katika hili nina ushahidi kamili ambapo hapa Dodoma limetendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa kuwa kuna kamati ya pamoja ambayo itatatua changamoto za Muungano kwa kuandaa utaratibu wa vikao vyta kamati, hapa nimefarijika sana lakini suala langu hiyo kamati ya pamoja Wazanzibar wako wangapi na watu wa Tanzania Bara wakp wangapi na ikiwezekana naomba nipatiwe majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero za Muungano zinaelewaka. Naomba zitatuliwe kwa haraka ili wananchi tuwape matumaini na waweze kuunga mkono Muungano kwa wale wachache waliobakia. Muungano tunaupenda, tatizo ni yale mapungufu hayatekelezwi. Pia naomba haya mazungumzo ya mgawanyo wa mapato yamalizike na *account* ifunguliwe na yale malimbikizo yetu ya mapato ya Zanzibar tupewe wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya juu pia sijui Zanzibar tunapewa vipi, naomba kama itawezekana utueleze nafasi hizi zinagawanywa vipi kama nilipotanguliza kwa kusema tulipoungana hatukujali wingi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kukishukuru Chama changu kwa kunitfea kuwa Mbunge. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Anna Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, upandaji wa miti ya kutosha utasaidia sana kuhifadhi mazingira. Lakini lazima kila kijiji, kila Wilaya na kila Mkoa upangiwe idadi ya miti ya kupanda. Vile vile miti yote iliyopandwa lazima itunzwe vizuri mpaka hapo itakapokuwa mikubwa. Lakini inavyoonekana hivi sasa ni kuwa zaidi ya asilimia 75 ya miti inayopandwa inakufa. Ni muhimu kuwe na takwimu sahihi kwa miti yote iliyopandwa na ile iliyohai na iliyokufa mwaka hadi mwaka. Takwimu hii iwepo katika kila Kijiji, Kitongoji, Wilaya, Mkoa na kote Tanzania.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu kero za Muungano na kwamba kwa hali ya kawaide wananchi wa Tanzania hawardhishwi na muundo wa Muungano, ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuwa na Serikali Tatu yaani Serikali ya Tanzania Bara, Serikali ya Tanzania Visiwani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hii itaondoa dhana ya kwamba kila upande ulivyo unamezwa na upande mwagine. Bara wanadai Tanganyika yao imemezwa na haipo na vile vile Zanzibar ikidai imemezwa na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itafanya kila upande ufurahie uhuru wao na kupanga mambo yao kwa uhuru bila manung'unico. Pamoja na hilo, sikubaliani na wanaosema Muungano uvunjike, bali udumu na uendelee kwani umoja ni nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Taifa letu limetambua umuhimu mkubwa wa kutunza mazingira, vivyo hivyo wananchi wote kwa ujumla wanatakiwa kufahamu umuhimu huo wa kutunza mazingira. Mfano, kulima kwa kufuata kilimo cha kisasa, kufuga kisasa, kupanda miti isiyokausha maji hasa katika maeneo ya ukame kama Kanda ya Kati, kusafisha mazingira wanayoishi bila kutegemea amri za Serikali na kuwa na utamaduni wa kushtakiwa ndani ya dhamira zao kwa kufanya vitendo vinavyopelekea uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mageuzi ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 yalitoa mwanga mkubwa katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika nchi yetu. Kwa kuwa sheria hii iliweka wazi kuwa miradi mbalimbali ya ndani na inayoendeshwa na wawekezaji haiwezi kuanzishwa bila kufanyiwa *Environmental Impact Assessment (EIA)* ili kuona madhara ya mradi husika na hivyo kama utaonekana unaweza kuhatarisha uchafuzi wa mazingira, mradi huo utatakiwa kusimamishwa katika hatua za mwanzo hata kama ushahidi wa kisayansi haujapatikana, hii inalenga katika kuchukua hatua za haraka kuzuia kuliko kuponya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii pamoja na mambo mengine ilieleza bayana endapo mtu yejote atachafua mazingira ikiwemo maji, anatakiwa kulipa fidia kwa wote aliowasababishia madhara hayo na pia kuyarejesha mazingira hayo katika nchi yake ya asili. Lakini cha kushangaza pamoja na sheria kutamka bayana masharti na adhabu hizi, bado tumeendelea kushuhudia uharibifu mkubwa katika mazingira yetu hususan sehemu za migodi ambapo wananchi wamepata madhara makubwa kwa kutumia maji yanayosadikika kuwa na sumu toka kwenye migodi, kwa mfano katika Ziwa Victoria na hivyo kuwaletaa maradhi makubwa ya ngozi na hata vifo katika hilo, pamoja na sheria hii nzuri, Serikali inafanya nini kuwanyamazia wawekezaji wa kigeni au hata wa ndani wanaodhulumu haki za msingi za watu wa nchi hii kwa kuwaribia mazingira yao ambayo sheria hiyo hiyo inatamka kwamba ni haki mojawapo ya msingi ya binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kutumia sheria hii na kuwachukulia hatua waharibifu hao? Kwa maana hiyo wimbo wa mazingira utabaki kwenye kufagia barabara na kuondoa maganda ya pipi basi, lakini mambo ya msingi na hatari yanayoleta madhara ya muda mrefu yanaachwa yaendelee. Kwa hili naomba Serikali ifanye kazi yake sawasawa na si kulalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka ngazi ya kaya, kuwe na utaratibu mahususi kwa watendaji wa vijiji, kuanzia Mabalozi wa kuhakikisha kwamba kila kaya inatunza mazingira yake, kuanzia usafi kwa maana ya kuwa na choo safi, kupanda angalau miti mitano, kuwa na mashimo ya taka ili watoto waanze kuzoea wanapokuwa majumbani kwamba usafi ni mahali popote na hii itasaidia mtu au mtoto kuwa na woga wa kutupa taka hovyo mahali popote anapokuwa mbali na nyumbani mpaka anapokuta kuna mahali pa kutupa taka. Familia zetu zinatakiwa kuwa na hulka ya usafi ndani ya mioyo yao na si kungoja kushurutishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya usafi kuwa endelevu na utunzaji wa mazingira kuwa ni suala la lazima, watendaji wa vijiji wanatakiwa kushirikiana na

wakazi wao kupanga adhabu ambazo watatoa kwa wale waharibifu kutoka ngazi ya kaya na kuwe na utaratibu wa kukagua usafi na vyote nilivyovitaja kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu uchomaji wa misitu yetu ovyo. Suala la uchomaji misitu ovyo limekuwa ni la jadi hasa katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Shinyanga na Tabora. Pamoja na uchomaji wa misitu kuharibu *O-zone layer*. Pia umepelekwa kupoteza *species* nyingi za mimea, ndege na wanyama ambaa ni muhimu kwa maisha ya binadamu. Uchomaji huu unasababishwa na elimu ndogo ya utunzaji mazingira walijonayo wananchi hasa wanapoandaa mashamba kwa ajili ya shughuli za kilimo au hali duni walizonazo wanachi na hivyo kuchoma moto kwa ajili ya kujipatia nishati ya mkaa ili kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu ya ziada inatakiwa katika kuwaelimisha wananchi juu ya madhara ya kuchoma misitu na pia sambamba na hilo, Serikali pia inatakiwa ipunguze gharama za umeme na kuanzisha vyanzo vingine vya nishati kama umeme unaotumia upepo, jua, gesi na kinyesi cha wanyama ili kuwafanya wananchi waondokane na tabia ya kuchoma miti ovyo ili kupata mkaa. Mikoa kama ya Dodoma, Singida na Tabora ni muafaka kwa umeme wa upepo au kinyesi cha wanyama na kama nilivyosema ndiyo inayoongoza kwa uchomaji misitu na hivyo kuendeleza ukame unaokumba mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa tajwa, wananchi washauriwe kuacha miti inayonyonya maji na kuua *species* zingine mfano, mikaratusi miti hii inatoa sumu inayokausha mimea mingine kuota pembeni mwa miti hiyo na vile vile ni miti inayonyonya maji mengi na kwa hali ya ukame ya mikoa hiyo wananchi waelimishwe ili wasiendelee kuipanda na hivyo wapande miti mingine ili kutunza kiasi cha maji kidogo kilichopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. SEIF S. RASHID: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia na kwa niaba ya Warufiji nianze kwanza kuzungumzia mazingira. Tanzania ina hatari kubwa sana ya kuwa jangwa kutohana na kushindwa kusimamia maeneo ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mgawanyo na matumizi bora ya ardhi, uhifadhi wa misitu na usimamizi wa vyanzo vya maji, mabonde ya mito na ufukwe wa Pwani. Katika hili kwa niaba ya Warufiji nailamu kasi kubwa ya uharibifu wa misitu na Bonde la Mto Rufiji unaendelea huku Serikali ikiwa inaliangali. Ukataji wa miti unaofanywa na wafugaji wanaongezeka kila siku wakiisha ndani ya Bonde la Mto Rufiji na kuharibu sio tu mazingira lakini pia wanapoteza maeneo ambayo yanaweza kuzalisha mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mifugo ndani ya Bonde la Mto Rufiji ni zito, naitaka Serikali kutoa tamko juu ya hali hii ili kila mtu na hasa Warufiji waelewe msimamo wa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa uwekezaji katika kilimo unahusu maeneo makubwa ya kufikia hekta laki moja na kuendelea unaotegemewa kufanywa Rufiji chini ya mpango wa *RUBADA*, ni lazima uangaliwe vizuri ili Rufiji isiwe jangwa na kuongeza uhaba wa mvua unaondelea kukuwa kila mwaka. Naiomba Serikali kuzingatia uhifadhi wa misitu ukienda sambamba na upatikanaji wa nishati ya umeme itakayopunguza kasi ya ukataji wa miti usiozuilika bila ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu uendelee kwa maslahi ya wote. Naiomba Serikali iangalie kwa makini zaidi changamoto zake na kuziweka bayana faida zake ili tunapojadili Muungano leo ni busara kuona mbele zaidi ili fursa walizopewa Wanzanzibar kunufaika na kuwa huru na kutumia eneo la kilomita za mraba laki 945, kutoka eneo la Zanzibar la 2,000 kilomita za mraba. Nashauri Serikali ipitie changamoto na kutoa fursa ya kujadili kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAID SULEIMAN SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 47(7) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinasema; “Endapo Rais wa Zanzibar atateuliwa au kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, ataacha kiti cha Urais wa Zanzibar,” na kifungu cha 104(2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinataja mambo yatakayosabaisha kiti cha Rais wa Zanzibar kuwa wazi, mionganii mwa mambo hayo, sababu iliyotajwa na kifungu cha 47(7) hapo juu haimo katika mambo yatakayosababisha kiti cha Rais wa Zanzibar kuwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ikitokea na Rais wa Zanzibar akateuliwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais, si itakuwa ni kinyume na Katiba? Hali hii ikitokea Wazanzibar itabidi wafanye tena uchaguzi wa kumchagua Rais wa Zanzibar, je, gherama za uchaguzi zitatolewa na Serikali gani? Ile ya Jamhuri ya Muungano au ile ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 54(2) Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinaneleza Mikutano ya Baraza la Mawaziri na kifungu hiki pia kinanelezea endapo Rais hayupo basi mikutano itaongozwa na Makamu wa Rais na kama wote wawili hawapo Waziri Mkuu ndiye atakayeongoza mikutano hiyo.

Pia hoja, je, kwa nini Rais wa Zanzibar asipewe nafasi ya kuongoza mikutano hiyo badala ya nafasi hiyo kupewa Waziri Mkuu? Hii si kumdhalilisha Rais wa Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 54 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinaneleza kuwa Baraza la Mawaziri litakuwa ndio chombo kikuu cha kumshauri Rais, na kwa maana hiyo ndicho chombo kikuu kinachotunza siri zote za Serikali hii inayoongozwa na CCM, Chama Tawala. Hoja ni je, endapo Rais wa Zanzibar atachaguliwa kutoka upande wa Vyama vya Upinzani ataendelea kuwa Mjumbe wa Baraza hili la Mawaziri?

Je, hali hii siyo inayopelekea mgombea wa Urais wa Zanzibar kutoka upinzani, hata kama watashinda uchaguzi kutokutangazwa mshindi kwa hofu kuwa atakuwa ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri na siri zote za Serikali inayoongozwa na Chama Tawala atazijua?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 55(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaelezea uteuzi wa Mawaziri, kinasema Rais atateua Baraza la Mawaziri baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na hoja ni kwa nini Rais asishauriane na Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar ambao kwa hivi sasa wanatoka upande wa pili wa Muungano wetu? Na hasa ukizingatia Baraza hili linakuwa na Mawaziri wa Wizara zinazoshughulikia mambo ya Muungano.

Hii inaionyesha Kikatiba Rais hulazimika kupata ushauri kutoka upande wa pili wa Muungano wa Tanzania Visiwani na kama ni kweli unashauriana na Makamu wa Rais wa Muungano na Rais wa Zanzibar anafanya hivyo kwa utashi wa Baraza lake mwenyewe tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii yenye manufaa makubwa kwa wananchi na hasa kwa kuokoa mazingira ya nchi yetu ambayo yanazidi kuharibiwa siku hadi siku baada ya maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kazi hii ifanikiwe inahitajika Wizara zote zishiriki kwa namna moja au nyingine na hasa kuelemisha wananchi suala zima la tabia nchi ili waelewe kuharibu mazingira kwa kuhamahama, kufyeka mashamba makubwa, kuchoma moto, ufugaji usio na tija na kadhalika ni hatari kwa mazingira. Naomba kujua kama kuna kitengo kilichoundwa kuratibu kazi hii na kujua kila Wizara inatimiza wajibu kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ni muda mrefu toka Serikali ilipoahidi kuandaa nishati mbadala ili kuepuka matumizi ya mkaa ambayo ndio sehemu kubwa inayochangia uharibifu wa mazingira. Naomba kujua ni lini hasa utaratibu huu utakamilika na iharakishe, hata hivyo naipongeza Serikali kwa mpango mzuri wa kusimamia na kuzuia uharibifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mpango huu wa kuokoa mazingira ufanikiwe na uwe endelevu ni kushirikisha matumizi bora ya ardhi na kwa maana hiyo hakutakuwa na eneo litakalokosa kazi. Baada ya hayo wananchi wahimizwe kuwa mashamba ya miti. Naomba elimu iongezwe kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanategemea kuni na mkaa kama vyanzo vyao vya *energy* kwa matumizi ya kawaida. Hata hivyo Serikali ina wajibu wa kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa utumiaji huu wa miti hauathiri misitu iliyopo na mazingira kwa ujumla. Hivyo basi wanachi wazidi kuelimishwa kuhusu matumizi bora ya miti na kufuata sheria na kanuni zilizopo kwa matumizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji vingi vinakauka na mito michache iliyopo hasa ile ipitayo mijini inatumika vibaya na kufanya mingine iwe michafu. Wananchi waelimishwe zaidi kuhusu matumizi mazuri ya mito na Manispaa za miji zifuatilie kwa karibu na ufuataji wa sheria zinazolinda mito hii.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Mchango wangu utajikita katika masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya uhifadhi wa mazingira ya bahari *vis a vis* umaskini, nipongeze juhudhi kubwa za Serikali katika suala zima la kuanzisha na kutekeleza shughuli (*programme*) mbalimbali za usalama na uhifadhi mazingira ya bahari na pwani. Ni ukweli usiofichika kuwa kumekuwepo na ongezeko la vitendo vya uvuvi haramu kama uvuvi wa kutumia mabomu, utumiaji wa nyavu za kuokota na ukataji miti (mikoko) ovyo ambavyo zinakuwa chanzo kikuu cha kuangamiza rasilimali za baharini kama matumbawe na maliasili nyinginezo zilizopo baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tunapozungumzia uhifadhi wa mazingira ya pwani/bahari ni muhimu pia kuzingatia maisha (*livelihood*) ya wananchi. Uvuvi ni shughuli kuu inayotegemewa sana na wakazi wa Ukanda wa pwani ikiwemo vijiji vingi vya Wilaya za Tanga, Mkinga, Pangani na Muheza katika Mkoa wa Tanga. Ni shughuli ambayo inagusa maisha ya kila siku ya wakazi wa mwambao ingawa pia kilimo kinafanywa kwa kiasi kidogo. Kwa kiasi kikubwa maisha ya wananchi huwa yanategemea bahari na hivyo kuwepo kwa shinikizo kubwa (*pressure*) la shughuli za uvuvi kadri idadi ya watu inavyoongezeka na mahitaji ya chakula (maisha) yanayoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na jitihada za Serikali zilizoanzishwa miaka ya karibuni za usalama na uhifadhi wa mazingira bado hakujakuwa na mwongozo mzuri wa jinsi ya kuhifadhi mazingira na uhusiano wake na umaskini. Hali hii imepelekea kuwepo kwa hisia mionganoni mwa wananchi wengi wa mwambao kuwa jitihada hizi zimegeuka kuwa chanzo kikuu cha umaskini kwa wakazi hawa. Kiukweli hali ya maisha ya wananchi hawa inazidi kuwa mbaya ukitembelea vijiji kama vya Mwambani, Chongoleani, Mchukuuni, Tongoni, Kigombe, Kipumbwi, Tongoni maisha ya wananchi hasa vijana, wanawake na watoto si ya kuridhisha ukifananisha na miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono uvuvi haramu, hoja yangu ni kuwa tunapokataza uvuvi usiozingatia usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari ni muhimu pia tukatilia mkazo katika mbinu mbadala zitakazowawezesha wananchi hawa kujishughulisha na shughuli za uvuvi bila kuathiri usalama na uhifadhi wa mazingira. Uvuvi ndio maisha ya wakazi wa mwambao. Ni muhimu tukawa na mikakati sahihi na thabiti ya kuwawezesha wavuvi hawa kuendelea na maisha yao kama vile kujishughulisha na shughuli za uvuvi. Tuweke mikakati ya kutambua chanzo cha tatizo la uvuvi haramu. Je, ni nani anayeleta/kuuza na kusambaza mabomu na nyavu zinazokatazwa? Je, ni kwa nini uvuvi haramu kama wa kutumia mabomu ni tatizo Tanzania na siyo Kenya au Mozambique?

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa kumekuwepo na miradi kadhaa ya usimamizi wa mazingira ya bahari na pwani kama vile *Marine and Coastal Environmental Programme (MACEMP); Tanga Coastal Zone Conservation and Development Programme* na kadhalika. Lakini tujiulize ni kwa kiasi gani miradi hii imesaidia kuboresha hali za wakazi wa vijiji vya mwambao? Je, kumefanywa tathmini yoyote (*external evaluation*) ya utekelezaji wa miradi hii? Je, umaskini wa wakazi wa vijiji vya mwambao wa bahari umepungua au umeongezeka na ni kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Waziri husika akazingatia ukweli kuwa ni muhimu kutunza na kuhifadhi mazingira ya bahari na pwani na kuangalia *at the same time* uhusiano wa jitihada hizi na umaskini wa wakazi wa vijiji vya mwambao wa bahari. Miradi/mipango mingi iliyopo inapangwa toka juu kwenda chini na mbaya zaidi ushirikishwaji wa wananchi/walengwa katika kubuni na kutekeleza miradi si wa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza tuendelee kuhamasisha uvuvi endelevu na wakati huo huo tukiendelea kutafuta njia sahihi mbadala za kiuchumi kwa wakazi wa mwambao. Tudhibiti mabomu na nyavu zisizofaa katika vyanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano ni jambo jema sana ila kama Taifa kuna mambo ya msingi ya kuzingatia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, raia wa Tanzania Bara wamekuwa wakibaguliwa Tanzania – Zanzibar bila sababu za msingi hasa kwenye masuala ya ardhi, dini na siasa, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kero ya kodi, ukiwa unatoka Zanzibar hata kama umebeba lagi la kuchemsha maji *TRA* wanataka ulipe kodi, sasa je, hii ni nchi moja au mbili? Mbona ukitoka Kenya hulipii? Hii ni udhalilishaji wa Watanzania ndani ya nchi yao!

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu suala la ajira hasa kwenye sekta za Mabalozi, Wazanzibar wachache wamekuwa wakijiriwa kwenye sekta za Ubalozi na pia wafanyakazi wa Balozi hizo wengi wao wamekuwa Wabara. Suala hili liangaliwe linaweza zua tafrani na mtafaruku!

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya nchi yetu bado ni tatizo kubwa hasa maeneo ya mjini, miji inanuka hasa Jiji la Dar es Salaam na sasa hata Dodoma! Hii ni aibu kwa Taifa na hasa Makao Makuu ya nchi ambayo ndio taswira ya nchi, miji yetu mikuu ni michafu sana.

Pili wananchi kujenga milimani hasa maeneo ya Maziwa Makuu kwa mfano Mkoa wa Kigoma wananchi wamekuwa wakijenga katika Mlole hili suala ambalo linafanya udongo mwingi kuwa *deposited* Ziwanu na hivyo kuathiri kina cha Ziwa na hali hii ikiendelea Ziwa letu litakuwa hatarini na hii imekuwa ikisababishwa na ukosefu wa Maafisa Ardhi katika Halmashauri zetu za Kigoma MJini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ningependa kushauri Serikali iweke na itunge sera ambazo zitawekewa sheria ambayo kila Mtanzania atahakikisha anakuwa mlinzi na askari wa Mtanzania mwingine atakaechafua mazingira hayo, tutaweza mbona Moshi wamefanikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha!

MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Muungano huu ni muhimu, sifa kubwa ya nchi yetu ni Muungano hatua za haraka zichukuliwe kuuimarisha. Kwenye kero za Muungano, kamati husika ifanye haraka.

MHE. ASHA MOHAMED OMARI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutoa elimu ya Muungano kwa wananchi wake kupitia vyombo vyake mbalimbali vikiwemo redio, luninga na majorida mbalimbali, naishauri Serikali kuwa elimu hiyo itolewe kwa kuwfafikia wananchi hadi vijijini kote, kwani wapo ambao hawana uwezo wa kununua redio, luninga na wengine hawana uelewe wa kusoma. Kwa hiyo, ni vigumu kwa wananchi hao kuelewa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kufanya jitihada kubwa za kuondoa kero za Muungano, lakini bado hakuna usimamizi wa kutosha juu ya jambo hilo, kwani wananchi wanaamini kuwa Serikali yao inawapuuza na hawasikii vilio vyao. Kwa hiyo, naishauri Serikali ifanye uamuzi wa haraka kuondoa tatizo hilo la kero za Muungano.

Pia nichangie katika suala la watumishi wa Muungano. Ningependekeza kwa Serikali kuajiri watumishi wake kupitia wananchi wake wa SMT na SMZ ili kufanya uwiano baina ya Zanzibar na Bara kwa lengo la kuepusha kutolewana baina ya pande hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ulipaji kodi mara mbili kwa wafanyakazi wa Zanzibar, kwani suala hili limepigiwa kelele siku nyingi na

wananchi hao lakini bado halijatafutiwa ufumbuzi, kwa hiyo, naishauri Serikali pamoja na jitihada wanazochukua lakini wachukue jitihada zaidi kuliondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la elimu, pamoja na Serikali inatoa nafasi kwa wanafunzi wa Kitanzania kwenda kusoma nje ya nchi, lakini inaonekana Wazanzibar wanaopata nafasi ya kwenda kusoma nje ya nchi ni asilimia ndogo kwa hiyo, naishauri Serikali inapotoa nafasi za kusoma lazima ziwe na uwiano wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mambo yanayohusu hifadhi ya mazingira, niongelee katika suala la wamiliki wa viwanda hapa nchini, pamoja kuwa wanajua uharibifu wa mazingira katika jamii na athari kubwa zitokanazo na uharibifu huo wa mazingira inaonekana dhahiri kwa wenyewe viwanda hao kukiuka masharti ya kuweka mazingira safi kwenye viwanda vyao. Kwani bado wananchi mbalimbali wanalamika juu ya suala hili la mazingira, kwani yale maji machafu mara nydingi yanapotoka huwa yanaelekea kwenye vyanzo vya maji vya wananchi hao. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye jitihada ya makusudi ili kuweza kuondoa tatizo hilo kwa wananchi wetu wa Tanzania ili jamii yetu iishi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie kwa umakini juu ya ukabiliaji wa mabadiliko ya tabia nchi kwani tatizo hili limekua tatizo la Kitaifa, kwa hivyo Serikali pamoja na jitihada wanazochukua hivi sasa bado haziridhishi kwa nchi yetu kwani majanga yanayotokea hivi sasa ni mengi ambayo yanaweza kuleta athari kubwa kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali kutilia mkazo juu utoaji wa elimu ya mazingira hadi vijiji kote, kwani imeonekana kuwa kwa walio wengi hawana uelewa wa kutosha juu kutunza mazingira, kwa hiyo, naishauri Serikali ichukue jitihada za makusudi ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tatizo la idara zinazoshughulikia ardhi kwani imejitokeza tatizo kubwa watu kujenga katika vyanzo vya maji na hao wanaotoka maeneo hayo ya kujenga ni Idara za Ujenzi, kwa hiyo basi, tuishauri Serikali izibane idara zake kutotoa viwanja kiholela katika viwanja vya maji au vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia suala la mazingira ambayo yanatuzunguka sisi wenyewe mahali tunamoishi, kwani mazingira si misitu tu na vyanzo vya maji tu, kwani tukiangalia kwenye vijiji vyetu wananchi hawapendi kutunza mazingira yao, kwa sababu hawana uelewa mzuri juu ya usafi wa vijiji kuanzia Manispaa zake hadi kata kuweka miji yetu safi. Kwani mazingira safi yanaanza majumbani kwetu tunakoishi kwanza ndipo baadaye tutunze mazingira ya Taifa kwa ujumla.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu kero ya Muungano, tatizo siyo elimu juu ya Muungano kama inavyodaiwa na baadhi ya watu. Tatizo ni utashi wa kisiasa juu

ya Muungano, iwapo pande zote mbili za Muungano zimeridhia na kuridhika na mfumo wa Muungano kero zinazojitokeza hazikuwepo. Mimi nashauri yale yote yanayoitwa kero za Muungano zitatuliwe. Katiba mpya si dawa iwapo wananchi hawajazinduka na mfumo wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji holela wa madini katika makazi ya watu. Imekuwa ni mtindo itokeapo dhahabu wachimbaji wanavamia maeneo hasa katika mito, mfano katika wilaya ya Mbulu siku za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchomaji mkaa, kwa vile Serikali imepandisha bei ya mafuta ya taa na kutokuwepo umeme sehemu kubwa, watu wengi wanatumia mkaa kama nishati. Hii inasababisha miti mingi kukatwa kiholela na kuleta athari zifuatazo:-

Kwanza sehemu kubwa ya nchi kuwa jangwa, pili, uharibifu wa hali ya hewa. Kwa kuvuja kwa hewa ya kaboni (*carbonmonoxide*) kwa sababu mkaa unaochomwa bila utaalamu wowote.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Makadirio ya Ofisa ya Makamu wa Rais, Muungano kwa ufafanuzi mzuri na nawapongezi watendaji wa Ofisi hii kwa namna wanavyojitahidi kusimamia mambo ya Muungano wakiongozwa na Waziri na Katibu Mkuu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utashi wa kisiasa na ukweli wa Muungano wenyewe ulivyojikita ndio daraja halisi linalosaidia kuwepo kwa Muungano huu. Mfano, nchi mbili hizi zimeungana kidamu zaidi kuliko kikaratasi (Mkataba), kihistoria na kijiografia nchi hizi ni moja na wazaliwa wengi (makabila) yako sehemu zote za nchi mbili hizo ni Wamakonde, Wanyamwezi, Wamanyema na kwa sasa hata Wamasai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumegandana zaidi kuliko tulivyokuwa hapo nyuma kwenye nyanja za biashara na kiuchumi. Wabara wako Zanzibar hawana wasi wasi wako nyumbani na Wazanzibar wamehamia Bara mpaka Kigoma na Ruvuma utawakuta.

Jambo la muhimu sasa ni kudumisha na kuuhuwisha kwa kila nafasi inapotokea. Kuna makosa tunafanya kwa kutotoa taaluma ya Muungano, tulidhani kila kitu huja chenyewe na tulijisahau kuwa tunao maadui na vibaraka wanaotaka wauone uvunjifu wa Muungano huu. Wapo wa duni na wapo wa juu. Muungano kweli ni usalama/amanu na upendo. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Hivyo basi naomba masuala ya kufanyika makongamano na mikutano ya pamoja yenye mwelekeo wa kujenga sio kulaumu hili na lile kwa dhana ya kuvunjika kwa Muungano haitosaidia. Wasomi, Mashekhe, Mapadri, Maimamu, Maaskofu na hata akina sisi wanasiasa tuone ukweli wa kuwepo kwa Muungano huu, kuvunjika kwake hakutatusaidia na haitakuwa rahisi kurejesha tena endapo utavunjika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona tatizo linalo tufikia sasa, kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki tunaitaka sasa taabu kuiunga tena. Ikimbukwe kujenga ni kazi lakini kuvunja ni rahisi. Tusaidie kuenzi Muungano kwa kuanzia sasa kutoa taaluma mashulenzi (umuhimu wake) kuanzia madarasa ya chini (*primary school*) ili vijana wajione ni jamii moja ya Kitanzania mpaka vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu sote tunajua kukua kwa shughuli za maendeleo ya mwanadamu kiviwanda na msukumo wa ukuzi wa uchumi ni tatizo kwa mazingira na hili hatuwezi kuliepuka. Dunia inapiga kelele, na Watanzania tukawa kati ya jamii inayoathirika. Jitihada zinazohitajika kwa Watanzania kujitahidi kulitetea hili, kupunguza hilo ni athari kubwa kuwa inaturudia sisi wenyewe kwa mfano, sasa umeme hamna kwa kukosekana kwa mvua. Uchumi unapotea, pia uvunaji wa kuni (miti) hauepukiki ni lazima Serikali ijikite kutafuta nishati mbadala ya kupikia. La sivyo nchi itakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii iendelee kuelimishwa juu ya athari zitakazotukibili kwa uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, *NEMC* ni taasisi ambayo imekuwa ikishughulika na uhifadhi wa mazingira katika Taifa letu, je, ni kwa nini sasa haipewi mamlaka kamili katika utendaji wake hususani katika *Environmental Impact Assessment* kwenye kutoa vyeti (*Certificate*) kwa *organs* (taasisi) zote inazozikagua. Badala ya utaratibu wa sasa ambapo Wizara ndiyo inayohusika na kutoa vyeti ambavyo Wizara haikagui na kujuu uhalisia wake zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi kwa nini Serikali (Wizara) sasa isitoe mamlaka kamili kwa *NEMC*?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la mazingira duniani linazidi kuwa tata na tete, na nchi yetu ni mojawapo duniani inayozidi kuathirika na mabadiliko ya tabia nchi hali inazidi kuwa mbaya. Bado eneo hili la mazingira kwa wananchi ni hafifu kutokana na uharibifu wa mazingira kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri iundwe Wizara maalum kulisimamia na kufuatilia kikamilifu suala la mazingira, muundo wa kuunda Wizara utazamwe.

Kuhusu magugu pori yaliyoshamiri (*chromolaena*) katika Wilaya ya Serengeti yachunguzwe kwa haraka sababu ya uharibifu mkubwa wa mazingira uliopo na magugu haya yanasaababisha hata mimea na miti ya asili kufifia pamoja na mifugo kupata upofu. Hivyo Wizara ya Mifugo, Kilimo na Maji na Mazingira washirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulinda mazingira na binaadamu ukiwemo utaratibu wa kuangamiza taka za elektoriniki (*e-waste*) uandaliwe na Watanzania wafundishwe kwa sababu taka za aina hii ni hatari kubwa.

Pia Halimashauri na Mikoa waimarishe uwepo wa maafisa mazingira na wapewe nyenzo., Serikali ipige marufuku kuuza magogo nje ya nchi hii, ni hatari kubwa kwa nchi yetu na pia upandaji miti hususani ya asili uimarishwe kwa sababu upandaji wa miti unaonekana ni mdogo, ikilinganishwa na ukataji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati mbadala ya kuni na mkaa itafutwe na gharama ya umeme ipunguzwe kwa vile ipo juu sana na kusababisha watu kutumia kuni na mkaa hata maeneo yenye umeme. Pia Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*)apewe Bajeti ya kutosha ili umeme usambazwe maeneo mengi ya nchi yetu ili isaidie kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kutoa maoni na mapendekezo yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na mazingira), kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Viongozi Wakuu wakahimizwa kuhusu umuhimu wa kutatua kero za Muungano kwa wakati. Ninaipongeza Serikali na Kamati mbalimbali, kwa kushughulikia kero hizo; hata hivyo, bado zipo hoja nyingine zenyne msingi ambazo bado hazijatatuliwa; ni imani yangu, mafanikio yatapatikana mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha malalamiko kuhusiana na rasilimali za Muungano yanatokomezwa, ni vyema na busara kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, kuwaelimisha Wananchi kuhusiana na masuala 22 ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuzungumzia machache kuhusiana na Mazingira. Kama tunavyofahamu kwamba, Chama cha Mapinduzi kuititia Ilani yake ya Uchaguzi ya Mwaka 2010 – 2015, kimeainisha kwamba, Hifadhi ya Mazingira inakuwa endelevu. Ili Serikali iweze kufanikiwa katika azma hii, ni vyema ikaongeza kasi ya upandaji wa miti kama vile miti ya asili, ambayo inastahimili ukame na mazingira mengine magumu. Serikali inafuutilia kwa kiasi gani zoezi hili na kutoa elimu kwa umma ili Wananchi wafahamu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Je, ni lini sasa Serikali itaandaa sera na kuleta sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala kwani kwa hali ilivyo sasa ni hatari, kwani uharibifu wa mazingira kwa kutumia mikaa kama nishati ni mkubwa na ni hatarishi.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo kadhaa katika Mkoa wa Dar es Salaam hususan Mikocheni, Nyerere Road, Port Access na kadhalika, yenye viwanda, yamekuwa yakichafuliwa mazingira yao kwa kutiririsha uchafu na kemikali zitokazo viwandani;

kwa kweli hatuoni hatua za kinidhamu na kisheria zinazochukuliwa dhidi ya viwanda vinavyofanya uchafuzi huo. Hatua gani zimechukuliwa dhidi ya Watendaji wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), ambao wamezembea kuchukua hatua dhidi ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchangia kuhusiana na utekelezaji wa programu ya kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa. Ningependa kupata ufanuzi kuhusu ni kiasi gani uelimishaji na kujenga uwezo wa wadau katika kuandaa na kutekeleza Miradi ya *Clean Development Mechanism* utekelezaji wake ukoje. Wadau wangapi ambao wamenufaika na mafunzo pamoja na Wananchi au Taasisi ngapi zimenufaika katika kutekeleza Miradi ya *Clean Development Mechanism* tangu Programu hii ilipoanzishwa nchini? Je, mpaka sasa nchi imenufaikaje kifedha na Programu ya *Carbon Credit*?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja.

MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO: Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mawaziri wote wawili na Wataalam, kwa hotuba nzuri na iliyolenga maeneo muhimu katika Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu uboreshwe na kuimarishwa kwa kutatua kero ambazo zimekuwa zikitajwa. Katiba zote mbili zihuishwe na kuwa *harmonized*. Taasisi za Muungano zitoe elimu kwa umma ili umma wote ufahamu, watu wawe na uelewa mzuri wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Mazingira itolewe kwa umma na Sheria zilizopo zisimamiwe ili kunusuru na kuhifadhi mazingira. Vyanzo vya maji, misitu, milima na *bio-diversity* vyote vipewe umuhimu maalum.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kuhamahama kidhibitiwe ili kunusuru misitu na nyanda za malisho katika maeneo yasiyofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, utafiti ufanywe na *NEMC*, ikishirikiana na Wizara ya Nishati, juu ya Nishati mbadala ili kupunguza utumiaji wa mkaa na kuokoa miti na mazingira. Pia nishati mbadala itafutwe itakayotumika kwa kuchoma matofali.

Mheshimiwa Spika, *EIA* zifanywe kwenye Miradi yote na *Management Plans* zisimamiwe kikamilifu ili ku-*mitigate against all negative impacts identified* katika *EIA* ilifanyika.

Mheshimiwa Spika, kwenye vituo vya kukusanya taka yawekwe mapipa ya taka za kuwa *recycled* na taka ambazo haziwezi kuwa *recycled*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mazingira ni *cross-cutting*, ninapendekeza kuwepo na Dawati la Mazingira katika kila Wizara, Mkoa, Halmashauri, Mamlaka na kila Ofisi.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, ninaomba niwapongeze Mawaziri wote wawili; wa Mazingira na Muungano, kwa hoja zao nzuri na makini.

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe makini zaidi kwenye suala zima la kutunza mazingira ya nchi yetu kwa sababu:-

- (i) Idadi ya Watanzania wanaongezeka kwa kasi na ardhi yetu inabaki ile ile. Isipowekwa mikakati madhubuti sasa hivi, nchi itageuka janga ghafla. Kutokana na watu kuongezeka, miti itafyekwa kwa wingi, vyanzo vyta maji kuharibika na kadhalika.
- (ii) Miradi mingi ya Maendeleo inayoanzishwa na Serikali na inayoibuliwa na Wananchi, yote izingatie utunzaji wa mazingira. Kama ni Waraka Mahususi kutoka Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) au kama ni *by-laws* za vijiji, basi vitumike haraka kunusuru mazingira yaliyo hatarini.
- (iii) Uwezeshaji na uwekezaji uliodhaminiwa na Serikali katika Mpango wa 2011 – 2016, maendeleo yazingatie utunzaji wa mazingira. Wawekezaji wa ndani na nje wote wazingatie hifadhi na utunzaji wa mazingira, hasa wale watakaoanzisha viwanda na wale watakaokuwa na kilimo cha maeneo makubwa.
- (iv) Serikali ifanye juhudzi za makusudi kushugulikia usafi wa mazingira kwenye maeneo ya migodi na uchimbaji hususan kule Mererani – Manyara.

Mheshimiwa Spika, eneo lile limechafuka halifai kutokana na makatarasi, malboro, chupa za maji na kadhalika na kadhalika ili mradi hapatazamiki.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua Wizara itachukua hatua gani kwanza:-

- (i) Kuwahimiza Wananchi wa maeneo hayo kusafisha mazingira yale?
- (ii) Pili, kupanda miti kwa kutumia maji ya visima ili ukame na jua kali vilivyopo pale Mererani ipungue kuleta mandhari ya eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, Ziwa Babati linaleta mandhari nzuri sana kwenye Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Manyara. Ziwa hili liko hatarini kutokomea kutokana na watu kuvamia na kulima kandokando na kuharibu Ziwa hilo. Pia magugu maji yanakaribia kudidimiza Ziwa Babati, lenye samaki watamu sana na tegemeo la Wananchi wanaozunguka Ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, ninauliza je, Serikali itatusaidiaje kunusuru Ziwa Babati kwa manufaa ya Wananchi wa Mkoa wa Manyara?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Muungano – Majengo na Taasisi za Muungano: Kimsingi, Serikali ilishaamua kuhamia Dodoma (Makao Makuu) na katika Bunge hili, Serikali imeendelea kuwahakikishia Watanzania kwamba, dhamira ya kuhamia Dodoma ipo pale pale. Hata hivyo, inasikitisha kuona Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kujenga Ofisi ya Makamu wa Rais Jijini Dar es Salaam. Ninapenda kujua hivi kweli Ofisi hii inayo dhamira ya kweli ya kuhamia Dodoma?

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni urithi ambao tuliachiwa na Waasisi wetu Mwalimu Nyerere na Mzee Karume. Muungano huo ndiyo uliozaa nchi inayoitwa Tanzania. Hata hivyo, yapo baadhi ya mambo ya Muungano ambayo yameanza kupigiwa kelele; kwa mfano, suala la mafuta. Inasikitisha kuona baadhi ya Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wameanza kuzungumza hadharani kwamba, suala la mafuta (ambayo bado hayajapatikana rasmi), siyo la Muungano! Bado Zanzibar inaanza kuzungumza suala la kuwa na Wimbo wa Taifa! Ninashauri mambo yote ya Muungano na ambayo yanaonekana kuwa ni kero kwa upande mmoja, basi yazungumzwe kwenye Vikao vya Muungano vinavyoongozwa na Makamu wa Rais ili ufumbuzi upatikane. Kuzungumza nje ya vikao, kunahatarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Tanzania una miaka 47 sasa. Hata hivyo, inasikitisha kuona Wananchi wengi, bila shaka na pande zote mbili za Muungano, hawana elimu ya kutosha kuhusu Muungano huu. Ninashauri Wizara hii ya Mambo ya Muungano, iongeze kasi ya kuwaelimisha Wananchi kuhusu Muungano huu na faida zake. Majorida mengi zaidi yachapishwe na kusambazwa vijijini na matumizi ya TV, Redio na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Mazingira: Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ni chombo muhimu sana katika suala la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Hata hivyo, inasikitisha kuona chombo hiki muhimu hakipewi pesa za kutosha katika utekelezaji wa majukumu yake. Ikumbukwe kwamba, nchi hii ni kubwa sana na changamoto za uhifadhi wa usimamizi wa mazingira ni nyingi sana. Ninashauri Serikali itengeta pesa za kutosha ili Baraza liweze kufanya kazi zake vizuri

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona *NEMC* ambayo ni chombo muhimu, hakina Bodi ambayo inaisimamia katika masuala yote ya kisera. Bodi ya *NEMC* iliyoteuliwa mwezi Juni, 2006 ilimaliza muda wake mwezi Juni, 2009, hadi leo hii haina Bodi rasmi, ingawa mwezi Oktoba, 2010 Bodi ya zamani ilipewa kipindi kingine cha miezi sita ambayo ilimalizika mwezi Machi, 2011. Ninapenda kujua kwa nini hali hiyo iko hivyo? Aidha, ninataka kujua nani au ni chombo gani kinachotimiza au kufanya kazi ambazo kimsingi hufanywa na Bodi?

Baada ya maswali hayo, ninapenda nishauri kwamba, ili *NEMC* iweze kutimiza wajibu wake; ni vizuri ipatiwe Bodi itakayoishauri katika masuala mbalimbali hasa yale ya kisera.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandaji miti na usimamizi wake, ninaishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa kuwa na utaratibu wa kupanda miti. Hata hivyo, pamoja na nia hiyo nzuri ya Serikali, bado zoezi hilo halifanywi kwa ufanisi katika maeneo mengi. Katika maeneo mengi ambayo miti hupandwa, usimamizi wake ni hafifu na matokeo yake miti mingi hufa! Ninaishauri Serikali ifanye usimamizi wa kutosha kwa miti inayopandwa. Aidha, baadhi ya Halmashauri hazitoi takwimu sahihi za miti iliyopandwa (hudanganya); ninashauri pawepo na *physical inspection* ili kujiridhisha na taarifa ambayo hutolewa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu mzuri wa Wizara hii kuwapatia wenye mabasi ya safari ndefu, vyombo maalum kwa ajili ya kutunzia takataka, lakini bado kwenye barabara zetu, na kwa kuititia mabasi, takataka nyingi zinatupwa ovyo, inaonekana vyombo hivyo havijasaidia sana. Ninashauri usimamizi (*Physical*) uimarishwe. Aidha, abiria wanaosafiri na mabasi hayo bado wameendelea kukojoa vichakani na kutupa taka ovyo; ni maeneo machache sana yenye vyoo rasmi. Ninashauri wenye mabasi waendelee kuagizwa ili wasisimamishe mabasi maeneo yasiyo na vyoo. Kwa kufanya hivyo, tutalinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri majarida mengi zaidi yachapishwe na kupelekwa vijijini ili kuwaelimisha Wananchi umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira. Aidha, ninashauri kuwe na mtaala kwa shule za msingi na sekondari kuhusu mazingira. Tusitegemee tu Redio na Televisheni kwa kuwa havipo sana vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa mikakati ya uhifadhi wa mazingira katika nchi yetu. Pamoja na mikakati hiyo, zipo changamoto nyingi ambazo Serikali inapaswa kutafuta njia ya kuzuia jitihada zisikwame.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaendela kufumbia macho uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na ufugaji holela unaoendelea katika maeneo mengi katika nchi yetu na kukata miti ovyo na wafugaji hao kutetewa na Viongozi wa Kisiasa; hivyo, kukatisha tamaa Wananchi kuendelea kupanda miti na kutunza miti ya asili iliyopo na inayoota katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa; baadhi ya Viongozi wa ngazi mbalimbali wa Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijijini, hupewa fedha na kuruhusu wafugaji kuingiza mifugo mingi katika hifadhi za vijiji zilizotengwa. Kutokana na uhaba wa ardhi, husababisha mifugo ya wafugaji kuzagaa ovyo kwa kutafuta malisho; elimu iendelee kutolewa kwa ufugaji usio na tija.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa gharama za umeme, hufanya kutafuta njia mbadala ya kukabiliana na tatizo hilo, ikiwa ni pamoja na kukata miti kwa matumizi ya kuni na mkaa. Ili kukabiliana na tatizo hilo, ninashauri Serikali itoe ruzuku kwa taasisi zinazohusika na umeme ili kumpunguzia Mwananchi gharama za tozo kubwa la umeme.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa kutosimamia vizuri Sheria za Mazingira zilizotungwa husababisha Vyombo vyta Sheria kuwa mbali na Wananchi na upungufu wa Watumishi wa Mahakama.

Kiwepo chombo maalum cha kufutilia na kusimamia hifadhi ya mazingira kwa kila Wilaya na kuzuia uchomaji moto ovyo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kukamilisha uzio haraka Bandarini Zanzibar kama ilivyotakiwa na *Coast Guards* wa Marekani kwa Sheria ya Kimataifa ya Usalama Bandarini (*International Ship and Port Security Code - ISPS Code*) ni muhimu sana. Hii itaepusha meli za Marekani na nyingine kutoka Ulaya zisizuiliwe kuja Zanzibar kwa hofu ya kulipuliwa kwa vitendo vya kigaidi, kwani wasafiri wanakwenda kwenye boti (*fast ferries*) kupita eneo la meli kubwa za mizigo pale Bandarini Malindi Zanzibar. Wizara husika ya SMZ ni vyema ikumbushwe kukamilisha utaratibu huu mapema, ingawa tuliongeza mwishoni mwa Mei, 2011 katika mkutano wetu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar/Serikali ya Muungano Tanzania kwa Wizara husika. Uchumi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano Tanzania unaweza kuathirika tukichelewa.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii, kutoa shukrani za dhati kwa Mawaziri; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na Mheshimiwa Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa kuwasilisha Hotuba nzuri mbele ya Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kuijadili hoja hii, mchango wangu utagawanyika katika vipengele vikuu viwili vifuatavyo: Masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na athari za mazingira katika Mgodi wa North Mara, Nyamongo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kabla ya yote, nichukue fursa hii pia kuwapongeza Waasisi wa Muungano wetu; Mwalimu Julius K. Nyerere na Sheikh Abeid Aman Karume. Ninawapongeza Waasisi hawa kwa sababu walijua wazi umuhimu wa umoja na mshikamano katika nchi zetu za Afrika, ndiyo maana waliamua kwa dhati kuziunganisha nchi zao na kuzaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ninawapongeza kwa sababu hawakuwa na tamaa wala uchu wa madaraka na ndiyo maana waliweka maslahi ya Utaifa mbele kwa kuwatetea wanyonge wa nchi husika, kwa kutambua usemi kwamba, umoja ni nguvu. Kwa hakika

walijitahidi kubuni aina ya Muungano ambao umekuwa ni mfano bora wa kuiga mahali popote pale duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninapenda kunukuu aliyowahi kuyasema Mwalimu Nyerere: "Hatukujenga nchi mbili, badala yake tukafanya kitendo cha pekee katika historia nzima ya Afrika Huru ... Tukaziunganisha zikawa nchi moja. Tanzania ni lulu ya pekee kabisa katika historia ya Afrika Huru. Nchi nyingine zote ni za urithiri kutoka katika ukoloni. Tanzania ni ya kuundwa na sisi wenyewe, kwa hiari yetu wenyewe, baada ya kukomboa sehemu zake mbili kutoka katika ukoloni."

Mheshimiwa Spika, ifahamike wazi kuwa, mbele ya Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar, ilizaliwa Nchi ya Tanzania. Kwa misingi hiyo, Muungano wa nchi mbili zilipoungana zilizaa nchi moja tu ambayo ni Tanzania. Hivyo basi, masuala ya kuzungumzia nchi mbili au tatu kwa visingizio vya kero za Muungano ni usaliti kwa Waasisi wa Nchi hii ya Tanzania. Usaliti huu unatokana hasa na wapinga Muungano, ambao hawaitakii mema Nchi yetu ya Tanzania. Usaliti huu unatokana na ushawishi wa vibaraka ambao wanaunga mkono kwa dhati maadui wanaouchukia Muungano wetu. Hao wote wanatumia mwavuli wa kero za Muungano ili kutimiza haja yao ya kuigawa Tanzania katika vipande vipande! Ninaishauri Serikali yetu isikubali kutumiwa na wanjanja wachache wasioitakia mema nchi yetu kwa manufaa yao wenyewe! Ushauri wangu ni kuwa, mambo yanayohusu Muungano tusiyaruhusu kujadiliwa hadharani kama siyo masuala nyeti ya Kitaifa. Itumike zaidi busara na hekima ili kuweza kuondoa kero za Muungano zilizopo, lakini si kuruhusu kila mtu ajadili kero hizo utadhani ni nyanya zinazouzwa sokoni ambazo hununuliwa na kila mpita njia. Suala hili lina unyeti na walioliasisi waliona kwa dhati unyeti huo. Waheshimiwa Wabunge, kudai hati za Muungano zijdiliwe bungeni, binafsi, ninaona kuwa kitendo hiki kitahatarisha mwelekeo wa Muungano wetu kama ilivyowahi kutokea miaka ya 1990.

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba kunukuu aliyyasema Mwalimu Nyerere: "Nilisema awali kwamba, nilionana na baadhi ya Wabunge wenyewe hoja ya Utanganyika. Wote walipokwisha kutoa dukuduku zao kuhusu madhambi ya Serikali, niliwaambia, Waheshimiwa Wabunge yote mliyyasema ni sababu nzuri za kuchukua hatua za kudhibiti viongozi wahusika; kwa nini badala ya kufanya hivyo mnachukua hatua za kutaka kuigawa nchi yetu"?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri na wazi kuwa, Mwalimu Nyerere hakupenda nchi yetu igawanywe katika vipande vipande. Hii inadhihirika wazi alipowashauri Wabunge waliotaka hoja ya Serikali ya Tanganyika kuwa watafute namna nyingine ya kutatua kero za Muungano, lakini si kuigawa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, kuruhusu masuala nyeti ya nchi yetu kujadiliwa hadharani, madhara yake ndiyo hayo ya kutaka kuigawa nchi yetu. Ukiirejea Uongozi wa Awamu ya Pili wa Mheshimiwa Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ambao baadhi ya Watendaji walijaa hila, janjajanja, utapeli pamoja na uchu wa madaraka, ulihamasisha Serikali ya Tanganyika ili kukidhi haja yao ya uchu wa madaraka! Hata hivyo, tunamshukuru Mwalimu Julius K. Nyerere, aligundua hila za Watendaji Wakuu wa

Serikali ya Mzee Ruksa. Alipinga kwa hali na mali, alipinga kwa nguvu zote. Kwa hili alikuwa mkali kama mbogo aliyejeruhiwa! Tunamshukuru Mwalimu Julius K. Nyerere, kusimamia kidete kuutetea Muungano wetu; hivyo, kudumisha umoja na mshikamano wa taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ifahamike wazi kuwa, nchi yetu bado changa; hivyo, tusikubali kuvurugwa na watu wachache ambao wakileta hoja zao, zinalenga kuiua Tanzania! Tusiwaonee haya, pia tusione haya kuendeleza taratibu ambazo japokuwa huko nyuma zilitufaa, lakini sasa zimepitwa na wakati! Huu ni wajibu wa kila mzalendo, anayetakia mema nchi yetu ya Tanzania. Ninasisitiza masuala nyeti yanayohusu Muungano, yajadiliwe na watu wenye akili timamu, wanaoona mbali, wenye hekima na busara, wasio na pupa ya madaraka! Kwa hakika, kwa Tanzania yenyne neema, Muungano utadumu! Ewe Mwenyezi Mungu, isaidie Tanzania idumishe Muungano wake.

Mheshimiwa Spika, athari za Mazingira katika Mgodi wa North Mara – Nyamongo: ninaomba nitumie fursa hii kuelezea kwa dhati tatizo linalowakabili Wananchi wa Tarime hususan wale wanaoishi eneo linalozunguka Mgodi wa North Mara, yaani Nyamongo. Huu ni ukweli usiopingika kuwa, tangu mgodi huu ubinafsishwe kwa wawekezaji uchwara, kumekuwa na athari kubwa za kimazingira katika Mgodi huu na hivyo, kuwaathiri wakazi wanaozunguka Mgodi huu. Athari kubwa ya kimazingira ni ile ya maji machafu, yenyne kemikali za sumu kama ilivyokwishariotiwa katika Bunge hili Tukufu. Hali hii ilisababisha iundwe Tume ya Bunge kwenda Nyamongo kuchunguza athari hizo. Kitu cha kushangaza; hadi leo hakuna kinachoeleweka!

Serikali pamoja na Baraza la Mazingira (*NEMC*), wanatoa majibu ya ubabaishaji ambayo hayana kichwa wala mkia. Mheshimiwa Spika, huu ni utani! Ninamtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ajibu maswali yafuatayo kwa umakini:-

- (i) Kwa nini Serikali inatoa majibu ya kubabaisha kuhusu suala la athari za mazingira katika Mgodi wa Nyamongo?
- (ii) Je, Serikali haioni athari za milipuko ya baruti kwa makazi ya wenyeji wa Nyamongo?
- (iii) Ni sababu zipi zilizopelekea Baraza la Mazingira (*NEMC*) lisitoe majibu huhusu utafiti walioufanya kuhusiana na maji hayo ya Mto Tigite?
- (iv) Kwa nini Wataalam wa Baraza la Mazingira (*NEMC*) hukimbilia Nyamongo mara kwa mara kwa visingizio vya utafiti na huku kukiwa na wasiwasi kuwa wanakwenda kuchukua rushwa kwa mwekezaji?

(v) Mheshimiwa Waziri alizuru Nyamongo mwezi Mei, 2011; kwa maoni yake anafikiri yale Makazi ya Nyamongo yanaridhisha kwa afya za Wananchi wanaoishi kuzunguka Mgodi huo?

(vi) Serikali ina uhakika gani juu ya afya za wakazi hao kuwa ni salama?

(vii) Je, ni halali Wakazi wa Nyamongo wanaozunguka mgodi huo kuendelea kukaa katika mazingira yale?

(viii) Sasa tufanye nini?

(ix) Serikali itoe tamko gani la uhakika juu ya athari hizo?

Mheshimiwa Spika, ninasisitiza na kuisihi Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu, ifanye kila linalowezekana ili kuhakikisha kuwa, inalinda afya za Wakazi wa Nyamongo. Ihakikishe kuwa, inalinda makazi ya Wakazi wa Nyamongo. Tuache kutania afya za Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litawezekana ikiwa Serikali yetu itaacha mara moja kuwaabudu wawekezaji na badala yake ihakikishe kuwa, inatetea Wananchi wake kwa hali na mali. Hivyo basi, ninaiagiza Serikali ihakikishe kuwa, inashirikisha Mwekezaji wa Mgodi wa North Mara ili iwalipe fidia halali Wakazi wote wa Nyamongo, wanaoishi kuzunguka Mgodi huo. Wakazi hao walishalipwa fidia halali waondoke eneo hilo na hilo eneo libaki kwa ajili ya shughuli za uchimbaji dhahabu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa jambo hili, ninaomba Serikali ihakikishe inatekeleza jambo hilo. Ikiwa utekelezaji wake hautafanyika haraka iwezekanavyo, ninaamini kuwa, Wananchi wa Nyamongo watajichukulia sheria mkononi dhidi ya mmiliki wa Mgodi wa North Mara: Nyamongo.

Mheshimiwa Spika, ninasisitiza kuwa, ikiwa Serikali haitatekeleza jambo hili haraka iwezekanavyo, nami nitaongoza mapambano makali ili kumwondoa mwekezaji huyo haramu!

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ninaiomba Serikali ijue wazi kuwa, maeneo yote ya migodi nchini Tanzania, kuna migogoro baina ya Wawekezaji na Wananchi, kwa sababu Wawekezaji wamekuwa matapeli. Wamekuwa matapeli kwa sababu kuna ahadi nyingi za kitapeli ambazo hazitekelezeki, ambazo waliwaahidi Wananchi wa maeneo husika. Ahadi hizo hi pamoja na huduma za barabara; huduma za zahanati/hospitali; huduma za maji safi na salama; huduma za elimu; huduma ya umeme; na malipo ya mrabaha halali ya rasilimali yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro zote hizo, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kukupongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais

(Mazingira). Pia ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Bilal, kwa ushindi mkubwa waliopata katika Uchaguzi Mkuu wa 2010.

Katika mchango wangu katika Bajeti hii, nitajikita zaidi katika kampeni dhidi ya uharibifu wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na janga kubwa la uharibifu mkubwa wa mazingira hasa kwenye maeneo ya migodi; mfano, Nyamongo kwenye Mgodi wa *North Mara Gold Mining*, Buzwagi na *Geita Gold Mining*. Maeneo mengine yanayokabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira ni katika maeneo ya wafugaji kwa ufupi ni Ngorongoro, Karatu, Shinyanga na Monduli.

Hili ni janga kubwa kama yalivyo majanga mengine kama vile vita, matetemeko ya ardhi, maradhi (magonjwa). Pia kadiri mazingira yanavyozidi kuharibika, yanaathiri moja kwa moja hali ya mvua, ambapo kama hatua madhubuti hazitachukuliwa, basi mvua kidogo tunazopipata zitakwisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, Shinyanga ni moja ya Mkoa unaoathirika zaidi na kwa kasi kubwa, ambapo imo katika tishio la kuwa jangwa kama hatua za makusudi hazitachukuliwa. Mvua imekuwa tatizo kubwa na hii ni kwa sababu ya ukosefu wa misitu (miti) na uvunaji mkubwa wa misitu kwa matumizi ya nishati na ufugaji mkubwa wa mifugo; ng'ombe wamekuwa ni chanzo.

Ukosefu wa mvua za kutosha, umekuwa sababu kubwa ya ukame na ukosefu wa chakula cha kutosha kwa wakulima. Njaa imekuwa ni tishio kubwa kwa Jamii ya Kanda ya Ziwa na hali hiyo itazidi kuwa mbaya katika miaka michache ijayo kama mikakati mahususi haitachukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, *climate change* ni tatizo kubwa duniani ikiwemo Tanzania. Je, Serikali inajiendaaje kukabiliana na changamoto hizi? Tanzania ukilinganisha na miaka ishirini iliyopita, imeporomoka sana katika utunzaji wa mazingira. Ninaishauri Serikali iongeze Bajeti ya Kampeni ya Utunzaji wa Mazingira kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya mpaka Taifa na Jamii. Taasisi zote zihimizwe kufanya kampeni za utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuchukua ni kama zifuatazo:-

- (a) Bajeti iimarishwe katika Idara hii ili iwe na uwezo wa kufanya kampeni na Miradi ya Mazingira.
- (b) Elimu ya umuhimu na madhara ya uharibifu wa mazingira.
- (c) Asasi na Taasisi mbalimbali zishirikishwe katika Kampeni ya Utunzaji wa Mazingira.

(d) Kampeni mahususi inahitajika katika Mkoa wa Shinyanga ili kuikabili athari kubwa ya kutokea jangwa hususan Kishapu, Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijiji, Kahama na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utunzaji wa Mazingira zisimamiwe ipasavyo ili hatua za kinidhamu na kisheria, zichukuliwe ili kukomesha vitendo vyta uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Hotuba nzuri ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Pamoja na pongezi nilizozitoa, nimeona kuna maeneo muhimu bado utekelezaji wake umekuwa wa maneno maneno mengi, yasiyo na tija kwa Watanzania. Haya nitakayoyaeleza, ninaomba nipatiwe majibu ya uhakika kwa vile siyo mara kwa kwanza kuyazungumza ndani katika Bunge hili Tukufu.

Ninaomba niseme kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Gairo, hawakunituma kuja humu kurudiarudia maneno na kupiga makofi na sitopenda tena kurudia haya niliyozungumza sana kuhusu uharibifu mkubwa unaofanywa na watu katika misitu asili ya Milima ya Ukaguru kwa makusudi na kusababisha vyanzo vyta maji kukauka kwa kasi ya ajabu. Ikumbukwe kuwa, mito mingi inayohudumia Wananchi wa Wilaya ya Kilosa kama vile Mto Mkondoa, Mto Rudewa na Mto Mvumi na Msowelo, yote inatoka Jimbo la Gairo Tarafa ya Nongwe. Pamoja na Mito hii hainufaishi watu wengi wa Jimbo la Gairo kwa vile inaelekeea Jimbo la Kilosa Kati.

Ikumbukwe Mito hii hujichanganya na kuwa Mto Wami. Cha ajabu, Wizara ya Mazingira pamoja na kupewa jukumu hili, haijaona umuhimu wowote wa utunzaji wa mazingira katika maeneo muhimu ya nchi kama haya, pamoja na maeneo ya Kata ya Rubeho kwenye vyanzo vyta maji yaendayo Wilaya mpya ya Gairo. Siyo siri tena, kutupianana mpira na Halmashauri ya Wilaya, nani mwenye jukumu ni kuendelea kuharibu mazingira kwa kasi ya makusudi. Nilikwishaeleza kwa kina kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, kushindwa kudhibiti kwa uwezo mdogo wa Watendaji wake, pamoja na uzembe. Je, tuache au tunyamaze tukiendelea kuona hali halisi ikizidi kuwa mbaya?

Nini maana ya Wizara hii na ina meno gani katika kuhakikisha mazingira ya nchi hii yanaheshimiwa na kutunzwa na siyo kutupiana mpira na baadhi ya Halmashauri zembe kama ya Kilosa wakati Wizara inajua madhara yake?

Kwa kuwa utunzaji wa mazingira ni muhimu sana; ni vyema Serikali ikazingatia changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Je, Serikali pia ina mkakati gani wa kuhakikisha Tanzania inanufaika na Mpango wa *Carbon Credit*; na kwa kiasi gani tangu Mpango huu ulipoanzishwa hadi kufikia sasa?

Kwa haya ninategemea Wizara itawajibika na utunzaji wa mazingira katika Jimbo lote la Gairo, ambalo sasa pamoja na kutoka vyanzo vingi vya maji, pia Jimbo hili lina milima mingi ya kihistoria, ambayo ilikuwa na misitu asili na sasa milima hiyo imekuwa mieupe bila sababu za makusudi za kuishughulikia na kuilinda.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Maafisa wao, kwa jinsi walivyoandaa na kuwasilisha Hotuba yao ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Viongozi wote ambao wameendelea kusimamia na kuulinda Muungano.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ili lifanikiwe linahitaji sana ushiriki na uelewa wa umma. Hivyo, elimu inahitajika sana mashulenii kwa makundi na kila mara nafasi inapojoitokeza. Tuweke *resources* nyingi kama tulivyoutangaza UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, uchomaji moto mbuga unaendelea kwa kasi. Mikakati iliyowekwa, kwa mfano, Mkoa wa Kagera, haijazaa matunda, pamoja na jitihada kubwa ya Viongozi; labda zifikiwiwe mbinu nyingine.

Mheshimiwa Spika, uchomaji mkaa umemaliza misitu, tujitahidi *ku-develop gas* na kuisambaza. Ikiwezekana tuzalishe *gas* yetu ya kutosha na isambazwe angalau mijini kwa bei nzuri ili matumizi ya mkaa yapungue na hivyo kuokoa miti.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia eneo moja tu lifuatalo:-

Kuchelewa kwa taarifa muhimu zinazohusu mazingira katika Miradi ya Maendeleo: Kama tunavyojua, Miradi mingi ya Maendeleo, inahitaji kutanguliwa na uchunguzi kama vile *Environmental Impact Assessment*; na pale ambapo kwa bahati mbaya Miradi imetekelizwa bila kufanyiwa uchunguzi wa mazingira, *Environmental Management Audit*, hufanyika kama kuhalalisha. Uchunguzi huu ni muhimu sana, tukizingatia athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza baada ya Miradi husika kutekelezwa. Uzoefu katika Miradi mingi, hasa ile ninayohusika nayo ya ujenzi wa mabwawa na Miradi mingine mikubwa ya maji na kilimo; ni kwamba, uchelewaji wa utekelezaji wa Miradi unachangiwa kwa kiasi fulani na kuchelewa kwa taarifa za uchunguzi wa mazingira. Inawezekana mkawa na upungufu wa wataalam. Mimi ninashauri pale ambapo wataalam katika fani husika hawapo, mtumie Wataalam Washauri (*Consultants*) ili kuharakisha zoezi. Kwa mfano, Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji ina maeneo mengi, ambayo siyo rahisi kupata wataalam wote katika Sekta moja. Mfano halisi; Bwawa la maji ya umwagiliaji na mashamba ya umwagiliaji:-

- (i) Athari ya *catchment degradation*;
- (ii) Athari ya chumvi ardhini – *sodicity na alkalinity*;

- (iii) Athari ya magonjwa yanayotokana na maji; malaria, kuhara, kichocho na kadhalika.
- (iv) Matumizi ya mbolea na athari kwa wanadamu na viumbe wengine (Lake Manyara ni mfano mzuri).
- (v) Ujenzi wa mabwawa karibu na Hifadhi za Taifa.

Mifano hiyo michache na mingine ambayo sikuitaja, inaonesha dhahiri uhitaji wa wataalam wa fani mbalimbali. Ushauri wangu ni kutumia washauri (makampuni ya binafsi) ili utekelezaji uweze kufanyika na taarifa zipatikane kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninawapeni pongezi kwa Hotuba nzuri inayohusu Muungano na Mazingira; hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, Hotuba yao imekuwa *comprehensive* kwa kuonesha maeneo yenye mafanikio. Mafanikio katika vikao vya pamoja kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya *Joint Finance Committee*, yafanyiwe kazi haraka ili kuondoa manung'uniko ambayo yanadhoofisha Muungano wetu. Mapendekezo mengine ya Kamati ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, yafanyiwe kazi na yawekewe *Programme of Action* ili kuweza kujipima hatua kwa hatua ili kuona ni kwa kiasi gani tunapunguza kero za Muungano. Katika kipindi hiki cha miaka 47 ya Muungano, Muungano wetu ni imara kisiasa, kiuchumi na kiulinzi. Serikali ya Umoja wa Kitaifa (*GNU*); ni kielelezo tosha cha kuimarika kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana katika kusimamia na kutekeleza Sera na Sheria za Mazingira. Hali yetu ya mazingira siyo mbaya sana, ila ipo haja ya kuimarisha elimu ya mazingira kwa Wananchi wetu. Wizara ya Mazingira iendelee kuzibana nchi zilizoendelea, ambazo zinachafua sana mazingira ya Dunia. Nchi zenyе viwanda vikubwa kama zile za G 20. Sisi kama nchi maskini ni lazima tufaidike na Mikataba (*Protocol*) mbalimbali ambazo tumeweka sahihi. Mikataba hiyo ni kama *Kyoto Protocol*, *Biodiversity Convention*, *Climate Change* na kadhalika. Dunia ni *Global Village*, uharibifu wa mazingira kwa nchi moja, huathiri nchi nytingine. Hapa nchini Baraza la Mazingira limefanya kazi nzuri, waendelee na kazi hiyo. Tunashauri yafuatayo:-

- (i) Bajeti: Baraza lipatiwe Bajeti ya kutosha ili waweze kufanya kazi zao kikamilifu.
- (ii) Wafanyakazi: Idadi ya wafanyakazi iongezwe ili ilingane na kazi kubwa ya kutunza mazingira yetu.
- (iii) Jengo la Mazingira: Serikali ikamilishe Ofisi ya *NEMC* ili wawe na mahali pazuri pa kufanya kazi

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebahatika na kuwa na madini ya aina mbalimbali; dhahabu, nichel, shaba, urani na kadhalika. Inasadikiwa kwamba, nchi yetu pia huenda ikawa na mafuta. Hivyo, inabidi kijiandaa mapema ili tuweze kukabiliana na athari za mazingira hasa katika eneo la mafuta (*oil industry*), iwapo tutagundua mafuta. Hii pia inahusu madini mengine kama urani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, athari za tabia nchi; Ninaipongeza ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa ukuta wa Bahari Pangani. Tayari tumepoteza Kisiwa cha Maziwe kutokana na athari za tabia nchi. Zaidi ya hayo, fedha zitolewe kwa kutunza mazingira na kuimarisha elimu kuhusu athari za tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania tumekuwa maskini wa uwezo wa kutafuta vyanzo vingine vya nishati hasa ya matumizi ya nyumbani; mpaka leo tunaingia miaka hamsini ya Uhuru bado tunategemea kupika kwa kuni vijijini na mkaa mijini. Hali hii ni ya hatari kwa nchi yetu, itaendelea kuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 katika Bajeti ya Wizara ya Mazingira, Serikali ilituambia imepunguza kodi kwenye mafuta ya motopoa, lakini mpaka leo hayo mafuta hayapatikani kirahisi. Vilevile mafuta hayo jinsi yalivyo, hayawezi kutumiwa na nyumba yenye familia kubwa au kutumika kwenye majiko yanayopika vyakula vigumu, ikiwemo maharage, makande na vyakula vingine vigumu.

Mheshimiwa Spika, tunayo *gas* lakini haitumiki kwa matumizi ya nyumbani, kwani *gas* inayotumika sasa inatoka nje ya nchi na ni ghali, Mtanzania wa kawaida wa kijijini hawezu kumudu.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Chumvi Uvinza, mpaka leo wanatumia kuni au magogo; hivyo, maeneo ya Uvinza yanaendelea kuathirika kwa kukatwa ovyo kwa miti. Serikali ihakikishe umeme unapatikana ili Kiwanda hicho kisiendelee kutumia magogo. Wakati umeme haujapatikana ni vyema basi Serikali ikawalazimisha watumiaji wenye kiwanda kupanda miti kadiri wanavyokata ili kunusuru eneo la Uvinza kuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hasa katika Miji yetu Mikuu, uchafu umekithiri, harufu mbaya pia ni tatizo linalosbabishwa na uchafu; ni vyema sasa Serikali ichukue hatua nzuri kama Mji wa Moshi ulivyojitetu kwa usafi. Mbinu iliyotumika Moshi itumike nchi nzima na elimu itolewe kwa Wananchi juu ya usafi shirikishi.

Mheshimiwa Spika, maji taka na yenye sumu yatokayo viwandani bado ni tatizo kubwa sana. Viwanda vingi havina *system* nzuri ya utupaji, utiririshaji maji taka na yenye sumu. Mfano, kiwanda cha *Mkuani Traders* na *Azania Wheat Flour Ltd* vinatiririsha maji taka katika mazingira ya makazi ya watu. Serikali ichukue hatua vivyo

hivyo *system* ya majitaka ya Mabibo Hosteli ifanyiwe marekebisho ili majitaka hayo yasiendelee kutiririka ovyo kwenye mito iliyoko katika mto pembedi ya makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, bado Wananchi wa Kigoma hawajapata elimu ya kutosha kuhusu suala zima la utunzaji wa mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kuhimiza ofisi inayoratibu Programu hiyo, iendelee kufanya mafunzo ili Wavuvi na Wananchi wa kawaida wafahamu umuhimu wa Programu hiyo na lengo lake, lakini vilevile umuhimu wa Wananchi kushiriki matunzo ya mazingira yao ya Ziwa Tanganyika.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, taarifa ni nzuri, yenye maelezo ya kina. Pamoja na hayo, ninapendekeza ufanuzi katika yafuatayo:-

(a) Je, Programu ya Mazingira Kitaifa ina *Vision* gani kuhusu Mazingira Kitaifa?

(b) Je, kumekuwa na changamoto zipi ambazo Wizara imekuwa inakutana nazo na mikakati gani inatumika au itatumika kukabiliana na changamoto hizo zinazohusu utekelezaji wa kemikali chakavu kwa Taasisi za Serikali na zile za binafsi hasa kutoka viwanda mbalimbali ambavyo sasa viko jirani au sehemu zingine vipo ndani ya makazi ya watu hasa vile vya Dar es Salaam?

(c) Je, Serikali ina Programu gani endelevu kwa ajili ya hifadhi hai (*Biosphere Reserves*) kwa manufaa ya nchi nzima hasa katika eneo la *Capacity Building* kwa Watendaji na Wasimamizi wake katika ngazi za Wilaya na Mkoa?

MHE. AMINA A. CLEMENT: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Waziri wa Mazingira, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuendeleza kufanya usafi katika miji yetu. Ninaomba changamoto hii isisite ili nchi nzima iweze kuweka miji yote safi.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hili lisiwe kwa nchi kavu tu, pia maeneo ya Ukanda wa Baharini yaangaliwe sana kwa sababu baadhi ya meli hutoka mbali na kuja kuchafua mazingira ya bahari kwa kumwaga mafuta machafu wanaposafisha matangi yao na kuchafua mazingira ya bahari yetu. Ninaomba sana Wizara yako, iweke ulinzi wa uhakika baharini ili inapotokea meli kufanya hivyo, ikamatwe na kuchukuliwa hatua zinazofaa. Kwa sababu wakimwaga mafuta hayo huua hata samaki wadogo na wakubwa; na pia wanapoingia mafuta machafu huwa hatarini kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana ulinzi wa kulinda bahari yetu uboreshwre kwa kuenzi na kutunza mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie suala la mazingira kwa upande wa Zanzibar. Zanzibar kuna misitu na wafugaji wa asili wapo, lakini Wizara haijafika huko kuwahamasisha wafugaji wa nyuki ili ipatikane asali ya kutosha na wafugaji hao baadaye wapatiwe mafunzo na vifaa kwa ajili ya ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Muungano, kwa hotuba nzuri sana. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ni naomba Muungano uendelee, lakini kama kuna upungufu unaoonekana uboreshwe; pia kama kuna maeneo yaliyokuwa siyo siri ya Serikali, basi Wananchi wafundishwe ili wajue makubaliano ya Muungano huo. Ninaomba Serikali iboreshe Muungano huu, kwani walioleta Muungano huu hawakuwa na nia mbaya, walipenda kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Mawaziri wote wawili, Muungano na Mazingira, kwani Wizara hizo zote ni nyeti, lakini ukweli wanawake hawa wanamudu vyema majukumu yao. Pamoja na pongezi hizo, naomba nimpongeze sana Makamu wa Rais kwa kuongoza vyema ofisi yake na kumsaidia Mheshimiwa Rais. Tunamwamini, lakini ningeomba sana yafuatayo yaangaliwe ili kuokoa mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Peramiho ni miongoni mwa maeneo machache yaliyopo Tanzania ambayo bado yanapata mvua za kutosha na kuzalisha chakula kwa wingi, lakini kutokana na tatizo kubwa la kutotunza mazingira, uko uwezekano wa nchi yetu kuharibu mazingira na kukosa mvua na hivyo kuongeza uhaba wa chakula. Halmashauri ya Wilaya ya Songea ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zinatamani sana kuboresha mazingira, imejitahidi kuwa na miradi kadhaa katika bajeti ya kuhifadhi mazingira lakini kutokana na ukomo wa bajeti Serikalini, miradi mingi imekosa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuitia Idara na nchi wafadhili, tunaomba watusaidie ku-*support* miradi miwili ya kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji. Tafadhali msaada huo ni wa haraka sana. Naomba kwa heshima yote Mheshimiwa Waziri atukubalie kusaidiana nasi katika hili. Mradi wa *biogas* (1) na uhifadhi mazingira (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uchafuzi mkubwa sana wa mazingira katika miji mingi, makazi ya watu barabara na kadhalika viko katika hali mbaya. Pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais kuzindua kampeni ya usafi nchini bado hali si njema, kwa nini Serikali isilete Bungeni Muswada wa Sheria ambaa utaweka masharti ya usafi ya jumla nchi zima kuliko kuachia sheria ndogo tu za Halmashauri zifanye kazi mfano njia kuu hazina vyoo, na kama viro haviingiliki.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Makatibu Wakuu

pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mipango madhubuti kuimarisha Muungano pamoja na kuboresha mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, napenda kuunga mkono hoja hii kabla sijaanza kutoa mchango wangu amba nina matumaini makubwa kuwa Serikali itapokea maoni yangu wakati Mawaziri wakijibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu, napenda kumpongeza kipekee Mheshimwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutatua kero za Muungano hasa Zanzibar ambako kulikuwa na matatizo makubwa kupitia Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuboresha Muungano wetu, napenda kushauri kama ifuatavyo: Kwa kuwa huwa kuna Wabunge wanatoka kwenye Baraza la Uwakilishi watano kuingia Bunge la Tanzania ni, vyema basi wakateuliwa Wabunge watano kutoka Bunge la Tanzania kwenda kwenye Baraza la Uwakilishi ili kuleta uwiano ulio sawa. Ningefurahi kupata maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Serikali kukataza wananchi kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa kwa matumizi ya nyumbani, kwani ni ukweli usiofichika kuwa wanamaliza miti na kusababisha ukame na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wanakata miti na kuchoma mkaa kwa sababu tu bado hawajapata nishati mbadala, ningeishauri Serikali kutenga fungu la kutoa elimu ya kutosha ya nishati ambayo ni bora ili wananchi waache kutumia mkaa kwa matumizi mbalimbali hasa matumizi ya nyumbani. Nina matumaini makubwa elimu ikitolewa kwa nishati mbadala wananchi wataacha tabia ya kukata miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji wa miti ya mikaratusi, kwa kuwa Serikali ilishatambua kuwa miti hiyo inanyonya maji sana na kusababisha ukame, hivyo Serikali ilitoa agizo kuwa miti aina ya mikaratusi sasa ianze kuvunwa na ipandwe miti mbadala ambayo haina madhara ya kuharibu ardhi kwa kilimo na kukausha vyanzo vya maji. Lakini bado kuna maeneo mengi ya uvunaji wa polepole sana mfano Manispaa ya Singida hii miti bado ni mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya Afisa Maliasili na Mazingira, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwepo Maafisa Maliasili na Mazingira kwenye kila Halmashauri ili kushughulikia masuala ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali mambo matatu kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa kila Halmashauri ili Wakuu wa Idara hii waweze kufanya kazi vyema;

(b) Serikali kuwapa usafiri Idara hii kwa maana ya magari, siyo pikipiki, kulinda na kazi zao hasa wanyama wakaao huko vijijini. Mfano, maafisa maliasili wa Wilaya ya Manyoni, Singida Vijijini na Iramba, Wilaya hizi ni kubwa na zina wanyama wakali; na

(c) Serikali kuongesa maafisa Maliasili hadi kwenye Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia tena kuunga mkono hoja kwa kuwataki kazi njema.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri wenyewe dhamana ya Muungano na Mazingira kwa hotuba nzuri ambayo imetoa ufanuzi mzuri kuhusu mambo yanayohusu Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujivunie Muungano wetu ambao sasa umetimiza miaka 47 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1964. Huu ni mfano wa kipekee Barani Afrika na pengine duniani. Napongeza juhudhi ambazo zimefanywa kutatua kero za Muungano. Nashauri juhudhi zaidi ziongezwe ili kero zilizobaki ziweze kutafutiwa suluhisho mapema iwezekanavyo ili kuimarisha Muungano wetu.

Naipongeza *NEMC* kwa kufanya *Environmental Impact Assessment (EIA)* kabla ya kuanzisha miradi mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo, uwezo wa *NEMC* kufanya kazi hiyo nchi nzima ni mdogo. Kutokana na hali hiyo, miradi mingi imechelewa kuanzishwa. Mfano mzuri ni Makapuni mengi ya simu yameshindwa kueneza mawasiliiano nchini kutokana na *NEMC* kuchelewesha kufanya *EIA*. Hivyo, kuna umuhimu wa *NEMC* kuimarishwa au Halmashauri ziwezeshwe kufanya kazi hiyo ili kupunguza ucheleweshaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchafuzi wa mazingira unachangiwa na wasafiri wa mabasi ambao hununua vyakula njiani katika mifuko ya karatasi au *plastic*, maji katika chupa na kadhalika na baada ya kutumia, abiria hutupa mifuko na chupa hizo barabarani. Kutokana na hali hiyo nashauri yafuatayo:-

(i) Kila Basi liwe na mahali ndani ya basi pa kutupa takataka badala ya kutupwa nje barabarani; na

(ii) Katika barabara zetu kuwepo na maeneo maalum yenyeye mapipa ambapo taka kutoka ndani ya basi zitamwagwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kutoka vyombo vya kisayansi zinasema kwamba mabadiliko ya tabia ya nchi yatazidi kuendelea katika miaka ijayo na hususan katika nchi za ukanda wa Mashariki mwa Afrika na kuleta majanga mbalimbali kama vile ukame na mafuriko. Baadhi ya majanga yamekwishajitokeza katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania. Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hili katika nchi yetu, ukanda wa Afrika na

dunia kwa ujumila, Tanzania imeweka mkakati gani wa dhati katika kukabiliana na tatizo hili?

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia 100 baada ya kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu *Rest House* ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, juu ya ubovu wa Jengo la Ikulu - Chakechake Pemba ambalo likiwa makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili linachafua hata mazingira ya eneo la Ikulu kwa kuwa ni bovu sana na sasa umekuwa muda mrefu halijafanyiwa ukarabati mkubwa au kulivunja na kuweza kujengwa lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu wa kitaifa wakifanya ziara zao Pemba wanapata taabu ya makazi kwa sababu wanafikia kiwango cha viongozi kukodiwa hoteli kitu ambacho siyo maadili mazuri kufanyiwa viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara hii iweze kufanya ukarabati mkubwa au kujenga upya *rest house* ya Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopo Ikulu Chake Chake Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iipe kipaumbele elimu juu ya Muungano, maana wananchi wengi hawaelewi Muungano wa nchi hizi mbili Zanzibar na Tanganyika. Wanaolewa zaidi ni wazee wetu ambao wameshafariki. Baadhi ya wananchi hasa vizazi vipyta hawaelewi undani na udhati wa Muungano wetu na ndio maana huwa wanajitokeza watu sasa wanaoupinga Muungano. Sababu kubwa ni kukosa elimu ya uraia juu ya Muungano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, somo la uraia ni muhimu katika shule zetu ili kuvifanya vizazi nya sasa kujua hali halisi inayoendelea juu ya faida ya Muungano, changamoto na suluhib sho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu haupo kipekee duniani. Kuna nchi kama Marekani ambayo ni matokeo ya Muungano wa Majimbo 49 na nchi ya *Texas*. *Texas* ilikuwa nchi kamili kama ilivyokuwa Tanganyika na Zanzibar. Siyo kweli kwamba Muungano wa Marekani hauna doa au raia hawaoni jambo lolote la kujadili. Lakini Serikali ya Marekani haina utani katika suala la Muungano. Sheria hairuhusu matendo ya mijadala inayoleta hisia za kuvunja Taifa lao. Mijadala mingi inalenga katika kuwaenzi waasisi wa Taifa lao.

Mfano, mwaka 1999, raia mmoja wa *Texas* alipandisha bendera ya *Texas* porini akidai uhuru wa *Texas*, alichukuliwa hatua kwa kufungwa miaka 93 jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa muundo wa Muungano unatofautiana, lakini utaratibu uliotumika kuunganisha Marekani na Texas unafanana na utaratibu uliotumika kuunganisha Tanganyika na Zanzibar. Ni kweli kwamba kuna matatizo ya msingi yanayohusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambavyo nadhani yanatokana na vitu vifuatavyo:-

- (a) Muundo wa Muungano;
- (b) Utendaji; na
- (c) Ubinafsi wa viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, matatizo ya namna hii yamekuwa yakiwakera sana wananchi kiasi cha kuuchukia Muungano huu, na wengine hata kutaka Muungano huu uvunjwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kuwa siku ya Maadhimisho ya Muungano itumike kuwakumbusha Watanzania kuwa Muungano wetu ni halali na umetokana na taratibu halali zilizokuwepo wakati hizi nchi mbili zinaungana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Muungano uliridhiwa na Bunge halali la Baraza la Wawakilishi na Bunge halali la Tanganyika kwa wakati huo. Kuuvunja Muungano hakufuti ukweli huo, na hata Muungano ukivunjika, kero za Muungano hazitatatuliwa, bali zitahamia Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za kuhamarisha Muungano zinazoibuliwa sasa, eti kwa sababu ulifikasiwa bila kura ya maoni kutoka kwa wananchi, hazina mantiki yoyote kwani utaratibu wa kura za maoni ni mpya kwa mafunzo ya sheria za nchi za Jumuiya ya Madola. Ulianza kutumika miaka ya 1970. Kwa hiyo, wakati Mwalimu Nyerere na Karume wanafikia Muungano wa nchi zao walikuwa sahihi walivyofanya kwani Katiba iliruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapendekezo yangu ni kwamba:-

- (1) Muundo wa Muungano ni vyema ukajadiliwa ili uwe ni Muungano unaoendana na wakati uliopo kwa lengo la kuuimarisha;
- (2) Serikali iendelee na juhudzi za kutatua kero mbalimbali za Muungano; na
- (3) Baadhi ya wananchi bado wana kasumba za kikoloni za kuuchukia Muungano, Serikali iendelee kuelimisha umma juu ya umuhimu wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dr. Gharib Bilali kwa kuteuliwa na kuaminiwa na wananchi kushika nafasi hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu - Waziri wa Nchi, Muungano katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri anayoifanya tokea ameteuliwa kushika wadhifa huo. Nampongeza pia Waziri wa Nchi, Mazingira, kwa kazi nzuri anayoifanya. Akina mama hawa wamethibitisha kuwa wakiwezesha wanawea. *Well done for the good job.*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira ni suala nyeti na linahitaji umakini mkubwa. Naomba tudhihirishe elimu ya mazingira kwa wananchi wetu kuititia radio na hata *television*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ifanye kazi kwa karibu sana na Ma-Jiji, Manispaa na Halmashauri za Mitaa kuhusu utunzaji wa Mazingira. Bado miji yetu ni michafu, takataka zinatupwa ovyo, mamlaka za miji zimeshindwa kutoa vifaa vya kuwekeea taka kama mapipa na kadhalika, kuwawezesha wananchi kutupa takataka ovyo. Kila baada ya nyumba mbili au tatu pawe na pipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri katika mapipa uwepo udhibiti mzuri wa taka kwa abiria wasitupe taka ovyo na mabasi yawe na vifaa ya kutunza taka. Mabasi yasiyo na vifaa, wahusika wachukuliwe hatua hasa wenye mabasi. Hatuwezi kutunza mazingira vizuri kama gharama za umeme zitaendelea kuwa ghali hasa za kuunganisha umeme majumbani. Miti itaendelea kukatwa ili kupata kuni na mkaa. Hili linahitaji kutazamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, inakushukuru kwa kunipatia nafasi nami nitoe mchango wangu. Ninaanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania -Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dr. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa kura nyingi na CCM kuendelea kushika dola. Aidha, nakupongeza wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge letu Tukufu ukiweka historia ya kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili halikuja hivi hivi tu, lakini wapigakura wako tumekupima na kuthibitisha kwamba unaweza, Mungu yupo pamoja nawe, chapa kazi bila hofu yoyote. Nasi Wabunge hasa wanawake tuko pamoja nawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia Muungano na wataalam wake kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu wa Zanzibar na Tanganyika sasa umetimia umri wa miaka 47. Katika kipindi chote hiki, mafanikio mengi yamepatikana ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Lakini lazima tukubali kwamba kwenye mafanikio na

matatizo hayakosekani. Muungano huu ni wa watu na sio wa vitu. Hivyo lazima changamoto zitakuwapo tu. La msingi ni kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto hizo zinapojitokeza, Serikali isitoe mwanya kwa watu kulalamika kwa muda mrefu. Majibu hayo hayawaridhishi Watanzania hata kidogo. Pale ufumbuzi unapopatikana kwa wananchi ambao hawakuelezw, inakuwa ni sawa sawa na *zero*, kwani inakuwa ni viongozi wahusika tu wanajua huku wakiwaacha wananchi wakiendelea kulalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba elimu kwa umma itolewe kwa kero zote ambazo zimeshpatiwa ufumbuzi, na manufaa gani wananchi watafaidika kutokana na ufumbuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa uwazi kabisa ni nini kinachelewesha kutekelezwa kwa mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, aanze kwa kutufahamisha ni mapendekezo gani yametolewa na Kamati hiyo? Jibu ya kuwa mapendekezo hayo yamewasilishwa tayari kwa Serikali zetu mbili kwa tafakuri, siyo jibu muafaka kwa Watanzania wa leo. Kila mmoja ameamka na yuko makini, tuelezwe kinagaubaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, mjadala unaendelea wa kuundwa Shirikisho la Afrika Mashariki, nafasi ya Zanzibar katika shirikisho hilo itakuwa ipi? Ni hoja ambayo inahitaji kufanyiwa kazi mapema na kuwekewa msimamo madhubuti ili isije ikaleta kero nyngine na Watanzania wakaanza kuvutana wenyewe kwa wenyewe. Nafikiria itashiriki kama Tanzania kwa mambo ya Muungano: Je, kwa yale mambo ambayo siyo ya Muungano itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazingira ya ulimwengu yameharibika sana, athari zake zinakumba nchi zote za ulimwengu huu. Hapa nchini kwetu tunashuhudia mambo ya ajabu ambayo hayajapata kutokea. Mfano, likitoka juu, linatoka kweli na kwa kipindi kirefu na kukausha miti na mimea yote, na watu kuathirika kwa ukame. Njaa inaenea katika Mikoa na Wilaya tele. Ikinyesha mvua, ni mafuriko hata nyumba na madaraja yanasonbwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na madhara mengi, ipo haja ya kuendelea kutoa elimu ya mazingira kwa Watanzania wote. Bila kuelewa athari zake, vyanzo vyaa maji vinaharibiwa. Watu wanachoma miti oyoo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ijitahidi kubadilisha *mindset* za watu ili wachukie uchafu. Miji mingi ya Tanzania ni michafu, lakini wakazi wa Miji hiyo wanaona ni sawa sawa tu. Hawakerwi kabisa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali ihamasishe Serikali za Mitaa kuunda sheria ndogo ndogo na adhabu kali zitolewe kwa ye yule anayechafua mazingira. Aidha, vijengwe vyoo vyaa umma (*Public Toilets*) katika maeneo ya biashara, maeneo ya mapumziko na barabara kuu zinazotumika na watu wengi kwa usafiri hasa wa mabasi yanayokwenda Mikoani kuchimba dawa porini iwe ni mwiko (baada ya kujengwa vyoo).

Asilimia kubwa ya Watanzania nyumba zao hazina vyoo hasa vijijini, waelimishwe madhara yake kupitia Serikali za vijiji hata ikibidi Wajumbe ujumla 10 na hatimaye kuhamasishwa kujenga vyoo. Tukijitahidi, inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri na Watendaji wote kwa hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri na kuomba ufanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya kutoka Zanzibar kuhusu kero za Muungano, chanzo kikubwa cha kero ni wananchi kutoridhia kuwa na nchi moja na kuendeleza dhana ya nchi mbili na/au nchi tatu. Bila ya kuridhia hoja moja ya dhana, ni wazi itachukua muda mrefu kuondoa kero toka Zanzibar dhidi ya Muungano. Serikali ya Zanzibar iko huru kukusanya na kutumia mapato ya Zanzibar kwa nchi ya Zanzibar, wakati kimsingi kwa mfumo wa Serikali moja ya Muungano, mapato ya Tanzania yanakusanywa na Serikali ya Muungano bila kuingia Zanzibar ila hutoa mgao kwa nchi ya Zanzibar. Ni vyema umma ukajua na kupata ufanuzi juu ya hisia za huo mfumo wa mapato kama ndivyo hivyo ulivyo au uko vipi kihalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa kodi *TRA* na uandikishwaji wa magari Zanzibar na Tanzania Bara, tumesikia malalamiko mengi ya mfumo usioridhisha wa kodi mara mbili na magari yenyenye namba zilizosajiliwa Tanzania Bara. Tumesikia hatua kadhaa zimechukuliwa kuondoa kero hizo, lakini bado zinalalamikiwa. Je, kuna nini? Majibu tunayosikia siyo sahihi au elimu kwa umma bado ni ndogo, au wapo Watendaji wakorofu wanaodharau maamuzi yanayotolewa? Kwa nini makubaliano hayo yasiainishwe katika sheria ili wanaokiuka wahesabiwe kuvunja sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar ina Serikali yake, inayo haki ya kuingia mikataba na wawekezaji katika Sekta ya Utafiti na utafutaji wa mafuta kama Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) inavyofanya. Kama Zanzibar imekamilisha ugunduzi wa mafuta, hivi ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano inayo mamlaka kuizua Zanzibar kuchimba mafuta? Hebu hili nalo liwekwe sawa, lisibaki kama kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhusiano gani kati ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Hifadhi ya Mazingira kwa mfanio, Wizara ya Maliasili na Utalii inayo misitu ya Lunguza (Muheza) na Kilombero ya miti ya mitiki. Eneo la shamba la Lunguza linapitiwa na Mto Zigi wenye chanzo katika Hifadhi ya msitu wa Amani – Muheza. Wizara ya Maliasili inavuna miti hiyo, sasa miaka ni minne mfululizo na maeneo kuwa wazi na meupe kwa miaka mingi (zaidi ya kumi na tano) kwa kuwa miti mipya inayopandwa ni midogo sana. Je, umefanyika utaratibu wa tathmini ya mazingira katika hali hii ya uvunaji ukizingatia

kwamba shamba hilo la Lunguza linapakana na Hifadhi ya Msitu wa Amani na vyanzo muhimu vya maji kama mto Zigi?

Pamoja na shamba hilo la Lunguza wiki mbili zilizopita, Wizara ya Maliasili na Utalii imetangaza gazetini tenda ya uvunaji wa eneo jipya karibu na Hifadhi ya Msitu huo wa Amani. Matokeo yake ni kuendelea na kuongeza eneo kubwa zaidi kuwa wazi na kukaribisha athari mbaya za ukame na uharibifu wa mazingira. Nashauri busara itumike kuvuna miti hiyo kwa awamu ili kupisha maotesha mapya kukua badala ya TAMAA ya sasa ya kupata fedha bila kujali athari. Kama Wizara inayosimamia Mazingira, ni jukumu lenu kuokoa Taifa la Tanzania dhidi ya uharibifu wa Mazingira hata kama mali husika (miti) imepandwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na ushauri, yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa Tanzania, hususan kwa upande wa Zanzibar wahaelewi Muungano, na hawaelewi vifungu vyote vinavyohusiana na suala la Muungano. Hivyo nashauri ni vyema Serikali ikaandaa mpango wa kuwaelimisha wananchi wote faida na hasara ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kwa upande wa Zanzibar kwamba wanakosa fursa muhimu za kiuchumi ambazo zinatokana na upande wa vianzio vya Muungano. Aidha, ili kuondoa kasoro zinazolalamikiwa na upande mmoja, hasa katika mfuko wa pamoja wa Akiba, tunashauri suala hili likamilishwe kwani kwa upande wa Zanzibar tayari kikao kimeshakaa na kimeshakubaliana, na lililobakia ni kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la wafanyabiashara ambao wanaleta biashara Tanzania Bara, imekuwa ni usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara hao wanapofika hapa Dar es Salaam, na imekuwa ni jambo la makusudi kwa Watendai wa TRA wa bandarini kuwanyanya wafanyabiashara na watu binafsi kwa kuwatoza mizigo yao mara mbili ambapo ni kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuweka uwiano wa uajiri, maofisi, vitendea kazi pamoja na wafanyakazi wenyewe, imeonekana kuwa kuna tofauti baina ya vitu hivyo. Aidha, katika kuweka usawa, ni vyema ukawekwa utaratibu mzuri, kama Bara imejenga jengo, basi Zanzibar lijengwe kama hilo, kama Bara imenunua gari VX basi na Ofisi ya Zanzibar inunuliwe gari kama hiyo, na ikiwa uajiri unafanyika kwa Ofisi za Zanzibar, basi upendeleo upewe kwa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira ni vyema Serikali ikalitia mkazo, hasa masuala ya utunzaji wa miti na kwa kuwa Serikali imedhamiria kwa kufanya Mkoaa

wa Dodoma kuwa Makao Makuu, nashauri ianzishwe operasheni maalum ya upandaji miti hasa maeneo ya mjini. Inatia unyonge sana kuona Mkoa wa Dodoma unakuwa hauna mandhari nzuri ya miti na bustani.

MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, *Gases* kama vile NO₂, PM10, SO₂ na kadhalika hutokana na muwako wa mafuta (*liquid hydrocarbon*) kwenye magari. *Gases* hizi husababisha uchafuzi wa hewa. Uchafuzi huu wa hali ya hewa husababisha magonjwa mengi kama vile pumu, nimonia, kansa za mapafu, magonjwa ya moyo (*heart – rhythm problems etc*) na kadhalika. Ninaamini uchafuzi wa hali ya hewa kwenye miji yetu mikuu kama vile Dar es Salaam, Mwanza na kadhalika, huongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kufahamu: Je, kuma vipimo vya NO₂, PM10, SO₂ vinapimwa kila siku kwenye jiji la Dar es Salaam? Pia ninaomba kufahamu kiwango cha juu na cha chini cha *air pollution* katika Jiji la Dar es Salaam. Je, kuna adhari zozote ambazo zimeripotiwa kutokana na athari za *air pollution* katika jiji la Dar es Salaam?

MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hizi mbili ambazo ziko chini ya Makamu wa Rais. Kwanza napenda kuwashukuru sana Mawaziri, Mheshimiwa Samia Suluh na Mheshimiwa Terezya Huvisa, kwani tumeona Wizara zote hizi mbili zikiongozwa na wamama wawili. Naamini akina mama tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kulipongeza Jiji la Mwanza. Pamoja na wakati wote wa jiji hilo kuendelea kuwa washindi wa majiji hapa nchini, kwa mara ya sita mfululizo huo ni umakini wa wakazi wa Jiji la Mwanza na kudhihirisha ni watu makini na pia ni rafiki wa mazingira. Nasema, nawapenda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za misitu kukatwa ovyo haitaweza kupungua, kwani nchi yetu inakabiliwa na tatizo hilo, hasa wale ambao wanakata miti kwa ajili ya nishati ya kupikia, mfano kuni na mkaa. Ukataji miti huu ni mkubwa sana hasa ukizingatia nishati ya umeme, bado ni kitendawili. Mijini bado ni mgao wa siku mbili hadi nne zote za mgao? Nishati ya gesi ni ghali sana, na Watanzania wengi hata hapa mjini ni wachache wanayoitumia. Watanzania wengi gesi ni maisha ya anasa. Je, misitu itapona kwa njia gani? Tukifanikisha kutokata misitu, tujue wazi Watanzania watakufa na utapiamlo. Ushauri wangu ni kutumia fedha tulizonazo kwa kupanda miti kwa wingi wa kuifutilia katika utunzaji ili kuepukana na athari. Serikali iwape elimu zaidi watu ili wawe na mwamko wa kupanda miti hata mara nne kwa mwaka pamoja na kuitunza. Pia tuwazawadie watu ambao wanapanda miti na kuitunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, Serikali kupitia Ofisi ya mazingira na Halmashauri zetu isimamie sheria za mazingira, pia kutoruhusu kufanya ujenzi karibu na vyanzo vya maji kama ilivyo katika Jiji la Mwanza ambapo kumejengwa hoteli nyingi kando ya Ziwa Victoria na nyingine kuta zake zimegusa maji, mfano hoteli ya Malaika huko Ilemela na nyinginezo. Nadhani huu ni uharibifu wa mazingira pia. Naiomba

Serikali ijaribu kwanza kutafuta nishati mbadala ili tuweze kuwaomba Watanzania wapunguze ukataji misitu kwa ajili ya mkaa na kuni. Pia elimu ya utunzaji wa mazingira ianzie Shule za Msingi kama somo, kama ambavyo wanafundishwa athari za Ukimwi tangu Elimu ya Msingi. Nina imani tutafikia lengo, kwani wote dhamira yetu ni moja na kutunza mazingira yetu ili nayo yatutunze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kero za Muungano, ni dhahiri tukitaka ziishe zitakwisha. Kama Wazanzibar CCM na CUF leo wanakula pamoja, ambapo ilikuwa haiwezekani hapo nyuma, itakuwa Zanzibar na Tanganyika ambapo ilizaa Tanzania? Kwanza naomba kusema Muungano udumu daima, lakini ni ndani ya Ilani ya Chama cha Wananchi – CUF, kwa kuwa na Serikali tatu (i) Serikali ya Zanzibar (ii) Serikali ya Tanganyika (iii) Serikali ya Muungano. Hapo tutafahamiana na hapo ndiyo maana CUF tulihitaji na bado hadi leo na kesho tutahitaji Serikali tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Kilio cha Muungano wetu kuwa na matatizo ni bora tukae chini tutafakari kwa makini, na njia nimewapa hapo juu, naimani tutafanikiwa kabisa na bugudha ndiyo mwisho wake. Ahsante.

MHE. RUKIA K. AHMED: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kuhusu Muungano. Muungano wetu wa nchi hizi mbili kwa kweli ni mzuri na inatupasa tuuenzi na tuuthamini umoja huu. Kwa kweli umoja huu tukiuchezza na kuukejeli, basi ukija kuvunjika tuna jukumu mpaka mbele ya Mungu. Watoto wetu watakuja kutulaumu, kwani panapo moja na moja siyo moja tena. Nguvu yake ni kubwa. Maadui hawawezi kutuchezza kirahisi. Watu wetu wameshazaana, hawa watoto waliozaliwa watatulaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wetu wanafanya biashara bara na wengine wanakuja visiwani kufanya biashara, hizi zote ni faida za Muungano. Hata Serikali ya Umoja wa Kitaifa kule Zanzibar, basi ni juhudzi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hizi kasoro zilizopo, basi zirekebishwe tena haraka iwezekanavyo, kwa sababu hali hii inatia uchungu. Kero zinajulikana kila siku tunazisema na Serikali ya Muungano wanazifumbia macho. Hali hii ikiachiwa bila ya kushughulikiwa, basi itazidisha uhasama kati ya pande hizi mbili. Naomba sana Serikali itatue kero hizi.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu suala la Muungano. Kwanza naunga mkono hoja ya Muungano kwamba uendelee daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Muungano yaliyo mengi yanatokana na wananchi kutokuelewa historia ya Muungano, sababu muhimu zilizosababisha nchi hizi mbili ziungane. Yote haya yanatokana na kutokuandika historia halisi ya nchi hizi mbili zilikotoka, hadi zikaungana. Kama imeandikwa historia, ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni watu wachache hasa wale wanaojua kusoma na kuandika na wale waliokuwepo wakati Muungano unaanzishwa. Ni zaidi ya miaka 40 idadi ya watu imeongezeka, hivyo ni vyema Muungano ufundishwe kuanzia Shule za Msingi hadi Chuo Kikuu, majarida yaandikwe, vipeperushi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano utadumu daima. Naomba kuunga hoja mkono bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Ahsante.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu ni mzuri, imara na wakupigwa mfano, hivyo na mimi naunga mkono kwamba ubaki kwa sasa na kwa wakati ujao, kwani huu tayari umekuwa ni Muungano wa damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 47 ya Muungano hatuwezi kukataa kwamba yapo mafanikio makubwa ndiyo ukaweza kudumu, lakini pia zipo changamoto ambazo zikipatiwa ufumbuzi zitaondoa kero kwa wananchi wetu. Nazo ni:-

- (a) Asilimia kubwa ya kizazi chenye umri wa chini ya miaka 50, hawaujui kwa kina Muungano, hivyo wanasiasa na wanaharakati wanatumia mwanya huo kuuelezea Muungano vile wanavyotaka wao na zaidi ni kupotosha ukweli halisi wa kuungana kwetu kwa nchi zetu mbili. Hivyo, elimu inahitajika. Kutokana na hali hiyo, Muungano wetu baadhi ya rika hilo wanauangalia kwa mtazamo hasi.
- (b) Kukosekana kwa ukweli, uwazi na uwajibikaji kwa baadhi ya Watendaji wanaopewa majukumu, hivyo nia ya dhati ya waasisi wa Muungano huu, kuanza kutoweka.
- (c) Muungano wa Serikali mbili ni sera ya Chama cha Mapinduzi na mimi naiunga mkono. Lakini pia wapo waliokuwa na wazo la Serikali tatu na hata nne wanaweza kutokea. La msingi tuwe na Tume itakayotathmini mfumo tulionao wa Muungano wa Serikali mbili, faida na changamoto zake kisiasa, kijamii na kiuchumi. Hali kadhalika na mifumo mingine itakayojitokeza bila ya kusahau nguvu ya msingi ya Umoja wetu wa kitaifa.
- (d) Serikali sasa ni vyema kuelezea kwa uwazi mambo mengi yaliyotekeliza ndani ya Muungano huu kwa nchi zetu mbili ili wananchi wawe na uelewa mpana zaidi badala ya kuwaacha wasioutakia mema Muungano huu kupotosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mohamed Gharib Billal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nawapongeza Waheshimiwa

Mawaziri, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Dkt. Terezya Luoga Huvisa kwa kuteuliwa kuongoza Wizara ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati aliyekuwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kusimamia kwa makini shughuli za mazingira ambayo imeboresha kwa kiasi kikubwa mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *NEMC* kwa jitihada wanazofanya kujizatiti ili kuondoa kero za uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini. Nimekuwa nikifutilia kwa karibu sana kazi nzuri inayofanywa na Baraza hilo katika sekta mbalimbali. Yako maeneo ambayo ingawa jamii yetu haijaona bado kuwa ni kero kubwa, lakini ikiachwa bila kushughulikiwa haraka, athari zake kwa mazingira na afya ya wananchi ni mbaya. Maeneo hayo ni:-

- (a) Viwanda. Viko viwanda mjini Arusha yanayomwaga maji kwenye mto Themti na Kijenge. Maji hayo yamekuwa yakiathiri afya za watumiaji. Tarehe 28 Machi, 2011 wananchi wa Kata ya Mlangarini waliwasilisha malalamiko kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuwa huko kwenye ziara. Ni vizuri ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais kuwa kero hiyo itashughulikiwa, ikatekelezwa haraka.
- (b) Magari. Yako magari mabovu yanayoendelea kutumia barabara zetu. Baadhi yao ni mabovu kiasi kwamba yanapopita humwaga moshi unaobadili hali ya hewa kuwa giza na hivyo kuathiri uwezo wa madereva wengine na watumiaji wengine wa barabara kuona mbele kwa karibu nusu kilomita. Nashauri kuwa *NEMC* ishirikiane na *SUMATRA* kupiga marufuku magari yote ambayo hayana hadhi ya kutumia barabara kwa sababu ya ubovu. Kazi hiyo isiachiwe Jeshi la Polisi, kwani imewashinda na moshi mchafu unaomwagwa na magari mabovu kwao siyo kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na kupongeza kwa dhati dhamira ya kuimarisha Muungano wetu iliyooonyeshwa na viongozi wetu Wakuu wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nashauri kuwa juhudhi hizi ziendelezwa ili tuwe na Taifa imara lenye amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa umma kuititia vyombo vyahabari itolewe juu ya masuala ya Muungano, faida zake na wajibu wa wadau mbalimbali katika kuyaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya kero/changamoto za Muungano hutokana na mambo yasiyokuwa ya Muungano yanapoanza upande mmoja na upande wa pili kuomba na hatimaye kugeuzwa kuwa haki. Nashauri kuwa masuala yasiyokuwa ya Muungano yanapotakiwa kuendelezwu upande wa pili yafanyike kuititia mkataba maalum na kuwa na ukomo.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi pamoja na Wabunge wengine kuwepo katika ukumbi huu leo, tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia hotuba hii kwa kuweka wazi yale ambayo yamekuwa yakizungumzwa mara nyingi katika Vikao vya Bunge, vikao vya uwakilishi. Pamoja na kuundwa Tume mbalimbali za kushughulikia kero za Muungano, lakini bado zinabaki palepale na kero ni zile zile. Kwa mantiki hii, inaonekana bado Serikali haiko tayari kuondoa kero za Muungano.

Mfano mdogo wa kero ambayo ni maudhi na inazungumzwa mara nyingi sana ni wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na *TRA*. Ni tatizo la muda mrefu sana ambalo linalalamikiwa sana, lakini linabaki vilevile, tatizo lisilopata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumzia Tume ya Uchaguzi ya Taifa (*NEC*). Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Muungano Tanzania (*NEC*) bado ina matatizo ambayo yanásababishwa kwa makusudi hasa kwa Wazanzibari. Mfano mzuri juu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*). *NEC* ni Tume yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) inashughulika na programu zote za uchaguzi kwa Bara. Kuhusu uandishi wa wapigakura katika Daftari la Kudumu. Mtanzania yeoyote mwenye umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura kwa kumchagua Rais wa Muungano, Mbunge na Diwani, wala hakuna masharti magumu kumkosesha haki yake ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii ambayo ina haki kusimamia uchaguzi wa Zanzibar wa Muungano inatumia Daftari la *ZEC* ambalo lina matatizo makubwa ya kiutendaji. Tume ya uchaguzi ya Zanzibar *ZEC* ambayo mamlaka ya uchaguzi wa Zanzibar imetofautiana kisheria. Mfano Zanzibar huwezi kuandikishwa kama huna (*ZENID*), kitambulisho cha ukazi wa Zanzibar. Kitambulisho cha ukazi wa Zanzibar ni kikwazo cha makusudi ambacho hakipatikani kiurahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazanzibar wengi walikosa kupiga kura kwa sababu ya kukoseshwa makusudi (*ZENID*). Ni ajabu lakini ni kweli tupu kwamba Wazanzibar ambao tangu ukoloni ni wapigakura wa Majimbo husika wamenyimwa kupiga kura.

Kwa kuwa *NEC* wanatumia daftari la *ZEC* ambapo sheria zao ni mbalimbali, utakuta *NEC* na wao wamefuata ile ile sheria ya Zanzibar kwamba ambaye hana *ZENID* hapigi kura. Watu wengi waliachwa kwa sababu hawakupata *ZENID*, kwa hiyo, wengine wakaandika kwa daftari la Bara lakini pia wakapewa kura moja tu ya Rais wa Muungano na wakati wao ni Watanzania, ni wakazi, wanazo haki zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utakuta walioandikishwa Bara na *NEC* wamepiga kura zote, lakini walioandikishwa Zanzibar kwa daftari la *NEC* wao wamepewa kura moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuzungumzia mazingira. Uchafuzi wa mazingira umekuwa mkubwa sana ndani ya nchi ya Tanzania. Uchafuzi wa mazingira pamoa na umuhimu wake, lakini hayajasimamiwa ipasavyo. Kutokana na umasikini ambao umekithiri kwa Watanzania vile vile unachangia kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wamekuwa wanajihuisha na ukataji miti ovyo hususan kwa kupikia mkaa kwa ajili ya chakula cha kila siku. Vile vile ukulima wa kukata ovyo miti unachangia uharibifu wa mazingira. Vile vile mifugo kama ng'ombe ambao wanafungwa kwa wingi, yaani makundi kwa makundi yanachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudu za makusudi zinapaswa zichukuliwe kupambana na uchafuzi wa mazingira. Inapaswa Serikali iandae mbinu mbadala ambazo ni endelevu, ambazo zitawatoa watu katika mipango mibovu ya uharibifu wa mazingira, mbinu zitakazosaidia mapato katika maisha yao ya kila siku. Itolewe elimu itakayowafikia wananchi hasa vijijini. Vile vile mifuko ya *plastic* inaharibu mazingira na ni hatari sana. Mifuko ya *plastic* imezagaa ovyo ndani ya nchi yetu mijini na vijijini pasipo uangalizi madhubuti. Mifuko hii inafukiwa na udongo na inabaki chini ya ardhi kwa muda mrefu pasipo kuoza. Hivyo inakuwa siyo rahisi katika ardhi hiyo kuzalisha mazao hasa ya matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso langu, kama hakuna hatua madhubuti za udhibiti juu ya mifuko hii, basi ni bora kupigwa marufuku ndani ya nchi yetu. Ahsante.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpanda Vijijini ambao walinipa dhamana ya kuwa hapa Bungeni kwa heshima kubwa ya kuwa mwakilishi wao, naomba niwashukuru kwa dhati sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia suala la Muungano wa Zanzibar na Tanganyika ambao ulizaa Taifa moja la Tanzania. Muungano huu ni muhimu sana kwa wananchi wa pande mbili za Muungano wa nchi hizi mbili zilizoungana kwa hiari na makubaliano yaliyofanywa na waasisi wawili, Hayati Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume ambao waliunganisha nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, waasisi hawa walitumia busara kubwa kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Mimi naunga mkono muundo wa Muungano uendelee kuwepo wa Serikali mbili na ziangaliwe kasoro zilizopo kwenye Muungano, zirekebishwe kwa maslahi ya wananchi wa pande zote mbili. Maeneo ambayo yanatakiwa kuangaliwa ni mgawanyo wa fedha kwa Serikali zote mbili, ushirikishwaji wa masuala ya kimataifa na mfumo wa kodi uangaliwe upya. Haya yakiangaliwa, naamini Muungano huu utadumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira ni muhimu sana katika maisha ya Watanzania. Tusipoangalia kwa undani zaidi, Taifa hili litaingia katika wakati mgumu sana. Serikali lazima iandae mpango mkakati wa kulinda mazingira, vinginevyo Taifa hili litakuwa Jangwa. Eneo la kwanza la kuangalia ni suala la mifugo. Mifugo inaharibu

sana mazingira ya nchi hii. Serikali isipodhibiti ufugaji wa bila mpangilio maalum, basi vyanzo vyote vya mito, mabwawa, ziwa na misitu itatoweka, kwani idadi ya mifugo ni mingi sana iliyopo katika nchi hii inayoendelea kuharibu maeneo mbalimbali na kuhamia katika eneo lingine la nchi hii. Hivyo naiomba Serikali idhibiti ufugaji wa kuhamahama. Tukiacha ufugaji holela, basi vyanzo vyote vya maji na misitu itakuwa katika hali ya kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali iandae mpango mkakati wa kueneza nishati ya umeme vijijini ili nishati hii ikienezwa itoe misitu inayotakiwa kwa wingi kwa ajili ya nishati ya kuni. Taifa hili pamoja na kuwa na misitu mingi, ipo hatari ya kutoweka kwa sababu wananchi karibu wote wa nchi hii wanatumia nishati inayotegemea misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo hayo yatafanyiwa kazi, naamini tutafaulu kuliona Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hajaonesha kabisa juu ya namna ambavyo Serikali ina mpango wowote wa haraka wa kupunguza zile kero zilizopo kwa watumishi wa Serikali katika posho za safari kwa wale amba wanapata likizo au uhamisho na matatizo hayo zaidi yanawakumba Walimu pamoja na Maaskari (Jeshi, Polisi n.k).

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Maaskari (Jeshi na Polisi) wanahamia katika vituo kwa muda mrefu sana bila kubadilishwa (kuhamishwa) eneo la kazi. Jambo ambalo linawafanya Maaskari hawa kuyazoea maeneo na hivyo kupelekeea wao kuzoleka sana na hivyo kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo bado suala la kufunguliwa kwa Akaunti ya Pamoja kwa SMZ na SMT bado imekuwa ni hadithi ya kifaranga na mama yake ya kwamba kifaranga kila anapomdai mama yake kunyonya anaambiwa kesho na hanyonyeshwi hadi anakuwa na yeye anapata watoto naye anaendelea kuwaimbia wimbo huohuo wa utanyonya kesho bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi za ajira za Askari (Jeshi na Polisi) mpango uliopo sasa wa kufanyiwa *interview* (mahojiano) kwa pamoja Bara na Visiwani, hii ni wazi kwamba ni utaratibu wa kuwanyima nafasi Wazanzibar. Naomba nafasi zigaiwe na zile za Zanzibar mahojiano yawe ni Wazanzibari pekee na zile za Bara ziwe wa Bara pekee. Wazanzibari tunaamini kwamba utaratibu huu wa kufanya usaili wa pamoja ni mapango wa Bara kuwanyima nafasi Wazanzibari, hivyo basi naishauri Wizara ibadilishe utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TRA* ni kama vile tuna *TRA* ya kweli ambayo ni hii iliyopo upande wa Bara na ile *TRA* iliyopo pale Zanzibar ni feki na ndio maana bidhaa zote zilizopitia Bandari za huku Bara kutokea nje ya nchi zinakuwa halali

zikienda Zanzibar, lakini kwa bidhaa ambazo zimepitia Bandari ya Zanzibar hata kama zimelipiwa ushuru (kodi) chini ya *TRA* sio halali. Inashangaza kwamba bidhaa hizo zikiingia katika Bandari zilizopo Bara, pamoja na uthibitisho unaooneshwa na wahusika kwamba bidhaa hizo zimelipiwa kodi lakini nyaraka hizo za kulipia hazitambuliwi huku Bara na Wazanzibari wananyanyaswa sana katika jambo hili. Naomba Serikali ituambie kama *TRA* waliopo Zanzibar ni matapeli tu ambao wamepata baraka za Serikali ili wawatapeli Wazanzibari fedha zao au lah. Kama tumeungana basi tusinyanyasane na Wazanzibari tusionekane kwamba tunapodai haki zetu za msingi ndani ya Muungano huu kama mtu anayepiga honi katika gari alilopewa lifti, sisi hatukupewa lifti, sisi ni wenye gari hili vilevile huu ni utaratibu wa kujiona kwamba Bara mna haki zaidi na Zanzibar ni watu wa kuwafikiria tu, jambo hili sio sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba haki itendeke na pasiwe na kuburuzana, sio madhumuni ya Muungano na hatukuungana kwa vigezo vya uwiano wa watu katika nchi hizi, kigezo ilikuwa u-inchi na kwa kuwa Zanzibar ilikuwa ni nchi huru na Tanganyika ilikuwa ni nchi, kwa hiyo zikaonekana kwamba nchi hizi zimekidhi kigezo cha kuunganishwa. Kuna mawazo kwamba Zanzibar tuko wachache na hivyo tunafaa na ni halali kunyonywa na Muungano huu, hao wamefilisika na mawazo yao hayo sio sahihi hata kidogo. Ahsante, naomba kuwasilisha.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za pekee na mimi kupata nafasi hii kuweza kutoa michango yangu katika hoja hii mahsus. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia kibali cha kuwepo mahali hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kushinda ushindi wa kishindo kuliongoza Taifa hili letu. Vilevile nampongeza Makamu wa Rais, Dokta Mohammed Gharib Bilal, kwa uteuzi wake pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge, kwa uteuzi wa kuliongoza Taifa hili. Mwenyezi Mungu, awajalie afya njema. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Anna Semamba Makinda, Spika wa Bunge, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili. Sisi wanawake wote tunajivunia kwa ushujaa, umahiri, hekima na busara alizonazo. Nakupongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kushika nafasi ya kuliongoza Bunge hili na Mungu akupe afya njema. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kubwa kwangu na kunitua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, nikishughulikia mazingira. Vilevile napenda kumuahidi kwamba sitamuangusha, nitafanya kazi kwa nguvu zangu zote alizonijalia Mwenyezi Mungu, kwa uadilifu mkubwa. Pamoja na shukrani hizo, napenda kumshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dokta Mohammed Gharib Bilal, kwa ushauri na maelekezo bila kuchoka yanayoniwezesha kufanya kazi bila kutetereka. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Samia Suluhu, kwa upendo na ushirikiano wake. Amekuwa hazina kwangu kutokana na uzoefu wake na kila wakati amekuwa akinishauri na kufanya kazi na mimi kwa karibu sana. Napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, nikianza na Katibu Mkuu, Naibu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wengine wote kwa sababu, wamekuwa msaada wangu wakati wote ninapowahitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau wazazi wangu, napenda kumshukuru baba yangu marehemu, Pius Wilbart Luoga na mume wangu, marehemu Dokta Lawrance Ntazama Gama, kwa kunipa maelekezo mazuri na kuniimarisha hadi kuwepo mahali hapa leo. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, amina.

Napenda pia kumshukuru mama yangu mzazi ambaye wote mmemuona, Anna Maria Luoga na mjomba wangu Ansgali Mapunda, kwa kuniombea, kunishauri na kunipa nguvu na kunipa faraja wakati wote. Nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitawashukuru watoto wangu Luteni Elisha Gama, Amos lawrance Gama na Happiness Lawarance Gama na wajukuu wangu Godboless Gama, Kelvin Mramba, Jonathan Chacha, ambao nao wanifariji kila wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kutoa majibu ya hoja zilizotolewa nikianza na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira. Mheshimiwa Dokta Charles John Tizeba, Mbunge wa Buchosa, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, alitoa hoja kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, ikutane mara kwa mara ili kutoa ufanuzi wa Sera na pia kujadili namna ya kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeanzisha Kikundi cha Mazingira (*Sector Environmental Working Group*) mwaka 2001 ambacho kinahusisha Waratibu wa Mazingira katika Wizara zote. Kikundi hukutana kila mwezi kujadili utekelezaji wa Sera, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Mikataba ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na jinsi Wizara zinavyojipangia kukabiliana na tabia ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Ofisi pia imeandaa mpango wa muda mfupi (*National Adaptation Program of Action – NAPA*) ambao utatumwa na Wizara zote katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni sekta mbalimbali kwa mfano, Sekta ya Nishati ya Umeme, Maliasili na Maji, hufaidika na mazingira mazuri yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, hivyo, wachangie gharama za usimamizi wa mazingira. Sekta hizi zinachangia kuitia *program* mbalimbali za uhifadhi wa mazingira, kwa mfano, Mradi wa Bonde la Mto Kihansi. Vilevile Ofisi imeanzisha Mfuko wa Taifa wa Mazingira, ambapo Sekta hizo zitatakiwa kuchangia gharama za utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni wananchi wengi hawana uelewa kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi. Napenda kusema ni kweli kabisa kwa sababu

suala hili ni jipya kabisa na limeanza kutumika hivi karibuni. Hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea kutoa elimu kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti. Mkakati wa kitaifa wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi unaandaliwa ambapo suala la elimu kwa umma limepewa kipaumbele na mkakati huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Kamati inashauri uteuzi wa Waratibu wa Mazingira katika Wizara za Kisekta na Halmashauri ufanyike kulingana na Sheria, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Kifungu Namba 33, kimeeleza kila Wizara ya Kisekta, itajiri au kuteua Mratibu wa Mazingira kwa kuwa, muundo wa Maafisa wa Mazingira umeshapelekwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na tunategemea uanze kutumika mwaka huu wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni Serikali iongeze bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ushauri huu tumeupokea na Ofisi itaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha, ili kuongeza fedha au kuweka *objectives* kwa ajili ya kutekeleza shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia *NEMC* ifanye tathmini mapema bila ushawishi wa uwekezaji katika maeneo yaliyogunduliwa kuwa yana *uranium* ili kubaini madhara ya ucharibifu wa mazingira yanayoweza kutokea. Ushauri huu umezingatiwa na tayari suala hili linafutiliwa kwa karibu sana na ushirikiano wa wadau wengine, wakiwemo Tume ya Mionzi ya *Atomic (Atomic Energy Commission Arusha)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwa nini Sheria ya Mazingira haisimamiwi kikamilifu kwa makampuni makubwa ya madini yanayochafua mazingira? Wizara inajitahidi kusimamia Sheria, lakini utekelezaji wake unachangamoto nyingi katika maeneo yote ikiwepo uchimbaji wa madini. Upungufu katika usimamiaji wa Sheria, unatokana na mambo yafuatayo:-

- (i) Sheria inaainisha hatua za kufuata katika kusimamia, ambayo imepanga muda maalum wa kuzingatia. Katika kufanya hivyo, utekelezaji wa kufuatilia mambo mengine unakuwa umechelewa.
- (ii) Ufinyu wa bajeti unaathiri usimamizi wa mazingira. Fedha hazitoshi kufanya ufuatiliaji wa kutekeleza mipango kwa wakati, vifaa vyta upimaji ni vichache, usafiri ni hafifu kuweza kukagua nchi nzima, wataalamu walioajiriwa ni wachache.
- (iii) Uelewa wa wananchi ni mdogo kuhusu majukumu hayo ya kisheria ya kusimamia mazingira kwa kusaidiana na Baraza.
- (iv) Pia sekta mbalimbali bado hazijajipanga kikamilifu kushirikiana na Baraza katika kutekeleza majukumu yao lakini Baraza linaona kuna umuhimu wa kuendelea kuweka mikakati ya ushirikiano kati ya sekta mbalimbali na kuendelea kuelimishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya hoja za Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani – Ofisi ya Makamu wa Rais, alitoa hoja kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya mwaka 2010 ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, inasema watu 24 walikuwa wamekufa kutokana na uchafuzi wa mto Tigite na Mgodi wa *North Mara*. Serikali imefuatilia jambo hili kwa karibu sana kwa kuchukua vipimo mbalimbali vya wanadamu na wanyama na suala hilo lilifanywa kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali kwa mfano, Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Nishati, Wizara ya Maji na pia tulishirikisha Serikali ya Mkoa wa Mara na Wilaya ya Tarime pamoja na wanakijiji wa pale. Kwa hiyo, bado Serikali inaendelea na uchunguzi ili kuhakikisha kwamba, kweli wale watu walibabuliwa na uchafuzi wa mazingira, utafiti inabidi ufanyike kwa muda mrefu. Mpaka sasa hivi majibu ya awali hayaoneshi kwamba athari zile zilitokana na uchafuzi wa kiwanda kwa sababu, historia ya Mgodi ule ni kwamba kwa muda mrefu watu walikuwa wanatumia *mercury* kusafishia dhahabu, mgodi hautumii *mercury* na athari nyingi za *mercury* ni ngozi kubabuka na madhara mengine. Pia hakuna binadamu aliyekufa kutokana na uchafuzi huo, lakini pia uchunguzi unaendelea. Wizara zote zikikamilisha, Serikali itatoa tamko rasmi kuhusu Mgodi wa *North Mara*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni viwanda kutiririsha maji machafu katika mazingira na makazi ya watu, hatua mbona hazichukuliwi? Hatua za ukaguzi zinachukuliwa, tatizo lililopo ni kwamba viwanda vingi vimejengwa bila tathmini, kwa sababu tunajua Sheria hii imeanza hivi karibuni lakini viwanda hivi na migodi tayari vilikuwepo. Kwa hiyo, Baraza linachofanya ni kujaribu kupitia kila kiwanda na migodi, kufanya tathmini ya sasa hivi lakini hatuwezi kulaumu sana Baraza, kwa sababu migodi hii na viwanda vilianza mapema zaidi kabla Sheria ya Athari ya Mazingira kutungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itahakikisha *cynide* haitumiwi na makampuni makubwa au kutengenezewa utaratibu wa kuihifadhi katika uchenjuaji wa dhahabu, kutokana na madhara yake? Maelezo ni kwamba, *cynide* ndio inayotumika katika teknolojia ya kisasa katika kuchenjua dhahabu hasa katika uzalishaji mkubwa. Udhhibit wa madhara yake kwa kiwango kinachotakiwa uko ndani ya uwezo wa mchakato wa uchenjuaji katika uzalishaji. Tatizo linatoka wakati wachimbaji wadogowadogo wanapotumia *chemicals* kama *mercury* kwa sababu hawana utaalamu na ile *chemical* ya *mercury* inayomwagwa hovyo ndio inayochafua mazingira zaidi lakini migodi mikubwa kuna utaratibu umefanyika na Baraza linapita kutathmini kila wakati na wao wanatumia zaidi *cynide*, hawatumii *mercury*. Mgodi wa *North Mara*, hautumii *mercury* kabisa, wanatumia *cynide* na yale madhara yaliyotokea, wataalamu walivyoangalia ni madhara yanayosababishwa na *mercury*, kwa hiyo uchunguzi unaendelea zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itachukua hatua dhidi ya migodi ambayo shughuli zake zinatoa *acid mine drainage* na kusababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira? Serikali imeshachukua hatua kupitia uperembaji na kaguzi dhibiti

zinazofanyika. Katika hali ya kawaida, *acid mine drainage* huelekezwa katika mfumo wa majitaka baada ya kusafishwa. Kwa hiyo, hata baharini tunaweza kuelekeza lakini ni lazima kuwe na mgodi madhubuti wa kusafisha maji hayo. Kwa hiyo, Baraza linachofanya ni kuhimiza viwanda vyote na migodi ambavyo vilikuwa havina hizo mashine pamoja na *North Mara*, kuhakikisha kwamba mashine hizo zinakuwepo. Kwa taarifa tu, *North Mara* tayari wameshatengeneza huo mgodi lakini bado hawajapewa kibali cha kumwaga mpaka Baraza lihakikishe kwamba yale maji yote yamesafishwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini *NEMC* itachukua hatua kwa mujibu wa Sheria kuzuia na kukomesha uchafuzi unaotokana na shughuli za migodi ili kuwalinda wananchi pamoja na viumbe ambao wanaathirika? *NEMC* inafanya ufuatiliaji kwa karibu na inapogundulika hitilafu yoyote, hutoa ushauri wa kuchukua hatua ya kisheria mara moja. Elimu kwa wananchi hutolewa mara kwa mara ili kuchukua tahadhari dhidi ya madhara ya uchafuzi. Vilevile wananchi wanahamasishwa kutoa taarifa kuhusu uchafuzi pindi unapotokea katika maeneo hayo, uchafuzi unapaswa kuhakikishwa kwa kuchukua sampuli na kufanya vipimo katika maabara na ndicho kilichotokea *North Mara*. Sampuli zimechukuliwa kwa mifugo, kwa binadamu, katika Mto Tigite, sehemu mbalimbali na katika mabwawa yale ambamo maji yaliwekwa kutokana na vina mbalimbali, kwa hiyo, tafiti hizi zote zikikamilika kwa sababu bado zinaendelea ili kuona *chemicals* gani zilikuwepo wakati ule na ambazo zipo sasa hivi katika mito mbalimbali na vyanzo vingine nya maji vinavyozunguka *North Mara* itatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka 10, Serikali imepokea malalamiko kuhusu uchafuzi wa mazingira katika eneo la Makuburi - Kibangu, ambako uchafuzi mkubwa wa mazingira hufanywa na kiwanda cha *Mkuani Traders/Azania Wheat Flours Ltd*, katika eneo la makazi ya watu. Ni kweli ofisi yangu ilipokea malalamiko ya uchafuzi na kero zinazosababishwa na kiwanda hicho. Baraza kwa kushirikiana na OSHA na Manispaa ya Kinondoni ilifanya ukaguzi wa kiwanda hicho na kubaini upungufu kadha.

Vilevile ukaguzi ulibaini kuwa kiwanda hicho kilipewa kibali cha kujenga katika makazi ya watu. Manispaa ya Kinondoni iliahidi kushughulikia suala hilo kwa kutafuta eneo lingine ili kiwanda hicho kihamishwe. Kwa taarifa iliyoko ofisini, eneo hilo limepatikana na mwekezaji anashughulikia ujenzi. Baraza linafuatilia kwa karibu sana utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nytingine ilikuwa katika eneo la Mabibo *External*, ambapo maji takaa ukiwemo uchafu wa vyoo toka *Hostel* za Mabibo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yanatiririka katika mto na pembeni mwa makazi ya watu na kuleta harufu na madhara mengine ya kiafya. Tunakiri tatizo hili kuwepo na Baraza limepatilia lakini Chuo Kikuu cha Salaam, siyo mmiliki wa yale majengo, mmiliki ni *NSSF*, kwa hiyo, Baraza limetoea taarifa kwa *NSSF* kutafuta mfumo mwengine wa kutoa majitaka kutoka *Hostel* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mabibo Hostel. Kwa hiyo, Baraza pia inafuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, wananchi wa Mbagala karibu na Kiwanda cha Nguo cha *KTM* wamekuwa wakilalamika sana kuhusiana na madhara wanayoyapata kutokana na uchafuzi wa Mto Kizinga. Kambi ya Upinzani inataka Serikali ieleze kwa nini *NEMC* imeshindwa kuchukua hatua. Kiwanda cha Nguo cha Mbagala kimefuatiliwa kwa muda mrefu na kimefungwa mara tatu na Baraza kwa nyakati tofauti. Baraza lilitoa masharti ya kukarabati mtambo wa kusafisha majitaka na vipimo vilivyo chukuliwa kwa sasa hivi vinaonyesha kukidhi viwango vinavyohitajika kisheria. Tatizo lililobaki ni kuondoa majitaka kwa kiwango cha mazingira. Kiwanda kimeajiri mtaalam wa kusafisha maji hayo ili kufikia kiwango kinachohitajika. Ufuatiliaji wa karibu unafanywa na Baraza kwa kushirikiana na Bonde la Wami-Ruvu, kuangalia maendeleo ya utekelezaji. Kwa sasa hivi Kiwanda hakijaruhusiwa kuzalisha kwa asilimia 100, kinazalisha kwa asilimia 50 mpaka hapo watakapokidhi taratibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, kuna tatizo la uchafuzi wa hewa unaofanywa na viwanda mbalimbali hapa nchini kama Kiwanda cha Ngozi Kibaha, maeneo ya Kihonda Morogoro, Himo na viwanda vingine vya ngozi nchini, hatua gani zimechuliwa? Wizara yangu imechukua hatua kadhaa kwanza kabisa Viwanda vya Ngozi kama vilivyo viwanda vya sabuni na machinjio ni viwanda vinavyojulikana kama *offensive trade* kutokana na uzalishwaji wa harufu kali sana. Hivyo, vinatakiwa vijengwe mbali na makazi ya binadamu. Kwa bahati mbaya makazi ya watu yamesogelea viwanda hivyo kwa karibu sana. Hata hivyo, jitihada zinafanya kuhakikisha vinasafisha majitaka kwa njia za kisasa ili kupunguza harufu. Baraza limekwishafanya ufuatiliaji kwa Kiwanda cha Ngozi Kibaha na kutoa maelekezo ya kimazingira. Hivyo, Baraza litaendelea kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, kutokana na utafiti wa Shirika la *Face the Future* ya 2001, zaidi ya asilimia 70 ya uchafuzi unatokana na viwanda mbalimbali Jijini Dar es Salaam, kama vile chuma, madawa na kadhalika na majitaka kuelekezwa baharini hivyo kuwa chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira. Ukaguzi wa mara kwa mara unafanyika na kutoa ushauri wa namna bora wa kudhibiti majitaka. Aidha, changamoto kubwa iliyopo ni viwanda vingi kutokuwa na mitambo ya kusafisha majitaka na kama nilivyosema viwanda hivi vingi vilianza kabla ya sheria na sasa hivi viwanda vyote vimepewa notisi ya kuboresha mifumo ya kusafisha majitaka, kinyume cha hapo, viwanda hivyo vitafungwa mara moja na mimi napenda niwathibitishie kwamba tutafanya ukaguzi huo tena na kiwanda ambacho kitakuwa hakijakidhi viwango tutakifunga mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, Serikali ihakikishe kuwa maeneo yote yaliyotumika kuhifadhi dawa za sumu mbalimbali za kilimo kama vile Kibaha na Korogwe *Areas for Disposal of Agriculture Poisons* yanahifadhiwa vizuri ili yasilete madhara kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo. Serikali imekwishachukua hatua zifuatazo, eneo za Korogwe, *NEMC* ilisafisha tani 110 za viuatalifu chakavu na kuteketezwa huku Ujerumanii. Shirika la Kiufundi la Ujerumanii la GTZ lilifadhili shughuli hiyo. Eneo lililochafuliwa na dawa la Korogwe lilisafishwa na sampuli za udongo zilichunguzwa na kuonekana kuwa salama kwa jamii. Eneo la Kibaha Vikuge, lenye shehena ya viuatalifu chakavu vipatavyo tani 250 na udongo ulioathirika

limezungushiwa uzio ili kuzuia wananchi kuingia katika eneo hilo. Shughuli hii ipo chini ya ufadhili wa Programu ya *ASP*. Tani 700 ya viuatilifu chakavu, kwenye maeneo 135 hapa nchini zitasafirishwa kwenda Ujerumani na kuteketezwa katika mwaka huu wa fedha kupitia Programu ya *ASP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya shule na sekondari ibadilishwe na iweke msisitizo katika umuhimu wa upandaji miti, elimu ya mazingira imehuishwa katika mitaala ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenister Joakim Mhagama, Peramaho; Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Kwela; Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Viti Maalum; Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Viti Maalum; Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Gairo; Mheshimiwa Salum Mbarouk, Wete; Mheshimiwa Aliko Nikosuma Kibona, Ileje; Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, Njombe Magharibi na Mheshimiwa James Mntangi, Muheza, wao walitoa hoja kwamba hifadhi ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji nchini vilindwe, kasi ya upandaji wa miti iongezwe, ufugaji holela usitishwe, uchomaji moto holela udhibitiwe, matumizi ya kuni na uchomaji mkaa idhibitiwe, kasi ndogo ya uvunaji miti ya mikaratusi inayofyoza maji kwa wingi tathimini ihusishe miti iliyopandwa na iliyopo na vilevile Kiwanda cha Chumvi cha Uviza kinatumia kuni nyingi na magogo kwa ajili ya kukausha chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, inaratibu na kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya mazingira hususani kwenye ardhi na vyanzo vya maji ya mwaka 2006. Mkakati huu unalenga kukabiliana na changamoto za mazingira, ikiwemo masuala ya kuhamia wafugaji na wakulima katika vyanzo vya maji, kudhibiti uchomaji moto hovsky, kuhamasisha upandaji miti na kutunza mazingira hususani kupitia mashindano ya tunzo ya Rais ya kuhifadhi vyanzo maji na kuondoa miti isiyofaa katika vyanzo vya maji. Mkakati huu unatekelezwa katika ngazi ya Wizara ya kisekta, Mikoa na Halmashauri na kusisitiza watumiaji wakubwa wa nishati ya kuni na mkaa zikiwemo taasisi na viwanda kuwa na mashamba yao ya miti kwa ajili ya kuni. Aidha, tathmini ya upandaji miti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 jumla ya miti 198,331,913 ilipandwa na miti milioni 152,404,333 iliota sawa na asilimia 77. Taarifa ya utekelezaji inaandaliwa kila mwaka na Mikoa na kuwasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutumia magogo kwa ajili ya kukaushia chumvi lipo, Serikali kupitia mkakati wa ardhi umeelekeza watumiaji wakubwa wa miti ikiwemo kiwanda kingine cha *21st century* kuwa na mashamba ya miti kwa ajili ya matumizi hayo. Aidha, wanashauriwa kutumia nishati mbadala kama vile *solar energy*, *bio-gas* na makaa ya mawe.

Mheshimiwa David Silinde, Mbozi; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Kongwa; Mheshimiwa Juma Sururu, Bububu; Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Viti Maalum; Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Tandahimba; Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Rufiji; Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Viti Maalum Kigoma; Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Rombo; Mheshimiwa Nasir Suleiman, Mfenesini; Mheshimiwa

Subira Khamis Ngatu, Viti Maalum na Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Viti Maalum, wao hoja yao ilikuwa uharibifu mkubwa katika misitu ya asili katika milima ya Ukagulu, vyanzo vya maji kukauka, kibali cha uvunaji wa misitu karibu na misitu, hifadhi ya Amani Tanga, udhibiti wa vibali vya uvunaji wa magogo, uharibifu wa misitu ya maliasili na Ushoro, Ndago hadi Uluguru katika Wilaya ya Iramba unaofanywa na Jeshi la Magereza, je, Serikali ina takwimu sahihi ya miti inayovunwa? Kwa kifupi, hoja hizi zote ni za Wizara ya Maliasili kwa hiyo nitaiomba Wizara husika wakati inahitimisha bajeti yake basi pia ijibu hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, ni mabadiliko ya tabianchi, kwa kweli ni tatizo kubwa, naomba Waheshimiwa Wabunge wote tusaidiane kwa sababu mabadiliko ya tabianchi hiyo ni *terminology* tu lakini ni kazi ambazo sisi wenyewe tumezifanya za kiuchumi, kuharibu mazingira kwa kuchimba madini, kwa kulima holela na kwa kuhamahama, kuwa na mifugo, kwa hiyo, hizo kazi zote athari yake ni mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, kwa vile Mbunge ana Jimbo lake basi kila mmoja ahakikishe Jimbo lake linapanda miti ya kutosha na vilevile Waheshimiwa Wabunge naomba muwaelimishe wananchi ili waweze kuizoea hii *terminology* kwa sababu kuna miradi tumeshapeleka Kilimanjaro pamoja na Arumeru.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA): Imeonekana kwamba wananchi wameweza kuelewa na wamefanya vizuri, ahsanteni sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA): Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Terezya Huvisa, Waziri Nchi, Ofisi ya Rais (Mazingira). Tunashukuru sana na tumhakikishie mama Terezya pale *gallery* kwamba binti yetu anafanya kazi nzuri kama Mheshimiwa Waziri wa Mazingira. (*Makofi*)

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambaye pia ni Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, karibu hapa mbele, karibu sana Mheshimiwa Sitta.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusaidia kidogo kutoa mchango kuhusu hoja za Wizara hii ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana, mimi ni mmoja wa watu ambao wanakuthamini sana kwa sababu naujua uwezo wako. Sijui kama Waheshimiwa

Wabunge wanafahamu kwamba Mheshimiwa Naibu Spika ndiye aliyeongoza Tume ya watu saba kutembelea Mabunge mbalimbali na hatimaye taarifa yake ambayo kwa kifupi inaitwa ‘Ndugai Ripoti’ ikaweza kuzaa Kanuni Mpya za Bunge tunazotumia hivi sasa. Nakutakia afya njema, nchi inakuhitaji, Jimbo linakuhitaji, Mwenyezi Mungu akuweke vizuri katika shughuli zako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia na hususan Mheshimiwa Samia, huyu amebobea, ni Waziri mzoefu, amekuwa Waziri wa SMZ na isitamkwe kwamba mchawi apewe mtoto kulea, hapana, Mheshimiwa Samia ana uwezo kamili na anaweza kuimudu Wizara yoyote, ni mmoja wa Watanzania naowafahamu kuwa hodari kwelikweli. Mheshimiwa Huvisa naye ni msomi aliyebobea na ndio amepangwa kushughulikia Mazingira na kazi ameianza kwa nguvu zote. Wote wawili nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa nafasi yangu kama Waziri wa Afrika Mashariki lakini pia kama mmoja wa Wazee katika Bunge hili. Nayajua mengi sana yaliyotokea wakati wa Muungano ulipoanzishwa lakini nimesikia upotoshaji mwingi ambao haufanani na hali halisi ilivyokuwa. Nikubaliane moja kwa moja na Mheshimiwa Jaddy, kwamba kuna gizagiza hivi katika kuufahamu Muungano. Hatuelezi vizuri mambo mazuri ya Muungano na hatutoi taarifa kikamilifu kwa wananchi. Hatuelezei tulikotoka hali ilikuwaje, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii niyaseme haya, siyo kwamba nayaamini mimi ila ni jinsi mambo yalivyo na mantiki yake ni ya wakati ule. Sasa tunaweza kupima kama kwa wakati huu bado yanafaa au mantiki ile ilikuwa vipi. Nianze na suala ambalo linanihusu kama Waziri wa Afrika Mashariki, nalo ni ushiriki wa Zanzibar katika mchakato mzima wa kutuunganisha sisi wananchi wa Afrika Mashariki. Napenda kuthibitisha kwamba katika masuala ya Afrika Mashariki, ushiriki wa Zanzibar ni wa moja kwa moja. Hakuna safari yoyote tunayokwenda kujadiliana na wenzetu majirani ambayo haikutanguliwa na mambo mawili, kwanza mikutano ya sisi wenyewe Watanzania humuhumu, kwa maana ya SMZ na Serikali ya Muungano kukaa pamoja, kuweka msimamo. Tunaanza ngazi ya wataalam halafu ngazi ya Mawaziri baada ya hapo ndiyo tunakwenda kama ni Arusha, kama ni Nairobi tunakwenda kwa pamoja. Mikutano mingi sana imefanyika ambapo hakuna hata mkutano mmoja uliofanyika kuhusu majadiliano ya Afrika Mashariki ambapo SMZ haikuwalishwa na sasa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar inashiriki kikamilifu katika yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mifano michache tu. Kutokana na ushiriki huo, tumeweza kuibua miradi ifuatayo ambayo inatekelezwa kwa kuombewa fedha siyo na Serikali ya Muungano tu bali na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mradi wa kwanza ni wa Uwanja wa Ndege wa Karume - Pemba, unatafutiwa fedha ili ujengwe kwa kiwango cha Kimataifa na huu ni mradi rasmi katika orodha ya miradi ya Afrika Mashariki. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Maruhubi, fedha inatafutwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu sisi sote tulikwenda pamoja kuomba hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa chelezo, chelezo ni *dry dock* na pia *roll on* na *roll off ferry*, kwenye bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa. Tunataka uwezekano uwe ni kwamba mtu akitoka Zanzibar na gari yake aingie katika *roll on, roll off ferry* aende hadi Mombasa akipenda, akifika kule *ferry* inafunguka gari inatoka au akija Dar es Salaam vivyo hivyo. Sasa hivi kuna usumbufu mtupu. Hatuna *roll on, roll off ferry* na ni kitu cha kawaida sana katika baadhi ya sehemu ili badala ya mtu kuingia kwenye meli yeye tu, halafu gari kwa matatizo makubwa kuliweka gari katika meli ya kawaida, lakini *roll on, roll off* inahakikisha kwamba mzigo, gari na kadhalika unashuka mahali na unaendelea na bidhaa zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanafanyika chini ya ushirikiano wa pamoja. Sasa hivi majadiliano yanaendelea baina yetu na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kufadhili mradi wa Uwanja wa Ndege wa Karume. Michoro tayari na ni wa kisasa kabisa na tunadhani ndani ya mwaka huu wa fedha tutapata majibu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ili tuanze kazi ya kuujenga. Vivyovivyo kwa Bandari ya Maruhubi na ujenzi wa chelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Wizara hii, mimi najisikia nina bahati kwa sababu katika Wizara yangu siwezi kukosolewa kwamba Wazanzibari hawamo. Naibu Waziri ni Dkt. Abdallah Juma Abdallah, maarufu kwa jina Mabodi, wale Wazanzibar wanajua, ndiye Naibu Waziri. Pia tuna Watumishi Waandamizi wafuatao mionganoni mwa Watumishi Waandamizi wa Wizara yangu ambaao ni 12, hawa wanne ni Wazanzibari, Dkt. Abdullah Hassan Makame, ndiye Mkurugenzi Msaidizi, Sekta ya Uzalishaji, Eng. Abdallah Mzee Mataka, ni Mkurugenzi Msaidizi Miundombinu ya Kiuchumi katika Idara ya Miundombinu, Bwana Othuman Maalim Othuman, ndiye Afisa Habari Mkuu wa Wizara na tunaye Mchumi kijana Bwana Othuman Seif. Kwa hiyo, kwa udogo wa Wizara yetu, uwakilishi huu mimi naona ni mzuri na nitaendelea kutafuta wenzetu wanaotoka upande wa Zanzibar kuweza kujaza nafasi ambazo hazijajazwa. Kwa hiyo, nadhani nimewatoa wasiwasi kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika mchakato wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa aliuliza kwa nini suala la kuchanganya mchanga siku ya tarehe 26 alifanya mtu mmoja tu ambaye ni Mwalimu Julius K. Nyerere? Ndugu zangu, baada ya makubaliano yale katika Bunge ambapo kulikuwa na uwakilishi wa Wazanzibar na baada ya Baraza la Mapinduzi wakati huo kutoa kibali chake na masikilizano baina ya Viongozi Wakuu wawili yaani Marehemu Mzee Nyerere na Marehemu Mzee Abeid Aman Karume walikubaliana kwamba Rais wa kwanza wa Muungano awe Julius K. Nyerere. Kwa hiyo, utaratibu ulifanywa kwamba watoke vijana wawili mwanaume na mwanamke kutoka Zanzibar na kutoka Bara vijana wawili pia yaani mwanaume na mwanamke. Kisha uchukuliwe mchanga wa kuchanganya, akapewa heshima Rais wa Muungano, hakuna la ajabu hapa wala hakuna haja ya kumsafirisha Mzee Jumbe kutoka kule aje eti ndiyo idhihirishe Muungano, hapana! Aliyepewa heshima ni yule ambaye ni Rais wa kwanza. Sasa uamuzi huo ukitaka kuukosoa unaweza kuukosoa lakini mantiki yake ndiyo hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwa nini Rais wa Zanzibar hawi Makamu wa Rais wa Muungano? Jamani, mantiki ya wakati ule ilikuwa hivi, tuisitengeneze Katiba ambapo inaonekana Wazanzibar daima watakuwa Makamu tu, Wazanzibar wanayo haki ya Kikatiba kuwa Rais na imekwishatoka, Mzee Ali Hassan Mwinyi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa ingekuwa imewekwa kwenye Katiba kwamba Makamu wa Rais ni lazima awe Rais wa Zanzibar maana yake kutatokea nyakati ambapo Rais na Makamu wake wote wanatoka upande mmoja wa Muungano. Hilo ndiyo lilikuwa tatizo lililotazamwa wakati ule, siyo hii ya kusema ooh, wanawenza kushinda *CUF* au wengine. Hiyo ni sababu ndogo sana. Kubwa lililotazamwa hapa, ukiweka nafasi moja ya Muungano iwe ya upande mmoja na raia wote wa Jamhuri ya Muungano ni sawa unakaribisha uwezekano kwamba katika nyakati ambapo Mzanzibar ameupata Urais basi kutakuwa kuna Rais wa Muungano Mzanzibar, Makamu wa Rais Mzanzibar, Rais wa Zanzibar Mzanzibar. Hii ndiyo ilikuwa inatazamwa kwa wakati huo, ndiyo maana ikasemekana kwamba atafutwe basi Mzanzibar awe Mgombea Mwenza. Sasa inawezekana inaonekana halifai, lakini sababu ndiyo hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu suala la mafuta kuwa suala la Muungano. Ndugu zangu, mpaka wa Tanzania baada ya tarehe 26 Aprili, 1964 ni kilomita 240 Mashariki mwa Zanzibar, Visiwa vya Pemba na Unguja. Kwa hiyo, hapa katikati tuna mkondo yaani *Zanzibar Channel* na ilionekana kwamba kuna uwezekano mafuta yakapatikana eneo hilo na mpaka sasa uwezekano upo. Liliwekwa kwenye Muungano lakini siyo kwamba maliasili yote iliyo chini ya ardhi iwe ni suala la Muungano, siyo! Suala la uchumi siyo la Muungano ndiyo maana hii hoja ya Dhahabu, kuna Mbunge mmoja alikuwa anasema jana mbona Dhahabu hatugawani? Mbona mnafuta mafuta ya Zanzibar? Halina mantiki hata kidogo kwa sababu suala lilikuwa siyo kuziweka rasilimali za ardhini chini ya Muungano, ilikuwa ni kuzingatia uwezekano wa kupatikana mafuta katika eneo ambalo limo ndani ya Jamhuri ya Muungano katika Bahari inayotunganisha. Sasa pale badala ya watu kugombana kama ilivyotokea Kuwait na Iraq kwa sababu miamba hii haina mipaka ya *sedimentary rock* na inawezekana kabisa chini ya Bahari kati ya Tanga na Zanzibar kukawa na mafuta, sasa ni ya nani? Ili kuweza kutatua tatizo hilo ndiyo ilipendekezwa kwamba jambo hili liwe la Muungano ili tugawane kistaarabu tu. Halihusu Madini mengine wala halihusu mafuta wala Gesi inayopatikana kwenye ardhi ya pande zote mbili. Siku hizi watu wanajisemea tu kwamba ooh, tugawane kila kitu, hakuna hilo! Suala la mafuta limewekwa mahsusii kuondoa ugomvi, hata kama tukitengana leo lazima tukae tuelewane kwa sababu mafuta haya hayana mipaka, yakipatikana kwenye Bahari pale yanakuwa ya nani? Msipoliwekea utaratibusi mtagombana na ndiyo mantiki ya kuliweka katika masuala ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la nne kuhusu Zanzibar kuzuiwa mikataba ya Kimataifa. Suala hili ndugu zangu siyo kwamba Serikali ya Muungano ni Jabali asiyesikia na anaiminya Zanzibar. Hii tafsiri haifai na wala si kweli. Sheria za Kimataifa zinailazimisha Zanzibar ipitie ndani ya Muungano, siyo kwamba tunalipenda sana jambo hili, wakitaka OIC sisi tunazuia, wakitaka hivi tunazuia, sivyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mimi niliwahi kuwa katika katika *Cabinet*, wakati mwengine tulijaribu kuiombea Zanzibar iingie ndani ya *OIC*, *OIC* wakatujibu

kwamba hapana! Tunachopokea ni ombi la *Sovereign State*. Vivyohivyo, kwenye mambo yote ya mikataba anayeruhusiwa kuweka saini mkataba ni yule mwenye mamlaka ya nchi ambayo inaitwa *Sovereign State*. Sasa kwenye Umoja wa Mataifa tuna kiti kimoja kwa hiyo, kinachotambuliwa hapa ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna furaha yoyote. Mimi ningependa sana wenzetu Zanzibar katika yale ambayo kwa historia yao wangepaswa kuwa wanachama kama vile *OIC* na kadhalika, ingekuwa vizuri lakini linashindikana kwa sababu hiyo niliyoitaja. Kwa hiyo, kusema Serikali ya Muungano inaizuia Zanzibar, si kweli hata kidogo! Ni sheria ya Kimataifa ndiyo inazuia. Sasa kama Wanasheria waliobobea tunaweza kujenga hoja tukawa na namna fulani kwamba Mamlaka ya Zanzibar yakatambuliwa kwa baadhi ya mambo kama vile tunavyohangaika katika *FIFA* na kadhalika, sisi ni furaha kubwa kwamba nchi zetu hizi mbili zitakuwa zimeingia katika uwanja wa Kimatifa, sasa hiyo ni hasara kwa nani? Ni faida kwetu sote lakini Sheria za Kimataifa kwa hivi sasa haziruhusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongezeka *Articles of Union*, hili nalo ni jambo la ajabu sana. Wasiojua eti wanasema Serikali ya Muungano ilikuwa inavamia na kuongeza tu hizi *Articles of Union* kutoka 11 hadi 22, siyo kweli! Kwanza kumekuwa na masikilizano na hii ya kusema eti Zanzibar ni wanyonge, sijui Viongozi wao ni mbumbumbu, haya ni matusi jamani, sivyo! Tuna mijadala mikali sana, kuna wasomi wazuri sana Zanzibar, kuna watu Zanzibar wanajua kupanga hoja vizuri kwani wana hekima. Hata baadhi ambaa mnawadhani hawana elimu lakini mambo yao ni makubwa kabisa. Mimi namkumbuka Mzee Thabit Kombo, ukikaa na kuzungumza naye unajua kabisa kwamba hapa kuna hazina ya hekima na akili! Kwa hiyo, tusiwe na huu ubaguziubaguzi wa kujaribu kuwanyanyasa wenzetu wa upande wa pili kwa sababu katika kila jambo kwa kweli tunakwenda kwa kusikilizana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yaliongezekaje? Mambo haya yameongezeka kiasi kikubwa wakati Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika mwaka 1977. Suala la Posta au Mahakama ya Rufaa, Bandari ilikuwa tayari ipo, Shirika la Ndege, Ofisi ya Takwimu ilikuwa ni Afrika Mashariki, Hali ya Hewa lilikuwa ni jambo la Afrika Mashariki, kwa hiyo, yalidondoka ghafla haya tarehe 3 Februari, 1977, je, unayapeleka wapi? Unaweza kusema kwa busara za sasa kwamba tungegawana, Afrika Mashariki ilipovunjika sasa tugawane, aah! Sasa hiyo ni hoja nyininge. Busara ya wakati ule ilisema kama tuliyakabidhi mambo ya ndege Nairobi, mambo ya *Cargo* Mombasa, mambo ya Posta na Simu Kampala, sasa yamedondoka na sisi ni nchi moja basi yarejee kwetu, Katiba na Sheria ilifuatwa katika kuyapitisha ndani ya Bunge hilihili na theluthi mbili ya Wabunge wote waliopiga kura. Kwa hiyo, hakuna raha yoyote ya kusema yaliongezwa tu hivihivi na mojawapo hili la Elimu ya Juu liliombwa na Zanzibar. Barua tunazo na tunaweza kuzionyesha. Suala la Elimu ya Juu halikutoka kokote, lilitoka Zanzibar wakati huo SMZ ilikuwa inahisi kwamba isingegekuwa rahisi kuanzisha mfumo mzima wa Vyuo Vikuu Zanzibar. Kwa hiyo, suala hilo liliombwa kwa barua mahususi kutoka SMZ na ndiyo likaingizwa katika Muungano. Tafsiri ya sasa ya kusema kwamba watu wanafaidi sana mambo haya ya Muungano yakiwa mengi, kwanza ni gharama tu nani anafurahia gharama zaidi? Kwa hiyo, si kweli! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushuru na kodi mara mbili. Jamani historia ya hili ni pale ambapo wafanyabiashara wasio waaminifu walipoamua kupitishia bidhaa Zanzibar ambako zilitozwa kodi na ushuru ulio chini zaidi. Pia ilifika mahali kwamba hata zile karatasi za uagizaji bidhaa zikawa zinaandikwa Zanzibar hata kama mzigo unashuka bandari ya Dar es Salaam. Kule Zanzibar hupigwa muhuri tu. Kwa hiyo, Serikali ya Muungano ilipoteza mapato makubwa sana na mazungumzo yetu na Benki ya Dunia na *IMF* yalikuwa magumu kwa sababu walikuwa wanasesma hii *Zanzibar route* hamuidhibiti na ndipo Serikali mbili zikakubaliana kuwa na viwango sawa vya kodi ingawa ilichukua muda. Sasa hivi kwa kuwa yamerekebishwa basi hakuna tena *Zanzibar route* na kwa hiyo hakuna haja ya kuwa na usumbufu wa kodi mbili. Kama alivyosema Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika hotuba yake kwamba wale watakaoendeleza haya kwa kiburi tu na ama kudai rushwa basi mkono wa Sheria utawafikia na wataaadhibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muundo. Kwa nini Serikali tatu? Namshukuru tena Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy hata Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, wamezungumza vizuri sana kuhusu Serikali tatu. Hapa akili tu inakwambia kwamba hiyo ni njia nyepesi ya kuua Muungano, hakuna shaka hata kidogo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ngoja niwaambieni, hivi sasa kwa bahati mbaya kwa sababu hatujakubaliana masuala ya kugharamia Muungano, upande wa pili hawagharamii chochote. Ingekuwa ni Serikali ya Tanganyika ingelipiza kisasi isilipie Muungano, tungekuwa na Muungano hivi sasa? Upande wa pili Zanzibar hawalipii umeme kwa kiwango kile ambacho kinatozwa Bara na kuna deni sasa la zaidi ya shilingi bilioni 50. Kwa hiyo, wana umeme nafuu lakini deni linakua. Serikali ya Muungano hailichukulii jambo hili kwa hamaki na kadhalika, lakini tumeliacha hivyo hivyo kwa sababu ya Serikali mbili ingekuwepo Serikali ya Tanganyika sidhani kama ingefanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuiunda Tanganyika hapa ni njia nyingine ya kumleta mbia wa kushindana na Zanzibar. Huo ndiyo ukweli kwa sababu huyu Tanganyika itawajibika kwa Watanganyika na wapo Watanganyika wakali kama walivyo Wazanzibar kwa maslahi yao. Kwa hiyo, kuwakutanisha hawa moja kwa moja kwa kuweka Serikali moja huku na moja kule halafu katikati ielee Serikali mnayoiita ya Muungano ambayo haina hata meno. Tuseme wazi tu kama Muungano hautakiwi, tuseme hautakiwi ili tukae kiungwana, tuelewane na mambo yaishe lakini kusema utaleta Serikali ya tatu, mtu mwenye akili unaona kabisa njia hii inavunja Muungano halafu unasema ni njia ya kusaidia, hakuna mantiki hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kulizungumza ni hili la kumuita Baba wa Taifa *Dictator* na kumdharaa Mzee Karume kwa kumwita mbumbumbu! Haya mambo jamani tuache. Katika mambo ambayo yanakera ni kuwatukana Viongozi wetu Waasisi. Mzee Karume alikuwa anakataa mambo mengi sana ambayo alikuwa anaambibiwa na Mwalimu Nyerere kwa wakati wake. Kuna wakati fulani upande wa Muungano walipungukiwa fedha za kigeni, wakajaribu kuomba toka Zanzibar wakati ule Zanzibar uchumi wa Karafuu ulikuwa umeshamiri, Marehemu Mzee Karume

alimwambia Marehemu Mwalimu Nyerere kwamba potelea mbali kwani hatuwezi na hatutoi hata senti moja. Sasa kusema huyu alikuwa mtu haelewi na kadhalika, huyu ndiye aliyejenga Michenzani, mambo yake mengi na makubwa aliyofanya Mzee Karume na yanaonekana na yamedumu hadi leo. Ukimchukua Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere, naye hivyohivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli rafiki yangu Mwanasheria Tundu Lissu alinifikasiha mahali damu ikawa inachemka kidogo, lakini kwenye ukumbi hapa kuna *rules* kwa hiyo sikuweza kufanya lolote lakini kumdhara Mwalimu Julius Nyerere sijui niseme ni kitu gani! Mtu ametuletea umoja, hivi leo Tanzania bila Mwalimu Nyerere ni kitu gani? Ni Mwanasiasa wa Kimataifa, alikuwa na msimamo, ameleta ukombozi kwa Bara la Afrika, kumwita *dictator* ni upuuzi kabisa! Marehemu Mzee Karume ndiye aliywambia Mwalimu Nyerere kwamba Mwalimu wewe uwe Rais mimi niwe Makamu wa Rais, Serikali ianze. Huyu aliyekataa Serikali moja unamwita *dictator*? Angekuwa *dictator* angesema ni Serikali moja tu, lakini alikataa akasema hapana Sheikh, Zanzibar iwe na Serikali yake, alisema Mwalimu Nyerere na siyo mtu mwingine, *dictator* gani huyu anayekubali vitu kama hivi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe mwezi Septemba, 1960 tulipopata Serikali ya Madaraka Tanganyika, Mwalimu Nyerere aliwaomba Waingereza watazame uwezekano wa kuahirisha uhuru wa Tanganyika ili itakapokuwa Kenya na Uganda wanapata uhuru tuungane tuwe nchi moja na akasema kabisa kwamba Marehemu Jomo Kenyatta ndiye awe mkubwa wetu. Leo mtu huyu anaitwa *dictator*? Mtu anayekubali kuahirisha uhuru wa nchi yake ili waungane iwe sehemu kubwa zaidi na yeze asiwe Rais. Kwa kweli mambo haya yanakera sana jamani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, Mwalimu Nyerere ni Kiongozi shupavu. Kumekuwa na lugha siku hizi kwamba ooh, wanatakiwa Viongozi wenyе kufanya maamuzi magumu. Maamuzi magumu sawa, lakini maamuzi magumu hayana maana kwa nchi yoyote kama hakuna uadilifu ndani yake. Ndani ya maamuzi magumu lazima kuwe na uadilifu siyo 10%. Kwa hiyo, watu wanasema maamuzi magumu tu na rushwa iendele? Sasa Mwalimu Nyerere ndicho alichosimamia hiki na ndiyo maana nchi yetu ikatukuka. Kitu kinachoharibu kabisa dunia ya tatu hivi sasa ni ulaji rushwa, ndiyo inayochelewesha maendeleo. Viongozi wanaleta miradi mibovu na mikataba ya kitoto. Yote haya ni mambo ambayo Mwalimu alikuwa hayataki kabisa. Sasa wanaomsema na kumchukia nadhani wana lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Samuel Sitta ambaye ni Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa maneno aliyatueleza hasa vijana wengi waliokuwa wakisema tangu jana kwamba wamekuwepo baada ya Muungano, yanasaidia sana hasa ukitilia maanani kwamba katika historia ya Afrika kesho ni siku ya kipekee sana kwani nchi moja ya Afrika iliyokuwa moja inagawanyika, Sudan ya Kusini inazaliwa kesho. Sudan haikuwa ni nchi iliyoungana ilikuwa ni nchi moja, sembuse sisi?

Kwa hiyo, maneno ya hawa wazee ni vizuri vijana kuyasikiliza kwa makini na kuyazingatia. (*Makof*)

Shughuli zilizopangwa mchana huu zitasimama sasa kwa sababu ni saa saba kamili, tutaendelea saa kumi na moja jioni kwa kumuita Waziri, Mheshimiwa Waziri Samia Hassan Suluhu ambaye ndiye mtooa hoja wetu kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge na baada ya hapo tutaendelea na hatua zinazofuata.

Kabla ya kusitisha shughuli za Bunge, naomba nitangaze kwamba kuna Mheshimiwa Mbunge alikwenda kwenye dawati la NSSF, jengo la Utawala, akasahau funguo za gari. Ziko hapa, mkimuona Mheshimiwa Mbunge yeoyote anatafuta fungua yake tuambiane kwani wanayo Makatibu wetu wa Bunge hapa Mezani.

Baada ya maelezo hayo, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, Mheshimiwa Waziri karibu sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah*, kwa neema na rehema zake, naomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru kwanza Mheshimiwa Spika pamoja na wewe na Wenyeviti wote kwa kusimamia na kuongoza kwa umakini mkubwa majadiliano ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Katiba, Sheria na Utawala na Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi kwa michango yao makini ambayo itasaidia kuboresha utekelezaji wa masuala ya Muungano na Uhifadhi wa Mazingira. Aidha, napenda niwashukuru Waheshimiwa Pauline P. Gekul na Susan J. Lyimo, Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia, kwani michango yao imewezesha kwa kiasi kikubwa Ofisi ya Makamu wa Rais kutambua maeneo ambayo yamefanikiwa na yale ambayo bado ni changamoto na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mohammed Ghali Bilal, kwa maelekezo na miongozo yake makini iliyoniwezesha kutekeleza

majukumu yangu kwa wepesi na ufasaha zaidi. Pia napenda nimshukuru kwa kujumuika nasi hapa Dodoma katika kipindi chote hiki cha kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Ofisi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niwashukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), Wakurugenzi Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kufanikisha uwasilishaji wa hotuba hii hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba sasa nichukue nafasi ya kumshukuru mtoto wangu Ameir, ambaye ameona kuna haja ya kunipa *moral support*, ametoka Zanzibar na sasa yupo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 112 walipata nafasi ya kuchangia. Waheshimiwa Wabunge 29 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja na Waheshimiwa Wabunge 83 wamechangia kwa maandishi. Kwa idhini yako niruhusu niwatambue kwa majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuongea Bungeni ni Mheshimiwa Angella J. Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum, akimwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mbunge wa Buchosa, akimwalikilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mbunge wa Viti Maalum ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani, akimwakilisha pia Mheshimiwa Susan A. Lyimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Tauhida Nyimbo; Mheshimiwa Salim Mbarouk Ali; Mheshimiwa Meshack J. Opulkwa; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed; Mheshimiwa Ali Khamis Seif; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu; Mheshimiwa Regia Mtima; Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba; Mheshimiwa Aliko N. Kibona; Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis; Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo; Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar; Mheshimiwa John J. Mnyika; Mheshimiwa Seleman S. Jafo; Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa; Mheshimiwa Tundu A. Lissu; Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa; Mheshimiwa Halima J. Mdee; Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile; Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh; Mheshimiwa Esther N. Matiko; Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy; Mheshimiwa Mussa Haji Kombo; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar; Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi na Mheshimiwa Samuel Sitta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Angella J. Kairuki; Mheshimiwa Benedict Ole – Nangoro; Mheshimiwa Martha J. Umbulla; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi; Mheshimiwa Ignas A. Malocha; Mheshimiwa Eng. Athuman Mfutakamba; Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine; Mheshimiwa Stephene J. Masele; Mheshimiwa Ahmed M. Shabib; Mheshimiwa Eustace O. Katagira; Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza; Mheshimiwa

Saleh A. Pamba; Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya; Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa na Mheshimiwa Amina A. Clement. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama; Mheshimiwa Diana M. Chilolo; Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla; Mheshimiwa Faida H. Bakar; Mheshimiwa Said R. Bwanamdogo; Mheshimiwa Mohammed H. Missanga; Mheshimiwa Kidawa H. Saleh; Mheshimiwa Herbert J. Mntangi; Mheshimiwa Juma Sururu; Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa Mnyaa; Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed; Mheshimiwa Thuywaiba Idrissa Muhammed; Mheshimiwa Joseph R. Selasini; Mheshimiwa Eng. Gaston Lwenge; Mheshimiwa David Silinde; Mheshimiwa Suleiman Suleiman na Mheshimiwa Waride Bakari Jabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wengine waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya; Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa; Mheshimiwa Job Y. Ndugai; Mheshimiwa Martha M. Mlata; Mheshimiwa Amina M. Mwidau; Mheshimiwa Rose K. Sukum; Mheshimiwa Subira K. Mgatu; Mheshimiwa Juma A. Njwayo; Mheshimiwa Amina Abdallah Amour; Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar na Mheshimiwa Christowaja Mtinda. (*Makofi*)

Wengine ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid; Mheshimiwa Said Suleiman Said; Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki; Mheshimiwa Omar R. Nundu; Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu; Mheshimiwa Sabreena H. Sungura; Mheshimiwa Mussa H. Zungu; Mheshimiwa Asha Mohamed Omar; Mheshimiwa Mustapha Akunaay; Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau; Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir; Mheshimiwa David Silinde; Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe; Mheshimiwa Salome D. Mwambu; Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha; Mheshimiwa Goodluck J. Ole – Medeye; Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis; Mheshimiwa Moshi S. Kakoso; Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed; Mheshimiwa Margaret S. Sitta; Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim; Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Esther N. Matiko. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Said Amour Arfi; Mheshimiwa Hamad Ally Hamad; Mheshimiwa Halima J. Mdee; Mheshimiwa John J. Mnyika; Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu; Mheshimiwa Kheri Ally Khamis; Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka; Mheshimiwa Dkt. Antony Mbasa; Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya; Mheshimiwa Philip G. Mturano; Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi; Mheshimiwa Modestus Kilufi; Mheshimiwa Kapt. John Komba na Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi. Nimepata *note* kwamba Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu na yeye pia alichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua wachangiaji kwa majina, naomba sasa niingie katika kufafanua na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge nikianza na hoja za Idara ya Mazingira. Naomba nijibu hoja za Idara ya Mazingira nikianzia pale ambapo Mheshimiwa Waziri mwenzangu wa Mazingira ameachia. Naomba nianze na hoja ya nishati mbadala. Hoja hii ilichangiwa na watu wengi na naomba niseme kwamba suala la nishati mbadala bado liko kwenye hatua ya utafiti na linafanyiwa kazi. Suala hili linafanyiwa utafiti kwa pamoja baina ya Baraza la Hifadhi ya Mazingira lakini pia na

Wizara ya Nishati. Kwa hiyo, bado wanaendelea kufanya kazi. Kwa mfano, suala la kutumia makaa ya mawe ambalo ndilo lilitawala mjadala kama nishati ya kupikia, utafiti umefanywa na imebainika kwamba zile hewa za gesi bado zinatoka kwa wingi na Baraza la Mazingira bado hawajatoa ruhusa kwamba mkaa ule uweze kutumiwa kwa sababu zile gesi zinazotoka zina madhara mengi kwa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyochangiwa ni hifadhi ya mito Ukanda wa Pwani, Baharini na Mabwawa. Nataka kusema kwamba hoja hii tumeizungumza na tumeitolea ufanuzi mzuri katika kitabu chetu cha hotuba ya bajeti, ukurasa wa 32, naomba Waheshimiwa Wabunge waangalie kwenye hotuba ile wataona jinsi idara ilivyoipanga kutekeleza hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni utafiti wa mkaa wa mawe ambayo tayari nimeishaitolea ufanuzi. Kulikuwa na hoja pia ya viwanja vya ndege kwamba viko karibu na makazi ya watu. Ni kwamba viwanja vya ndege vilikuwa mbali na makazi ya watu ila watu ndiyo wanafuata viwanja vya ndege. Kwa hiyo, tutaongea na mamlaka inayosughulika na viwanja vya ndege kuweza kulinda na kuhifadhi maeneo yao ili watu wasiyavamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja pia ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ambaye alitaka kujua fedha za miradi mitatu zilizotengwa hazikuwa zinaonekana. Miradi hii kwanza ni mradi wa MKUHUMI ambaao unafadhiliwa na Serikali ya Norway chini ya NORAD, lakini unatekelezwa na *Institute of Research Assistance* ya Chuo Kikuu Dar es Salaam. Pesa za mradi huu huwa haziletwi Wizarani, lakini NORAD huwa wanawapa moja kwa moja Chuo Kikuu Dar es Salaam lakini kwa sababu sisi ni Waratibu wa miradi ya mazingira, tumeona hoja ya kuiweka katika hotuba yetu ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwengine ulikuwa ni *African Adaptation Program* ambaao mfadhili mkuu ni Serikali ya Japan na UNDP ndiye anayetekeliza mradi huu. Kwa hiyo, Japan wanaingiza pesa moja kwa moja UNDP.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na mradi wa stahamili tabianchi ambaao mfadhili mkuu ni GEF, Mfuko wa Mazingira wa Dunia na mtekelezaji wa mradi huu ni UNEP. Kwa hiyo, pesa pia inakwenda hukohuko. Fedha za miradi hii haijaweza kuingizwa kwenye vitabu vya maendeleo kwa sababu bado Wizara hajakamilisha mchakato wa kuweza kuomba *code number* ya miradi hii. Tayari tumesaini Memorandum of Understanding (MoU) lakini bado hatujamaliza mchakato na kuomba *code number* ya miradi hii. Kwa hiyo, tutakapomaliza process yote Hazina wataweza ku-capture pesa hizi na kuzionesha katika maeneo mbalimbali ya pesa za maendeleo ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni kuhusu Bodi ya NEMC ambayo Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, alitaka kujua itaanza kazi lini. Ni kwamba bodi iliyokuwepo zamani iliongezewa muda wake mpaka March, 2011, kuanzia March imeanza process ya kuunda bodi mpya na itaanza kazi mwezi Septemba, mwaka huu wa

2011. Tayari Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi wameshateuliwa lakini bado haijatangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia kuna suala la wafanyakazi wanaoumia na *acid ya cyanide* ambayo Mheshimiwa Regia Mtema, amelizungumzia. Kwa kuwa Idara ya Mazingira ni wafuatiliaji na waratibu tu wa hifadhi ya mazingira, tutazungumza na wenzetu wa Wizara ya Kazi na Ajira, ili watumie Sheria za Kazi pamoja na Usalama Kazini, kuona kinachotokea kule kiwandani. Pia tutazungumza na watu wa Nishati na Madini ili kwa pamoja tuweze kufuatilia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na suala la Mheshimiwa Regia Mtema la kiwanda cha *KPL* ambacho kipo Mgeta. Baraza la Usimamizi wa Mazingira hawakuwa na taarifa ya kiwanda hiki lakini niahidi tu kwamba tutafutilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la *plastic bags* ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia, katika hotuba niliyotoa tulitamka kwamba katika mwaka huu wa fedha Serikali inajipanga, tunatizama sheria zilizopo ili kuangalia uwezekano wa kupiga marufuku kabisa mifuko ya plastiki kama ilivyopendekezwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Idara ya Mazingira, suala la mwisho ambalo nitalitolea ufanuzi ni suala la usafi katika miji ya Moshi na Mwanza. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Pauline Gekul, alisema kwamba miji hii imekuwa misafi na imepata ushindi chini ya Uongozi wa Chadema. Taarifa nilizonazo ni kwamba miji hii kwa mfano Mwanza umekuwa ukichukua ushindi huu kwa mwaka wa sita (6) sasa, wakati wote huo ulikuwa kwenye utawala usio CHADEMA. Hata mji wa Moshi wenye kwenye walitoka Moshi akina Mheshimiwa Joseph R. Selasini, wanajua kwamba ushindi huu ni kutokana na tabia ya muda mrefu ya watu wa Moshi na Moshi imekuwa safi kwa muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa ufanuzi huo kwa upande wa Mazingira, naomba sasa niingie katika masuala ya Muungano na nitaanza kuzungumzia masuala yale ya jumla yaliyzungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na baadaye nitakwenda kwenye hoja za Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala ya jumla suala kubwa ambalo limezungumzwa ndani ya Bunge hili ni lile la elimu kwa Watanzania na hususani kwa Waheshimiwa Wabunge humu ndani. Naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwenye hoja hii kwa sababu hata katika hoja nilizozipokea unakuta Mheshimiwa Mbunge anauliza muundo wa Tume ya Pamoja ya Kutatua Kero za Muungano, mwingine anauliza Zanzibar wanapata kiasi gani kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mwaka? Kuna maswali mengi ambayo ukiyatifikari unahisi kwamba elimu kwa Waheshimiwa Wabunge ni ndogo. Kwa hiyo, nikubaliane kabisa na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna haja ya kuzidisha nguvu katika kutoa elimu kwa Watanzania, lakini pia kuna haja ya kuwa na vipindi maalum vya kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge. Naiomba ofisi yako na yangu tulifanyie kazi suala la kuwaelimisha Wabunge

na niahidi tu kwamba kuptitia Ofisi ya Makamu wa Rais tutazidisha nguvu katika kutoa elimu kwa Watanzania na hasa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii pia tulitakiwa kutoa elimu kabla ya mchakato wa marekebisho ya Katiba kuanza. Sasa kazi hii kwa bahati nzuri itakuja kufanya na Tume itakayoundwa ili kuangalia mchakato wa marekebisho ya Katiba na sisi tutajitahidi kuweka nguvu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumzwa ndani ya Bunge ni kumalizika kwa kero zilizopo. Nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutajitahidi kuongeza kasi ya kufanya sekta zenye kero zikutane, tukae tuzungumze na kuondoa kero zilizopo. Mwelekeo unajionesha kwamba kama tutakuwa tunafanya vikao vyta sekta basi mambo mengi tutaweza kuyaondosha kwa haraka bila kusubiri Kamati kubwa inayoongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumzwa kwa nguvu lilikuwa ni Tume ya Pamoja ya Fedha (*JFC*) na ndani ya hoja hii kulikuwa kuna masuala ya Akaunti ya Pamoja, Mgawanyo wa Mapato na suala la asilimia nne pointi tano (4.5%) kwamba ni ndogo ibadilishwe lakini pia kulikuwa kuna suala je, huu mchakato utaisha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa pamoja tu nijibu kwamba wakati wa kuptisha bajeti ya Serikali suala hili lilizungumzwa sana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alitoa ahadi kwamba sasa wataanza kulifanya kazi *seriously* na baada ya muda si mrefu itakuja Kauli ya Serikali hapa Bungeni. Kwa hiyo, niahidi tu kwamba na mimi nitajitahidi kuwahimiza na kuwakumbusha Mawaziri wa Fedha wa pande zote mbili wakae kitako wayazungumze ili tuweze kutoa kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge iliyotolewa ilikuwa inahusiana na masuala ya Katiba.

Michango hiyo ni kama Muundo wa Muungano, Serikali mbili au tatu, utaratibu wa kuingiza na kutoa mambo kwenye mambo ya Muungano, utaratibu wa Mikutano kuzungumzia mambo ya Muungano uwekwe kwenye Katiba, Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais SMT kwamba imetoka kwenye Katiba, Vifungu vyta Katiba vinavyopingana baada ya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar. Kulikuwa na suala la mchakato wa Katiba Mpya iwe shirikishi zaidi, kumetoka pia pendekeso la Bunge kwamba kuwe na vikao makusudi vyta Bunge na Baraza la Wawakilishi Kikatiba vizungumzie masuala ya Muungano, kumetoka pia pendekeso kwamba kwa kuwa kuna nafasi tano za Waheshimiwa Wawakilishi wanaoingia Bungeni basi kuwe na nafasi tano za Wabunge waingie Baraza la Wawakilishi kudumisha Muungano. Pia kulikuwa na masuala mengi yanayohusu Mahakama ya Katiba, Serikali ya Tanganyika kuwa ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yote haya ni ya Kikatiba na kwa sababu ni ya Kikatiba na tuna fursa nzuri ya kuja kuchangia Katiba ijayo, basi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja hizi zote tuje tuzichangie wakati huo. Kwa

sababu kwa sasa hivi hapa, itakuwa vigumu kwa Waziri wa Muungano kuyatolea majibu mambo haya. Kwa hiyo, niwaombe tu kwamba tuje kuyachangia vizuri katika mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na suala la wafanyakazi wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili. Naomba suala hili nije nilizungumze wakati nitakapozungumza kero ambazo tayari zimefanyiwa kazi. Limezungumzwa pia suala la mafuta na gesi namshukuru Mheshimiwa Samuel Sitta amelitolea ufanuzi. Lakini ninaloweza kusema ni kwamba suala la mafuta na gesi tulilizungumza kwa miaka kadhaa katika Kamati ya SMT na SMZ na tumefika mahali suala hili kuliacha kwenye mikono ya Serikali Kuu na bado tunasubiri kupata maelekezo kutoka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia kuna suala la hadhi ya Rais wa Zanzibar akiwa Tanzania Bara. Ufanuzi ni kwamba, Rais wa Zanzibar akiwa Tanzania Bara anahesabika kama Kiongozi wa Kitaifa na yuko namba tatu. Kuna Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anafuatia Rais wa Zanzibar na ndiyo maana gari zake zinaandikwa E3 kwamba ni Kiongozi nambari tatu. Sasa kulikuwa kuna suala pia je, akiingia kwenye Baraza la Mawaziri anakuwa na hadhi gani? Kama inavyoonesha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, Rais wa Zanzibar anaingia kwenye Baraza la Mawaziri kwa hadhi inayobainishwa humo. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge wamesema anakuwa kama Waziri wa kawaida, sasa hili nalo pia ni la Kikatiba, naomba basi kama halitupendezi tuje tulirekebishe kule mbele tutakapozungumzia marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna maswali kama nilivyosema kwamba, Waheshimiwa Wabunge wanaauliza Muundo wa Tume ya Pamoja au Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ inayoshughulikia kero za Muungano. Kamati hii inaongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, kunakuwa na Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalam kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Upande wa pili kunakuwa na Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalam wa sekta wakiongozwa na Mheshimiwa, sasa hivi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwa hiyo, huo ndio Muundo wa Kamati ya Pamoja ya Kutatua Kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea mchango pia wa Mheshimiwa Sabreena Sungura. Katika mchango wake alikuwa analalamikia kwamba Zanzibar kuna ubaguzi wa masuala ya ardhi, dini na siasa. Sasa nimeona ni bora nilitolee ufanuzi suala hili kuliko kuliacha kama lilivyo kwenye kichwa chake, ni kwamba Zanzibar ni ndogo mno. Ukichukua Zanzibar yote *population* iliyokuweko ukiileta Bara wala Bara haitikisiki wala haitetemeki kwamba kuna watu wameingizwa kwa sababu Tanzania Bara ni kubwa na maeneo yapo ya kutosha, lakini chukua watu elfu hamsini tu kutoka Bara waingize Zanzibar kile kisiwa kitakuwa kinavimba mpaka karibu kipasuke. Kwa hiyo, unapozungumzia ubaguzi kwenye ardhi hili si kweli kwa sababu hawezi kufika mtu Zanzibar akaomba labda apewe eka elfu thelathini au elfu kumi zikawepo, hakuna. Sana sana atapewa eneo la kujenga nyumba na eneo la kishamba chake, wenyewe kule tunaita

konde, atakuwa na nyumba yake na konde yake basi. Wahamiaji wapo, wanaishi bila ya bughudha, tupo nao, kwa hiyo, hakuna suala la ubaguzi kwenye ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ubaguzi kwenye dini, nataka nilisemee hili kwamba si kweli. Lakini kwanza nitangaze kuhusiana na hili kwamba mimi pia nimetoka Zanzibar. Katika umri wangu huu wa miaka 51 wakati nikiwa na miaka 12 nilikuwa nafahamu Makanisa matatu tu Zanzibar. Tulikuwa tunaita Kanisa la Magola, Kanisa la Anglikan na la Anglikan lakini la kwanza kwenye *East Africa* liko Kiungani pale Zanzibar. Ukifika Zanzibar leo kuna Makanisa zaidi ya 90, wanapewa ardhi wanajenga nyumba za kuishi wanajenga nyumba za ibada. Kwa hiyo, si kweli kwamba kuna ubaguzi wa dini. Kuna kipindi kimoja nilikuwa naangalia Maadhimisho ya Krismas na kukaoneshwa Kitaifa kwenye Kanisa moja kule Zanzibar sikuifahamu sura hata moja katika wale ambao wameoneshwa wanafanya ibada. Hii inaoneshwa kwamba Watanzania wanaingia Zanzibar, wanaabudu wanavyopenda bila ya bughudha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hakuna ubaguzi wa kisiasa kwa sababu Sheria ya Vyama vya Kisiasa inasema hivi, ili uweze kupata usajili kama chama cha siasa, lazima uwe na Wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar, Mkoaa mmoja Pemba Mkoaa mmoja pale Unguja. Sasa kwa sababu vyama vyote vilivyopata usajli Tanzania vina wanachama kutoka Zanzibar na wote wanakuja Zanzibar kufanya mikutano yao na wanapata watu wa kuwasikiliza, wanachama wao na wengine ambaio sio wanachama wao. Kiongozi wa CUF akipita akiona CHADEMA husimama na kusikiliza kunasemwa nini, wanasesmajie anasikiliza na CCM vivyo hivyo. Kwa hiyo, si kweli kwamba kuna ubaguzi wa aina hii. Naomba Mheshimiwa ndugu yangu Sabreena hili litoke kabisa katika mawazo yake na ikiwa anapenda kuja Zanzibar, naomba niwe mwenyeji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja pia ambayo Mheshimiwa Halima Mdee ameizungumza na yeche kwa ufupi alitaka kujua kero zilizopata ufumbuzi mpaka sasa, alisema vizuri pia kwamba, kuanzia mwaka 2006 mpaka sasa hivi kuna vikao sita tu vimefanyika. Naomba nimwambie kwamba, Vikao hivi ni vya Kamati ya SMT na SMZ. Lakini kumekuwa na vikao kadhaa katika ngazi ya Makatibu Wakuu, Mawaziri na wataalam pia vimefanyika na katika vikao hivi, yafuatayo tumeweza kuyafanyia kazi. Kwanza ni yale mawili uliyoyazungumza kwamba tumeweza kuyatolea hati ya kwamba kero ile imemalizika na haipo tena. Lakini kupitia vikao hivyo hivyo tumeweza pia kuelewana katika mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje ambayo Zanzibar haikuwa ikipata kabla. Lakini kuanzia mwaka 2009/2010 kwa sababu ya vikao hivi Zanzibar tumeweza kupata asilimia 4.5 kwenye *General Budget Support (GBS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni misamaha ya mikopo ya kifedha kutoka *IMF* ambazo *IMF* ilikuwa inasamehe lakini hakukuwa na mtitiriko mzuri wa Zanzibar kupata *share* yake. Sasa hivi *share* hii imekuwa inapatikana Zanzibar wameshapata Dola za Kimarekani milioni 15.12, kwa hiyo, kidogo kidogo mambo yanatatuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala pia la uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi. Ni kweli kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Mnayaa kwamba Zanzibar inapokopa nje lazima wapitie Hazina ya Jamhuri ya Muungano, wapewe dhamana ili waweze kukopa. Lakini hakujakuwa na usumbufu mkubwa kwamba labda wanazuiwa SMZ itimize masharti. Hazina inachukua dhamana na kukopa kwa mikopo ya ndani, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakopa kwa dhamana yake yenye, kwa hiyo, hayo pia tumeweza kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lile la wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, suala hili linakwenda linearudi. Ni kweli kwamba wafanyabiashara kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba wakitoka Zanzibar na vitu vyao wakifika Bandari ya Dar es Salaam wanatozwa kodi mara nyingine. Niliwahi kulitolea ufanuzi katika kipindi cha maswali na majibu, kwamba kero ile inatokana na kipengele cha sheria kinachosema, mkadiriaji anaweza akakadiria kiwango cha chini au juu. Mara nyingi Zanzibar wanakadiria kiwango cha chini wakifika Bara wanakadiria juu na kutakiwa kulipa tofauti, hii ndiyo kero iliyokuwepo, wakati huo huo kuna sheria inasema bidhaa ikishaingia *entry point* moja ya nchi na kama kuna *document* zote halali ichukuliwe kwamba imeshaingia nchini na isitozwe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa kuna suala la *harmonisation* ya kodi, kilichofanyika ni nini? Kilichofanyika *TRA* wametengeneza *import export valuation data base* na ni kweli kwamba imeanza kutumika kuanzia tarehe 25 Februari, 2011. Lakini kwa Zanzibar haikuweza kutumika bado kwa sababu bado *TRA* wanawasiliana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kutafuta sababu zilizofanya Zanzibar isiweze kutumia mfumo huu kulikuwa kuna sababu tatu za muhimu. Moja SMZ wanadai kwamba haikushirikishwa kwa namna yoyote katika dhana au *concept* ya uandaaji na uidhinishaji wa *concept* hii ambayo inatumika. Lakini la pili ni kwamba mfumo unakwenda kinyume na Sheria ya Forodha inayotaka tathmini ifanyike kwa kutumia utaratibu wa *agreement on customs valuation* ambao unaweka misingi ya kufuatwa kwa tathmini ya bidhaa. Kifungu hiki katika Sheria ya *Customs* hakijarekebishwa bado kipo, sasa kuanzisha mfumo mwengine juu ya kifungu cha sheria, Zanzibar hawakukubaliana na hilo. Lakini kubwa zaidi ni kwamba utaratibu huo utaathiri sana biashara na mapato ya Zanzibar. Kwa hiyo, bado *TRA* wako kwenye mazungumzo na Serikali ya Zanzibar na kuona nini waweze kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ambayo hatujayapatia ufumbuzi kamili lakini yako kwenye hatua nzuri ni kama yafuatayo. La kwanza, ni ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama alivyofafanua Mheshimiwa Sitta, kwa sasa hivi tunakwenda vizuri, tutakapoingia kwenye hatua ya *federation* mazungumzo yatakuwa ya aina nyingine, vipi Zanzibar inaweza kushiriki kwenye hatua ya *federation* ya Afrika Mashariki, lakini kwa sasa hivi mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni utafutaji na uchimbaji wa mafuta, ni kama nilivyolitolea maelezo hapo kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la uvuvi kwenye ukanda wa bahari kuu. Suala la uvuvi kwenye ukanda wa bahari kuu SMT na SMZ wamekubaliana kwamba Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi kwenye Ukanda wa Bahari Kuu yajengwe Zanzibar. Ujenzi ulizorota kwa muda mrefu lakini sasa hivi jengo linakuja juu linajengwa. Wamekubaliana kuweka akaunti ya pamoja na wamekubaliana mgao katika mapato yatokanayo na meli zinazovua kwenye bahari kuu. Kwa hiyo, kwenye hili kuna tatizo moja kwamba Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu bado haijapitishwa na Bunge, iko mikononi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanyiwa marekebisho, itakapokamilika italetwa na tutaijadili hapa kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na lina mwelekeo mzuri ni ushirikiano au ushiriki wa Zanzibar kwenye Taasisi za nje, kama lilivyozungumzwa na Wabunge wengi hapa. Katika suala hili Kamati ya Pamoja imetuamuru kuunda Kamati Ndogo, Kamati Ndogo inajumuisha Ofisi ya Mwanasheria Mkoo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkoo na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kamati hii imekaa na kuangalia kwa undani mambo ya ushiriki wa Zanzibar katika Taasisi za Nje au Taasisi za Kikanda na maeneo manne makubwa, kwanza, Zanzibar inaweza ikashiriki katika ziara za viongozi wa Kitaifa wanaokwenda nje. Pili, katika maombi ya pesa za kusaidia miradi ya maendeleo nchini. Tatu, katika suala la elimu ya juu na jambo la nne, ushiriki katika Mikutano ya Kimataifa na Kikanda. Kwa hiyo, baada ya ku-*identify* maeneo hayo sasa tunaweka mwongozo vipi Zanzibar itawezeku kushiriki na pengine baadaye kwa idhini yenu mkipenda, hilo basi linaweza likawekwa Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano. Hili nalo nililijibu juzi kwamba sekta za Utumishi wa Umma Serikali zote mbili wamefanya vikao ngazi ya wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri na wamekubaliana mambo kadhaa kurekebisha tatizo hili. Tatizo lingine ni mgawanyo wa mapato yatokanayo na faida ya Benki Kuu na hisa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, haya yamo ndani ya Kamati ya Pamoja ya Fedha na kama nilivyosema tutazihimiza sekta za fedha zikae wajadili na watupe kauli ya makubaliano yao na Serikali iweze kutoa kauli. Kwa hiyo ,changamoto kubwa ni suala la *JFC*, ndilo ambalo halijafanyiwa kazi, lakini mengine tumeyafanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kodi nyinginezo, kodi nyinginezo hapa tuna kodi ya mapato (*Pay As You Earn*), hii ni kodi ya watumishi wa Taasisi za Muungano wanaofanya kazi Zanzibar. Kodi hizi zinakatwa lakini zinaingia katika Mfuko wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Zanzibar wanataka kodi hizi zikatwe ziingie katika Hazina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili ku-*support* utoaji wa huduma ya wafanyakazi wale ambao wako Zanzibar, kwenye maji, huduma ya umeme afya na elimu, kodi hizi zinasaidia, kwa hiyo, hilo ni moja. Lakini pia kuna kodi ya mapato inayozuia *withholding tax* ambayo nayo tumeijadili kwa undani tumekubaliana aidha, turekebishe sheria au iondoshwe kabisa isiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni usajili wa vyombo vya moto na utambuzi wa leseni za magari. Haya yote tumeyazungumza na tulichokubaliana ni kwamba, pande zote mbili zikarekebishe sheria zao na Mabunge yajayo baada ya bajeti sheria ziletwe Mabungeni kwa ajili ya marekebisho. Kwa hiyo, kwa kupitia vikao vya Kisekta na vikao vingine tunasogea kidogo, kuna maendeleo ambayo yanapatikana. Niahidi tu kwamba tutazidisha juhudhi ili kero hizi ziweze kuondoka, hazitaondoka kabisa tutaondosha hizi zitakuja nyingine mpya. Kwa sababu kwenye Muungano lazima kero zitakuwepo au changamoto zitakuwepo, kama sio hizi zitazuka nyingine, kwa hiyo, tutamaliza hizi tuweze kufanya kazi nyingine zitakazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba suala la Muungano kama walivyosema Wabunge wengi, ni suala muhimu, ni suala nyeti na ni suala ambalo linataka kukubaliana, kuridhiana, kupendana. Nikubaliane na kauli au misemo inayosema kwamba “Nyumba isolongwa haime” maana yake nini? Nyumba ambayo hamzungumzii matatizo yenu mkayatafutia ufumbuzi, haiwezi kuimarika, itavunjika tu. Kwa hiyo, kama kuna matatizo na yanatokea upande mmoja au upande mwingine, la kufanya ni kukaa na kuyazungumza, tukamaliza tukaendelea na sio sisi Wanasiwa kuyachukua tukayaeneza visivyo, tutavunja Muungano wetu, lakini pia kuna usemi mwingine unaosema hivi “Kwenye Mapenzi Usihesabu Visa”. Kama mnakaa, mnapendana, unaanza kusema, wewe juzi ulipika chakula kimeungua, wewe juzi umeleta tungule zimeharibika, wewe juzi umefanya hivi, mtaishia kuhesabiana visa na hamtawezza kuishi pamoja, mtaamua kuvuja uhusiano na kuondoka. Lakini *tulonge*, tukae, tuyazungumze yanayotokea kwa dhati kabisa tukubaliane tuyaondoshe ili Muungano wetu ukue. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kuna hoja kama mbili, tatu muhimu ambazo ningependa kuzitolea ufanuzi na nadhani muda unaniruhusu. Katika mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria walipendekeza kwamba ile sheria iliyounda *JFC* au Tume ya Pamoja ya Fedha ina mapungufu, iletwe Bungeni ili ifanyiwe marekebisho. Nitoe ahadi tu kwamba, nitaiwasilisha kwenye sekta inayohusika ili waweze kulifanya kazi suala hilo. Lakini lingine ni lile ambalo ndugu yangu Tundu Lissu alilizungumza. Nataka niseme tu kwamba, kama nilivyosema Muungano ni Mtoto, mtoto aliyezaliwa kutokana na uhuru tulio pata Tanganyika na Zanzibar, tukaunganisha tukapata mtoto. Mtoto huyo anayeitwa Muungano tumemlea kwa miaka 47, sasa hivi ni mto mzima. Kama umelea mtoto wako amefikia miaka 47 katikati hapo kuna misukosuko mingi ambayo mme pata, unalolifanya ni kurekebisha na kuondosha ile misukosuko, kubadilisha mfumo na kufanya mtoto yule akue vizuri. Ukianza kutafuta mtoto huyu alizaliwa vipi utakuwa unatafuta matatizo. Kwa sababu mtoto ni mtoto awe amezaliwa kwa *scissor section*, amezaliwa kwa njia ya kawaida, amezaliwa kwa kuvutwa na *machine* ya *vacuum*, ni mtoto na anahitaji matunzo, anahitaji umkuze, anahitaji umuimarishe. Huyu mtoto wetu ametimia miaka 47, tusitafute huku nyuma alikuwa vipi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la maana ni kumfanya mtoto huyu sasa ajitegemee, aweze kuzalisha, afae kizazi kile ambacho ye yeupo lakini na kizazi kinachomfuata na

wote ndivyo tulivyokuzwa. Sasa huyu Muungano, mtoto wetu ni mtoto mzuri, mtoto ni mtoto hakosi kasoro. Kwa hiyo, kasoro tuziondoshe lakini tusifikue makaburi. Nayasema haya nikitizama siasa zetu, kama nilivyosema mimi ni Mzanzibari, siasa zetu za Zanzibar *by gone* tumesema iwe *by gone*. Tumezungumza, tumeelewana, tunaendesha Serikali kwa pamoja. Kwa hiyo, tafadhalini tuacheni tutulie, tufanye kazi kwa pamoja, tujenge Zanzibar yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja zilitoka hapa kwamba, watu hawakushirikishwa kwenye Muungano wakati unaundwa, watu hawakuulizwa, kwa wakati ule jamani nani angeulizwa? Naomba niulize, kwa mazingira ya wakati ule tuchukue mifano halisi iliyokuwepo. Sisi Zanzibar, kuna Unguja, Pemba, kuna Tumbatu na visiwa chungu nzima. Lakini Zanzibar ya zamani tulikuwa pamoja na Mombasa na *Coast* yote ya Bagamoyo mpaka Lindi na Mtwara. Lakini Zanzibar ambayo tunayo sasa hivi sisi hatukuulizwa kwamba je, Mombasa iende Kenya au isiende? Ilikwenda tu kwa mazingira ya wakati ule. *Coast* ya Bagamoyo na Lindi ilikwenda Tanganyika kwa mazingira ya wakati ule. Tuchukueni Tanganyika ya wakati huo. Ukienda Tukuyu, nyumba hii Tanganyika, nyumba inayofuata Zambia, ukienda Kigoma vivyo hivyo, ukienda kwagine vivyo hivyo. Je, wakati wa kupiga ile mistari ya mipaka tuliulizwa? Kwa wakati ule hakukuwa na mazingira ya kuulizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema tuache *by gone* iwe *by gone* Zanzibar imetulia, Zanzibar inafanya kazi vizuri, tafadhalini, msitufukulishe makaburi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ninayotaka kuitolea ufanuzi, hapana si hoja ya mwisho, nina hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Mheshimiwa Mnyika alikuwa anauliza kuna kifungu ndani ya Baraza la Mazingira kuna pesa zime-shoot mpaka kufikia bilioni 2.7 nadhani. Ku-shoot kule kunatokana na kufanya muundo mpya wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira na Hifadhi ya Mazingira baada ya kutolewa muundo mpya na Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, *shooting* ile ni masuala ya mishahara, posho na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kulikuwa kuna suala la ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam na kwamba kama mnaendelea kujenga Dar es Salaam, je, kuna nia ya kujenga Dodoma? Niseme tu kwamba, pesa zilizombwa kwa ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais yalikuwa majengo mawili, moja la Tunguu Zanzibar na moja lile la Dar es Salaam. Makamu wa Rais kwa sasa hivi yuko Ikulu lakini *crew* yake iko ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kule ana chumba kimoja tu. Kwa hiyo, tumeona kuna haja ya kumjengea jengo ambalo anaweza akakaa na *staff* yake yote na hilo jengo liko ubavuni mwa jengo la Makamu wa Rais pale Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam. Kwa hiyo, pesa tulizoziomba mwaka huu ni pesa za kumaliza malipo ya *contractors* ambao wameshafanya kazi au wanaendelea kumaliza. Kwa Tunguu Zanzibar pamoja na pale Dar es Salaam. Lakini pesa hizi zimeombwa mwaka jana nusu na mwaka huu tunamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia masuala ya mazingira *component* ambayo Mheshimiwa Mnyika aliongelea ilikuwa ni *component* moja tu kwenye miradi ya mazingira. Lakini ukienda kwenye kitabu cha fedha za maendeleo kuna jumla ya bilioni

saba na pesa nyingine. Sasa ukitazama bilioni saba na bilioni 3.4 si kwamba mazingira hayakupewa uzito unaostahiki. Lingine, ni kwamba, shughuli za mazingira ni *continuing activities*, kila mwaka zinaombewa fedha lakini ujenzi wa jengo tumeomba pesa mwaka jana na mwaka huu likiisha limekwisha. Kwa hiyo, hakuna hoja kwamba hatuyapi uzito masuala ya mazingira, tunajitahidi kuyapa uzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni ile hoja yako kwamba Zanzibar wageni wakiingia *passport* zao zinagongwa tena mihuri, *passport* zilezile zinakuwa zimeshagongwa mihuri Tanzania Bara. Je, Zanzibar kwa nini wanafanya hivyo. Si kwa sababu hatuamini au tunaanza *process* mpya kule, ni kwa sababu ya ku-check usalama wa nchi. Kinachofanyika pale ni ku-check, je, mgeni huyu ameingia kwa njia halali kupitia Tanzania Bara, kama kuna muhuri wanaona ameingia kwenye njia halali, kwa hiyo, *Zanzibar* nao wanaweka tu muhuri kwamba amepita *immigration*. Lakini la pili, *process* ile inasaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujua wageni wanaoingia, wako wapi, hoteli zipi na mwisho wa siku tunajua Watalii wangapi wametembelea nchi yetu kwa kuchukua *record* za *immigration*. Kwa hiyo, kazi ile haina nia mbaya ile ni ku-check usalama wa nchi yetu kwamba je, wale watu wameingia kwenye njia za kawaida? Vile vile inasaidia Serikali kujua wageni wanaoingia nchini na kuweka takwimu nzuri za watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufanuzi wa hoja hizo niseme kwamba, sikuzimaliza zote kwa hakika, lakini majibu kitita, tumeyajibu kwa maandishi, tutayasambaza kwa upande wa Muungano na kwa upande wa Mazingira. Kwa hiyo, hoja yoyote ambayo tumeiacha, hatukuiacha kwa makusudi, ni kwa sababu ya muda na tukitakiwa kutoa ufanuzi basi tuko tayari kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba kutoa hoja. (*Makofifi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu kwa majibu mazuri sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunakushukuru sana sana kwa ufanuzi mzuri sana. Hili la mwisho, Bunge hili liliwahi kupata wageni kutoka nje ya nchi na wageni wetu ilikuwa ni pamoa na kuelekea Zanzibar. Mimi sikulijua hili, kwa hiyo, walipopita Dar es Salaam wakagongewa *Immigration* na walipokwenda Zanzibar wakagongewa tena mihuri ya *immigration*. Walipokuwa wanatoka Zanzibar wakagongewa tena mihuri ya *immigration*. Kwa hiyo, waliporudi ofisini kwangu wakaniliza vipi, mbona wanatujazia *passport* zetu mihuri kila mahali. Ndiyo maana nikalileta kwenye Mamlaka zinazohusika. Nadhani iko haja ya kulitazama vizuri zaidi.

Hoja imetolewa na imeungwa mkono, kabla hatujakwenda hatua inayofuata nitoe tangazo moja tu. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Terezya Huvisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Dkt. Said Gharib Billal, ambaye ni Mbunge wetu wa

Bunge la Afrika Mashariki tuliyemchagua sisi wenyewe hapa Bungeni. Hongera sana kwa kazi nzuri unayofanya huko na karibu sana. Katibu kwa hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 26 - Makamu wa Rais

Kif. 1001 - *Admin. and General*.....Sh. 4,523,675,000/=

MWENYEKITI: Waliosimama waendelee kusimama, wanaotembea wakae chini. Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Nassib Suleman Omar, Mheshimiwa Tundu Lissu. Tuanze na Mheshimiwa Nassib.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, *program 10, sub-vote 1001, Administration and General, item 220400, Medical supplies and services.* Napenda kupata ufanuzi kwamba kwenye mwaka 2010/2011 kulikuwa na Sh. 24,000,000 lakini mwaka huu naona hakuna kitu, sasa sijui Mheshimiwa Waziri anaangalia jambo hili na fedha hizi zilizotengwa. Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri anaomba urudie swali lako vizuri.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Program 10, sub-vote 1001 Administration and General, item 220400, Medical supplies and services.* Mwaka wa fedha 2010/2011, kifungu hiki kilitengewa shilingi 24,000,000/=, mwaka huu hakuna kitu ni zero. Mwaka huu hakuna shughuli za matibabu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo hili limetokana na ukomo wa Bajeti ambayo tumepewa na Wizara ya Fedha. Lakini iko haja ya matibabu ila bajeti haikutosha.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. *Program 10, subvote 1001 kifungu kidogo 221100, travel out of country.* Ukiangalia mwaka 2009/2010 walikuwa wamepanga sh. 25,000,000/=, lakini 2010/2011 walipanga sh. 57,500,000/=. Lakini zilizotengwa mwaka huu wa 2011/2012, kwenye bajeti ambayo ndio tunaijadili ni sh. 300,000/=. Sasa nataka njue kwamba, watu ambao wanafanya kazi katika sehemu hii hawatasafiri nje ya nchi au ziko eneo lingine au fungu tunalolifuata mbele kama hivyo labda waniridhishe *otherwise* ilivyo hapa inawezekana ikawa na makosa. Shilingi laki tatu zinamwezesaji huyu mtu aweze kwenda nje ya nchi. Nashauri tuandike vitu ambavyo ni *realistic*. Nashukuru.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kifungu cha malipo ya *visa* kwa wafanyakazi wa *Private Office* ya Makamu wa Rais. Mara nyangi wengi wanakuwa na *Diplomatic*

Pass, visa zao hazilipiwi na hizi tumeziweka just by the way kwa wale ambao hawatakuwa na Diplomatic Pass.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Nafikiri unavyosema hela kwa ajili ya kusafiri nje ya nchi zina-*involve* pia kukata tiketi na gharama nyingine ambazo huyu mtu anaposafiri nje anakwenda kuzitumia. Kama ni suala la *visa* peke yake sijui. Sasa pesa nyingine ambazo watakuwa wanalipia nauli zitakuwa zinatoka katika fungu gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia mafungu mengine mbele huku kuna mafungu ya *allowances* za safari, nilikuwa najaribu kuangalia haraka haraka. Kuna *travel in country* na kuna *travel out of country* ambapo kuna Sh. 59,400,000/= na *travel in country* kuna Sh. 151,400,000/= ni kifungu 221000 na 221100.

TAARIFA

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu, Bunge lako Tukufu lilivunja Kanuni ile ya mtu kurudia mara mbili katika kipindi hiki cha Kamati ya Matumizi. Ahsante.

MWENYEKIDI: Nashukuru kunikumbusha na tuzingatie hilo.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKIDI: Kidogo tu kwanza tumalizane na Mheshimiwa Mbunge aliye maliza kuongea, lakini kwa suala ambalo limezungumzwa hapa ilikuwa ni *issue* ile ile, ilikuwa ni kutaka kukielewa kifungu kilekile, haikuwa *issue* mpya. Ingekuwa ni *issue* mpya nisingemruhusu. Lakini jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge ametuweka sawa, ni jambo zuri, sio baya. Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Tundu Lissu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 150(4), inazungumzia namna ya kutengua kanuni na inasema kwamba: “Kanuni itatenguliwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa tu na sio kwa madhumuni mengine yoyote.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ambayo Kanuni za kupitisha haya mafungu ilitenguliwa ilikuwa inahu upitishaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, haikuwa inahu upitishaji wa Mafungu ya Wizara zote zingine. Kwa hiyo, naomba sana tafadhalii muda wa Bunge wa kujadili mafungu haya uheshimiwe kama zilivyo Kanuni. Dakika tano tano *nothing less, nothing more*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimpe taarifa na bahati nzuri Mheshimiwa

Mnyika tulikuwa wote katika Kamati ya Uongozi na tukakubaliana kwamba tutakwenda tuone Wizara mbili tatu halafu tutakwenda ku-review. Haikuwa kwa ajili ya Wizara moja. Tulisema mazingira yanavyokwenda sasa endapo kila mara watoa hoja wataanza ku-wind up saa kumi na moja hofu yetu ilikuwa hiyo. Sasa imetoea kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, imetokea juzi hapa mnakumbuka na hii ya juzi haikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeongeza na muda wa saa moja. Lakini tulisema tuchukue huu uzoefu wa siku hizi za mwanzo, halafu tutakuja ku-review tena. Hoja niliyoitoa ya kutengua Kanuni haikuwa na wala haikutaja Ofisi ya Waziri Mkuu. Tulisema katika Bajeti hii hatukutaja Wizara na ndiyo maana tumeitumia juzi kwenye bajeti ya Ofisi ya Rais.

KUHUSU TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo yaliyotolewa na Waziri, naomba nitoe taarifa kwamba, ni kweli tulikubaliana kuhusu utaratibu wa kupunguza muda kwenye Wizara zenyе Ofisi zaidi ya moja, lakini hatukukubaliana kukiuka Kanuni kwa kutokutoa hoja ya kutengua Kanuni. Kwa hiyo kama hoja hiyo bado inasimama, kwa kuwa leo tuna *special case*, majumuisho yalianza kuanzia mchana, kama bado Serikali inaona kuna haja ya muda kuwa mfupi, ingepaswa itolewe hoja ya kutengea Kanuni jambo ambalo halijafanyika.

MWENYEKITI: Sasa ngoja niweke sawa, ni kwamba, jambo lililoletwa mbele yetu ni jambo la maana, lina nia njema ya kutendea haki mambo yanayoletwa mbele yetu sisi kama Wabunge, lakini kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera na Uratibu, hicho ndicho kilichotokea kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi mimi nilihudhuria na Kambi ya Upinzani iliwakishwa na Mheshimiwa Mnyika.

Waheshimiwa Wabunge, hoja ilikwishatolewa na ikaungwa mkono na Bunge hili, lakini makubaliano kwenye Kamati ya Uongozi yalikuwa ni kwamba jambo hili litakuwa ni la muda mfupi kama alivyosema Mheshimiwa Lukuvi, Wizara mbili, tatu, naamini wiki ijayo kitaitishwa kikao kwa ajili ya kuangalia namna bora zaidi ya kwenda na jambo hili, tutakuwa tumepata uzoefu wa namna ya kwenda kwa namna bora zaidi. Kwa sasa hivi, naomba tuendelee haitatukwaza.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kitabu hiki.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Huwezi kunyanyuka, nimeshafanya *rulling*.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo.

MWENYEKITI: Katika *issue* ile ile au nyingine?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo unaombwa baada ya Mwenyekiti kuwa ameshatoa uamuzi. Siombi utaratibu, naomba Mwongozo kwa *rulling* ambayo imeshatokea na ndivyo Kanuni zetu zinavyosema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge kaa chini kidogo. Mheshimiwa Tundu Lissu wewe ni Mnadhimu Mkuu wa upande wa Upinzani kama alivyo Mheshimiwa Lukuvi, Mnadhimu Mkuu kwa upande wa Chama Tawala, wanadhimu ni watunza nidhamu wa pande zao na kazi yao ni kusaidiana na mimi hapa ili kuona kwamba, mambo yanakwenda sawa sawa. Tulichokieleza ndicho kilichotokea na nimekwishatoa *rulling* ya nini ambacho kinaendelea. Kwa hiyo, tukiendelea na majadala huo na mimi ndiyo nipo kwenye kiti hapa, hivi kweli si tutakuwa tunafanya ubishi ambao hautakuwa na sababu yoyote. (*Makofit*)

Ndiyo maana nikasema tusonge mbele nimeshamaliza, kama una kitu cha kusema kwenye kitabu hiki tuendele, nakupa nafasi, kama huna nasonga mbele.

Tunaendelea na Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho ya Waziri, hoja yangu hakuieleza vizuri. Kutokana na kifungu hiki naomba kwanza nizuie mshahara wake ili nipate maelezo zaidi.

Kamati ya kudumu ya Bunge...

MWENYEKITI: Siyo nia yangu kuwakatisha Wabunge wanapoongea lakini hapa hakuna mshahara wa Waziri. Endelea.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria, imeelezwa kwamba Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar hawakuweza kukutana kutokana na kazi zao nyingi walizokuwa nazo. Maelezo ya Waziri yanasema kwamba Serikali itajitahidi masuala haya yatamatilizika na ikiwa hawa watakuwa bado wana kazi nyingi sioni ni namna gani kero hizi zitaweza kumalizika. Naomba kupata maelezo zaidi ni namna gani haya matatizo au majukumu yataweza kupunguzwa ili Waheshimiwa hawa waweze kupatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassib kama nilivyosema mwanzo si nia yangu kumkatisha Mheshimiwa Mbunge lakini katika hatua hizi tunakwenda moja kwa moja kwenye kifungu kinachohusika kwanza, halafu ndiyo unaeleza tatizo lako. Uko kwenye kifungu namba ngapi ili twende pamoja sote.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 31 - OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kif. 1001 - Administration and General....Sh.1,920,409,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Kombo, Mheshimiwa Lissu, Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Nassib, Mheshimiwa Ndugulile, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Mnyika. Ahsante

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, kwa kuokoa dakika zangu niseme tu kwamba, naongelea kifungu cha mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi nilizungumzia kuhusu uharibifu wa Mazingira ambao umefanywa na Jeshi la Magereza katika eneo la Tarafa ya Ndago, eneo lile limeharibiwa sana, nikawa nimeomba Wizara inayohusika kwanza ikatoe mafunzo lakini bado ikaomba wale watu warudishie ile miti ambayo tayari walishaiharibu kwa kupanda miti mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimemwomba Waziri.

MWENYEKITI: Katika makubaliano yale ni jambo moja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize kuhusu masuala ya Muungano, naomba Waziri anifafanulie na Watanzania wote tuelewe ni nini faida ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara na upande wa Visiwani ili wananchi waweze kuelewa faida za Muungano na waendelee kuulinda.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Martha Mlata ametaka maelekezo kuhusu uharibifu wa mazingira unaotokea sehemu za Magereza, nakubaliana nae kabisa kabisa kwamba Nishati kuu inayotumika na siyo sehemu za Magereza tu hata mashulenii, kwenye *Institution* mbalimbali, hata majumbani kwetu tunatumia kuni na mkaa. Lakini tunachosema matumizi haya yawe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mlata kwenda sehemu mbalimbali za *Institution* pamoja na Magereza na kwa wao ni vizuri kama wataweza kutumia *biogas* kwa sababu watu wapo kwa pamoja na *biogas* hii ni ya *latrine* nimeshaona Kenyatta University Nairobi wanatumia *biogas* ya *latrine* ambapo kuna mkusanyiko mkubwa wa wananchi kwa hiyo zile *latrines* zinaweza kutoa *biogas* ya kutosha na hapo hapo wakapanda miti msitu wa kwao kabisa ili ku-supplement hiyo *latrine biogas* na kulinda hifadhi ya mazingira yanayozunguka.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Muungano Mheshimiwa anataka kujua faida za Muungano, ni somo refu pengine lingetolewa zaidi kwenye semina ya Waheshimiwa

Wabunge, lakini kwa haraka haraka labda nimwambie kwamba faida za Muungano kwanza una faida za kijamii, watu wameweza kuingiliana kwa Watanzania Bara na Zanzibar, wameoana, wamezaa na mambo kama haya.

Lakini faida ya kiuchumi kwa *individually* ni kwamba, mtu anaweza kwenda popote akafanya kazi zake, akafanya biashara zake na akaendelea na maisha yake. Kisiasa kama nilivyosema kwamba Vyama vyetu vya Siasa vina *operate* Tanzania nzima bila bughudha. Yapo mambo mengi tukija kwenye semina ya Waheshimiwa Wabunge, tutasoma zaidi.

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, kwanza nikiri majibu ya Waziri leo ni mazuri mno na yametufurahisha sana. Kwa hili ambalo nataka ufanuzi, ningefurahi sana kama Waziri wa Fedha angekuwepo.

Katika mchango wangu ambao sikusikia Waziri akijibu ni kwamba, bajeti na uchumi wake ni mdogo na hii shilingi ya Tanzania inadondoka thamani na inayo-control kudondoka kwa thamani ni upande wa Jamhuri ya Muungano. Ikiwa shilingi itazidi kudorora na bajeti ya Zanzibar imeshapitishwa, je, Jamhuri ya Muungano italipa fidia ya tofauti ya bajeti yake kwa sababu Jamhuri ndiyo imeiachia shilingi?

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Nimelisikia swali la Mheshimiwa Habib Mnyaa, ukweli ni kwamba msingi aliouweka kuulizia swali siyo sahihi, kuongezeka kwa bei au kupungua kwa thamani ya shilingi siyo kwa vitendo vinavyotokea eneo la Tanganyika tu, huo siyo uchumi, kwa sababu sarafu yetu ni moja, thamani ya shilingi inadorora kuhusiana na mambo yote yanayotokea katika uchumi wetu hapa pamoja na Zanzibar. Kwa hiyo, sababu haiwezi kuwa ni ya upande mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende mbali zaidi kwamba hivi sasa kwa sababu tuna ushuru wa forodha wa pamoja wa Afrika Mashariki, thamani ya shilingi ya Uganda imeporomoka mpaka maduka yote yamefungwa Kampala, thamani ya shilingi ya Kenya imeshuka kutoka 74 leo hii ni shilingi 92 kwa dola. Kwa hiyo, suala hili tusilichukue tu. Unajua chini ya utandawazi, huwezi kusema sababu ni moja, ni mchanganyiko wa yote haya ndiyo unaleta hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna uhalali wowote wa upande mmoja wa Muungano kuulipia upande mwengine wanaotumia sarafu moja kuhusu suala la kuporomoka kwa bei ya shilingi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, sasa niweke utaratibu vizuri ili tuelewane, kwamba tulikubaliana nini na ni vizuri sana waungwana kuzingatia makubaliano. Siyo tunasema ndiyo, halafu kesho yake tunaanzisha utaratibu mwengine, ndiyo maana tunahojiana hapa. Spika alikuja akahoji na Bunge likaidhinisha kama ifuatavyo: kwamba atakayesimama kwa wakati huu ataongea si zaidi ya dakika tatu, tulikubaliana hivyo na tulikubaliana hatasimama tena baada ya hapo na Mawaziri wakaambiwa watajibu si zaidi ya dakika tatu, tulikubaliana, kwa hiyo, tufuate utaratibu huo ambao nimekwishaueleza.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu bado ni lile lile ambalo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria iliona kwamba kero za Muungano hazitatuksi kutokana na kwamba viongozi wa juu mara nyingi wanakuwa na dharura hawaendi mikutanoni. Waziri alipokuja hapa hakuliweka wazi kwa sababu bado viongozi hawa watakuwa na sababu hizo za dharura. Je, Waziri anaweza kutuhakikishia hapa kwamba hizi dharura zitapungua na hivyo kero zitazungumzwa na kumalizwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa ufanuzi wa hoja, nilisoma baadhi ya changamoto ambazo tumeweza kuzifikisha pazuri kutokana na mikutano ya Watalaa, Makatibu Wakuu na Mawaziri. Kwa hiyo katika mtiririko ule kuna changamoto au kero ambazo tunaweza tukazitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kawaida tunapokutana katika Kamati Kuu ya SMT na SMZ kinachofanywa ni kutoa taarifa ya yaliyofanyika huku chini, labda kama kuna jambo zito kama suala la mafuta na gesi ndilo tunaloliacha kule kwa ajili ya maamuzi. Lakini vikao hivi vya ngazi za chini tatu zinaweza zikamaliza kero hizi na kama nilivyozungumza kwamba mwelekeo umeonesha kwamba kama vikao vya kisekta vitakaa vitajadili mambo, basi kero hizi zinaweza kuondoka katika ngazi ya vikao vya sekta. Ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, katika mchango wangu nilieleza kwamba chanzo kikuu cha uchafuzi wa mazingira ni kutosimamiwa kwa Utawala wa Sheria na *nili-site* baadhi ya maeneo na katika hitimisho, Waziri amekiri kwamba kweli kuna uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo ya Mabibo, lakini amesema kwamba kunafanyika maandalizi ya mfumo mpya badala ya kuelekeza moja kwa moja hatua za kisheria kuchukuliwa. Pili, ni kwamba kuna uchafuzi wa mazingira wa ukataji miti ambao umechangiwa na sababu nyingine kupanda kwa bei ya mafuta na kadhalika, kuna uchafuzi vile vile wa mto Tigit ambao vile vile Waziri amekiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata kauli ya moja kwa moja ya Serikali, baada ya kugundua kwamba kweli kuna ukiukwaji wa sheria, kwa nini hazichukuliwi hatua za moja kwa moja kwa mujibu wa sheria, badala yake Serikali inasema kwamba mfumo unaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Muungano nilitaka kauli ya Serikali kuhusiana na Muswada wa Katiba mpya ambao umeondolewa kwenye ratiba ya Bunge na Mkutano uliopita tulihakikishiwa kwamba utaletwa kwenye Mkutano huu wa Bunge, niliuliza mahususi kwa sababu suala hili lilihusiana vile vile na mvutano wa Muswada huo kutokuhusisha maoni ya upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kauli ya Serikali, maana kauli iliyotolewa hapa Bungeni ni kwamba Muswada bado upo kwa Spika, utaletwa pamoja na *amendments*, lakini kilichokubalika Bunge lililopita ilikuwa ni kwamba, ulikuwa

unakwenda kuandikwa upya, nataka kujua kwa sababu tukikosea kwenye Muswada wa Katiba tutakosea kwenye mchakato, tutakuwa na Katiba mpya yenye Muungano wenye kasoro kama ambavyo ipo hivi sasa. Naomba Kauli ya Serikali kuhusu maswali hayo mawili.

MWENYEKITI: Kinachoombwa hapa na Mheshimiwa Mnyika ni ufanuzi na kwa hiyo, naomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

WAZIR WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mnyika linalohusu uchafuzi wa mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba uchafuzi huo upo na tatizo la mazingira ni suala mtambuka, lipo kila sehemu hatuwezi tukayafanya yote kwa siku moja, kwa sababu hata Mji wa Dar es Salaam tumeanza kuufanya usafi, tunafagia na ningewomba Mbunge wakati tunafagia Jimbo lake la Ubungo ahudhurie kwa sababu asifikirie kwamba ni mtu mmoja tu anatakiwa kufagia ni sisi sote tunatakiwa kufagia. Sheria inachukua mkondo wake kwa watu wa Ubungo, wanaokojoa barabarani wameanza kuchukuliwa hatua, wanatozwa faini shilingi elfu hamsini. Juzi wakati nakuja Bungeni njiani tulikuta basi moja la Abood watu wake wanarusha chupa za maji nje tukalishika tukalipeleka Polisi, sasa sidhani kwamba nitaweza kutangaza kila adhabu inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inaendelea na hata Halmashauri ya hapa Dodoma tumeshawafuata sasa hivi mnaona hata mkija huku Bungeni usafi unaendelea. Kwa hiyo, taratibu zinafuatwa na suala la Mabibo *hostel* kuna mamlaka inayohusika tumeshawapa *notice*, kwa hiyo, tutafutilia. Lakini hatuwezi kutangaza kila kitu. Ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muswada wa Marekebisho ya Katiba ni suala la Wizara ya Katiba na Sheria, ndio maana sikuweza kulitolea kauli kwa sababu wenyewe Katiba na Sheria wapo. Sasa kama watakuwa tayari kutoa kauli sasa hivi au wakati wa bajeti yao ni suala la Wizara nyingine siyo la kwangu. (*Makofii*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba SMZ haikushirikishwa katika maandalizi ya Muswada wa Mchakato wa kubadili Katiba ili kupata Katiba Mpya. Utaratibu uliopo baina ya Serikali hizi mbili ya Muungano na ya SMZ ni wananchi Wakuu wawili kuwasiliana, barua ipo na siku ya *Cabinet* tulipoamua barua ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ilisomwa ikielekeza maoni ya Serikali ya Mapinduzi. Sasa sijui mwenzetu anapata wapi taarifa hizi, lakini ukweli ndio huo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Lile la kupata ufanuzi zaidi kuhusu mambo hayo litatolewa wakati wa Bajeti ya Wizara husika, Wizara ya Katiba na Sheria.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa, *vote 31 program 10*, Mshahara wa Waziri. Taarifa za kitafiti zinaonyesha kwamba kuna upungufu wa theluji katika Mlima Kilimanjaro, hali ambayo ukubwa wa mlima huu na umaarufu wa mlima huu na jinsi ulivyo katika sura ya dunia unaweza kuathiri mambo mbalimbali hasa kwenye shughuli nzima za tabia nchi. Mheshimiwa Waziri anatuambia nini Watanzania juu ya umuhimu wa mlima huu tatizo hili na upungufu wa theluji katika Mlima Kilimanjaro.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, theluji ya Mlima Kilimanjaro kukamata Mshahara wa Waziri. Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud linalohusu barafu inayopungua Mlima Kilimanjaro, ni kweli kabisa barafu hiyo inapungua na hilo ni suala zima la mabadiliko ya tabia nchi na mabadiliko ya tabia nchi yametokana na mabadiliko ya wanadamu kutokana na matumizi mabaya ya rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu ametupatia, tumekata miti, wote tumeshuhudia miaka iliyopita, wale wenzetu Wachaga wakichoma moto ule mlima kwa hiyo, ukichoma moto barafu haiwezi kubaki lazima iyeyuke na pia Wamekata miti sana. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote na nitafurahi sana kama Wabunge tutaamua siku moja wote tuelekee kwenye ule mlima tukapande miti kwa pamoja ili kurudisha hali ya mlima ule. Kwa hiyo, naomba wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, wote wanaotoka kule wakahamasishe upandaji wa miti, tuache kuchoma moto ili turudishe barafu ya Mlima Kilimanjaro. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niliuliza swali ni lini watu walioathirika na uchafuzi wa Mto Tigit watakuwa *compensated* lakini Waziri amelijibu hili *very lightly* na akasema kwamba hakuna watu waliokufa kule na kwamba hakuna *connection* ya uchafuzi wa Mto Tigit na madhara waliopata wakazi wa Nyamongo na mifugo na mimea. Ningependa Waziri anifafanulie zaidi kwa sababu kuna ripoti zinaonyesha wazi kabisa hata hiyo *cyanide* aliyosema ambayo na-*deny* hapa kwa sababu kabla ya kampuni ile kuja kulikuwa hakujatokea madhara haya kwa wananchi wale wanaozunguka mgodi, ni kwa miaka mingi wananchi wadogo wadogo walikuwa wanachimba madini yale bila kupata madhara yoyote yale na haya yametokea baada ya huo mgodi kuja pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye maelezo ya Waziri, ukurasa namba 65 ameeleza kwamba katika *ku-store situation* wamejitahidi kuchimba visima zaidi ya saba na vingine vinafanyiwa upembezi yakinifu. Ukweli uliopo ni visima viwili tu vimechimbwa na hamna visima zaidi na viji ni vingi zaidi. Kwa hiyo, wananchi bado wanateseka wanatumia yale yale maji ambayo yamekuwa *contaminated*. Kwa hiyo, ningependa pia Waziri anitolee majibu kwa hilo. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu la msingi lilisema kwamba masuala ya kuchunguza wanadamu jinsi walivyoathirika ni utafiti wa muda mrefu. Huwezi kupata jibu kwa mara moja. Nilisema kabisa wakati tunakwenda kule Waziri wa Afya alikuwepo, Waziri wa Nishati alikuwepo na Waziri wa Mifugo. Kwa hiyo, kila sekta ilichukua utafiti unaotokana na sekta yake. Ni kweli kabisa damu za ambao walidhaniwa wameathirika zilichukuliwa, zilivyokwenda kupimwa, kipimo kimeonyesha *mercury* na siyo *cyanide*, *North Mara* haitumii *Mercury* inatumia *cyanide*. Sasa huwezi ukasema kwamba watu hawa wamekufa kwa sababu ya *cyanide* itakuwa ni uongo kwa sababu mimi siwezi kushuhudia uongo. Kinachoonyesha kwenye kile kipimo ni *mercury*, ndio maana tunasema bado tunaendelea kufanya utafiti. Hata hawa ng'ombe wanaodaiwa kufa tumejaribu kuwaliza, tuonyesheni makaburi ya hao n'gombe hakuna anayeonyesha, tufukue tupate mifupa tukame. Lakini hawajaonyesha, ni *fabrication* mitaani, siyo kitu kizuri, tuwe wakweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nimekwenda kule tarehe 16 Mei, wakati wa tukio la *North Mara* la waliokufa, hii vita ya mwisho nilikuwepo kule na nimeona kila kitu, nilionyeshwa mpaka *camera*. Kitu kilichotokea ni kwamba wananchi walivamia mgodi na niliongea na Wenyeviti wote wa Vijiji vyote saba na wao walinipeleka mpaka sehemu mbalimbali na visima nimeviona. Ahsante sana.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimesimama kwenye fungu ili nipate ufanuzi kwenye mafungu yote yanayohusu mafunzo ndani na nje ya nchi. Ofisi ya Makamu wa Rais, ina mafungu tisa, ukianza *vote* 26 na *vote* 31 ambayo tuko sasa yaani yanahu mafunzo ndani na nje ya nchi. Lakini suala liliilonisikitisha, nimepiga hesabu kidogo mafungu yanayohusu mafunzo nje ya nchi yana jumla ya Sh. 608,150,000 mafunzo ndani ya nchi yetu ni Sh. 73,600,000 bajeti ya nchi yetu ni tegemezi kwa kiwango kikubwa sana. Sioni kwa nini tutumie hela nyingi hivyo kwenda kupeleka watu wasome nje ya nchi wakati tuna Vyuo Vikuu zaidi ya 30 katika nchi yetu na vyuo vingine vingi tu ndani ya nchi ambavyo vingeweza kuwafundisha watu hawa na hela hizi zikabaki ndani ya nchi. Naomba Serikali itoe maelezo madhubuti kwa nini tunakuwa na *trend* hii kutumia fedha nyingi namna hii kwa ajili ya mafunzo nje ya nchi wakati tungeweza kuwafundisha watalaam wetu ndani ya nchi yetu na hizi fedha zikabaki katika nchi hii. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kifungu cha mafunzo nje ya nchi kina fedha nyingi kuliko mafunzo ndani ya nchi. Lakini ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kuna shughuli za mazingira. Kuna fani nyingine ambazo hazisomeshi ndani ya nchi hasa kwenye *specialization*. Fedha za mafunzo nje ya nchi zinakuwa nyingi kwa sababu ya ununuizi wa tiketi, *tuition fees* na kwa sababu ya *upkeep* kwa maofisa wetu wakiwa kule mafunzoni. (*Makofi*)

Mafunzo ndani ya nchi kwa vyovyote itakuwa rahisi kwa sababu hakuna *travelling expenses*, kama zipo ni za ndani. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile mafunzo nje ya nchi kitakuwa kina fedha nyingi kuliko ndani ya nchi. Pengine ukute wanaokwenda nje ya nchi ni kidogo kuliko wanaosomeshwa ndani ya nchi kwa fedha hizi hizi. Kwa hiyo, huo ndio ufanuzi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika mchango wangu wa maneno na maandishi nilijadili masuala mawili, la kwanza lilikuwa la masuala ya Muungano, lakini la pili lilikuwa la suala la mazingira. Nilijikita kwenye matatizo ambayo yako kwenye Jimbo langu na hususan viwanda ambavyo vinatoa kemikali kali ambazo zina madhara kwa binadamu maeneo ya Mikocheni na ambayo yanapitishwa kwenye mikondo ya maji ambayo inapita kwenye nyumba za wananchi wangu. Sasa Mheshimiwa Waziri nilimtajia mpaka majina ya viwanda, lakini naona katika majumuisho yake hajazungumza chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nilimwambia kuhusiana na huyu mtu anayeitwa Robert Mgisha ambaye anajenga Mto Mbezi licha ya kwamba Kamati iliundwa inayojumuisha Ofisi zote tatu ya Ardhi, ya Makamu wa Rais na *NEMC* ili kuweza kuangalia uhalali wa hati zake. Hati zake zikagundulika ni feki. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri, kwa sababu majibu yake alisema kwamba sheria ya mazingira ilitungwa wakati hivi viwanda viwo. Sasa anatuhalalishia hapa kwamba kwa kuwa sheria ilikuta viwanda maana yake watu wangu wafe kwa sababu wenye viwanda wanakiuka sheria na taratibu. Naomba Waziri alitolee ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye suala la Muungano kuhusiana na suala la mafuta. Kuna taarifa ambayo inasema kwamba Serikali ilimwagiza Mshauri Mwelekezi wa *OPEC* kuhusiana na mustakabali wa hili suala la mafuta. Lakini vile vite kuna hoja kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mliandika barua kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuomba hili suala la mafuta lisiwe la Muungano, sasa nataka nipaye *clarification* kuhusiana na haya mambo ili kuondoa utata uliopo. Lakini muhimu ni la watu wa Jimboni kwangu nataka majibu yanayojitosheleza.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumjibu Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Wajibu mkuu wa Serikali ni kulinda maisha ya wanadamu wa Tanzania nzima na siyo wa Jimbo lako tu. Napenda kusema kwamba hili suala kwa vile wote tuko Dar es Salaam ungelileta ofisini tungekuwa tumeshalifanyia utafiti. Lakini sasa kwa vite umelileta hapa nakubaliana na wewe na tukitoka hapa twende pamoja tukamuone huyo ndugu Robert Mgisha na sheria itaangalia jinsi hizo hati zake kama zipo, mimi siyo mtaalam lakini nina watalaam ofisini, tutakuwa pamoja kwa hiyo, tutafanya kazi pamoja. Lakini suala la kumwaga maji baharini kwa ujumla nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba tunaangalia sasa hivi na tumeshatoa *notice* kwa viwanda vyote ambavyo havina mtambo wa kusafishia maji taka. Kwa hiyo, tutaendelea kukagua na kuhakikisha hivyo viwanda ambavyo havitii sheria hiyo vifungiwe mara moja. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):
Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyojasema Mheshimiwa Halima Mdee ni kweli. (*Makofii*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufanuzi wa mambo mawili, moja la Muungano na lingine la Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Muungano nilizungumzia sana juu ya haja ya kuwaelimisha Watanzania juu ya Muungano kwa mambo yote yaliyotokea wakati wa Muungano. Lakini maneno yamezungumzwa hapa na Mawaziri kwamba *let by gones be by gones*, tunachokonoa mambo na nini. *Impression* inayotokea ni kwamba hakuna utayari wa kukiri makosa yaliyofanyika wakati Muungano unaundwa au yaliyotokea baada ya Muungano. Hii si namna ya kuelimisha wananchi juu ya Muungano. Sasa ufanuzi naomba kama Serikali inaanini kwamba jukumu letu ni kuwaambia Watanzania yaani tunayofikiria ni mambo mema tu ya Muungano halafu yale mabaya yaliyotokea kwetu kama kuua watu maana niliuliza Kasi Mhanga yuko wapi aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa *People's Republic of Zanzibar*? Abdul Twara yuko wapi, Othman Sharif yuko, Mdungi Ussi yuko wapi? Wote hawa walikuwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawajulikani walipo, historia yetu haiwatambui na wote hawa ni *victims* wa Muungano. Sasa inaelekea haya mambo mabaya yaliyotokea wakati wa Muungano *they should be by gones*, tuonyeshe tu picha na hiyo siyo namna ya kufundisha watu. Nahitaji kama hiyo ndio sera ya Serikali, naomba ufanuzi huo.

Pili, kuhusiana na mazingira. Nina ripoti tatu hapa zinazohusu uchafuzi wa Mazingira katika Mto Mara unaotokana na shughuli za uchimbaji wa dhahabu za *North Mara Gold Mine* za huo mgodi na zote moja ni ya Juni, 2009, nyingine mwezi Aprili, 2009 zote zinasema kwamba shughuli za uchimbaji dhahabu katika eneo la Nyamongo limesababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira. Moja imefanywa na watalaam wa hapa kwetu. Nyingine imefanywa na watalaam kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi za Uhai *Norway*. Nahitaji ufanuzi kutoka kwa Waziri.

MWENYEKITI: Ufanuzi kuhusu nini?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Kuhusu kama anakubali kwamba Mgodi wa *North Mara Mine* ni *responsible* kwa kuchafua mazingira na kuhatarisha maisha ya watu kama ambavyo watalaam hawa wanasema.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, kama ifuatavyo:-

Mgodi wa *North Mara* haujaanza wakati wa wawekezaji walipokuja ulianza kabla. Kwa hiyo, mazingira haya yalichafuliwa kabla kwa wananchi kutumia *mercury*. Unavyojuwa wananchi wetu hawajapata *training*, wanapotumia ile *mercury* wanaitupa tu inakwenda kwenye mito, kwa hiyo, ndio maana kunatakiwa ukaguzi yakinifu kabisa kubaini kwamba madhara haya yalianza kabla au baada ya wawekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwezi ukawazushia kwa sababu hata kwa wachimbaji wengine wadogo wadogo sehemu ziliko mbalimbali Tanzania wachimbaji hawa wanatumia *mercury* hakuna mtu anaweza kubisha. Lakini wanamwaga wapi ile *mercury* hawana mitambo, kwa hiyo, hatuwezi tukawasingizia wawekezaji kwa sababu tuna hasira kwamba wawekezaji wapo, kwa hiyo, tuwe wakati mwingine tunafikiria vizuri na siyo kutoa kauli ambazo si kweli na kuwapotosha wananchi. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tena ufanuzi kwa Mheshimiwa Tundu Lissu kama ifuatavyo:-

Kwanza nirudie swal lake wale wote watu alioniliza wako wapi, *Wallah* sijawahi kuona sura zao, kwa hiyo, siwajui. Kwa umri wangu sikuwahi kuona sura na mimi nasoma kama unavyosoma wewe, siwajui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sikukataa elimu ya Muungano kwa Watanzania, iko haja ya kutoa elimu ya Muungano kwa Watanzania. Yaliyopita ni historia imepita na ni vizuri kufundishwa. *Whether* ni nzuri au historia mbaya lakini historia ni historia. Ninachokataa hapa ku-*trumpet* yale yaliyotokea ikaingizwa sumu Zanzibar na kuchafua tena siasa zetu. Hilo ndilo ninalokataa kama kuna watu walikufa *whether* kwa Muungano au kwa nini ni Wazanzibari, tulioCAA kitako kupatana ni Wazanzibari tuachie tuendelee na siasa zetu. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ningekuwa na nishani ningemvisha Mheshimiwa Waziri Suluhu kwa majibu mazuri.

TAARIFA

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunafanya fujo, hizi meza zimetengenezwa kwa makaratasi, sasa kupiga makofi haisaidii kitu, hapa tumekuja kufuata maneno na vitendo. Sasa tunavyopiga makofi hivi, hizi meza tunategemea Wabunge wanaokuja wasizitumie? Ni uharibifu. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo mmepewa Wabunge wote, taarifa hiyo mnaipokea ama mnaikataa?

WABUNGE FULANI: Tunaipokea.

BAADHI YA WABUNGE WENGINE: Tunaikataa hiyo.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Kombo.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati nilipokuwa nachangia nilimuomba Mheshimiwa Waziri anapokuja anipe ufanuzi wa

bei ya petroli kwa ile kodi ya ushuru ambayo inatolewa huku na ikatufanya sisi Zanzibar tuwe *affected*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilikuwa naomba...

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Kombo kama ungefafanua kidogo kodi ya petroli iliyofanyaje?

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya petroli hapa Bara ni sawa na ya Zanzibar, lakini kodi yake mpaka ikafikia sawa na ya Bara kuna *road toll*, kuna *EWURA* na mambo mengine ishirini na moja wakati haya mambo kule Zanzibar hakuna, hakuna *road toll*, hakuna *EWURA*, hakuna *wolfage*, mafuta yanakuja moja kwa moja kwenye matanki sasa nilikuwa nikiomba ufanuzi huu.

La pili, nilikuwa nikiomba anifafanulie ile elimu ya juu ambayo nilizungumzia *share* ya Zanzibar iwekwe ili isichanganywe pamoja na watu wa Tanzania Bara kwa sababu *population wise* ya huku na *population wise* ya Zanzibar ukichanganya pamoja basi hakutatokea kitu chochote nafasi arobaini zilizopo au elfu moja zote zitakwenda Bara. Sasa naomba ufanuzi lakini pia namshukuru sana kwa majibu yake mazuri hasa ya wale watu aliokuwa hakuwaona yeeye awajue, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mussa Haji Kombo ananiingiza kwenye fani sio yangu ya mafuta, nimuhidi tu kwamba tutalifanyia kazi na sekta za nishati za SMZ na SMT, tutakaa nao tulifanyie kazi halafu tutaleta majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ya juu kuna malalamiko upande mmoja imo katika changamoto za Muungano tunalifanyia kazi, tutakapofikia tutatoa kauli ya Serikali Bungeni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Wa mwisho ni Mheshimiwa Ndugulile, sio kwa umuhimu, karibu sana Dokta Ndugulile.

MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali. Nimejikita katika *sub vote 1001*, mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 32 ameongelea mkakati wa kufadhi mazingira ya bahari ukanda wa Pwani, maziwa, mito na mabwawa. Katika Jimbo langu la Kigamboni, Tarafa ya Kigamboni hususani maeneo ya Kigamboni, Mji mwema, Somangila, Kimbiji na Pemba Mnazi kuna tatizo kubwa la uvuvi haramu. Nilitaka kujua

kuna mikakati gani ya kuelimisha na kuisaidia hii jamii ya wavuvi ili waondokane na uvuvi haramu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili katika mchango wangu niligusia kwamba kuna viwanda ambavyo vinachafua mazingira katika Jimbo langu la Kigamboni, kiwanda cha *Mian Gas* ambacho kiko Kidongoni Vijibweni na *KTM* na Kiwanda cha Simenti ambavyo viro Mbagala. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuja kuvikagua na kuchukua hatua stahili?

MWENYEKITI: Ahsante sana, tuanze na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndugulile kama ifuatavyo:-

Kwanza nikubaliane nae kwamba niko tayari kuja kufanya huo ukaguzi, pili watendaji wa ofisi yangu wako hapa na katika mkakati wa kufadhi ukanda wa Pwani, Wizara yangu inatoa mafunzo kwa wananchi jinsi ya kufadhi ukanda wa bahari na vilevile namna ya kutumia matumzi bora ya uvuvi. Kwa hiyo, elimu hiyo tutakuja kuitoa wala hakuna wasiwasi na labda niseme tu sio kwenye Jimbo lako tu ni ukanda wote kuanzia Tanga mpaka Mtwara. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda nilishajibu mara nyingi kwamba kuna mitambo hiyo lazima wawe nayo na tutakuja kucheki kama hawakidhi basi tutavifunga. (*Makofifi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri kulikuwa na swali la pili? Lilikuwa ni hili hili moja?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuondoa shilingi, Kanuni ya 103(2).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, ukae kidogo. Nilikwisha kukuruhusu kuzungumza katika eneo hili kama ulikuwa na nia hiyo ungefanya wakati ule ule, lakini sasa tumeshaendelea tulikuwa kwa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, sasa ukinyanyuka tena huku itakuwa kigodo si sawa sawa kwa sababu ya yale marekebisho ambayo tulishayakubali humu ndani kwamba tutasimama mara moja tu, kwa hiyo, mimi naomba twende na utaratibu huo. Basi kwa hatua hiyo naomba kuuliza fungu hilo mnaliafiki lipite?

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Shs. 280,040,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Shs. 737,171,500

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, niko kifungu kidogo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa.....

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Susan Lyimo.

MWENYEKITI: Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 220800, *Training Domestic*, naelewa kwamba wakati Mheshimiwa Zambi ameulizia suala la *training*, Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba kuna *courses* nyingine hazipatikani hapa nchini, lakini kifungu hiki kiko katika Idara ya Sera na Mipango na mimi naamini katika vyuo vyetu hapa nchini tuna Chuo kama Chuo Kikuu ambacho kina *Economics Departments* ambayo inatoa *courses* mpaka za Uzamivu yaani *Ph.D*.

Sasa tukiangalia kwanza moja nilitaka kupata ufanuzi kwa nini katika kifungu hiki hakina pesa mwaka huu hata kidogo na pili ni kwa nini basi wanawapeleka watu nje wakati ni suala la sera na mipango ambapo hapa nchini kuna *course* hiyo. Kwa nini kifungu hiki hakijapata hata senti tano mwaka huu?

MWENYEKITI: Kwa nini kifungo hicho hakijapata pesa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hakikuwekewa pesa kwa sababu kwa mwaka huu Idara ya Sera na Mipango hawajapanga kusomesha, lakini kwa nini wanakwenda nje na sio mafunzo ya ndani. Mafunzo ya Idara ya Sera na Mipango yote yanaweza yakapatikana Tanzania, nafasi za nje ni zile nilizosema ni *special profession* za mazingira katika fani mbalimbali za Idara ya Mazingira sio Idara ya Sera na Mipnago.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1004 - *Information, Edu. and Comm.*Shs. 283,046,000

Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*..... Shs. 194,869,000

Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.....Shs. 207,042,000

Kifungu 2001 - *Union Secretariat*.....Shs. 31,103,453,500

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 5001 - Environment.....Shs. 5,686,012,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika *sub vote* hiyo 5001 *item 221300 Educational Material, Supplies and Services*. Tumekuwa na malalamiko ya muda mrefu juu ya elimu kwa umma, juu ya utunzaji wa mazingira, fukwe za bahari zinaendelea kuharibiwa pia kwenye Maziwa na Mito na inaonekana tatizo hili bado linaendelea na ukiangalia mwaka 2010/2011 kulikuwa na *nine million*, mara hii pamoja na kwamba Serikali inasema inaandaa mikakati madhubuti, mipango kabambe ya utunzaji wa mazingira na elimu kwa umma, lakini kuna shilingi milioni sita, sijui ningeomba nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hii elimu kwa umma hasa tupunguze fedha, yaani elimu imakamilika vizuri au vipi? Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa umeeleweka, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, fedha kidogo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi kwa Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Hizi fedha zilizotengewa hapa ni fedha za *educational material* kama inavyosomeka pale, vipeperushi na vitu kama hivyo, lakini si kwamba ni hizo tu. Pia kuna fedha za wafadhili ambazo tumeshindwa kuziweka huko kwa sababu taratibu zake hazijakamilika. Kwa sababu unakuta kwenye fedha zetu za wafadhili kwa mfano *MKUHUMI, REDI* ambayo ipo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, zote hizo ni fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya kuelimisha wananchi, kwa hiyo, zipo nyingine ambazo hatukuziongesha hapa, lakini za wafadhili ambazo lengo lao kubwa ni kuelimisha na hiyo ni kutokana na ufinyu wa Bajeti ndiyo maana tumeona afadhalii tuweke hata hizo kidogo, ahsante. (*Makofii*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu cha 5001, *programme 50*, kasma 270800, *Current Grant to Non- Financial Public Units*.

Niliomba ufanuzi kuhusiana na kasma hii ambayo kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilikuwa na takribani shilingi bilioni 3.7 ikaja kuwa shilingi bilioni 2.7 na mwaka huu wa fedha tunaombwa kuidhinisha shilingi bilioni nne na ushee, ufanuzi niliokuwa nimeuomba ulikuwa kwenye mambo mawili; moja kwa kuwa hiki kiwango ni kikubwa shilingi bilioni nne na hakina *breakdown*, niliuliza ni kwa nini Wabunge hatujapewa nakala ya randama ambayo ingetuwezesha wakati wa kupitisha matumizi kujua hizi shilingi bilioni nne zinakwenda kwenye taasisi zippi na kwa utaratibu upi.

Lakini la pili nikaomba ufanuzi kuhusu matumizi ya pesa zenyewe. Mheshimiwa Waziri kwenye ufanuzi wake amesema kwamba sababu ya kiwango kuongezeka kutoka shilingi bilioni 2.7 mpaka shilingi bilioni nne ni kupanuka kumuundo na hivyo kuongeza masuala ya posho na masuala la mishahara, hii *logic* nashindwa kuielewa kidogo kwa sababu mwaka wa fedha wa nyuma yake yaani mwaka 2009/2010 ulikuwa na shilingi bilioni 3.7 halafu zikapungua zikawa shilingi bilioni 2.7 halafu zimeongezeka gafla kwenda shilingi bilioni nne na ushee kwa hiyo ningeomba bado kupata ufanuzi kuhusu makusudio ya matumizi haya na ufanuzi vilevile ni kwa nini hatukupewa randama kwa sababu tukipitisha hiki kifungu bila *breakdown* tunakuwa kama vile tunauziwa mbuzi kwenye gunia. Kwa hiyo, ningeomba ufanuzi wa kina sana kuhusu hiki kifungu, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: La randama ni la kwetu la Bunge zaidi, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi ujibu hayo mengine.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama ulivyosema randama sisi tulishakabidhi. Kuhusu kifungu anachokizungumzia ni kweli kabisa kwamba fedha tulizopangia hapo kiasi hakitoshi, lakini bado ongezeko hili ni kubwa kutokana na ongezeko la mishahara kwa ajili ya taasisi ya *NEMC* kwa sababu Baraza la *NEMC* lipo chini yetu kwa hiyo mishahara inatoka hapo na kuanza kutumia muundo mpya kwa mfano kwa mwaka jana mishahara ilikuwa shilingi bilioni 1.2, mwaka huu mishahara ni shilingi bilioni 2.6 na kwa sababu wote tunajua kwamba watendaji wa Baraza hili hawatoshelezi kwa hiyo tunategemea kifungu hiki kiwe kinaendelea kuongezeka kila mwaka mpaka hapo tutakaposema watendaji wametosha, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, nitoe ufanuzi kuhusu suala la randama.

Waheshimiwa Wabunge, mkishika *Order Paper* yoyote ile na hata ile ya leo utaona kwamba ile ya leo kwa mfano imewekwa mezani hapa randama za Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 maana yake ni shughuli itakayofuata tutakapokutana tena hapa ndiyo Wizara ambayo tutakayoishughulikia kwa hiyo randama zake zinakuwa tayari zimekwishawasilishwa hapa, mbona mnaniwahi si mnisikilize basi.

Waheshimiwa Wabunge, zinakuwa zimekwishawasilishwa hapa mezani na ni kitabu cha aina hii. Hii ni randama kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inayohusu Makadirio na Matumizi ya Mapato ya Fungu 26 na 31 na kadhalika ambayo ilipelekwa kwenye Kamati zetu, Kamati zetu zote kabla ya kufika hapa tulishughulika na randama mbalimbali kwa hiyo zimewekwa hapa mezani na zinawekwa Maktaba. Kitu ambacho ningependa tukishughulikie tutaongea katika Kamati ya Uongozi na Wenyeviti wenzangu wa Kamati kwa sababu vitabu hivi ni vya kawaida, nilisikia maelezo kwamba Serikali walikuwa wameambiwa walete *copy* fulani chache, *copy* kumi. Hilo la *copy* kumi ndiyo sijui hata sababu yake ni nini kwa kweli, lakini naomba mtuachie katika Kamati ya Uongozi wiki ijayo tutakaa tuongee kwa sababu baadhi inaweza ikawa kubwa sana, lakini baadhi wala si kubwa kiasi hicho ni za kawaida.

Mimi naamini kabisa tunaweza tukalizungumza tupate utaratibu ambao unawenza ukaraphisisha kwamba kila Mbunge aweze kupata nakala kwa urahisi. Kwa sasa kwa wakati huu, kwa sasa randama hizi zinapatikana kwenye Maktaba yetu ya Bunge hapo ghorofa ya pili,, naomba kila anayehitaji afike pale kwa sasa. Ahsante sana. Mheshimiwa Lissu.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri taarifa.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Tisa tuliazimia kwamba randama ziwe kumi na sababu kubwa ni gharama na sasa ndiyo zaidi tena, tukitoa randama nakala 350 kwa kila *vote* sio Wizara *of course* inawekwa kwenye nanii ya Wizara, tulipiga hesabu wakati ule ilionekana ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, mtu ambaye ana hamu ya kujuua kuhusu Wizara fulani ni vizuri aweze kwenda Maktaba asome basi anarejea. (*Makofi*)

Kusema kwamba tutachapisha randama 350 kila siku na sio 350 na nakala za Ofisi na kadhalika kwaa kila *vote*, gharama yake ni kubwa sana ndiyo maana tulifika uamuzi huo. Mimi ningesihi utaratibu huu uendelee. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na isitoshe hayabebeki, tulifanya hesabu ukichapicha Randama 350 kwa kila Mbunge kwa *vote* 90, kila Mbunge atakuwa na randama zaidi ya 90, *vote books* tu yanaachwa hapa, yanatupwa, sasa ukileta na randama juu yake unafanya kitu ambacho hata hakiwezekani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, mimi nashukuru sana kwa maelezo haya ni mazuri na yametujenga. Kama nilivyosema kwenye Kamati ya Uongozi tutaliangalia vizuri zaidi jambo hili, kwa sababu kwa vyovyyote vile kwa Wabunge 350 kwa nakala 10 ni chache sana kwa Wizara yoyote, Wabunge hata 30 tu wangependa kuchangia kwa kuongelea randama ya kwanza, kwa hiyo, tutalitazama kwa maana ya kufanikisha zaidi katika mazingira ya sasa, si kwa nia ya kuchapisha, maana hebu tazama wangapi ambao hawapo hapa, sasa randama zao zingekuwa mezani, lakini tupate idadi ambayo *is workable*, tutaliangalia na tutalifanyia kazi ili tusiulizane habari ya randama tena huko tunakokwenda, ikiwezekana tunaweza tukatenga hata kama ni Maktaba au na chumba kingine cha ziada au tukawa tunatoa hata kwenye kambi mbalimbali Kambi ya Upinzani nakala kadhaa. Lakini tutaliangalia ili turahisishe zaidi namna ya kuenenda. (*Makofi*)

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Taarifa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Nashukuru sana. Nilikuwa nataka na mimi niongezee katika hili suala la randama. Nilitaka nitoe wazo kwamba njia mojawapo ya kurahisisha ni kutumia *TEKNOHAMA* kwamba hizi randama tunaweza tukazi-upload katika website yetu ili basi Waheshimiwa Wabunge waweze kuwa wanazi-access badala ya kuwa wanafanya printing. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Makofi hayo maana yake wanakubaliana na wewe. Ahsante sana. Mheshimiwa Tundu Lissu. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaomba ufanuzi wa hili kwa sababu tu randama hazijatolewa kinyume na Kanuni ya 99(4). Kwa hiyo, nitauliza kwa sababu hiyo. Swali langu kwa kuangalia kasma zote ambazo zimetolewa kwa ajili ya utunzaji wa mazingira hakuna fungu hata moja linaloonyesha Idara ya Mazingira imetengewa kiasi gani, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limetengewa kiasi gani. Ni fedha kiasi gani zimetolewa kwa ajili ya *Environmental Monitoring and Enforcement* na matatizo ya kutokuainisha haya mafungu au pengine yameainishwa kwenye randama ambazo hazijaletwa Bungeni ni kwamba tunaweza tukawa tunapitisha mafungu hapa bila kufahamu tunapitisha kitu gani.

Sasa mimi naomba niambiwe, naomba nipewe ufanuzi kuwa fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kufanya *monitoring* ya uchafuzi wa mazingira, kwa ajili ya *environmental monitoring* ni kiasi gani, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili *enforcement* ya Sheria za Mazingira kama katika maeneo haya ya migodi ambayo tunaambiwa kwamba yana matatizo ni kiasi gani. Kwa sababu katika kasma zote hizi hayaonekani na hakuna randama za kutusaidia hapa. Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Tundu Lissu. Lakini tatizo ni kwamba hizi *vote*, ni *vote* ambazo ziko *standard* na ziko katika mfumo ambao Hazina wameuteremsha. Kwa hiyo, fedha hizi unazozizungumza ziko *imparted* ndani ya vifungu tofauti katika hivi vifungu tunavyozungumza. Ni *standard format* ambayo hatukuweza ku-*identify monitoring and evaluation*. Lakini nakubaliana na *concern* yako. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zambi ulisimama?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama.

MWENYEKITI: Ahsante endelea.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Lakini hoja yangu iliulizwa na Mheshimiwa Mnyika na kwa sababu ya Kanuni sipaswi kuendelea nayo tena. Ilishajibiwa.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kifungu 1001 – *Administration and General*.....Shs. 5,900,000,000

MWENYEKITI: Ni Mheshimiwa Mnyika peke yake. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kifungu 1001, Kasma 6389, *Construction of Vice President Office Dar es Salaam*. Niliomba ufanuzi kuhusiana na hoja ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam na nilitoa hoja mbili. Hoja ya kwanza nilisema kwamba sera ya Serikali ya CCM ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa kuhitimisha hoja ni kuhamia Dodoma kwa kuachana na kujenga maofisi ya Kiserikali Dar es Salaam.

La pili nilisema kwamba kiwango tunachotaka kikitenga hapa cha shilingi bilioni 3.4 ni kiwango kikubwa sana. Ni shilingi milioni 3,400 wakati ambapo na hiki ni fedha zetu za ndani, wakati ambapo kwenye kazi yenewe ya kudumisha Muungano *Union Secretariate* imetengewa kwa pesa zetu za ndani shilingi milioni 133 peke yake fedha zetu za ndani. Kwenye kazi ya kulinda mazingira masuala ya tabia nchi pesa za ndani tumetenga shilingi milioni 92 peke yake. Kwenye masuala ya usimamizi wa Sheria za Mazingira pesa zetu za ndani tumetenga shilingi milioni 200 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo nitaomba nipewe ufanuzi wa kina na kama ufanuzi hautanitisha Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kabisa kusudio la kuondoa shilingi kwenye kifungu hiki ili niweze kupewa maeleo ya kina. Maeleo yaliyotolewa ya kwamba ujenzi huu kwa ujumla pesa zote ni shilingi bilioni saba peke yake. Lakini kwenye mazingira ni shilingi bilioni 7.5. Ni maeleo ya kutaka kufanya *propaganda* kuonyesha kwamba kweli Serikali inajali mazingira. Lakini ukweli ni kwamba kwenye ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais peke yake ukijumlisha na fedha zilizotumika mwaka uliopita ambazo ni shilingi bilioni 3.7 na pesa za mwaka huu ambazo ni shilingi bilioni 3.4 ujenzi wa Ofisi peke yake Dar es Salaam unatumia shilingi bilioni saba na ushehe. Kwenye mazingira pesa zetu wenewe za ndani tunakwenda kutumia shilingi bilioni 1.3 peke yake kwa miradi yote ya mazingira na kwenye miradi ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa tunazozitegemea za mazingira ni pesa za wahisani takribani shilingi bilioni 7.5. Sasa Kamati imesema hapa kwamba kwa mwaka wa fedha uliopita wahisani mpaka ilipofika mwezi Aprili kati ya shilingi bilioni 23 walizokuwa wametuhidi kwa ajili ya mazingira walikuwa wametupa mpaka mwezi Aprili shilingi milioni 482 peke yake, yaani tulionomba shilingi milioni 23 tukapewa shilingi milioni 482 peke yake mpaka mwezi Aprili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo maana naona matatizo ya mazingira tulionayo iwe ni kule kwangu Mabibo, kule kwenye uchafu *Mabibo Hostel* pale, iwe ni Mto Tigit na kadhalika, yanachangiwa na kutoweka kipaumbele katika kuelekeza pesa kwenye mahali kambapo tunaakwenda kushughulikia masuala ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba kutoa hoja kwamba kwenye hili nisipopata ufanuzi niondoe shilingi. Naomba nipewe fursa ya kuondoa shilingi kama ufanuzi hautaniridhisha. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoa ufanuzi kwamba kifungu hiki cha ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ni majengo mawili, jengo la Tunguu Zanzibar na lile la Dar es Salaam. Pesa hizi ziliombwa kwenye Bajeti ya mwaka jana hazikutoka, sawa sawa na vile tunavyoomba za wafadhili zikawa haziji. Kwa hiyo, kwa sababu tuna ma-contractor wameshajenga, wanatudai tumeziomba tena mwaka huu, ili tulipe *contractors*. Tatizo ni lile lile, lakini anaposema kwamba pesa za mazingira ni kidogo tunategemea sana wafadhili, pesa za wafadhili ni *general budget support* ambayo tukishakuipokea inakuwa ni pesa ya kwetu. Kwa hiyo, *wether* imetoka kwa wafadhili au imetoka, Hazina ni pesa ya kwetu na mazingira kwa mwaka huu imepangiwa shilingi bilioni 7.5. Hii huku ni shilingi bilioni 3.4 ambayo ma-contractor wameshafanya kazi, wanatudai. Huo ndiyo ufanuzi nilionao. Asante Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 103(2), niweze kutoa hoja ya kuondoa shilingi na kwa kweli katika hili nitaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba nasikitishwa na maelezo yaliyotolewa. Kwa sababu kwa mujibu wa kitabu kilichopo hapa mbele yetu masuala ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais yana vifungu viwili. Kuna Kifungu 6309 *Construction of Vice President Office and Residence in Zanzibar* ambacho kilitengewa shilingi bilioni tatu mwaka 2009/2010 ambazo hatujaelewa zilitolewa au hazikutolewa, kitatengewa tena shilingi bilioni moja mwaka wa fedha uliopita, kimetengewa tena shilingi bilioni 1.5 mwaka huu. Mimi sina ugomvi kabisa na Ofisi ya Makamu wa Rais kujengwa Zanzibar na ndiyo maana sikuzungumza chochote kuhusu hiyo Ofisi ya Zanzibar pamoja na kuwa niliona mabilioni yaliyotengwa hapa. (*Makofi*)

Mimi nazungumzia Ofisi ya Dar es Salaam ambayo iko kwenye Kasma 6389 ambayo mimi naelewa kwamba toka mwaka wa fedha uliopita Makamu wa Rais wetu anafanya kazi. Makamu wa Rais ni Msaidizi wa Rais na taasisi hii inafanya kazi kama kawaida. Kwa hiyo, sielewi kabisa mantiki ya kuja kuamua kutenga shilingi bilioni 3.4 ambayo ni pesa nyingi kwenda kujenga Ofisi Dar es Salaam kwa Serikali iliyosema inakusudia kuhamia Dodoma. Kama ingeandikwa hapa kujengwa Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma ningelewa kwamba hapa Serikali inatekeleza sera yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu hili la kwamba kweli pesa za wahisani zinakuja. Mimi naelewa *principal donor funding* na *budget support*. Mimi ninachokisema hapa na natumia ripoti ya Kamati ya Bunge *unless* Waziri atuambie Kamati ya Bunge imelidanganya Bunge, nasoma ukurasa wa 10 maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikaachana na dhana ya kutegemea wafadhili wa Bajeti na kadhalika. Mwisho inaendelea, iliomba shilingi bilioni 23 ambayo ni milioni elfu

ishirini na tatu. Imepewa shilingi milioni mia nne peke yake mpaka mwezi Aprili, kama hali ndiyo hii, hii miradi ya maendeleo ya mazingira itatekelezwa vipi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Natoa nafasi kwa sababu ni suala la shilingi kwa Wabunge wasiozidi watatu wanaotaka kuchangia jambo hili kwa dakika zisizozidi tatu, tatu wowote wale. Kwa dakika sizozidi mbili, mbili kufuatana na Kanuni yetu tuliyopitisha juzi. Wamesimama wawili, nitawapa hawa wawili ambao ni Mheshimiwa Tundu Lissu halafu Waziri Mheshimiwa Samuel Sitta. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sana na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwamba Serikali imekuwa inazungumza kwa ndimi mbili. Ulimi wa kwanza unasema tunahamia Dodoma. Ulimi wa pili unasema tunapeleka hela za kujenga Ofisi za wakubwa hawa Dar es Salaam. *We have to make a choice*, tunataka kuhamia Dodoma au hatutaki. Kama tunataka kuhamia Dodoma hizi Ofisi zijengwe Dodoma, kama tunadanganya watu tu kwamba tutahamia Dodoma lakini tuko Dar es Salaam basi tutangaze kwamba ni sera tubaki Dar es Salaam na ijulikane. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhamia Dodoma lipo pale pale, kilichopo hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri ameeleza jengo lilikuwepo, lilifikia hatua fulani. Sasa si lazima ulikamilishe. Hivi tutaacha magofu Dar es Salaam kwa sababu ya kuhamia Dodoma? Mimi nadhani itakuwa haina maana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mimi kama Mwenyekiti niseme kwa kweli kabla ya Mheshimiwa Mnyika, jambo hili ni jambo jema tu lenye afya kwa nchi yetu na Bunge letu. Picha tunayoipata hapa siyo zaidi kwa hili lililopo hapa ni kwa Wizara zinazokuja, kama Wizara zinazokuja zina makasma ya kujenga majengo yao Dar es Salaam hii ndiyo *message* kwamba mwelekeo ni kujenga Dodoma na hiyo ni Sera ya Chama cha Mapinduzi kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri mkija tena na mambo ya Dar es Salaam hapa huo ndiyo ujumbe wenywewe. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo mawili tu, la kwanza niseme kwamba nina tatizo na utaratibu wetu wa kuamua kujenga na ku-*invest* pesa nyingi shilingi bilioni 3.4 kwa mkandarasi halafu ndiyo baadaye ndiyo kuja kuliomba Bunge lipitishe pesa za kulipa kitu ambacho kilishafanyika. Kwa hiyo, kwa tafsiri ya moja kwa moja Bunge hili linataka kutumika kama *rubber stamp* na Serikali kitu ambacho mimi sikiafiki. (*Makofi*)

La pili, binafsi nitalegeza msimamo kuhusu hili kama Serikali itanihakikishia kwamba ipo tayari kupunguza kutoka kwenye hili fungu kuongeza pesa za ndani kwenye miradi hii ya kwenda kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, kwenye miradi hii ya usimamizi wa Sheria za Mazingira kama tutawategemea wahisani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Nina dakika mbili Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITU: Mheshimiwa Mnyika, tayari. Ni hivi wazo la kusema kwamba katika hatua hii unaweza ukatoa fungu kushoto ukapeleka kulia, hilo wala haliwezekani, halimtegemei Waziri. Lakini la pili kwa nini nimekuita ukae chini kwa hatua hii kwa sababu maelezo yalikwishatolewa na Waheshimiwa Mawaziri. Kwa hatua hii ya kusimama sasa ulipokuwa umesimama ni mahali pa kutuambia tu endapo unairudisha shilingi uliyokuwa umeishika au unaendelea kukaa nayo ili sasa unipe Mwenyekiti nisogee mbele katika hatua ambayo inatakiwa isogee. Lakini ukianzisha hoja upya sasa utanipa ugumu wa namna ya kuendesha. Maana yake majibu yalikwisha kutoka kuhusu jambo hilo. Sidhani kama kuna majibu mapya, majibu ni yale yale.

Kwa hiyo, nafasi uliyo nayo ni ya kutusaidia katika kikao hiki kwamba ile shilingi uliyosema umeikamata bado unayo baada ya maelezo haya au umeirudisha.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kanuni zifuatwe. Kwa mujibu wa Kanuni ya 103(8), baada ya Waziri kujibu kwa mujibu wa Kanuni ya 7 inanitaka mimi ambaye nilikuwa mtoa hoja nijibu kile alichosema Waziri na nipewe muda wa kujibu kabla ya kukubali kama ni kurudisha shilingi ama naiondoa, napewa fursa ya kujibu hiyo hoja. Kwa hiyo, nilichokuwa nakifanya kipo ndani ya Kanuni kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba unipe fursa ya kujibu hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri, kabla ya Wabunge wengine kuweza kufanya maamuzi. (*Makofi*)

MWENYEKITU: Umejibu nimekupa dakika, ukumbuke ni dakika mbili na nimekuvumilia umetumia zaidi hata ya dakika mbili. Mimi ninachokisubiri huku katika majibu yako kama Mwenyekiti wa Kikao hiki pamoja na yote utakayoyaeleza, ni je, unarudisha shilingi au hurudishi, hiyo ndiyo *interest* yangu mimi pale. Maana lazima tuelewane kila mmoja kwenye kazi yake anataka kufanya jambo gani. Kwa hiyo, nakupa nafasi basi dakika mbili, lakini *interest* yangu uifahamu iko wapi. Maana ukiuliza maswali Waziri hawezি kukujibu tena. Lazima useme mwisho wake uniambie kama unarudisha au hurudishi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti na nitazingatia mwongozo wako. Niseme tu kwamba sijaridhika na maelezo yaliyotolewa na Serikali kwa sababu maelezo hayo yana sura ya kulifanya Bunge chombo cha kupitisha fedha za matumizi ambayo Serikali ilikwisha yafanya na wakandarasi wanasubiri tu kulipwa kitu ambacho kwa mujibu wa Katiba si jukumu la Bunge katika hatua ya sasa.

Lakini la pili, majibu ya Waziri hayajanionyesha moja kwa moja dhamira ya kuelekeza pesa za ndani kwenye maeneo muhimu sana ya usimamizi wa mazingira. Hali inayonipa mashaka kama kweli kwa mwaka huu wa fedha tutaweza kweli kwenda kupambana kikamilifu na uchafuzi wa mazingira unaoendelea maeneo mbalimbali ya nchi. Kwa sababu hiyo basi Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisiirudishe hiyo shilingi

ili suala hili sasa liweze kwenda kwenye maamuzi tuweze kupiga kura. Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tuwekane sawa kwa ajili ya kumbukumbu za *Hansard*. Naomba niwahoji sasa kwamba wanaoafikiana na Mheshimiwa Mnyika kwamba mshahara wa Mheshimiwa Waziri utolewe shilingi moja... ndiyo maana lilinipa taabu kidogo kwamba hoja ni nini sasa hapa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Hoja ni kifungu cha ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Kasma ndogo 6389 ya kifungu la 1001 Utawala na Matumizi ya Ujumla.

MWENYEKITI: Tumelewana, yaani ni shilingi moja ipungue katika fungu hili. Si ndiyo jamani? Wanaoafikiana na Mheshimiwa Mnyika, kwamba shilingi ipungue katika Fungu hili la Ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, waseme ndio! Wanaosema kwamba, isipungue kiasi chochote, Fungu hili litumike kama lilivyopangwa, waseme ndio!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu, kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1003 - *Policy And Planning Unit*Shs. 0

MWENYEKITI: Hata sifuri nayo niulize kama inaafikiwa ? (*Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu, kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 5001 *Environment*.....Shs. 7,510,379,000

MWENYEKITI: Nimemwona Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Mnyika.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi hapa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, kwanza na Susan Lyimo? Eh, basi ngoja, hebu twende kwa utaratibu kidogo. Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Mnyika. Waheshimiwa, ni tayari hao? Ahsante sana, ni hao hao. Naomba tuenze na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu kidogo 5301, *Climate Change Adoption Project*. Nilikuwa ninaomba kujua ni nani anayefadhili, kwa sababu nikiangalia sehemu zote inaonesha kwamba ni *grant* au ni

donor na huyo *donor* ni nani. Lakini katika kifungu hiki haioneshi lakini kuna fedha kutoka nje. Nilikuwa ninaomba maelezo ya ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, *Climate Change Adoption Project*, pesa hizi zinatolewa na Serikali ya Japan na *implementor* ni *UNDP*. Kwa hiyo, pesa hii haionekani hapa kwa sababu inatoka kwa *donor* inaingia *UNDP*. Lakini sisi kama *co-ordinator*, tunaweka ile *contribution* yetu ya ndani lakini pesa nyingi zaidi zinatoka Japan zinakwenda *UNDP*.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri hajanielewa. Fedha hizi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo, ufanuzi tu kwa sababu hajakuelewa. Si ndio eeh! Maana hatusimami zaidi ya mara moja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu. Kwa sababu, ye ye anachosema ni kwamba fedha ya *foreign* haionekani, inaonekana. Nilitaka tu kujua ni nani huyo anayetoa hizi fedha.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema. Japan kwenda *UNDP*. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma namba 6507, *NEMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kasma hiyo ya *NEMC*, kwa mwaka huu Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira limetengewa shilingi milioni 420 na zote ni fedha za ndani, hakuna hata senti kumi ya fedha za kigeni. Mwaka jana kufuatana na Kasma hiyo hiyo, *NEMC* ilitengewa shilingi milioni 300 fedha za ndani, hakuna hata senti tano ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inaelekea kwa kuangalia *breakdown* ya hizi Kasma, inaelekea kwamba Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira halipewi rasilimali za kutosha za kuweza kuliwezesha kusimamia uhifadhi wa mazingira na kuliwezesha kuangalia uchafuzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi hii na ninaomba nitoe taarifa mapema kabisa, kama sitapewa maelezo ya kutosha kuhusiana na hii nitaondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka nielezee kwamba, linganisha na Kasma zingine, *Climate Change Adoption Project* ina shilingi 1,587,414,000; *Montreal Protocol Implementation Project* milioni 212, *Environmental Management Act Implementation Support* shilingi bilioni mbili! Sasa *NEMC* ndio chombo kikuu cha usimamizi na uhifadhi wa mazingira katika nchi hii. Lakini fedha ambazo zinatengwa kwa ajili yake, ni wazi kabisa kwa kuangalia hizi *breakdowns* ni wazi kabisa kwamba *NEMC* haiwezi ika tekeleza wajibu wake kwa kukosa rasilimali! Na kama nilivyosema, kama sitapata maelezo ya kuridhisha hapa, nitaondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Napenda kutoa ufanuzi kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* ni Baraza letu na lina kazi muhimu na ndio maana hatuwezi kutegemea wafadhili kwa sababu tunataka kazi ifanyike kwa ukamilifu. Pamoja na ufinyu wa Bajeti, lakini tumepeleka hela nyingi *NEMC*, fedha za ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile *NEMC* inapata wafadhili kutoka nje, fedha ambazo hapa hatuwezi kuzionesha kwa sababu mchakato wake bado. Ni kama hizo fedha ambazo hazionekani lakini kuna fedha zinapita Chuo Kikuu, ufadhili wa *Norway*. Sasa hatuwezi kuziandika hapa lakini wanapofanya kazi wanafanya pamoja. Sasa kutokana na hilo na kwa sababu tumelalamika fedha za wafadhili hatuna uhakika nazo, ndio maana tumeweka fedha za ndani nyingi. Ahsante sana.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi kwa sababu, sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja kwamba *NEMC* ina fedha za wafadhili lakini hazionehwi hapa ni hoja ambayo haina ukweli wowote. Kasma nyingine zote zilizooneshwa hapa ambazo zinapata fedha za wafadhili, fedha zake zimeoneshwa. *NEMC* ina siri gani hiyo ambayo fedha zake za wafadhili, haziwezi zikaoneshwa kwenye kasma hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa sababu *NEMC* kupewa fedha kidogo ni wazi! Shilingi milioni 420, ukilinganisha na hivi vi-project vingine, *project* sio taasisi! Taasisi inapewa shilingi milioni 400, *EMEA Project* inapewa bilioni mbili! *EMEA Project*, inapewa bilioni 1.5! *EMA Implementation Support* inapewa bilioni 1.4! Inaonesha hatuko *serious!* Hatuko *serious* kuiwezesha taasisi kuu ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira, kufanya kazi ambazo tumeipa kisheria! *We are not walking the talk!* Tunawapa mamlaka ya Kisheria, hela tunawanyima! Halafu tukiuliza unaambiwa kuna fedha za wafadhili lakini haziwezi kuoneshwa hapa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haiwezekani! Haiwezekani, ni lazima Mheshimiwa Waziri, atueleze hapa, hizo fedha anazosema za wafadhili, kwa nini hazijaoneshwa hapa? Na ni wafadhili gani? (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Natoa nafasi ya wachangiaji kama wawili, kabla ya Mheshimiwa Waziri. Kabla ya hapo, Mwongozo wa Mheshimiwa Mnyaa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika Kamati yako hii, wakati unapotoa Mwongozo uwe *consistent*, usibague kwa mtu gani na mtu gani. Wakati nilipopata jibu la mambo ya fedha, mambo ya Zanzibar, akanyanya Waziri Mheshimiwa Samuel Sitta, kutoa maelezo ambapo sikuridhika, nikasimama. Kabla ya kutaka kusimama, ulipoona nasimama, ukasimama ukaeleza kwamba kwa mujibu wa Kanuni tulizotengua, mtu akishakueleza Kifungu mara moja, haruhusiwi kusimama mara ya pili. Sasa hivi Mheshimiwa Susan Lyimo umempa mara ya pili na Mheshimiwa Tundu Lissu, unampa mara ya pili. Naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa, kwanza ni makosa sana kumsingizia Mwenyekiti na kuanza kumvalisha kengele! Nimesema Susan Lyimo alikuwa anafafanua kwa Mheshimiwa Waziri kwamba alichokiuliza yeze sicho. Kwa hiyo, ilikuwa ni kufafanua tu swalii kwamba yeze nia yake ilikuwa ni Mfadhili wake wa hicho Kifungu ni nani, jina la Mfadhili tu basi na Mheshimiwa Waziri, amejibu, basi. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, tumekwenda vizuri tu, wala haina tatizo. Wanaosimama mara ya pili hapa ni wale waliokamata shilingi. Kwa hiyo, hakuna ubaguzi wala nini na waliozungumza leo hapa, nafikiri tangu tuanze kipindi hiki wanaweza kufika hata 25 hata 30 na wote tumewa-*treat* sawasawa. Mimi ninaamini tunakula muda bure, sasa nina wachangiaji wale wawili au watatu kwa hii hoja ambayo inaendelea hivi sasa ili Mheshimiwa Waziri afike mahali pa kusema chochote.

Wanaotaka kuchangia katika hili la shilingi hili, wasimame sasa niwatambue. Mheshimiwa Maige atachangia, mwingine Mheshimiwa Mwambalaswa na Mbunge wa Kawe Mheshimiwa Halima Mdee.

Tuanzie Kawe. Zisizidi dakika tatu, ni dakika mbili mbili.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niungane na mtoa shilingi kwa sababu moja kubwa. Kwanza juu ya majukumu ya *NEMC*, lakini pili juu ya tatizo kubwa la mazingira kwenye nchi yetu ambalo kuna Mheshimiwa mmoja leo asubuhi alisema kuna haja ya kutangaza mazingira kama janga la Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri akitoa maelezo juu ya hoja ya Mheshimiwa Mnyika, katika *Vote* ya 31, ukurasa wa 124, alizungumzia ongezeko la shilingi bilioni nne! Eti kuna shilingi bilioni mbili *point* kadhaa kwa ajili ya mishahara na marupurupu! Sasa hoja ya msingi hapa ya Mheshimiwa Lissu, ni kwamba kwa nini shughuli za msingi za maendeleo kwenye Baraza nyeti kama hili, itengewe kiasi finyu kiasi hiki, wakati kuna anasa nyingine ambazo zingeweza kuzuiwa fedha zikaletwa huku!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wa Nyamongo, wananchi wetu wa Kawe, wananchi wetu wa Ubungo, waweze kunufaika na utatuzi wa kero suga ya

takataka na uchafu na uharibifu wa mazingira, hiyo ndio hoja. Kwa hiyo, msiangalie hoja ameileta nani! Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwahi kusema usiangalie amesema nani, angalia mantiki ya hoja. Tunataka Mawaziri mtusaidie mantiki ya hoja. Ni hayo tu Mheshimiwa. (*Makofi*)

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hapa nadhani sisi wanasiasa hapa ndani tunataka tu tuonekane kwenye luninga, watu watuone huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye Kitabu cha Maendeleo. Ina maana kuna *project* fulani ambayo wanataka shilingi milioni 400. Sasa si wameshasema pale shilingi milioni 400! Wanetaka hela ya *operations*, wangekamata kitabu cha pili, hiki ni cha maendeleo! *Project* inayotaka shilingi milioni 400 unapewa shilingi milioni 400! (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa niseme tu kwamba sikubaliani na wazo la kuondoa shilingi kwenye eneo hili. Kama ambavyo wengi wa wasemaji wamezungumza, tuko kwenye Fungu la Maendeleo, fedha kidogo zinazowekwa kwenye *co-ordinating units* ni za usimamizi. Tunapozungumzia kwa mfano mradi wa *adoption*, tunataka kufundisha watu kutengeneza majiko sanifu na vitu vingine kama hivyo. Kwa hiyo, fedha nyingi zinakwenda kwenye miradi yenyewe na ndio kilichofanyika hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* yenyewe ni Kitengo cha Uratibu na hapa wameomba fedha na ukiangalia kwenye fedha za ndani shilingi milioni 420 ndio pesa nyingi kuliko sehemu nyingine yoyote kwenye Fungu hili, yaani kwa maana ya fedha za ndani. Kwa hiyo, kwa fedha za ndani hapa, *NEMC* wamepewa nyingi ukilinganisha na sehemu nyingine na fedha nyingi zinakuwa zimelenga kwenye miradi moja kwa moja. Kwa hiyo, mimi nilifikiri kwamba pengine suala lilikuwa ni ufanuzi na ufanuzi ukishatolewa ukaeleweka, mimi nafikiri kuonesha tu kwamba unakataa kuitisha fungu hilo, sidhani kama ni sifa njema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumsihi Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba, fedha ziende, watu watengenezewa majiko, watu wapande miti, watu wafanye hivi. Hizi kidogo kwa ajili ya uratibu, ndivyo imeonekana kwamba *NEMC* wanawenza wakafanya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwamba wazo hili la kutenga shilingi milioni 420 kwenye eneo hili, liendelee hivyo bila kutoa shilingi hata moja. Nashukuru. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kutoa ufanuzi tena kwamba fedha za *NEMC* zipo chini ya Idara ya Mazingira na hii ni kutokana na mfumo wa Bajeti na kuna Mheshimiwa mmoja amesema kuna usiri; hakuna usiri wowote, kwa sababu, kwa mfano mradi wa vyura, vyura wale wapo *University of Dar es Salaam*, sasa sisi hatuwatunzi!

Tunawezaje kusema hizo hela hapa kwamba tunazo wakati vyura wapo *University of Dar es Salaam*, wanalishwa kule, wanatunzwa kule, wanazaliana kule, lakini sisi tunahusishwa na *NEMC* inakwenda kuangalia wale vyura kila siku. Kwa hiyo, kuna miradi kama hiyo tumesema hatuwezi kuiweka hapa kwa sababu pesa zinaenda moja kwa moja kwa taasisi inayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *REDI* ambao unafadhiliwa na Norway. Unaingia *IRA – University of Dar es Salaam*, lakini kila wakati tunapofanya miradi tunafanya pamoja. Sasa sisi hatuwezi kusema kwamba hizi pesa tunazo sisi, wakati wafadhili wanataka ule mradi uende *University of Dar es Salaam* na kuna miradi mingine iko *SUA*, lakini tunafanya kazi pamoja. Lakini kwa sababu *NEMC* wote tunaipenda na tunajua inafanya kazi nzuri, fedha za ndani tumeziweka nyingi kwa sababu hatuwezi kutegemea tu fedha za wafadhili. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyopewa kwenye Kanuni ya 104, inabidi niongeze muda wa dakika 30 ili tumalizie hii shughuli iliyo mbele yetu. Baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lazima turudi kwa mtoa hoja ya shilingi, Mheshimiwa Tundu Lissu, utuongoze na mwisho utuambie unatuelekeza nini. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesikia hoja za Wajumbe ambao wamechangia hoja hii na ninaomba niseme tu kwamba, sikubaliani na hoja hizi ambazo zinasema kwamba niirudishe hii shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia mahesabu kwenye hili fungu, *projects* zimetengewa shilingi bilioni sita na ushee, *projects, local and forex!* Sasa *NEMC* ambayo ndio yenyewe jukumu kubwa la kusimamia mazingira na kasma yenyewe inaitwa *Environmental Protection*, *NEMC* ambayo ndio yenyewe jukumu kubwa katika *environmental protection*, imetengewa shilingi milioni 420 all local! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mjumbe anasema kwamba wametengewa na kwenye fedha za Matumizi ya Kawaida. Tumewauliza hapa ni ngapi? Hakuna aliyejibu! Kwa hiyo, hata hiyo ya kwamba wametengewa kwenye matumizi ya kawaida ni halina majibu! Sasa katika mazingira ya aina hii mimi *I can only conclude* kwamba Serikali hii is not walking the talk!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sirudishi shilingi. Naomba kura ipigwe for the record. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Tundu Lissu, anachosema ni kwamba Baraza la Hifadhi ya Mazingira, lililotengewa shilingi milioni 420 ni pesa kidogo sana. Katika kidogo hicho anataka na shilingi itoke. Sasa nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)

MWONGOZO SPIKA

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Mwongozo, Mheshimiwa Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kwa sababu napata wasiwasi kwamba Mbunge anapotoa shilingi Kifungu fulani kisipite, wengine tukaunga mkono, yeze akaondoka na shilingi yake. Nina wasiwasi mkubwa kwamba Singida, tunahitaji fedha za maendeleo na hasa kwa ajili ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mbunge anapotoa shilingi, kwenye mgao yumo?

MWENYEKITI: Nitautoa huo Mwongozo baadaye, fungu hili limeafikiwa?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama tafadhalii.

MWENYEKITI: Ni kweli kulikuwa na watu wawili, tuwatendee haki, Mheshimiwa Zambi, halafu Mheshimiwa Mnyika kwa kifupi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe pia Makatibu Mezani wakuongoze vizuri ili watendewe haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hivyo, fungu ambalo nataka kupata ufanuzi ni 5304 ambalo ni *O-zone depleting substance project* ambayo haikutengewa pesa. Nilitaka kujua kama *project* hiyo imemalizika au namna gani, lakini moja la jumla katika mafungi haya ukiondoa lile la *NEMC* yote yametengewa fedha nyingi sana za nje, kwa sababu tunaona shilingi bilioni 6.3 ni fedha za nje, lakini shilingi bilioni 1.1 ndiyo fedha za ndani, nataka kujua na Serikali ituhakikishie ina uhakika wa kwamba pesa hizi za nje zitakuja kwa maana ya kwamba miradi hiyo haitaathirika, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizo tunauhakika zinakuja na ni mradi wa *UNDP* tumeshamaliza awamu ya kwanza, mazungumzo yanaendelea ili kuanza awamu ya pili. Kwa hiyo, pesa hizo zipo tuna uhakika zinakuja, ahsante. (*Makofii*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho lakini kasma 6571 katika ukurasa wa 37, *EMA implementation support* ambayo ni mradi wa *Environment Management Act*, mradi wa kuhusiana na sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata ufanuzi kuhusu mambo kadhaa, kwenye hotuba mbalimbali, kwenye taarifa mbalimbali zinaonyesha kwamba changamoto kubwa tuliyonayo ni kusimamia Sheria ya Mazingira ambapo kuna vitu mahuusi vinakosekana, Wizara mbalimbali kuandaa mipango kazi ya sekta ya kimazingira, Serikali za Mitaa kuandaa mipango hiyo na vilevile kuunda zile Kamati mbalimbali mpaka kwenye ngazi ya mtuu na vijiji zile Kamati za Mazingira ndiyo kitu ambacho kinakosekana katika mfumo wetu wa usimamizi.

Sasa nataka kufahamu, hiki kiwango kilichotengwa hapa ambacho ni shilingi milioni 200 peke yake ndiyo pesa zetu za ndani za mradi mzima wa kimaendeleo wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na shilingi bilioni 1.8 ndizo ambazo ni pesa za nje, nataka kufahamu tu, ni kwa vipi kiwango hiki cha pesa ambacho ni shilingi bilioni 1.8 hatuna uhakika nao tuna uhakika na hii shilingi milioni 200 tu ya kwetu, kitawezekweli kwenda kuhakikisha kwamba mtandao huo unaundwa, taarifa zinapatikana, mipango inapatikana na vilevile ripoti ya hali ya mazingira inaandaliwa? Kwa sababu changamoto mojawapo ni kwamba ripoti ya hali ya mazingira imekuwa haiandaliwi kwa wakati. Hili nalo kama maelezo yatakayotolewa hayataniridhisha nitaomba nitoe hoja ya kuondoa shilingi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Mbunge John Mnyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba pesa za ndani tumezitenga hazitoshi na pesa za wafadhili tulizoziaandika hapa tuna uhakika nazo kwa sababu zote ambazo hatuna uhakika nazo hatujaziweka, tulizoweka ni zile ambazo tuna uhakika nazo. Na kutohana na maelezo hayo ni kwamba hizi pesa ni za Serikali Kuu, Halmashauri iko chini ya Wizara nyingine na Halmashauri tunaomba mjisimamie vizuri zitenge pesa za mazingira kwa sababu Halmashauri zipo karibu na wananchi na wananchi wanatumia mazingira kama tunavyojua. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, nyie ni wajumbe kwenye Halmashauri mhakikishe Halmashauri zinatenga fedha kwa ajili ya kutunza mazingira, ahsante. (*Makof*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wajibu wa kutoa maelezo ya ziada kwenye jibu zuri tu la Mheshimiwa Waziri mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuilewewe hii shughuli ya *environment management act* kwa maana ya ukaguzi. Mradi huwa unatozwa siyo kwamba Serikali inalipia kwenda kukagua, yule ambaye anakaguliwa yeze ndiyo hulipa gharama za kukaguliwa. Kwa hiyo, hakuna suala hapa la kusema hela ziwe nyingi sana ili Serikali ilipie ukaguzi. (*Makof*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kwa kweli naomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi na tusingekuwa tunaondoa shilingi mara kwa mara kama tungekuwa na fursa ya tukisema tunapewa fursa ya kujibu walau dakika

mbili. Sasa kwa sababu hakuna fursa nyingine ya kujibu basi natumia hii fursa hii ya shilingi kuweza kujibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, nilivyokuita si ndiyo umepewa fursa ya dakika mbili hii uweze kujibu? Maana yake unapotosha Taifa hivyo kuwa huna fursa ya kujibu wakati nimeshakupa hiyo fursa. Haya endelea. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ieleweke kwamba nisingetumia hoja ya kuondoa shilingi.

MWENYEKITI: Endelea, bado dakika mbili hapo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ahsante, kwa dakika hizo hizo, maelezo yaliyotolewa mwishoni kuhusiana na tozo zinazotozwa na Kampuni ya Ukaguzi kimsingi yanalipotosha Taifa. Kwa sababu mimi naelewa kabisa ni kweli kwamba makampuni yanayofanyiwa ukaguzi wa kimazingira yanatozwa *fee fulani* na si ile inayojitokeza kwenye vitabu vya mapato, halafu inapangiwa matumizi, sisi tunachoangalia hapa ni matumizi sasa ya kazi, je, yamepangiwa pesa za kutosha kwa maana ya mradi wa maendeleo, pesa zilizotengwa hapa hazitoshi. (*Makofi*)

La pili, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani na kule tunashika sana kuhusu masuala ya usafi wa mazingira na kadhalika. Lakini naelewa wajibu wa *NEMC* na wajibu wa Wizara, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ni uratibu kuhakikisha kwamba zile mamlaka zimeandaa mpango, zimeandaa taarifa na kufanya huu ukaguzi pamoja na vilevile na kuandaa taarifa za mwaka. Haya ni mambo ambayo yanatumia pesa nyingi, ndiyo maana leo Wizara kwa mradi wa kutafuta tu hali ya mazingira Dar es Salaam unategemea pesa kutoka *UNEP*, sasa kama hali ipo namna hii hizi pesa kwa vyovyyote vile haziwezi kututosha katika mradi mzima wa maendeleo wa kuhakikisha kwamba tunakabiliana na tatizo la uchafuzi wa mazingira. Kwa hiyo, ningependa bado kupata majibu kabla sijakubali kuondoa shilingi ama kurudisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Wakati huu ni wakati wa kuwa *categorical*, maana yake ni wakati ambao ama tunapanua mjadala kwa maana ya wachangiaji au vinginevyo, unaendelea kutoa shilingi au unairudisha ili tusonge mbele. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kutoa shilingi katika hili.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Anayemuita Mwenyekiti, ni vizuri kusimama.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikipata shida na hasa ninapowasikiliza wenzangu, nilimsikiliza Mheshimiwa Tundu Lissu na msimamo wa Mheshimiwa Mnyika. Mimi ninavyoona kwenye vitabu vyangu

hana nikiangalia kitabu maana alichokisema Mheshimiwa Tundu Lissu na sasa ndicho hicho hicho kinachosemwa na Mheshimiwa Mnyika, ni kama vile *NEMC* imetengewa shilingi milioni 420 tu, lakini ukweli siyo hivyo. Fedha iliyotengwa ni nyingi tu, labda kama kuna jambo maalum lisemwe ambalo wao wanalionia halijapatiwa fedha. Kwa mfano...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simbachawene, hoja iliyoko mezani hapa ni lile Fungu 6571 *Environment Management*.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Na ndiyo nasema hilo hilo, kwa mfano *environmental management*, hii ni ya *NEMC* shilingi bilioni mbili, ukija hii *Lake Tanganyika Environmental Management Project* na yenewe ni ya *NEMC*, ukijumlisha hizi fedha zote hizi ni nyingi sana *African Stockpiles* mambo ya dawa, kukagua dawa zilizoharibika na mambo mengine shilingi bilioni 1.4 lakini ukija kwenye *administration* kwa mfano katika kitabu hiki cha pili nilikuwa nataka kujenga vizuri hoja yangu hapo uniruhusu, ingawa natoka kwenye hoja ya msingi lakini *NEMC Environmental protection* hii pesa yote hii ni ya *NEMC* shilingi bilioni tano, ukijumlisha shilingi bilioni tano na ukajumlisha na hizi hapa karibu 1, 2, 3 na kidogo karibu unapata shilingi bilioni tisa, zote hizi ni za *NEMC*. Kwa hiyo hii *environmental* ni mradi ambaa umeombwa katika Bajeti mahususi kwa ajili hiyo. Maana yake hata hii shilingi milioni 420 iliyowekwa hapa haijasemwa ni kwa ajili ya kitu gani? Hii maana yake itafanya shughuli yoyote itakayojitokeza na ndiyo maana haikuwekwa hapa.

Kwa hiyo, nilitaka tu kuweka vizuri na nilitaka niingie kwa mlango wa taarifa lakini nikaona hoja inayojadiliwa ni ile ile, nadhani tusipotoshe umma, fedha iliyotolewa kwa *NEMC* ni nyingi sana kiasi cha shilingi bilioni karibu tisa kwa ajili ya *NEMC*. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Simbachawene haina ukweli wowote, kwenye *breakdown* yote ya hilo fungu imetajwa miradi, haionyeshi hiyo miradi ya *IRA* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au ya Idara ya Mazingira au ya Chuo Kikuu cha Biashara Moshi au ya nani? *Item* pekee inayotaja *NEMC*, ni *item* yenye shilingi milioni 420, kwa hiyo, maelezo kwamba hizi fedha zote shilingi bilioni tisa ni za *NEMC*, ushahidi uko wapi na hatujaonyeshwa randama. Ni maneno ya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Tundu Lissu mmetutoa kwenye hoja ya Mheshimiwa Mnyika, sasa mmeingiza ya kwenu hapa katikati, mimi niko kule kwa Mheshimiwa Mnyika, kwa wanaotaka kuchangia kuhusiana na suala la Mnyika. Mheshimiwa Waziri unasema nini kuhusu suala la Mheshimiwa Mnyika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tu Waheshimiwa Wabunge kwamba suala hili tumelipa umuhimu wa hali ya juu na wote tumeona umuhimu wa kuongezewa fedha nadhani Bajeti ijayo tutashirikiana vizuri kuhakikisha kwamba fedha hizi zimeongezeka

lakini kwa sasa hivi kutokana na ufinyu wa Bajeti tunashukuru hata hiki tulichokipata, tutakitumia vizuri sana kutokana na maagizo yenu na naomba tushirikiane, ahsante. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ameahidi kwamba mwaka ujao ataongeza pesa kwenye suala la Sheria ya Usimamizi wa Mazingira naomba kuirudisha hiyo shilingi moja. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKIDI: Muongozo wa Mwenyekiti.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.Naomba Mwongozo wako katika Kanuni ya 64(1)(g); “Bila ya kuathiri masharti ya Ibara 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, akichangia hoja ya Fungu la Maendeleo ya *NEMC* alisema kwamba wanasiwa tunapenda kuonekana kwenye luninga. Hii ni lugha ya kuudhi na ya kudhalilisha kwani sisi kama wanasiwa na hasa Wabunge tunawajibu wa kuisimamia Serikali na hasa wakati huu wa Bajeti na siyo kuonekana katika luninga, *issue* ya Wabunge, Bunge hili kuonyeshwa *live* katika luninga sidhani kama kuna Mbunge aliomba Bunge lonyeshwe *live* ili sisi tupate faida ya kuonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli yako. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Ofisi ya Makamu Rais kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mbadiliko yoyote hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.
(*Makofî*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa hiyo, naomba kutangaza Makadirio haya sasa yamepata kibali rasmi cha Bunge letu, naomba kuwapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais na kuwatachia kila la heri, Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuruguenzi na watusika wote wa utekelezaji wa Bajeti hii na hasa kumtakia kila la heri Mheshimiwa Makamu wa Rais mwenyewe awe na afya njema kwa mwaka mzima ujao. (*Makofî*)

(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira)
kwa mwaka wa fedha, 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Tunaziomba Kamati za Katiba na Sheria na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira zipo changamoto zimejitokeza hapa tunawaomba mzifanyie kazi ili mwakani tukikutana basi baadhi ya mambo yasijirudie.

Nilikuwa nimeombwa nitoe ufanuzi wa mambo mawili moja, la habari ya wanasiasa kuonekana katika luninga, nikubaliane tu wote wawili waliozungumza, ni kweli kuna wakati kuna wanasiasa wanaopenda kuonekana kwenye luninga, lakini si kweli kwamba kila mwanasiasa anayetaka kuonekana humo anataka kuonekana tu kwa sababu ya kuonekana. Kwa hiyo, nikutumia vizuri muda wetu ambao tumepewa na Taifa, huo ndiyo Mwongozo wangu. (*Makofî*)

La pili la Mheshimiwa Martha Mlata, yeeye aliulizia habari ya shilingi kama Mheshimiwa akiondoka nayo sasa wale tunaotaka maendeleo itakuwaje wakati huo Mheshimiwa kaondoka na shilingi, hili ufanuzi wake ni kwamba katika fungu husika kubwa, kama shilingi imetolewa katika fungu kubwa, lakini fungu hilo likapitishwa, basi maana yake matumizi ya mwaka huu yatafanyika na hasi ile ya shilingi moja, pungufu ile shilingi moja. Kama shilingi itatolewa kwenye mshahara wa Waziri maana hii taswira ya kwanza ni kwenye fungu kubwa, taswira ya pili ni kutolewa shilingi kwenye mshahara wa Waziri, maelezo yake ni yale yale kwamba atapata mshahara wake wa mwaka pungufu shilingi moja. Lakini katika mshahara wa Waziri sasa hili ni katika Mabunge mbalimbali, ikitokea Bunge hili limekubali kwamba Mheshimiwa Waziri fulani, kutokana na kutokuwajibika kwa jambo fulani itolewe shilingi katika mshahara wake, *implication* yake kwa kweli ni Bunge hili likikubaliana hivyo ni kwamba Bunge halina imani na Waziri yule. (*Makofî*)

Kwa hiyo, katika nchi nyingine huko, kinachofuata huwa ni kukaa pembeni. Kwa hiyo, si jambo dogo hili la kutoa shilingi kwa mshahara wa Mheshimiwa Waziri tunaposema ndiyo au hapana tutende haki, tusifanye tu masihara, kwa sababu ni jambo ambalo linakwenda katika rekodi mbalimbali lazima pawe na sababu za msingi hasa kwa nini mshahara wa Waziri uondoke bila shilingi, kwa sababu ile shilingi ni *symbolic* lakini

kielelezo cha kutokuwa na imani kwa kiwango kikubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa Mheshimiwa Waziri kwa kiasi cha kumpa adhabu ya kutoa shilingi tu katika mshahara wake.

Kwa hiyo, ningewaomba kuanzia sasa kwenda mbele tuwe makini sana na zoezi hili hasa kwenye shilingi ya Mheshimiwa Waziri, ile ya Fungu ile haina neno.

Mwisho wa matangazo, oooh! Matangazo, Kaimu Katibu wa Bunge, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kuwa wamealikwa kushiriki katika mkutano wa wadau wa maduka ya dawa muhimu utakaofanyika katika Ukumbi wa *St. Gasper Dodoma* kesho Jumamosi, tarehe 9 Julai, 2011 kuanzia saa tatu asubuhi. Mkutano huo umeandaliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa za ufuatiliaji na tathimini ya mpango wa maduka ya dawa muhimu. (*Makofi*)

Tangazo la semina, Kaimu Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba ile semina tulioitangaza mchana ambayo itafanyika siku ya Jumapili, tarehe 10 Julai katika Ukumbi wa Pius Msekwa, itaanza saa tano, lakini sasa badala ya zile Kamati chache, Mheshimiwa Waziri wa Afya, amekubali na Serikali imekubali kwamba semina hii sasa ambayo itatolewa na Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*), kutokana na umuhimu wake sasa ni vyema ifanyike kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria badala ya Kamati chache za Bunge. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa Jumapili saa tano asubuhi tarehe 10 Julai katika Ukumbi wa Pius Msekwa kwa ajili ya semina hii muhimu sana ya *MSD* ili tuweze kufahamu shirika letu hili muhimu sana kwa afya zetu na za wananchi wote wa nchi yetu lina mipango gani kuhusiana na afya ya wananchi wetu.

Kwa kumalizia baada ya hapa kuna tafrija ya *ZANTEL* kwa Waheshimiwa Wabunge na niwahakikishie kabisa kwamba maandalizi ni ya uhakika *straight* tukitoka hapa burudani imeandaliwa vizuri, kila kitu kimepangwa kwa viwango vilevile. Mmenielewa eeh! Kwa hiyo, mnaalikwa nyote ni pale nyuma ya Jengo la Utawala, si ndiyo Makatibu? Wote mnakaribishwa. (*Makofi*)

Baada ya maelezo haya, Waheshimiwa Wabunge shughuli zote zilizokuwa zimepangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika na kwa hiyo basi, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuruni Wabunge wote kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kwa siku ya leo ya kuwawakilisha wananchi wetu. Hivyo basi, naahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu, tarehe 11 Julai, 2011 saa tatu asubuhi.

(*Saa 2.04 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,
Tarehe 11 Julai, 2011 saa tatu asubuhi*)

